# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 23 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU WA MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Hotuba ya Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA- MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 115

**Kambi za Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi Nchini**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Utekaji nyara na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) vilikithiri kwenye miaka ya 2000 hali iliyopelekea Serikali kuanzisha kambi maalum kwa ajili ya usalama wao.

(a) Je, Serikali imeanzisha kambi ngapi mpaka sasa na ni katika Mikoa na Wilaya zipi?

(b) Je, ni watu wangapi wenye ulemavu wa ngozi wanaoishi katika makambi hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA A. IKUPA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b)kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kambi iliyoanzishwa na Serikali kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa ngozi hadi sasa, isipokuwa kuna shule katika baadhi ya Mikoa kama vile Shule ya Buhangija iliyoko Mkoani Shinyanga ambayo imepokea watoto wenye ulemavu wa ngozi kwa kuletwa na wazazi, viongozi wa vijiji, Maofisa Ustawi wa Jamii na Polisi. Hii yote ni katika kunusuru uhai wao, kwani Sera ya Taifa ya watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 inakataza watu kuishi kwenye Kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la (b) jibu ni kwamba idadi ya watu wenye ulemavu wa ngozi waishio

kwenye Shule ya Buhangija ni 309 ambapo wanaume ni 152 na wanawake ni 157.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa baadhi ya watoto wanaosoma katika kituo hiki au Shule ya Buhangija wengi wao wametelekezwa kabisa na wazazi wao, kwa maana ya kwamba wazazi wakati ule wa mauaji waliwafikisha watoto wao getini katika ile shule na kuwaacha; na hivi sasa wakati wa likizo na muda wote yamekuwa ni makazi yao katika kituo hiki; Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba angalu siku moja basi, watoto hawa wanawapata wazazi wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia swali langu la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu ameeleza idadi ya watu wenye ulemavu wa ngozi waishio kwenye shule ya Buhangija; je, ina mpango gani pia wa kuhahakisha kwamba tunapata idadi kamili ya watu wenye ualbino na hata watu wengine wenye ulemavu ili basi tunapopanga au tunapotunga sera/ sheria kujua kwamba idadi kamili ya watu wenye ulemavu Serikali iweze kupeleka maendeleo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kilikuwa kinafanywa na Serikali baada ya kutokea lile wimbi la mauaji kwa watu wenye ualbino ilikuwa ni kunusuru maisha yao kama nilivyosema, kwa kuweka kwenye vituo mbalimbali, lakini sasa hivi kitu ambacho kimefanyika Serikali kwa

kushirikiana na viongozi wa vijiji na vitongoji pia na halmashauri ambako wanatoka iliweza kuangalia jinsi gani hawa watu wanaweza wakarudishwa kwenye familia zao kwa kuangalia usalama na kama ile hali inakuwa imeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa upande wa Kituo cha Buhangija na vituo vingine, Serikali ambacho inafanya sasa hivi ni kutembelea hivi vituo, lakini kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza, kama itabainika kwamba kuna watoto wako kwenye hivi vituo, basi Serikali itafanya utaratibu wa kuwapata wazazi wao ama walezi wao ama familia zao na kuweza kuwarejesha kwenye familia zao ama wakati wa likizo sasa waweze kurudi kwenye famila zao kama ambavyo ilivyo kwa watoto wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilijibu kwenye swali la Mheshimiwa Khadija Nassir na wakati pia natoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba sensa inafanyika kila baada ya miaka kumi. Ilifanyika mwaka 2012, lakini pia itafanyika mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kwa kuona umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi za watu wenye ulemavu kwa ujumla wake, wakiwemo watu wenye ualbino, basi inaandaa mpango ambapo yaani inafanya majadiliano ya ndani kwa kuona kwamba ni jinsi gani sasa tunaweza tukapata takwimu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaweka mipango, kwa hiyo, tutawatumia Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vijiji ili kuweza kupata takwimu sahihi za watu wenye ulemavu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, limeelekezwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

Na.116

## Upungufu wa Watumishi wa Hospitali ya Wilaya - Mbulu

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Mbulu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi; upungufu huo wa watumishi umeathiri utoaji wa huduma wa Hospitali hiyo na Vituo vya Afya vya Tawi na Daudi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza watumishi katika Hospitali hiyo?

(b) Serikali inatekeleza mpango wa upanuzi wa Vituo vya Afya zaidi ya 200 nchini; je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na changamoto za watumishi, fedha na vitendea kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya watumishi wa sekta ya afya katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ni 345, watumishi waliopo ni 206 na upungufu ni watumishi 139. Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa afya kadri wanavyohitimu na kupangwa moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliajiri watumishi 2,058 wa kada za afya kwenye Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hao, Halmashauri ya Mji wa Mbulu ilipangiwa watumishi kumi wakiwemo Madaktari wawili, Matatibu wawili; Afisa Muuguzi mmoja; Afisa Afya Mazingira mmoja na Msaidizi wa Afya, Mazingira mmoja; Mteknolojia Msaidizi mmoja na Wauguzi daraja la pili wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imeomba kibali cha kuwaajiri watumishi 91 ili kupunguza upungufu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inaendelea na ujenzi wa Vituo vya Afya 208 nchi nzima ili kuboresha huduma ya dharura kwa mama wajawazito. Ujenzi wa vituo hivyo utagharimu shilingi bilioni 132.9 hadi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi huo, vituo hivyo vimetengewa shilingi bilioni 35.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaatiba ili kuviwezesha kutoa huduma kwa wagonjwa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeomba kibali cha kuwaajiri watumishi wa kada ya afya wapatao 25,000 ili kuhakikisha kunakuwepo na watumishi wenye sifa stahiki kwenye hospitali, vituo vyote vya afya na zahanati.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Mbulu, kwanza kuishukuru sana Serikali kwa ujenzi wa Vituo vya Afya vya Daudi na Tlawi katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu na Kituo cha Afya cha Dongobeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba pamoja na shukrani hizi ninazotoa, naishukuru pia Serikali kwa kutenga fedha za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbulu ambayo iko kwenye Halmashauri ya Mji wa Mbulu takribani shilingi bilioni moja na nusu katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili sasa; upungufu huu wa watumishi umepelekea watumishi waliopo kufanya kazi ya ziada kutokana na kwamba hospitali hii ya Halmashauri ya Mji wa Mbulu iko mpakani mwa Halmashauri ya Babati, Halmashauri ya Karatu na Halmashauri ya Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapokea huduma wa afya katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mbulu, karibu asilimia 30 wanatoka kwenye maeneo ya pembezoni, hali inayopeleka watumishi walioko kufanya ya ziada.

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali iniambie inachukua hatua gani sasa kuongeza fedha za *OC* kwa ajili ya wale watumishi wanaofanya kazi ya ziada ili waweze kuwahumia wananchi wetu wanaotoka ndani ya Halmashauri ya Mbulu na Halmashauri nyingine za jirani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa sasa fedha zinazotengwa za dawa na vifaa tiba ni kidogo kulingana na idadi ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini na kwa kuwa wale wanaotoka nje ya Jimbo la Mbulu Mjini hawapo kwenye mpango huu; Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kutazama takwimu ya wananchi wanaopokea huduma ya Afya katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu. Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazipokea pongezi alizotoa kwa kazi ambayo inafanywa na Serikali, lakini ameuliza maswali mawili. La kwanza ni suala zima la kutoa *allowance* kwa wale watumishi wachache ambao wanalazimika kufanya masaa ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba kila Mtumishi na hasa wa sekta ya afya pale anapofanya kazi masaa ya ziada, ndiyo maana kuna kipengele cha *on-call allowance* ili waweze kulipwa stahili zao na wahakikishe kwamba wanafanya kazi ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeomba kibali cha kuweza kuwaajiri watumishi 25,000. Kibali hiki kitakapokuwa kimepatikana ni imani yangu kubwa Hospitali yao ya Mbulu nayo itapata watumishi kama ambavyo ameomba watumishi 91, ni ukweli usiopingika kwamba itapunguza uhaba uliojitokeza kufikia sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa matatizo ya Mbulu yanafanana kabisa na Halmashauri ya Mji wa Mafinga ambao kwa juhudi za wananchi pamoja na Serikali tunatarajia kukamilisha Kituo cha Afya cha Ulole, Kisada na Bumilahinga na pia Kituo cha Afya cha Ihongole kufuatia kupewa fedha shilingi milioni 500 na Serikali; lakini kwa kuzingatia kuwa Hospitali Mafinga iko kandokando ya barabara kuu na kati ya Iringa na Makambako hakuna hospitali hapo katikati.

Je, Serikali iko tayari kutuongezea idadi ya Watumishi ili tutakapofungua Zahanati na Vituo vya Afya hivyo, ufanisi wa kukaribisha huduma za afya kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga uwe wa dhati na wa vitendo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, na wewe ni shududa kwamba wakati tunapitisha bajeti yetu Mheshimiwa Mbunge Cosato Chumi

alikiri kabisa kwamba sasa hivi Mafinga ni motomoto kwa sababu kuna upanuzi wa hospitali. Pia hali iliyoko Mafinga ukilinganisha na Mbulu kuna utofauti mkubwa, maana wenzetu wana kituo. Kwanza kuna Chuo ambacho kinafundisha Waganga pale. Kwa hiyo, wakati wa kwenda kufanya *practical* inakuwa rahisi kwa wao kwenda katika Zahanati na Vituo vya jirani ikiwa ni pamoja Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba Vituo vya Afya vyote na Zahanati zote zinakuwa na wahudumu kwa maana ya Waganga pamoja na Wauguzi ili hicho ambacho kimekusudiwa na Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma kwa wananchi kinakuwa kweli na siyo nadharia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Waheshimiwa Wabunge, bado tupo Ofisi hiyo hiyo ya Rais, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Viti Maalum, kwa niaba yake namwita Mheshimiwa Hawa.

Na. 117

**Ujenzi wa Kiwanda cha Kubangua Korosho - Mtwara Mikindani**

**MHE. HAWA B. MWAIFUNGA (k.n.y. MHE. TUNZA I. MALAPO)** aliuliza:-

Je, ni eneo gani limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Kubangua Korosho katika Manispaa ya Mtwara Mikindani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani imetenga maeneo kwa ajili ya viwanda vya kubangua korosho kwa ajii ya wajasiliamali wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015 mpaka mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipanga na kupima viwanja vyenye ukubwa wa ekari 239.13 katika eneo la Mtepwezi na Mtawanya kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho na maghala. Katika viwanja hivi jumla ya ekari 28.41 imegawiwa kwa mfumo wa wakfu wa kuhudumia zao la korosho *(CIDTF)* na Chama cha Ushirika cha Mtwara na Masasi *(MAMCU)* kwa ujenzi wa viwanda vya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ina jumla ya ekari 210.72 ambazo zipo tayari kwa ajili ya waombaji mbalimbali walio tayari kujenga viwanda hasa vya kuchakata korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Halmashauri inaendelea na utengaji wa maeneo kwa ajili ya ujasiliamali wadogo wadogo kwa mwaka 2016/2017. Halmashauri imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 7.8 kwa ajili ya wajasiliamali. Maeneo hayo yapo eneo la Chikongola, Skoya, Ufukoni A, Ufukoni Stendi na eneo la SIDO.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA B. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu ya Serikali ya utengaji wa maeneo, lakini je, mpaka sasa ni waombaji wangapi ambao tayari wameshapewa maeneo hayo kwa ajili uwekezaji wa viwanda vya kuchakata korosho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo inalima tumbaku kwa wingi; je, ni lini Serikali itatenga maeneo ya uwekezaji wa viwanda vya korosho/ulimaji wa tumbaku ili wakulima wetu waweze kunufaika na tumbaku yao? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anauliza ni wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaungana na mimi kwamba suala la kitakwimu linahitaji kupata *data* mapema. Namwomba Mheshimiwa ili apate jibu la uhakika, angeleta kama swali la msingi ili tuweze kumtafutia takwimu ili tumpe majibu ambayo yanastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya Mkoa wa Tabota kutenga eneo kwa ajili ya wakulima wa korosho; kasema korosho na wakati mwingine kasema tumbaku, sasa *I am not so sure* ni kwa ajili ya nini? Kwa sababu hata ukienda Tabora pia korosho zinastawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama msingi ni kwa ajili ya wakulima wa tumbaku, namwomba Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri yeye ni Diwani katika eneo lake, mchakato ni vizuri ukaanzia kwenye Halmashauri, maana yeye analifahamu vizuri eneo la Mkoa wa Tabora ili wahakikishe kwamba maeneo kwa ajili ya wajasiriamali yanawekwa na yanatunzwa ili watu wetu waweze kupata maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa inayolima zao la korosho na yapo maeneo mengi ambayo ni rafiki kwa ujenzi wa viwanda vya korosho ikiwemo Wilaya ya Tunduru na Namtumbo ambapo zao la korosho linalimwa katika Wilaya hizo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha tunajenga viwanda katika maeneo hayo ili wakulima sasa waweze kubangua korosho zao katika Wilaya hizo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi kwanza nampongeza Mheshimiwa Chikambo, lakini pia nawapongeza wote wanaofuatilia suala hili la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa rai kwa sisi sote ambao tuko hapa na Watanzania wengine ambao watafanikiwa kuwafahamu wanaohitaji kuwekeza katika viwanda vya korosho; tafadhalini Tanzania ni katika nchi ambayo inatoa korosho bora sana. Hali kadhalika kupitia *SIDO* tunatengeneza viwanda vidogo vidogo vya kuweza kuendeleza ubanguaji au viwanda vya korosho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata. Linaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na.118

**Ujenzi wa Barabara na Mitaro Katika Jimbo la Segerea**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Jimbo la Segerea ni moja kati ya Majimbo ya Dar es Salaam ambalo wakazi wake ni wengi na wa kipato cha chini na sababu kubwa ikiwa ni ubovu wa miundombinu ya barabara hasa madaraja na mitaro, hivyo kusababisha mafuriko ya mara kwa mara.

Je, ni lini Serikali itajenga madaraja ya Tabata Kisiwani na Kisukuru sambamba na kujenga mitaro ili kupunguza adha ya mafuriko katika Kata za Jimbo hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuhudumia wananchi wa Jimbo la Segerea katika kuboresha na kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara, madaraja pamoja na mitaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua tatizo la adha ya mafuriko yanayotokana na mvua maeneo ya Tabata, Halmshauri ya Manispaa ya Ilala kupitia mradi wa *DMDP* imepanga kujenga mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 9.82 na vivuko katika bonde la Msimbazi – Tenge – Lwiti – Sungura na Tembomgwaza kwa gharama ya shilingi bilioni 15 ambazo zabuni za ujenzi huo zinatangazwa mwezi Mei, 2018. Hivyo, baada ya ujenzi wa mifereji hiyo na vivuko, tatizo la mafuriko kwa wananchi wa Tabata Kisiwani na Kisukuru litapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mawenzi - Tabata - Kisiwani kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitengewa shilingi milioni 180 za kufanyia matengenezo kwa kiwango cha Changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Manispaa ya Ilala imeyenga shilingi milioni 40 za kuifanyia matengenezo ya kawaida na kukarabati daraja lililopo eneo la Mwananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Majibu ya Naibu Waziri tumeyasikia wakati wote. Mradi wa mfereji anaousema wa *DMDP* ni mradi ambao tumeambiwa utatekelezwa tangu mwaka 2014 na wakazi wa kata zinazopitiwa na mradi huo waliambiwa wasiendeleze maeneo yao tangu 2014 wakiendelea kuhangaika na mafuriko kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna changamoto ya madaraja na barabara Kata ya Bonyokwa, Kata ya Kinyerezi, Kata ya Segerea, Kata ya Liwiti na kubwa kuliko ni Kata ya Tabata katika barabara ya kwenda Mwananchi, kalvati limebomoka na kwa sasa ninavyoongea...

**MWENYEKITI:** Swali, swali, swali.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali; je, ni lini mradi huo mkubwa wa *DMDP* utajengwa na barabara au Daraja la Kisiwani? Swali la kwanza.

Swali la pili, uanzishwaji wa *TARURA* umeondoa uwajibikaji wa Halmashauri sambamba na Madiwani moja kwa moja katika ujenzi wa barabara za mitaa. Je, Wizara ina mkakati gani kuhuisha kazi za *TARURA* ili waweze kutoa *report* katika Baraza la Madiwani ambalo moja kwa moja ndiyo wanawajibika kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kujua kero zao za moja kwa moja za barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Theonest amesema imekuwa ni muda mrefu hadithi imekuwa ikisemwa, lakini utakubaliana nami kwamba katika majibu yangu kwenye swali la msingi, nimemwambia kwamba kandarasi tunatarajia itatangazwa mwezi Mei na mwezi Mei siyo mbali sana, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, tumeahidi tutatekeleza katika hili ambalo nimelisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameongelea juu ya suala zima la uanzishwaji wa chombo hiki cha *TARURA* na anachoomba ni namna gani *TARURA* watahuisha ili

wananchi waweze kupata ushiriki wao kwa kupitia Waheshimiwa Madiwani na Wabunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* ina wajibu wa kuhakikisha kwamba taarifa zake zinapelekwa *DCC* na *DCC* Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe, lakini Mwenyekiti au Meya ni Wajumbe na Wakurugenzi ni Wajumbe. Kwa hiyo, taarifa itakuwa inatolewa hapo na tutapata fursa ya kuweza kuwahoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, pia kwenye chombo cha *RCC* ambapo sisi Waheshimiwa wote ni Wajumbe, naomba tushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijaribu kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba kabla ya kuanzishwa kwa *TARURA* kila Mbunge na hasa kila Diwani alikuwa anaomba apate angalau hata kilomita moja ya kipande cha barabara au kalavati litengenezwe upande wake kiasi kwamba ule ufanisi *(value for money)* ilikuwa haionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tukienzi chombo hiki, bado ni mapema kabisa. Maeneo mengine ambayo *TARURA* imeanza kufanya kazi, wanapongeza. Naomba tukiunge mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni; kwa niaba yake linaulizwa na Mheshimiwa Halima Bulembo.

Na. 119

**Kuliendesha Shirika la Umeme *TANESCO* kwa Faida**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO (K.n.y. MHE. JAMAL KASSIM ALI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulifanyia Shirika la Umeme *(TANESCO)* lijiendeshe kwa faida?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO)* linakabiliwa na gharama kubwa za uendeshaji ambapo zaidi ya asilimia 80 ya gharama zinatokana na uzalishaji wa umeme, ukarabati wa mitambo na miundombinu mingine muhimu ya umeme. Mapato ya Shirika yamekuwa hayakidhi vya kutosha gharama za uendeshaji hususan katika maeneo ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta mazito ambayo ni ghali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika pia linakabiliwa na tatizo la malimbizo ya madeni ya wateja wakubwa, wa kawaida na wadogo kushindwa kulipa ankara za umeme kwa wakati zikiwemo Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na wateja wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati madhubuti ya kuliwezesha Shirika la *TANESCO* kujiendesha kibiashara na kuondokana na hasara. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kufanya uwekezaji katika mitambo ya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia na maji ili kuepukana na mitambo inayotumia mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari mipango inaendelea kuanza utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 2100 wa *Rufiji Stigler's Gorge* utakaozalisha umeme kwa gharama nafuu na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za kuzalisha umeme na kulifanya Shirika lijiendeshe kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ni megawati 300 zitokanazo na gesi asilia eneo la Mtwara pamoja na megawati 330 katika eneo la Somangafungu Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha karibuni, maeneo ya Kibiti, Ikwiriri na Ngara yameunganishwa katika gridi ya Taifa, hivyo kupelekea kupunguza gharama za uendeshaji iliyokuwa ikitokana na matumizi ya mafuta mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingine ya Serikali ni kuunganisha baadhi ya maeneo katika Gridi ya Taifa kwa utekelezaji wa miradi ya njia kusafirisha umeme kwa Mikoa ya Ruvuma, Rukwa na Kigoma na hivyo kuachana na mitambo inayozalisha umeme kwa mafuta ambayo ni ghali. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa unaoendelea kwa *TANESCO* hasa eneo la uzalishaji, lakini hasara ya Shirika la *TANESCO* imekuwa inaongezeka kwa kasi zaidi. Kati ya mwaka 2015 mpaka 2017 ambapo *TANESCO* wameongeza hasara ya shilingi bilioni 124 mpaka shilingi bilioni 346.

Swali langu, Serikali ina mkakati gani unaotekelezeka kuhakikisha inapunguza hasara hizi na hatimaye kupata faida? *(Makofi)*

Swali langu la pili, *TANESCO* itagawanywa lini ili kutofautisha uzalishaji na usambazaji wa umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri. Namwona Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kwa muda mrefu Shirika letu limekuwa likijiendesha kwa hasara. Napenda kutoa taarifa tu katika Bunge lako kwamba hivi sasa Shirika la *TANESCO* limeanza kuongeza uzalishaji kuliko miaka iliyopita. Kipindi cha Julai mwaka 2017 hadi Machi mwaka huu, *revenue* ya *TANESCO* kwa wiki imeongezeka kutoka shilingi bilioni 29.1 mpaka shilingi bilioni 32.5. Kwa hiyo, ni maendelea mazuri ya Shirika letu katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zilizochangia ni pamoja na kwanza kuzuia kuingiza vifaa kutoka nje, kitu kilichokuwa kinaligharimu shirika kwa kiwango kikubwa sana. Kitu cha pili ni kuwaunganisha wateja na LUKU kwa nchi nzima ambao ni mpango unaendelea na ni matumaini yetu Shirika litaendelea kuwaunganisha wateja na kupata mapato makubwa, na lingine ni kuondo kana na mafuta kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu.

Mheshimiwa mwenyekiti, swali la pili kwamba ni lini Shirika litagawanywa? Mantiki kubwa ya Shirika hili ni kulionyesha kwamba linafanya kazi kwa manufaa. Suala la kuligawa ni suala ambalo ni endelevu, ni suala ambalo tunatakiwa kulitafakari kwa kina sana kwa sababu kufanya hivyo ni lazima pia tuangalie madhara yake. Mantiki kubwa vile vile ni kwamba lazima Shirika lijiendeshe kifaida na liweze kumudu majukumu yake na kazi hizo zinaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mtasubiri wakati wa Bajeti ya Wizara hiyo. Tunaendelea. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Nishati.

Na. 120

**Fidia kwa Wananchi wa Jimbo la Kibaha Waliopisha Mradi wa Umeme**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Mradi wa umeme wa 400KV kutoka Kinyerezi hadi Arusha umepita maeneo mengi ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na Jimbo la Kibaha Mjini, uthamini wa mali za waathirika ulishafanyika toka mwaka 2015.

Je, Serikali itawalipa lini wananchi hawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshiiwa Mwenyekityi, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 400 kutoka Kinyerezi hadi Arusha. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolti 400 yenye urefu wa kilometa 664 pamoja na kilometa 40 kutoka Kibaha hadi Zinga na kilometa 60 kutoka Segera hadi Kange - Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze, Segera, Kange, Tanga na Zinga Bagamoyo. Mradi huu utejengwa ka mkopo kutoka Benki ya *Exim* ya China

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 kazi ya uthamini wa mali za wananchi kutoka Kibaha hadi Chalinze ilifanyika ili waweze kulipwa fidia na kupisha ujenzi wa mradi. Kazi inayofanyika kwa sasa ni kukamilisha taratibu za maandalizi ya malipo kwa wananchi waliohakikiwa kwa ajili ya malipo ya fidia. Zaidi ya shilingi bilioni 21.56 zimetengwa na Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wanaopitiwa na mradi katika maeneo ya Kisarawe, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wataanza kulipwa fidia baada ya uhakiki wa madai ya fidia hiyo kukamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa miradi mikubwa ya maendeleo inayoendelea ikiwa ni pamoja na hii ya umeme, pia Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi kubwa wanayofanya kufuatilia miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kulipa fidia ni kuwawezesha wananchi wanaoathirika na miradi hii mikubwa ya maendeleo ili waweze kupata fedha za kuweza kufanya shughuli nyingine mbadala za kiuchumi wanapopisha maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia zimekuwa zikichelewa sana, wakati mwingine takribani mpaka miaka mitano huku wananchi hawa wakitaabika bila kuweza kufanya shughuli mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mawili ya nyongeza. nafahamu uhakiki wa tathmini na hususan katika maeneo ya Kibaha Mjini, Vijijini na mpaka Chalinze ulikwishakamilika toka 2017.

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Je, ni lini sasa kwa uhakika wananchi hawa watalipwa fedha zao?

Swali la pili, Serikali sasa haioni kwamba kuna haja ya kufanya maandalizi ya malipo haya mapema ili tathmini ikishafanyika wananchi waweze kupata malipo yao mapema bila kupata usumbufu na malalamiko makubwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, Koka. Kwanza napenda kumshukuru sana na kumpongeza kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia miradi yetu kwenye sekta ya nishati na hususan katika suala hili la fidia kwa mradi huu wa Kinyerezi hadi Arusha, pia tumepokea pongezi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo swali letu la msingi limesema kwamba fidia hii ya shilingi bilioni 21.56 zimetengwa kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018. Ni matarajio yetu kwa kuwa uhakiki wa fidia hii umekamilika na matarajio yetu kwamba mwisho wa mwaka huu wa fedha, pesa hizi zitalipwa na naomba niendelee kuwashukuru wananchi wa maeneo ya Kisarawe, Kinyerezi yenyewe, Kibaha, Chalinze kwa uvumilivu wao. Napenda niwathibitishie Serikali italipa fidia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili; tunapokea huo ushauri na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kweli nia ni hiyo ya kuona kwamba maeneo wanayochukua kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa, wananchi wanawezeshwa. Ndiyo maana wakati wa bajeti tutaomba atuunge mkono. Tumetenga kabisa kiwango kikubwa tu cha fidia kwa miradi mikubwa ambayo inatarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha huo 2018/2019 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige na Mheshimiwa Zuberi, basi.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa umeme wa 400KV ni mkubwa sana na unahitaji transfoma zenye ubora wa hali ya juu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutumia transfoma zetu za kiwanda cha *TANELEC* cha Arusha ambazo zina ubora wa hali ya juu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na ninamshukuru sana Mheshimiwa Catherine na ninampongeza pia kwa kufuatilia masuala ya nishati akiwa pia ni Mjumbe wetu wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba umeme unaosafirishwa kwa njia hii ya msongo wa 400KV ni mkubwa na kwa kuwa ni mkubwa, Wizara yetu ya Nishati ilishatoa maelekezo kwamba kuanzia sasa vifaa vyote vinavyotumika kwenye miradi ya umeme vinatakiwa kutoka kwenye viwanda vyetu vya ndani na kimojawapo ni Kiwanda na *TANALEC*-Arusha. Mara kadhaa takribani kama zaidi ya mara mbili Mheshimiwa Waziri amefanya ziara katika kiwanda kile. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha transfoma kama 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niendelee kutoa wito kwa Wakandarasi wote wanaotekeleza miradi ya umeme nchini pamoja na Shirika la umeme, *TANESCO* kwamba bado agizo letu liko pale pale, vifaa vyote vitoke ndani ya nchi na viwanda vyetu vina uwezo na mara kadhaa tumekutana navyo na vimetuthibitishia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; wakati wa upanuzi wa Kiwanda cha Umeme cha Liwale wakati wanapanua ile *plant* yao, walichukua mashamba ya wananchi ambapo mpaka leo hii zaidi ya miaka mitano wananchi wale hawajui hatima ya malipo yao. Nini kauli ya Serikali namna ya kuwalipa wale wananchi mashamba yao?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Kuchauka kwa swali la nyongeza na ninampongeza pia kwa kazi zake, lakini nataka niseme kwamba suala la fidia kwa mashamba ambayo yamechukuliwa kwa upanuzi wa kituo cha kuzalisha umeme Liwale, naomba kwa kuwa kwa takwimu kwa sasa hivi sina, naomba nilichukue.

Naomba tu nimpe Mheshimiwa Mbunge taarifa ya nyongeza kwamba kwa sasa kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa laini ya msongo wa Kv 132 inayotoka Kituo cha Kuzalisha Umeme *Mozambique,* nataka nimthibitishie na jitihada ambazo zinaendelea za Wizara kuhakikisha Mikoa ya Kusini, Lindi na Mtwara inapata umeme kutoka Gridi ya Taifa kwamba kwa hivi karibuni Wilaya ya Liwale itapata umeme kupitia kituo hicho na kwamba hata yale matumizi ya mafuta ya kuzalishia umeme Wilaya ya Liwale yatapungua na umeme utapatikana kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la fidia nitalichukua, baada ya Bunge hili tutalifanyia mchakato wa kupata taarifa ya uhakika. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Chritstine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, nalielekeza kwa Mheshimwia Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Na. 121

**Hitaji la Utafiti wa Dawa za Kisukari**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Mpaka sasa inadaiwa kuwa hakuna dawa sahihi za kutibu ugonjwa wa kisukari.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti kuhusu dawa za kisukari?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa kisukari ni moja kati ya magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza. Ugonjwa huu husababishwa na ukosefu wa kichochezi kiitwacho *insulin.* Aidha, kwa kushindwa kutengenezwa kabisa na kongosho au kwa jina kitaalam unaitwa *pancreas* au kwa kufanya kazi chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina tatu za kisukari. Kisukari ambacho kinategemea *insulin* ambayo tunaita *type one* ambacho huanza utotoni; kisukari kinachotegemea *insulin* ama *type two* ambacho huwapata watu kuanzia miaka 35 na kuendelea ingawa watoto na vijana wameanza kupata aina hii kutokana na kutaozingatia misingi ya lishe; na kisukari cha mimba hii ni aina ya tatu ambayo inatokea wakati wa ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo yanachangia mtu kuugua kisukari ni pamoja na kuwepo historia ya kisukari ndani ya familia, magonjwa ya kongosho kama saratani na maambukizi, uzito unaozidi na unene uliokithiri, shinikizo la damu, mtindo wa maisha usiofaa hususani kutofanya mazoezi, ulaji usiofaa , uvutaji wa bidhaa za tumbaku na masuala mengine kulingana na aina ya kisukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mpaka sasa duniani kote haijagundulika dawa ya kutibu ugonjwa wa kisukari na kupona kabisa. Matibabu yote yanayotolewa mpaka sasa ni yale yanayompatia mgonjwa kiwango bora cha kuishi ikiwemo kuhakikisha kwamba kiwango chake cha sukari mwilini kinakuwa ndani ya kiwango cha kawaida kila siku ili kuvilinda viungo vingine vya mwili visidhurike na hivyo

kumpunguzia mgonjwa magonjwa ya mara kwa mara, kulazwa wodini mara kwa mara na kupunguza uwezekano wa kifo. Dawa hizi ni pamoja na sindano ya aina ya *insulin* ambazo mgonjwa hulazimika kuchoma kila siku kwa maisha yake yote na vidonge ambavyo kila mgonjwa humeza kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tafiti nyingi ambazo zinaendelea duniani kote kutafuta dawa itakayoweza kutibu kabisa ugonjwa huu, lakini tafiti hizi bado hazijazaa matunda. Tafiti hizi ni pamoja na zile za kujaribu kutengeneza *cell* za kongosho na kuzipandikiza kwa maana ya *Pancreas Stem Cell Transplantation* ili kuweza kuweka *cell* mpya za kongosho na kuipa kongosho uwezo wa kutengeneza *insulin* kwa wingi zaidi. Njia hii pekee ndiyo itakuwa ufunguzi wa kudumu wa tiba dhidi ya ugonjwa huu. Mara tu tafiti hizi zitakapokamilika na kuonesha mafanikio, Serikali ya Tanzania itakuwa mstari wa mbele kuhakikisha huduma hii inapatikana hapa nchini.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Licha ya majibu mazuri, nina maswali mawili mafupi ya kumuuliza.

Kwa kuwa mpaka sasa hivi tafiti zinaendelea hapa duniani kuhusu ugonjwa wa kisukari, lakini mpaka sasa hivi azijazaa matunda, napenda kujua; je, tafiti hizi zimehusishaje tiba mbadala au tiba asilia kuhusu kutibu ugonjwa huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa ugonwja huu umeenea sana na unaleta vifo na inaonekana kuwa inawashambulia pia watoto wadogo na wajawazito na njia mojawapo inahusisha mambo ya lishe; je, kuna mkakati gani wa kutoa elimu kwa watu wote na hasa tukianza na Waheshimiwa Wabunge humu ndani kuhusu ugonjwa huu wa kisukari na hasa na mambo ya lishe? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sisi kama Serikali, tunatambua kwamba sasa hivi hatuna tiba dhidi ya ugonjwa wa kisukari, lakini Serikali vilevile inatambua umuhimu wa tiba asili na tiba mbadala, ndiyo maana ndani ya Wizara ya Afya tuna Kitengo Maalum ambacho kinasimamia tiba asili na tiba mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia taasisi zetu za Utafiti za Magonjwa ya Binadamu *(National Institute of Medical Research)* na Taasisi ya Tiba Asili ambayo iko Muhimbili, tumekuwa tunaendelea kufanya utafiti wa tiba mbalimbali ambazo zinapunguza kiwango cha sukari mwilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hatujapata tiba mbadala, lakini mtu yeyote ambaye amekuja na dawa ambayo anadhani inaweza kusaidia kupunguza makali ya ugonjwa wa kisukari, tumekuwa tunazifanyia utafiti na kuziangalia ili ziweze kutumika kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ameuliza kuhusiana na masuala ya lishe. Serikali mwezi Julai, 2017 imezindua mkakati wa Kitaifa wa masuala ya lishe na uzinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na lengo ni kuhakikisha sasa tunaongeza nguvu na kuongeza juhudi kuhusiana na magonjwa ya kuambukiza. Magonjwa ya kuambukiza yanazidi kuongezeka. Tunakadiria kwamba wastani wa asilimia 13 za Watanzania wana ugonjwa wa kisukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasi tunaendelea kuhamasisha wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea hapa Bungeni, wenzetu wa Bima ya Afya tumeleta Madaktari Bingwa wa magonjwa yote pamoja na kisukari na mimi nitoe

rai kwa Waheshimiwa Wabunge, twende pale kliniki tupime afya zetu; siyo suala tu la Kisukari lakini magonwja yote pamoja na Saratani huduma hizi zinapatikana Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishie kwa kutoa rai kwa wananchi wa Tanzania, magonjwa yasiyoambukizwa ikiwa ni pamoja na kisukari na shinikizo la damu, yanatokana kwa kutozingatia masuala ya lishe, kutofanya mazoezi na matumizi yaliyopindukia ya vilevi na sigara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwasisitiza Watanzania kuzingatia msingi ya afya bora. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Rukia.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kama alivyokiri Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mgonjwa wa kisukari ili aweze kuishi ni lazima apate dawa za kisukari kila siku. Sasa kule Jimboni Bagamoyo kwenye Hospitali ya Wilaya kuna tatizo kubwa sana la upatikanaji wa dawa hizi kwa wagonjwa wa kisukari. Pia hata vipimia vya kiwango cha sukari navyo havipatikani hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba dawa hizi na vipimo vinapatikana kwa urahisi ili wananchi wetu wa Tanzania waweze kuendelea kuishi?

**MWENYEKITI**: Ahsante. Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi na vilevile majibu ya nyongeza ni kwamba tunatambua sasa hivi ongezeko kubwa

sana la wagonwja wa kisukari, na sisi kama Serikali tumeelekeza nguvu zetu katika bajeti ambayo tumeitenga ya fedha kwa ajili ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi, bajeti ya ugonjwa wa kisukari nayo imo ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuongeza wigo wa utoaji wa huduma hii kwa kushirikiana na wadau, kusambaza vifaa vya upimaji, vilevile kusambaza dawa za *insulin* pamoja na vidonge vyake na katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya kununua matumizi ya *insulin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba hili suala la Bagamoyo tutajaribu kulifuatilia kuhakikisha kwamba sasa huduma hizo za dawa pamoja na vipimo vinapatikana.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la maradhi ya kisukari mpaka kuna baadhi ya watoto wachanga wanazaliwa wakiwa na maradhi haya; je, Serikali inaweza kutuambia nini chanzo kinachosababisha watoto wadogo kuzaliwa wakiwa na kisukari?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi nilisema kuna aina tatu za kisukari. Aina ya kwanza ni kisukari ambacho kinawapata watu katika umri mdogo na changamoto ya aina hii ni kwamba mtoto anazaliwa zile *cell* zake za kongosho ambazo kwa lugha ya kitaalam tunaita *pancreas* mwili wake wenyewe

unaanza kuishambulia ikiona kwamba kile ni kitu ambacho ni kigeni ndani ya mwili. Kwa hiyo, hiyo ni aina moja ya kisukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya pili ya ni kisukari ambacho kinawapata watu katika umri mkubwa; na hiyo ndiyo hali ambayo ilikuwepo kutokana na jinsi tunavyokula, masuala ya uzito, matumizi ya vilevi na kutofanya mazoezi. Sasa hivi hali imeendelea kubadilika, hata watoto wadogo kwa sababu ya lishe. Mara nyingi ukiona mtoto anakuwa na uzito mkubwa na sisi kama wazazi tunaona kwamba ni faraja. Uzito uliopitiliza wa aina yoyote hauna tija na ni moja ya kitu ambacho kinapelekea sasa hivi watoto wetu kuanza kupata kisukari wakiwa na umri mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya tatu ni kisukari ambacho kinatokana na ujauzito. Mama anapokuwa mjamzito kuna baadhi wanapata kisukari na mara nyingi kinaisha baada ya yule mtoto kuzaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu na kwa kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim, ni kwamba ni lazima sisi kama wazazi tuzingatie misingi ya lishe kwa watoto wetu, tusiwalishe chakula kilichopitiliza na watoto wetu wakawa wazito na uzito mkubwa kwa sababu nayo ina mchango mkubwa sana katika kupata kisukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kikundi kidogo ambacho miili yao tangu wamezaliwa zile *cells* zao za kongosho sinashindwa kufanya vizuri, hazizalishi *insulin* ama kwa kuwa na *deformity* ama kwa kuwa haikuumbwa vizuri zaidi au zikawa zimeshambuliwa; hawa wako wachache na wao watakuwa wanahitaji *insulin* tangu wakiwa na umri mdogo. Kubwa la msingi ni kuzingatia suala la lishe hususan kwa watoto hawa wasiwe na uzito mkubwa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Na. 122

**Kuongezeka kwa Maambukizi ya Ugonjwa wa TB**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Imebainika kuwa ugonjwa wa Kifua Kikuu *(TB)* umeendelea kuathiri jamii ya Watanzania.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa *TB*?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TB* au Kifua Kikuu ni ugonjwa wa kuambukizwa na huambukizwa kwa njia ya hewa. Ugonjwa wa *TB* hushambulia mapafu na viungo vingine ikiwa ni pamoja na mifupa, uti wa mgongo, ubongo, moyo, ngozi na sehemu nyingine za mwili. Kwa ujumla *TB* inaweza kushambulia kila kiungo katika mwili. Ugonjwa huu husababishwa na vimelea aina ya *bacteria* na mgonjwa akitibiwa kwa dawa tulizonazo anaweza kupona kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote anaweza kuambukizwa au kuugua *TB* lakini makundi yafuatayo yako katika hatari kubwa zaidi kuugua ugonjwa huu ni pamoja na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, watoto wadogo chini ya miaka mitano, wazee, watu wanaougua magonjwa ya muda mrefu ikiwemo saratani, kisukari, wenye utapiamlo, wafungwa, wachimbaji wadogo wadogo migodini na wale wanaotumia madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumgundua mgonjwa wa *TB* mapema na kumweka katika matibabu ndiyo njia kuu ya kupambana na kushinda tatizo la kifua kikuu. Hivyo basi,

mikakati ya Serikali imejikita katika afua za kuongeza uwezo wetu wa kuwafikia watu wote wanaohitaji huduma za *TB* ili kuwagundua wagonjwa hawa mapema na kuwatibu kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati na hatua zinazochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya upimaji wa *TB* kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI;

(ii) Kuingiza teknolojia mpya nchini ya upimaji na ugunduzi wa uhakika na uharaka wa vimelea vya *TB* kwa kutumia *Gene Xpert*. Hadi hivi sasa mashine 97 zimeshafungwa katika Hospitali za Mikoa na baadhi za Halmashauri na mashine nyingine 90 zimeshanunuliwa na zinatarajiwa kufungwa kwenye Hospitali za Wilaya zilizobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia hii inawezesha sasa hivi badala ya siku za nyuma ambapo mgonjwa alihitaji kupima makohozi mara tatu kwa siku tatu, sasa hivi ugunduzi unaweza ukanyika ndani ya masaa mawili badala ya siku tatu kama ilivyokuwa awali.

(iii) Tumewezesha maduka muhimu na Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala kufanya utambuzi wa dalili za *TB* na kutoa rufaa kwa wahisiwa wote kwenda katika mfumo wa tiba.

(iv) Kufanya uchunguzi kwa wafanyakazi wote migodini na kwenye mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena, Wizara yangu inatoa wito na kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge kushiriki kikamilifu katika mapambano ya kutokomeza *TB* na kuhakikisha kwamba *TB* inakuwa ni ajenda yao ya kudumu katika vikao vyote vinavyoendelea na wanavyovihutubia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza.

Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba wamekuwa na teknolojia mpya ya upimaji na ugunduzi wa vimelea vya *TB* kwamba sasa ndani ya masaa mawili badala ya siku tatu.

Napenda kujua nini hasa mkakati wa Serikali wenye kutoa kampeni maalum ya elimu ambayo itaweza kuenea kwa kasi zaidi katika maeneo ya migodi, viwanja vya michezo, mikusanyiko ya wavuvi pamoja na mikusanyiko ya wasafiri?

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, inaonekana kwamba mkakati wa kukabiliana na tatizo hili ni kwamba ndani ya taratibu hizi za kibajeti, fedha hizi wameachiwa wahisani ambao ni Wazungu. Matatizo ni ya Watanzania, ugonjwa ni wa Watanzania, lakini matibabu ni kwa wahisani wafadhili, Wazungu.

Napenda kujua, kwa nini Serikali imetenga shilingi bilioni 33.3 na ni fedha za nje, hakuna hata senti tano ambayo ni fedha za ndani ambapo fedha hizi za nje huwa hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazitolewi kabisa. Kwa nini Serikali isipange mkakati wake wa kuweka fedha za ndani badala ya kutegemea fedha za wahisani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Masoud kwa kuwa amekuwa ni mfuatiliaji mzuri sana wa masuala ya afya, *TB* pamoja na masuala ya UKIMWI. Nakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri ambayo umeendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijielekeza katika maswali yake ya msingi, ni kwamba sasa hivi Serikali baada ya kuona kwamba tumekuwa na changamoto kubwa sana katika utambuzi wa makundi maalum ambayo wengi wamekuwa wanaathirika kama nilivyoyataja katika majibu yangu ya msingi, tumeelekeza juhudi mahususi katika masuala ya makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka, mara nyingi ugonjwa huu wa UKIMWI umekuwa ni ugonjwa pacha vilevile wa ugonjwa wa UKIMWI. Sasa hivi mikakati ambayo tunayo, kwanza tumejielekeza kutoa elimu kwa njia mbalimbali kwa vyombo vya habari pamoja na mitandao ya jamii. Vilevile sasa hvi tuna mkakati mahususi wa kuwatafuta wagonjwa wa *TB* katika migodi. Sambasamba na hilo, katika mikakati yetu tumetengeneza mikakati jumuishi kati ya ugonjwa wa UKIMWI na ugonjwa wa *TB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeanza kijielekeza mahali pengi ambapo tunaweza tukapata wengi kwa pamoja na hususan wanaume. Tumeelekeza nguvu kwenye migodi, tumeelekeza nguvu kwenye kambi za uvuvi na sasa hivi tunataka twende mbali sana katika upande huu wa UKIMWI, hata kule ambapo wanaume wanakuwa katika *bar*, msishangae na sisi tukiwa tunapita kule tunawaomba kufanya upimaji wa masuala ya UKIMWI pamoja na masuala ya *TB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali lake la pili alilielekeza katika suala la fedha akihoji kwa nini Serikali na katika kitabu pale inaonesha kwamba kuna fedha za nje na kwa nini sisi kama Serikali hatujaweka fedha za ndani. Naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 kufikia shilingi bilioni 269 katika mwaka wa fedha 2017/2018 na katika bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetupitishia hapa juzi, bajeti ya dawa imeongezeka mpaka shilingi bilioni 270. Katika hiyo bajeti, ni kwa ajili ya dawa,

vitendanishi na vifaatiba na ndani ya hiyo tumetenga shilingi bilioni tano kwa ajili ya ugonjwa wa *TB*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, samahani kidogo. Kwenye *gallery* ya Spika kuna mgeni ambaye anahitajika mahali pengine muda siyo mrefu kuanzia sasa. Tunaye Spika ambaye ni Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Roger Nkodo Dang, *he is there standing.* Karibu sana. *It is pleasure to be with you here. Thank you. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, kwa niaba yake, Mheshimiwa Haule.

Na. 123

**Kuimarisha Ushiriki Katika Mashindano ya Kimataifa**

**MHE. JOSEPH L. HAULE (K.n.y. MHE. ZUBEDA H. SAKURU)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mrefu katika kuimarisha ushiriki wenye tija kwa Tanzania katika mashindano mbalimbali ya kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri kuipongeza timu yetu ya vijana ya *Serengeti Boys* kwa kuweza kufuzu kuingia mashindano ya nusu fainali katika mashindano ya *CECAFA* ambayo yanafanyika nchini Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na timu zetu za michezo kuonesha kuwa matokeo yasiyoridhisha katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa, dalili za Tanzania kurejesha sifa yake ya zamani ya umahiri katika michezo zimeanza kuonekana baada ya mwanariadha wetu nyota Alphonce Simbu kushika nafasi ya tano katika mashindano ya mbio ndefu za *Olympic Brazil* mwaka 2016. Simbu na wanariadha wengine wa Tanzania waliendeleza rekodi hiyo ya ushindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Januari 2017, Simbu alinyakua medali ya dhahabu kwenye mashindano ya Kimataifa ya mbio ndefu ya Mumbai – India; Aprili 2017 Cecilia Ginou Kapanga aliipatia Tanzania medali ya dhahabu kwenye mashindano ya *Beijing International Marathon* nchini China; lakini vilevile tarehe 23 Aprili, 2017 Magdalena Chrispin Shauri alishika nafasi ya tano kati ya wanariadha 25,000 kwenye mashindano ya *Hamburg Marathon* nchini Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili, 2017 Emmanuel Ginouka Gisamoda alikuwa mshindi wa kwanza na kuipatia Tanzania medali ya dhahabu kwenye mashindano ya Shanghai *International Half Marathon*. Lakini vilevile mwezi Aprili, 2017 Simbu alishika nafasi ya tatu kwenye mashindano makubwa ya *London Marathon.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeona mafanikio yaliyojitokeza kwenye mchezo wa mpira wa miguu ambapo timu ya Taifa vijana Serengeti *Boys* ilifuzu kucheza fainali za michuano ya kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON)* kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17 nchini Gabon na kufuta historia hasi tuliyokuwa nayo ya timu zetu kushindwa kufika ngazi hiyo kwa miaka yote 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, somo kubwa tunalojifunza ni umuhimu wa mazoezi toka umri mdogo hivyo mkakati wa Serikali wa muda mrefu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuimarisha michezo shuleni ili kuibua na kulea vipaji vinavyojitokeza. Hivyo basi, shule 56 za sekondari zilizoteuliwa mwaka 2013 na mwaka 2014 na Serikali kila mkoa kuwa shule za michezo hazina budi kuimarishwa kwa vifaa, ufundishaji na miundombinu ili ziweze kutekeleza wajibu wake.

(ii) Katika kuimarisha uongozi katika vyama vya mashirikisho ya michezo mbalimbali nchini kwa kuvisimamia kwa karibu ili vizingatie katiba na sheria za michezo.

(iii) Kuimarisha mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA ambayo ndiyo kisima kikubwa cha kuwapata wanamichezo wa michezo yote nchini. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nitoe pole sana kwa familia za wasanii wenzangu, Jebby Mubarak na Agnes Gerald Masogange ambao wametangulia mbele za haki. Mungu awalaze mahali pema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba moja, pamoja na jitihada hizo tunazoziona za watu mmoja mmoja, wanariadha kuweza kufanya vizuri katika michezo mbalimbali, lakini imekuwa tabia ya Watanzania kupeleka timu mbaimbali kwenye mashindano mengine bila kuwaandaa.

Je, kwa nini sasa Serikali isiache kuwapeleka kwanza wanamichezo hao huko nje mpaka ihakikishe imewaandaa na kuweza kufanikiwa kuleta medali na kuitangaza vizuri Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili, changamoto kubwa ya wanamichezo wa Tanzania ni viwanja kukosa ubora na nadhani ile shilingi trilioni 1.5 ingeweza kupunguza kwa kiasi kikubwa sana changamoto hiyo. Mara baada ya mfumo wa chama kimoja kusitishwa mwaka 1992 Chama cha Mapinduzi kimeonekana kuhodhi

viwanja vikubwa karibu vyote vikubwa hapa nchini na kushindwa kuviendeleza...

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Je, hamuoni kwamba huu ni wakati muafaka sasa wa Chama cha Mapinduzi kurudisha viwanja vya michezo hivyo Serikalini ili viweze kutumika na Watanzania wote kwa ujumla? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa maswali mazuri ambayo yameulizwa na kaka yangu Profesa Jay. Nikianza na swali lake la kwanza ambapo ametoa ushauri kwamba kwa nini Serikali haipeleki wanamichezo nje kwa ajili ya kwenda kufanya maandalizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ushauri ambao ameutoa ni mzuri lakini nachukua pia nafasi hii kuweza kumtoa hofu kwamba katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 kwa sababu sisi kama nchi tunajua kabisa vijana wetu wa *Serengeti Boys* wanakabiliwa na mashindano makubwa na *AFCON* ambayo Tanzania itakuwa ni mwenyeji mwaka 2019. Kwa hiyo sisi kama Serikali kwa kushirikiana na *TFF* tuko kwenye mpango wa kuwachukua vijana wetu kuwapeleka Sweden kwa ajili ya kwenda kupata hayo mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili ambapo amedai kwamba viwanja vingi vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi, niseme kwamba imekuwa ni Sera ya Michezo ya mwaka 1995 kuhamasisha wadau wote kuwa vyama vyote na taasisi zote vina hali ya kuweza kumiliki viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, viwanja vyote ambavyo vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi

vinamilikiwa kwa halali na ni haki yao na hakuna hata kiwanja kimoja ambacho kimeporwa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuweza kuhamasisha Wabunge wote ambao mpo ndani ya Bunge hili, Halmashauri zote, wadau na taasisi zote kuhakikisha kwamba vinatenga maeneo kwa ajili ya michezo kwa sababu ni sera yetu ya mwaka 1995. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKIITI:** Ahsante. Tunaendelea. Swali letu la mwisho kwa leo linaulizwa na Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum. Linaulizwa kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Na. 124

**Malalamiko Juu ya Uvuvi Katika Ziwa Victoria**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto nyingi katika uvuvi wa Ziwa Victoria unaosababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa uvuvi.

Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inamaliza malalamiko hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uvuvi wa Ziwa Victoria umekuwa na changamoto nyingi zikiwemo shughuli za uvuvi haramu uliokithiri ambapo takribani asilimia 90 ya

wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi hufanya vitendo vya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo hivyo ni pamoja na kuvua kwa kutumia nyavu zilizounganishwa *(vertical integration),* kutumia nyavu za utali/timba *(monofilament nets),* kuvua kwa makokoro na nyavu zenye macho madogo chini ya kiwango kinachokubalika kisheria cha milimita nane na kadhalika. Aidha, uchakataji na biashara ya samaki wachanga na utoroshaji wa mazao ya uvuvi yakiwemo mabondo na kayobo kwenda nchi jirani bila kuzingatia sheria ni mojawapo ya vitendo vinavyoshawishi uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na vitendo hivyo, Serikali imedhamiria kulinda rasilimali za Taifa kwa kufanya Operesheni Sangara mwaka 2018 dhidi ya uvuvi haramu katika Ziwa Victoria. Operesheni hii ni kweli imeleta malalamiko kwa baadhi ya wadau wa uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia malalamiko hayo, Serikali inaendelea kuhamasisha wavuvi, wafanyabiashara, watendaji wa Serikali na wadau wengine wote kufuata sheria na kanuni za uvuvi na kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 ili kuendana na mabadiliko ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imetoa elimu na inaendelea kutoa elimu kwa wadau wote kuhusu uvuvi endelevu. Pamoja na kufanya tafiti mbalimbali zinazosaidia wadau katika kuendeleza Sekta ya Uvuvi nchini katika kuchangia ukuaji wa uchumi wetu na wananchi wetu kwa ujumla. Tafiti hizo zinalenga kufanyika katika samaki wa maji ya asili na ukuzaji viumbe katika maji *(aquaculture).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kufanya tafiti zitakazopendekeza zana na njia sahihi za uvuvi zisizo na ahari katika uvunaji wa rasilimali za uvuvi. Pia kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi na kuandaa mwongozo wa kuvifanya vikundi hivyo kufanya kazi zake kwa ufanisi ili kutokomeza uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatarajia kufanya semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania kwa lengo la kutoa uelewa mpana kuhusu uvuvi haramu na jitihada zinazofanywa na Wizara yetu kupambana na uvuvi haramu kupitia operesheni zinazofanyika zikiwemo Operesheni Sangara, Jodari na ile ya *MATT.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndilla Kangoye.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa naishukuru Wizara kwa lengo lake la kutoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge kwa uelewa wa masuala ya uvuvi, lakini kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mwanza ambao wananufaika na uvuvi wa Ziwa Victoria ambao wengi wao ni wanawake na vijana, napenda kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa changamoto nyingi za uvuvi zinatokana na sera na sheria zilizopitwa na wakati ikiwemo Sheria ya mwaka 1972 inayohusisha masuala ya nyavu; je, ni lini Serikali itakaa kuzipitia sheria hizi kwa lengo la kuzirekebisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; licha ya Ziwa Victoria kutumika na nchi tatu, yaani Tanzania, Kenya na Uganda, bado kila nchi imekuwa na sera zake juu ya uvuvi. Je, ni lini Serikali itaanzisha mchakato kuhakikisha kwamba kunakuwa na sera moja ya uvuvi katika Ziwa Victoria yaani *One Lake, One Policy? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Maria Kangoye kwa kuweza kusimamia vyema kabisa maslahi mapana ya wananchi waliomtuma wa Mkoa wa Mwanza wakiwemo vijana na akina mama. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameniuliza maswali mawili; la kwanza ni juu ya mapitio na maboresho ya Sheria ya Uvuvi. Naomba nimhakikishie kwamba sheria ile aliyoitaja ya mwaka 1970, Sheria Namba 6 ya Uvuvi tayari ilishaboreshwa, ndiyo maana tuna Sheria Namba 22 ya mwaka 2003 ambayo inakwenda na kanuni zake za mwaka 2009 ambayo na yenyewe sasa tuko katika hatua ya kuiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunavyozungumza, wataalam wetu katika ngazi ya Serikali, *IMTC* kwa maana Makatibu Wakuu wanaijadili na baadaye itaingia katika vikao vyetu vya Baraza la Mawaziri ili kuweza kuboreshwa zaidi na hatimaye kwa maslahi mapana ya sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Maria Kangoye kwamba Sheria yetu ya Uvuvi kabla ya mwaka huu wa 2018 haujakamilika, tutahakikisha kwamba inaingia humu Bungeni kwa ajili ya kuweza kupata baraka na kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni juu ya sera moja ya uvuvi, kwa maana ya kwamba Ziwa Victoria ni ziwa ambalo liko *shared* na nchi tatu, kwa maana ya Tanzania, Kenya na Uganda ambapo sisi kama Tanzania ndio tunaomiliki eneo kubwa la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli na nimwambie tu kwamba katika siku ya tarehe 2 Machi, 2018 Mawaziri wa nchi hizi tatu akiwepo Waziri wetu Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alishiriki katika kikao ambacho kilikwenda na maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maazimio makubwa kabisa ni kuhakikisha kwamba katika kila nchi, zile taasisi zetu za utafiti zinafanya utafiti na kuweza ku-*compromise* (kuweza kwenda kwa pamoja) juu ya sera zetu, sheria zetu ili zisiweze kugongana; ili wavuvi wote wanaoshiriki shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria wawe wanajua kwamba sheria hii hapa Tanzania, Kenya au Uganda ni sawasawa bila kuvunja sheria za nchi nyingine.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, najua eneo hili lina maneno mengi na ndiyo maana mnataka kuuliza maswali ya nyongeza, lakini muda wetu umekwisha na maswali ya leo yamekwisha.

Matangazo; wageni waliopo Bungeni, wageni waliopo Jukwaa la Spika; tuna wageni 180 wa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa (Mbunge) Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni *Engineer* Joseph Nyamhanga - Katibu Mkuu Ujenzi; Dkt. Leonard Chamuriho, Katibu Mkuu - Uchukuzi; Dkt. Mary Sasabo - Katibu Mkuu, Mawasiliano; Ndugu Angelina Madete - Naibu Katibu Mkuu Mawasiliano; Ndugu Fabio De Stefano - Mkuu wa Idara ya Miundombinu na Ushirikiano wa Kikanda wa Umoja wa Ulaya na Ndugu Ally Mwichande, Meneja Miradi ya Miundombinu wa Umoja wa Ulaya. *(Makofi)*

Sasa hawa sioni kama ni 180, lakini wameambatana na wageni wengine ambao ni Wenyeviti wa Bodi, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi na wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(National Institute of Transport).* Wako wapi? Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mbunge na Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ambao ni Madiwani kutoka Jimboni kwake Ushetu, Mkoani Shinyanga. Mko wapi Waheshimiwa? Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Pia kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mbunge na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni wapiga kura wake kutoka Pangani Mkoani Tanga. Pangani huko, karibuni sana. Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Alex Gashaza kutoka Ngara, Mkoani Kagera ambao ni Katibu wa CCM Kata ya Kirusha - Ndugu Zadock Kimonyo na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM - Ndugu Bahati Elikana. *(Makofi)*

Tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Ester Mahawe, Mbunge, ambao ni familia yake kutoka Mkoani Manyara, walioongozwa na mama yake mzazi, Ndugu Elizabeth Peter. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge ambaye ni rafiki yake kutoka Dar es Salaam Ndugu Abraham Ngoti. *(Makofi)*

Kuna *w*ageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge ambao ni watoto wake wakiongozwa na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kikulyungu, Mkoani Lindi, Ndugu Miraji Saidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kuwatangazia kwamba tutakaopata nafasi tunakaribishwa Wabunge kwenye uzinduzi wa Ofisi ya Makao Makuu, Ofisi ya Kanda ya Kati na Tawi jipya la NMB, tawi jipya la Kambarage leo. Uzinduzi huo utafanywa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia saa nane mchana katika Jengo la *PSPF,* barabara ya 18 ya Jakaya Kikwete. Wote mnakaribisha. *(Makofi)*

Hayo ndiyo matangazo tuliyonayo. Ahsanteni sana.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Ngoja tuchukue majina, Mheshimiwa Lubeleje umesimama kwa ajili ya Mwongozo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, Dkt. Raphael Chegeni, nahama huku nimemuacha mtu? Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Haule, Mheshimiwa Hawa, Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Gekul.

Waheshimiwa Wabunge, wale mnaorudiarudia

miongo zo nitakuwa nawaacha ninapokuwa hapa kwenye Kiti, haiwezekani kila siku tu ninyi mwongozo. Tunaanza na Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI akijibu swali namba 118 alitaja *TARURA*, nilitaka maelezo ya Serikali *TARURA* ni chombo ambacho kimeundwa hivi karibuni lakini nilitaka maelezo kwa Waziri hiki chombo kimetengewa fedha au fedha ya *TANROADS* ndiyo watagawana na *TARURA?* Kama watagawana na *TARURA* haitawezekana, kwa sababu fedha ya *TARURA* itakuwa ni kidogo sana na barabara za vijijini ni nyingi sana. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba maelezo kwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba mwongozo wako kwa kuhusiana na swali namba 124 ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi alikuwa anamjibu Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wote tunaheshimu sana misingi ya kuhifadhi rasilimali na hasa uvuvi wa samaki. Sheria zipo, sera zipo, miongozo ipo lakini kumejitokeza sana tatizo kubwa la wavuvi wengi kuonewa na kudhulumiwa mali yao, kibaya zaidi kuna wale akina mama ambao wanachuuza samaki, wanakaanga samaki wanakwenda kuuza kwenye magenge. Hawa samaki ndani ya Ziwa Victoria wako wa aina mbalimbali kuna Furu ambaye angekaa hata miaka mitano hadi 10 hakui, kuna Nembe hawakui, kuna samaki aina ya Gogogo hawakui wako vilevile, lakini lazima wavunwe waliwe na wananchi, hawa samaki wanapatikana kwenye mito hasa kipindi cha mvua sasa hivi samaki hawa ni wengi sana wanavuliwa kwa aina mbalimbali hata kwa kutumia nyavu au ndoano na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama

wanapokwenda kufanya biashara hii ya kuuza au kuchuuza samaki hawa wanakamatwa, wananyang'anywa samaki na wanafanyiwa vitendo vya ajabu ajabu. Kwa mfano wananchi wangu hasa akina mama wa Lamadi, unajua Lamadi kwenda Bariadi kule Jimboni kwako wanatumia sana samaki hawa Nembe, Furu, Gogogo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata mwongozo wako, ni lini Serikali sasa itaacha kuwaonea hawa akina mama na hasa wanaojitegemea kupata kipato hiki, ni kauli ipi ya Serikali ambayo pamoja na kurasimisha suala zima la ulindaji wa rasilimali hii, ni mkakati gani ambao hataendelea kuwaonea wanachi hawa ambao wanaonewa sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) juu ya swali la Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka ambalo limejibiwa asubuhi na Naibu Waziri wa Nishati kuhusu fidia ya umeme wa KV 400. Nilidhani tatizo hili ni la kwetu Manyara kwa sababu tuna umeme huu wa KV 400 kutoka Singida ni muda mrefu sana, nikimfuata Waziri au Naibu Waziri kueleza jinsi gani ambavyo wananchi wamechoka kusubiri fidia, lakini wameshahakikiwa zaidi ya mara tano, leo Waziri anajibu kwamba fidia inaendelea watalipwa fedha itakapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu hivi Wizara ya Nishati na Wizara ya Fedha ni mbingu na nchi kwamba hazikutani ndiyo maana hizi fedha hazitoki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, majuzi tulipitisha katika Bunge hili Sheria ya Fidia kwamba ikifika miezi sita kama watu hawafidiwi wananchi wanabaki na maeneo yao. Tunafahamu umuhimu wa umeme katika nchi hii na kuongeza hizo megawati. Naomba nifahamu kwa nini Serikali mnatudanganya kila siku wakati wananchi wetu wamechoka na nyumba zao zinadondoka na ninyi hamtaki kusema ni lini

mnalipa, huu udanganyifu mnaacha lini Serikali mtuambie mko humu ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Naomba Mwongozo wako na nimesimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati likijibiwa Swali Namba 123 lililoulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Zubeda Sakuru na Mheshimiwa Joseph Haule, Naibu Waziri wa Michezo nimemsikia akisema kwamba viwanja vyote vile vimemilikiwa kihalali, lakini kwa ufahamu wangu najua kuna viwanja ambavyo vilikuwa ni vya Halmashauri, vikachukuliwa vikaingizwa kwenye chama. Kwa mfano, Uwanja wa Mkwakwani Mjini Tanga, hatukatai kwamba CCM imevimiliki hivi viwanja lakini vingine vimewashinda, vingine vimekuwa viko chini ya kiwango. Sasa Upinzani hatutaki viwanja vile tupewe, lakini angalau virudishwe katika Halmashauri, fedha za viwanja hivyo ziingie katika Halmashauri zilete maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viwanja kama huo Uwanja wa Mkwakwani baba zetu walikatwa fedha wakati huo chama kikiwa ni kimoja, sasa hivi ni vyama vingi. Sasa viwanja tusipewe Wapinzani lakini virudi kwenye Halmashauri kwa sababu Halmashauri zimenyang'anywa *property tax,* Halmashauri zimenyang'anywa mabango ya biashara, angalau viwanja hivyo vikirudi vitaweza kukusanya mapato na kutoa huduma za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo ni lini sasa viwanja hivi vitarudishwa katika Halmashauri? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako katika swali namba 124. Kwa mujibu wa sheria, samaki aina ya Sato anayeruhusiwa kuvuliwa na kuliwa kwenye soko la Tanzania ana sentimita 25 na kwa mujibu wa sheria ileile Sangara ambaye anaruhusiwa kuvuliwa nadhani ni kwa ajili ya soko la nje anaanzia sentimita 50, lakini nyavu ambayo inaruhusiwa kuvuliwa wa sentimita 25 aina ya Sangara inategwa kwenye ziwa lilelile ambalo samaki aina ya Sangara wamo, nyavu hiyo ina uwezo wa kukamata samaki chini ya sentimita 50 ambazo ni za Sangara na zaidi ya sentimita 70 ambazo ni za Sato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa sababu katika Bunge hili Mheshimiwa Naibu Spika aliwahi kutoa Mwongozo kwamba wananchi wasiendelee kukamatwa kwa sababu, kwanza kuna hiyo *contradiction* ya zana za uvuvi kwamba nyavu tulizonazo za Sato ambazo ni chini ya sentimita sita ni inchi nne zinaweza kuvua Sangara ambaye ni chini ya sentimita 50; lakini watu wameendelea kukamatwa. Naomba Mwongozo wananchi ambao sasa wanachanganyikiwa watumie zana zipi ambazo zinaweza kuchagua samaki ndani ya ziwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema leo niliuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Tunza Malapo swali namba 117 ambalo majibu yake yamejibiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, TAMISEMI. Majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri yako hapa lakini wakati nikiuliza swali la nyongeza kutokana na majibu yake ya msingi, majibu aliyoyajibu alisema kwamba swali hilo lipelekwe kwenye swali la msingi. Sasa sikuona tofauti ya majibu aliyoyajibu kwenye swali la msingi na swali la nyongeza ambalo nililiuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa Naibu Waziri kutoa majibu sahihi kulingana na maswali ambayo tuliuliza. Je, swali hili ni sahihi kupelekwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ama lilitakiwa kupelekwa kwenye Wizara nyingine husika ambayo ilikuwa inatakiwa kujibu swali hili? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haule

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) ikiwa sambamba na Kanuni ya 46(1) ambayo inasema Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama ilivyoulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nauliza swali namba 123 kwa niaba ya Mheshimiwa Zubeda Sakuru, Waziri hakunijibu maswali yangu yote mawili ya nyongeza. Swali la kwanza nilimuuliza kwamba kwa nini Serikali isisitishe kuwapeleka wanamichezo nje ya nchi ambao wanakwenda kutumia gharama nyingi pia wamekuwa wakifanya vibaya na kuwa kama kichwa cha mwendawazimu, kwa nini isisitishe kuwapeleka, iwaandae kwanza hapa nchini waive ili wakienda kushiriki kwenye mashindano mbalimbali waweze kutuletea medali na sifa nchi yetu. Waziri yeye wakati ananijibu ameniambia kwamba mimi nimemshauri Serikali ipeleke wanamichezo nje na akasema wana mpango wa kupeleka *Serengeti Boys* Sweden mwakani kwa ajili ya *AFCON* na vitu kama hivyo, kwa hiyo swali la kwanza hakulijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili pia nilimuuliza kwamba moja ya changamoto kubwa ni viwanja na mwaka 1992 wakati tumetoka kwenye mfumo wa chama kimoja, Chama cha Mapinduzi kilihodhi viwanja vyote vya msingi, viwanja vikubwa hapa nchini na imeshindwa kuviendeleza. Sasa nikamuuliza kwa nini Chama cha Mapinduzi kisivirudishe vile viwanja Serikalini ili viweze kutumika na Watanzania wote. Yeye akanijibu kwamba kwa sera ya mwaka 1995 ndiyo imeweza kuwaweka CCM waweze kuhodhi viwanja hivyo na kuendelea kuvitumia na kwamba vyama vyote

vinaruhusiwa kuwa na viwanja na vitu kama hivyo. Mimi nilizungumzia mwaka 1992 ambapo viwanja vyote hivyo vilijengwa kwa kodi ya Watanzania pia ni vyote vinahusika na Watanzania lakini sasa hivi vimekuwa vikihodhiwa na Chama cha Mapinduzi ambapo ni kama imevipora. Kwa hiyo, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amepotosha Bunge amejibu ndivyo sivyo maswali yangu yamekwenda hivi yeye amekwenda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sitachoka kuwarudisha kwenye mstari, naona Kanuni hii ya 68(7) matumizi yake bado yanatupa shida; "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema siku hiyo ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge."

Waheshimiwa Wabunge, nikiwa na hiyo kama sheria inayoniongoza, Mheshimiwa George Lubeleje naanza kutoa Mwongozo wangu. Majibu ya Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ndiyo umeingilia hapo, fedha kama zimetengwa za kutosha kwa chombo hicho cha *TARURA*.

Nirudie msimamo ambao ndiyo mwongozo kama swali la msingi limeulizwa na majibu yametolewa na wewe unauliza swali la nyongeza au hukuuliza swali la nyongeza, huwezi ukaliombea Mwongozo, ndiyo Kanuni zetu hizi kama unataka uliza swali *specific,* kama *TARURA* imetengewa fedha za kutosha katika mwaka huu unaokuja wa fedha, lakini kwa vile Serikali wako hapa wayachukue tu, wayasikie na leo tunaanza Wizara ya Ujenzi zinashabihiana kwa sababu mgao ule wa asilimia 70 kwa 30 mmesema sana wakati wa TAMISEMI nadhani mtaendelea kusema; huo ndiyo Mwongozo wangu.

Mheshimiwa Chegeni naunganisha na Mheshimiwa Kanyasu swali namba 124 linalohusu uvuvi katika Ziwa

Victoria, ndiyo maana nilisema suala hili lina wasemaji wengi waliokuwa wanataka kuomba maswali ya nyongeza. Limejibiwa na Serikali kama wanavyoona wao, lakini yawezekana hatujaridhika katika jibu lao wanasema watawafanyia Wabunge wote semina ili tuweze kuelewa kwa pamoja suala hili.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu kwa suala hilo ni kwamba tusubiri hiyo semina ya Serikali na waifanye mapema iwezekanavyo kabla wao hawajawasilisha hotuba yao ya bajeti ili tuelewane vizuri kwa suala hili, kwa sababu hata mimi mwenyewe pamoja na kwamba nakalia Kiti hiki linanihusu, nina *personal interest*, tukae vizuri tusije tukaparurana bure, huo ndiyo Mwongozo wangu kwa Mheshimiwa Dkt. Chegeni na Mheshimiwa Kanyasu.

Mheshimiwa Mbarouk narudia hukuridhika tu na majibu ya Serikali haya ndiyo majibu. Mheshimiwa Joseph Haule kajibiwa inawezekana usijisikie vizuri na majibu hayo lakini hilo ndilo jibu. Sasa wewe kama una hoja yako, hukatazwi kujenga hoja kwa swali, uliza swali kama unataka viwanja hivyo utajibiwa vizuri tu, lakini mwongozo wangu kwa hilo narudia hivyo hivyo, tuendelee kuzingatia tu Kanuni tutazifahamu tu.

**MBUNGE FULANI:** Samaki umejibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu samaki nimejibu huo ndiyo mwongozo wangu, Mheshimiwa Mbarouk, uliza swali *specific* utajibiwa vizuri tu. Mheshimiwa Pauline Gekul, hayo hayo nitafanya nini Serikali imejibu. Naelewa wewe unataka wananchi wa Babati Mjini wakusikie, ni hiyo tu nadhani unachotaka, wamekusikia, lakini mimi kwa Mwongozo wangu ni kwamba hukuingia ndani, maana limejibiwa, sasa wewe kama unataka uulize tu *specific question* kuhusianna na fidia kwa wananchi wa Babati Mjini ambao wanadai fidia ambayo Serikali haijawalipa, lakini siyo suala ambalo linaruhusiwa au linakatazwa ili niweze kutoa majibu kwa mujibu wa Kanuni ya 68.

Mheshimiwa wa mwisho ni Mheshimiwa Joseph Haule naunganisha na Mwongozo wa Mheshimiwa Mbarouk na Mheshimiwa Haule. Hapana, Mheshimiwa Hawa bado, *I am sorry.* Mheshimiwa Joseph Haule na Mheshimiwa Mussa Mbarouk nadhani kama mnataka majibu sahihi mtapewa ulizeni maswali tu, lakini hayo ndiyo majibu ya Serikali mimi nasimamia Kanuni tu.

Waheshimiwa Wabunge, nitachukua la Mheshimiwa Hawa, *no, I think* nimtendee haki na Mheshimiwa Haule, ngoja tuyachukue majibu ya Serikali kwa swali namba 117 na majibu ya Serikali kwa swali namba 123, hebu tuone *Hansard* inasema nini halafu nitakuja kutoa Mwongozo wangu kwa hayo mawili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

**MWENYEKITI:** Mtoa Hoja, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Profesa Mbarawa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuweka mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuijalia nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kipekee nimpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri unaoonesha nia ya dhati ya kuipeleka nchi yetu kwenye hatua kubwa zaidi ya maendeleo. Uzalendo uliotukuka na uthabiti wake katika kulinda rasilimali za Taifa letu una manufaa makubwa kwa nchi yetu sasa na kwa vizazi vijavyo. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na kumpa nguvu na afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali hapa nchini na katika Bunge letu hili. Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Bunge letu tukufu, familia ya marehemu na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuondokewa na Mheshimiwa Leonidas T. Gama. Kifo cha Mbunge huyu kimeleta majonzi makubwa kwa familia, Bunge na Taifa kwa ujumla. Marehemu atakumbukwa kwa michango yake katika maendeleo ya nchi hii. Mungu amweke mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati natoa pongezi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hususan Mwenyekiti Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu, kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati hii. Aidha,

nawapongeza Wajumbe wapya walioteuliwa kujiunga na Kamati na Wajumbe wa zamani kwa kuchaguliwa kuendelea kuwepo kwenye Kamati hii. Wizara inathamini ushirikiano na ushauri wenu mnaotoa katika kuboresha utendaji ka wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hotuba yake iliyotoa Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mwelekeo wa Mpango wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kuwasilisha bajeti zao katika Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini; Mheshimiwa Justin Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini na Mheshimiwa Stephen Kiruswa Mamasita, Mbunge wa Jimbo la Longido kwa kuchaguliwa na wananchi. Ushindi walioupata unaonesha imani waliyonayo wananchi kwao na kwa Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim, Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mheshimiwa Zainab Amir, Mheshimiwa Sonia Magogo, Mheshimiwa Alfredina Kahigi na Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Sekta zilizo chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Sekta ya Ujenzi; Bajeti ya Matumizi ya Kawaida; kwa mwaka wa fedha 2017/2018, sekta ya ujenzi ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 36.032 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 39.977 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa sekta ya ujenzi na taasisi zake na shilingi bilioni 2.055 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

hadi Machi, 2018 sekta ya ujenzi ilikuwa imepokea kutoka Hazina kiasi cha shilingi bilioni 22.904.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti ya Maendeleo; kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sekta ya ujenzi ilitengewa shilingi trilioni 2.411 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa ni shilingi trilioni 1.865 na shilingi bilioni 545.582 zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha shilingi bilioni 642.284 za Mfuko wa Barabara. Hadi Machi mwaka huu, fedha zilizotolewa na Hazina ni shilingi trilioni 1.673; kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.435 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 237.882 ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 424.702 za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara na madaraja. Kwa ujumla kiasi kilichotolewa hadi Machi, 2018 ni sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo wa mwaka 2017/2018. Miradi ya barabara na madaraja:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza sera ya kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote pamoja na barabara za kuunganisha Tanzania na nchi za jirani kwa barabara za lami. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilipanga kutekeleza kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kuu na za Mikoa. Kwa upande wa barabara kuu, miradi ya barabara iliyokamilika hadi mwezi Machi mwaka huu ni pamoja na barabara ya Mayamaya – Mela – Bonga yenye urefu wa kilometa 188.15; Tabora – Puge – Nzega kilometa 113.9; Tabora – Nyahua kilometa 85 na Kaliua – Kazilambwa kilometa 58.9.

Miradi mingine iliyokamilika katika kipindi hiki ni barabara ya Sumbawanga – Kanazi kilometa 75; Kanazi – Kizi – Kibaoni kilometa 76.6; Kyaka – Bugene kilometa 59.1;

Magole – Turiani kilometa 45.2; Uyovu - Bwanga kilometa 45; *KIA* – Mererani kilometa 26; Usagara – Kisesa *(Mwanza bypass)* kilometa 11 na Mwigumbi – Maswa kilometa 50.3 pamoja na madaraja ya Kilombero Mkoani Morogoro na Kavuu huko Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara kuu iliyoendelea kutekelezwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami ni pamoja na barabara ya Sumbawanga – Matai – *Kasanga Port* kilometa 112; Kidahwe – Kasulu kilometa 63; Kakonko – Nyakanazi kilometa 50; Mafinga – Igawa kilometa 137.9; barabara ya Mchepuo Arusha kilometa 42.4; Makutano – Nata kilometa 50; Maswa – Bariadi kilometa 49.4; Bwanga – Biharamulo kilometa 67; Bulamba –Kisorya kilometa 50; Ushirombo – Lusahunga kilometa 110; Tabora – Koga – Mpanda kilometa 370; Nyahua – Chaya kilometa 85.4; Mbinga – *Mbamba Bay* kilometa 66; Itoni – Ludewa – Manda sehemu ya Lusitu – Mawengi kilometa 50; Mpemba – Isongole kilometa 50.3; Njombe – Ndulamo – Makete kilometa 109; Mtwara – Newala – Masasi (sehemu ya Mtwara – Mnivata – kilometa 50); Mto wa Mbu – Loliondo (Waso mpaka *Sale Junction* kilometa 49); Urambo – Kaliua kilometa 28; Mpanda – Vikonge kilometa 35; Sanya Juu – Elerai kilometa 32.2; Chunya – Makongolosi kilometa 43 na Kidatu Ifakara kilometa 67. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ujenzi wa madaraja ya Sibiti Mkoani Singida, Mto Mara Mkoani Mara, Lukuledi Mkoani Lindi; Ruhuhu, Momba, Mlalakuwa na Magara uliendelea kutekelezwa. Wizara pia iliendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili ya Tatu na ya Nne, Daraja jipya la Selander Dar es Salaam na Daraja jipya la Wami Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za Tanga – Pangani – Saadani – Bagamoyo, sehemu ya Tanga – Pangani kilometa 50; upanuzi wa barabara ya Kimara – Kiluvya kuwa njia sita sasa, barabara ya Kakonko (Kabingo) – Kibondo – Kasulu –

Manyovu Sehemu ya Nduta – Kibondo – Kabingo inayojumuisha barabara ya kupitia Kibondo Mjini kilometa 87.7 na barabara ya Uvinza – Malagarasi kilometa 51.1. Kwa ujumla utekelezaji wa miradi ya barabara hadi mwezi Machi mwaka huu, ulikuwa asilimia 72 ya malengo ya fedha kwa mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TANROADS* iliendelea kutekeleza mpango wa matengenezo katika barabara kuu na barabara za Mikoa. Hadi mwezi Machi mwaka huu, jumla ya kilometa 17,055 zilifanyiwa matengenezo katika barabara kuu na barabara za Mikoa. Aidha, jumla ya madaraja 996 ya barabara kuu na barabara za Mikoa yalifanyiwa matengenezo. Kwa ujumla, utekelezaji wa matengenezo ya barabara hadi Machi mwaka huu, ulifikia asilimia 67 ya malengo ya mwaka wa fedha 2017/2018. Maelezo zaidi kuhusu miradi hii yanapatikana kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa saba mpaka ukurasa wa 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya vivuko, nyumba na majengo ya Serikali; kazi zilizotekelezwa katika miradi ya vivuko hadi mwezi Machi mwaka huu, ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa kivuko kinachotoa huduma ya usafiri kati ya Magogoni na Kigamboni - MV Kazi. Aidha, ukarabati wa kivuko cha MV Pangani umekamilika ambapo ujenzi wa kivuko cha Kigongo – Busisi unatarajiwa kukamilika mwezi Machi mwaka huu. Hatua za utekelezaji kuhusu miradi hii zinapatikana kutoka ukurasa wa 37 mpaka 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uchukuzi; Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; kwa mwaka wa fedha 2017/2018, sekta ya uchukuzi iliidhinishiwa fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi trilioni 2.477 na shilingi bilioni 91.142 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi mwezi Machi mwaka huu, fedha za maendeleo shilingi trilioni 1.035 sawa na asilimia 41.7 ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa zimetolewa na fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 61.17 sawa na asilimia 67 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya muundo wa taasisi; katika mwaka 2017/2018 Wizara iliendelea kuzifanyia kazi ya marekebisho sheria za sekta ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa taasisi za umma. Sheria ya Shirika la Reli Namba 10 ya mwaka 2017 ilipitishwa kwa lengo la kuunganisha majukumu ya Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli *(RAHCO)* na Kampuni ya Reli *(TRL)* na kuunda Shirika jipya la Reli *(TRC)*. Shirika hili lilianzishwa rasmi tarehe 28 Februari mwaka huu. Aidha, ili kukabiliana na changamoto zilizoko katika usafiri wa majini ikiwa ni pamoja na kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, Sheria ya Wakala wa Meli Namba 14 ya mwaka 2017 ilipitishwa ili kuanzishwa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania *(TASAC)*. Shirika hili lilianzishwa rasmi tarehe 23 Februari, 2018. Mapendekezo ya kutunga sheria kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi kavu yapo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara; sekta binafsi imeendelea kuchangia sekta ya usafiri wa nchi kavu kwa njia ya barabara. Katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu, Wizara kupitia *SUMATRA* ilitoa leseni za usafirishaji 112,457 kwa magari ya abiria na mizigo ikilinganishwa na leseni 103,739 zilizotolewa kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Aidha, *SUMATRA* imekamilisha usimikaji wa mfumo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa mabasi ya masafa marefu mwezi Disemba mwaka jana. Mfumo huu wenye lengo la kuimarisha udhibiti wa mwendokasi wa mabasi ya abiria hadi sasa umeshafungwa katika mabasi 446. Taratibu za kupanua matumizi ya mfumo huu zinaendelea kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri na uchukuzi kwa njia ya reli; Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali kupitia *TRC* imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Reli ya kiwango cha *Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kuanzia na sehemu ya Dar es Salaam mpaka Morogoro kilometa 300 na Morogoro hadi Makutupora kilometa 422. Kwa sehemu ya Dar es Salaam – Morogoro, utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba mwakani.

Aidha, kwa sehemu ya Morogoro hadi Makutupora, mkataba wa ujenzi ulisainiwa mwezi Septemba mwaka jana na ujenzi ulizinduliwa tarehe 14 Machi mwaka huu, mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa reli kwa sehemu ya Makutupora – Tabora kilometa 295; Tabora – Isaka kilometa 133; Isaka – Mwanza kilometa 250; Tabora – Uvinza – Kigoma na Kaliua – Mpanda – Karema, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha. Aidha, zabuni kwa ajili ya kununua treni na mitambo itakayotumika kutoa huduma ya usafiri kwenye reli ya *Standard Gauge* ilifunguliwa mwezi Februari, 2018 na tathmini inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu jumla ya tani 276,769 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 217,331 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la asilimia 27. Aidha, katika kipindi hicho, kazi zilizotekelezwa ili kuboresha huduma ya reli ni pamoja na ukarabati wa mabehewa 107 ya mizigo na mabehewa 20 ya abiria. Ukarabati wa njia ya reli ya Korogwe – Mombo – Buiko kilometa 90 na kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kuelekea katika Bandari Kavu katika eneo la Kwala, Kibaha huko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia *(TAZARA);* katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali iliendelea kuboresha huduma za usafiri wa reli ya *TAZARA*. Hadi mwezi Machi mwaka huu zabuni kwa ajili ya ununuzi wa *Traction Motors* 42 pamoja na ukarabati wa mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo ilikuwa imetangazwa na mkandarasi kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAZARA* imeendelea kuboresha huduma zake ambapo muda wa kusafirisha mizigo kati ya Dar es Salaam na *New Kapiri Mposhi* huko Zambia umepungua kutoka wastani wa siku 8.5 kwa mwaka 2016/2017 mpaka wastani wa siku 6.5 kwa mwaka kufikia mwezi Machi mwaka huu. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi

Machi mwaka huu *TAZARA* ilisafirisha tani 173,000 za mizigo ikilinganishwa na tani 124,393 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la asilimia 28. Maelezo zaidi kuhusu *TAZARA* na *TRC* yanapatikana kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 62 mpaka 71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri na uchukuzi majini; huduma za uchukuzi katika maziwa; Kampuni ya Huduma za Meli imeendelea kutoa huduma za usafirishaji majini kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya ya Ziwa Tanganyika zimefunguliwa tarehe 18 Aprili, 2018 na kazi ya uchambuzi inaendelea. Kuhusu ujenzi wa meli mpya ya Ziwa Victoria, taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea. Mikataba ya ujenzi wa meli hizi itasainiwa hivi karibuni. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia ujenzi wa meli moja yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa. Meli hii inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za bandari; katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi mwaka huu, Mamlaka ya Bandari ilihudumia jumla ya tani milioni 9.822 za shehena za mizigo ikilinganishwa na tani milioni 8.572 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Utendaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia 14.6. Aidha, shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda na kutoka katika nchi jirani ilikuwa ni tani milioni 3.9 ikilinganishwa na tani milioni 3.1 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hili ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu na huduma za bandari ili kuimarisha utendaji wake. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ifuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa jengo la kuwaweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam, jengo hili limeanza kutumika Machi, 2018.

(ii) Ujenzi wa Gati la Bandari ya Mtwara umekamilika kwa asilimia 20.

(iii) Kukamilisha ujenzi wa Gati la Pangani ambao ulikamilika Septemba, mwaka jana.

(iv) Ukarabati wa gati la Lindi umekamilika kwa asilimia 60.

(v) Ujenzi wa gati la Ndumbi umekamilika kwa asilimia 30; na

(vi) Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati la Karema umekamilika mwezi Machi, mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Bandari ya Dar es Salaam wa kuboresha na kuongeza kina katika Gati Namba 1 mpaka Namba 7, kujenga gati jipya la kushushia magari eneo la Gerezani *Creek* na kupanua na kuongeza kina cha lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli, unaendelea vizuri. Kazi ya usanifu kwa gati la kutoa huduma meli za magari zimekamilika na ujenzi unaendelea. Pia usanifu wa Gati Namba 1 mpaka 3 unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa bandari ya Mbegani, Bagamoyo majadiliano kati ya Serikali na wawekezaji yapo katika hatua za mwisho na yanatarajiwa kukamilika na mkataba kusainiwa mwezi Juni, 2018. Maelezo zaidi kuhusu usafiri wa majini yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 72 hadi 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri na uchukuzi kwa njia ya anga; udhibiti wa usalama wa usafiri wa anga; katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga iliongezeka hadi kufikia abiria 4,950,994 kutoka abiria 4,725,094 waliotumia usafiri huu mwaka 2016/2017. Hili ni ngezeko ya asilimia 4.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea kuimarisha na kuboresha

huduma za usafiri wa anga. Katika mwaka 2017/2018 *TCAA* imesaini mkataba wa kununua na kusimika rada nne za kuongozea ndege za kiraia. Mkataba wa mradi huu wenye thamani ya shilingi bilioni 67.3 ulisainiwa mwezi Agosti, 2017 unaogharimiwa na Serikali kwa asilimia100. Rada hizi zitafungwa katika viwanja vya ndege vya *JNIA*, Mwanza, Kilimanjaro na Songwe. Mradi huu utakamilika mwezi Machi mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri wa anga. Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* pamoja na Kampuni za sekta binafsi zimeendelea kutoa huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 *ATCL* ilitoa huduma katika vituo vya Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Songea, Tabora, Zanzibar na Hahaya huko Comoro. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Kampuni ilisafirisha abiria 156,518 ikilinganishwa na abiria 107,207 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka fedha 2016/2017; hili ni ongezeko la asilimia 46. Ongezeko hili limeiwezesha *ATCL* kuongeza mapato ghafi kutoka shilingi bilioni 34.4 mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni 43.8 mwaka mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka fedha 2017/2018 Serikali ilipanga kupokea ndege nne, ndege moja aina ya *Bombardier* Q400 ilipokelewa nchini tarehe 2 Aprili, 2018. Aidha, ndege moja aina ya *Boeing* 787 *Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262 na ndege mbili aina ya *Bombardier* CS300 zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja zinatarajiwa kuwasili nchini mwaka huu. Maelezo zaidi kuhusu usafiri wa anga yanapatikana kwenye kitabu cha bajeti ukurasa 82 mpaka 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za hali ya hewa; katika mwaka fedha 2017/2018, Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* imeendelea kupata cheti cha ubora wa huduma za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga kwa

mujibu wa matakwa mapya ya Shirika la Viwango Duniani (ISO 9001:2015). Mafanikio hayo yameifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi tatu katika Afrika kutimiza makubaliano ya kimataifa kwa kutumia mfumo mpya wa ukaguzi wa viwango kabla ya mwezi Septemba, 2018. Aidha, Tanzania imekuwa ni nchi ya pekee katika Afrika iliyotumia wataalam wake wa ndani katika kufikia viwango hivyo na hatimaye kupata cheti cha ubora. Maelezo zaidi kuhusu *TMA* yameoneshwa kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 90 mpaka ukurasa 92. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za mafunzo; katika mwaka wa fedha 2017/2018 sekta ya uchukuzi iliendelea kusimamia Chuo cha Bahari - Dar es Slaam, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Usafiri wa Anga, Dar es Salaam na Chuo cha Hali ya Hewa huko Kigoma. Maelezo zaidi kuhusu utendaji wa taasisi za mafunzo yameoneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 108 hadi 114.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano; ukusanyaji wa mapato; katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2017 hadi Machi 2018, Wizara kupitia *TCRA* imekusanya jumla ya shilingi bilioni 20.011 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 11.296 zinatokana na asilimia 15 ya pato ghafi la mamlaka ambazo zimepelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi bilioni 8.716 ni kutokana na Mfuko wa *TTMS*. Kati ya fedha za *TTMS* kiasi cha shilingi bilioni 6.226 zilipelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha shilingi bilioni 2.489 zilielekezwa katika Mfuko wa Utafiti na Maendeleo uliopo *COSTECH*. Vilevile sekta kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imechangia kiasi cha shilingi bilioni moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, dola za Kimarekani 4,890,647 zilikusanywa kutokana na mauzo ya huduma za mkongo wa mawasiliano na kuhifadhiwa katika akaunti maalum ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Matumizi ya Kawaida; katika mwaka wa fedha 2017/2018 sekta ya mawasiliano ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 4.104 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni

2.267 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 1.837 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 shilingi bilioni 2.654 zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 14 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Sehemu ya fedha hizo inatarajiwa kutolewa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo; ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; sekta ya mawasiliano inasimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini, ambao kwa sasa upo katika Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne ya utekelezaji. Katika kipindi cha mwaka 2017/2018 sekta ya mawasiliano imeanza utekelezaji wa sehemu ya pili ya Awamu ya Tatu ya mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kutunza *Data;* Kituo cha Taifa cha Kutunza *Data* cha Dar es Salaam kimeendelea kutoa huduma bora kwa taasisi za Serikali na binafsi. Hadi kufikia mwezi Machi 2018 jumla ya wateja 52 wanatumia huduma hii. Kati ya wateja hao, 41 ni taasisi za Serikali na 11 ni kampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za Serikali kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini; sekta ya mawasiliano kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano katika mwaka wa fedha 2017/2018, imefikisha huduma ya mawasiliano vijijini katika kata 451 zenye vijiji 1,954 na wakazi 3,158,628. Aidha, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iliendelea na utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya TEHAMA kwa upande wa Zanzibar ambapo ujenzi wa vituo 10 umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya miundombinu ya TEHAMA ya Kikanda; sekta ya mawasiliano imetekeleza

Awamu Kwanza ya Programu ya Miundombinu ya Kikanda ambayo imekamilika mwezi Desemba, 2017. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na mradi wa shule mtandao katika shule za sekondari 80 na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu. Pia mradi umeweka usimikaji wa mitambo ya *video conference* katika Makao Makuu ya Mikoa ya Tanzania Bara na baadhi ya taasisi za Serikali. Kwa upande wa Zanzibar, ufungaji umefanyika katika Makao Makuu ya Mikoa Minne na Ofisi ya Rais – Ikulu. Pia programu imewezesha kujenga Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali katika taasisi 72 za Serikali na Halmashauri 77. Maelezo zaidi kuhusu taasisi zilizo chini ya sekta ya mawasiliano upo kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 103 hadi 108.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019; sekta ya ujenzi - Fungu 98; bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya sekta ya ujenzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni shilingi bilioni 42.898. Aidha, jumla ya shilingi trilioni 1.822 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.386 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 435.927 ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, shilingi bilioni 636.166 ni fedha za Mfuko wa Barabara. Mgawanyo wa fedha hizo umeoneshwa kwenye Kiambatisho namba1 katika kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Miradi ya Maendeleo; miradi ya vivuko, nyumba na majengo ya Serikali; katika mwaka wa fedha 2018/2019 miradi ya vivuko, nyumba na majengo ya Serikali imetengewa jumla ya shilingi bilioni 30.45. Wizara itaendelea na ununuzi wa vivuko vipya na ukarabati wa vivuko vilivyopo. Aidha, Wizara itaanza ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Nyamisati na Mafia Mkoani Pwani. Maelezo ya kina kuhusu miradi ya vivuko, nyumba na majengo ya Serikali yapo ukurasa wa 124 hadi 127 wa kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara na madaraja; katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi trilioni 1.573 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa

barabara, ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 636.166 ni bajeti ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara itaendelea kutekeleza kazi za ujenzi na ukarabati wa miradi mbalimbali ya barabara na madaraja ili kufikia maeneo mengi zaidi ya kiuchumi na kijamii. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa barabara kuelekea kwenye Mradi wa Kufua Umeme katika Maporomoko ya Mto Rufiji ambazo ni Ubena Zomozi - Ngerengere – Kisaki – Selous yenye urefu wa kilometa 166 na Kibiti – Mloka – Selous yenye urefu wa kilometa 201.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara, Bwanga – Biharamulo kilometa 67; Urambo – Kaliua kilometa 28; Sakina – Tengeru na mchepuo wa Arusha kilometa 56.5; upanuzi wa sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo utakaojumuisha upanuzi wa sehemu ya Tengeru – Usa River kilometa nane kuwa njia nne, ujenzi wa Daraja jipya la Kikavu na upanuzi wa sehemu ya barabara za Moshi Mjini kilometa nane kuwa njia nne.

Miradi mingine ni ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – *Kasanga Port* kilometa 112; Ushirombo – Lusahunga kilometa 110; Kidatu – Ifakara kilometa 67; Tabora – Sikonge sehemu ya Usesula kilometa 30; Usesula – Komanga kilometa 115.5; Komanga – Kasinde kilometa 112.8; Kasinde – Mpanda kilometa 111.7; Makutano – Sanzate kilometa 50, Waso – *Sale Junction* kilometa 50; Mpanda – Vikonge kilometa 35; Kisorya – Bunda kilometa 51; Maswa – Bariadi kilometa 49.7; Kidahwe – Kasulu kilometa 63; Nyakanazi – Kakonko kilometa 50; Nduta – Kibondo – Kabingo inayojumuisha barabara ya kupitia Kibondo Mjini kilometa 87.7 na barabara ya Uvinza – Malagarasi kilometa 51.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia itaanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara

za Tanga – Pangani kilometa 50; Geita – *Bulyanhulu Junction* kilometa 58.3 na *Bulyanhulu Junction* – Kahama kilometa 61; Kazilambwa - Chagu kilometa 42; Ludewa – Kilosa kilometa 24; Noranga – Itigi – Mkiwa kilometa 56.9; Lusahunga – Rusumo kilometa 91; Sanzate – Nata – Mugumu kilometa 85; Kibaoni – Sitalike kilometa 71; Vikonge – Magunga – Uvinza kilometa 109; upanuzi wa barabara ya kwenda kiwanja cha ndege cha Mwanza kilometa 12; Nyanguge – Simiyu/*Mara Border* kilometa 100.4; Turiani – Mziha – Handeni kilometa 104.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya madaraja makubwa itakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Magara huko Manyara, Sibiti - Singida, Ruhuhu - Ruvuma, Momba - Rukwa, Songwe, Mlalakuwa - Dar es Salaam, Lukuledi - Lindi, Mara - Mara; Mkenda - Ruvuma; kuanza ujenzi wa Daraja jipya la Wami huko Mkoani Pwani, Daraja jipya la Salender Mkoani Dar es Salaam, Msingi Mkonai Singida, Sukuma na Simiyu Mkoani Mwanza pamoja na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Kigongo – Busisi - Mwanza, Mtera hapa Dodoma na Malagarasi Chini huko Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea na jitihada za kupunguza msongamano barabarani katika jiji la Dar es Salaam kwa kuendelea na ujenzi wa barabara mbalimbali za Jiji. Jumla ya shilingi bilioni 20.15 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kimara – Kilungule – Majichumvi kilometa sita; Mbezi – Msigani kilometa Mbili; Mbezi Mwisho – Goba kilometa saba; Madale – Goba kilometa tano, Tangi Bovu – Goba kilometa tisa; Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni kilometa 2.6; Kibamba – Mloganzila kilometa nne na Goba - Makongo kilometa nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Mloganzila – *Mloganzila Citizen* kilometa nne; Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda kilometa 2.5 na Mjimwema – Kimbiji kilometa 27. Aidha, Wizara itakamilisha ujenzi wa barabara ya juu *(flyover)* katika makutano ya *TAZARA* na kuendelea na ujenzi wa *interchange* ya Ubungo pamoja na kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu

na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili itakayohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang'ombe kilometa 20.3. Awamu ya Tatu itakayohusisha barabara za Nyerere, Uhuru, Bibi Titi, Azikiwe na Lindi kilometa 23.6 na Awamu ya Nne itakayohusisha barabara za Sam Nujoma na Bagamoyo kilometa 25.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali itaendelea na maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje yaani *(outer ring road)* ya Mtumba – Veyula – Nala – Matumbulu - Mtumba yenye urefu wa kilometa 104 na barabara nyingine katika Mji wa Dodoma. Aidha, Wizara itaanza ukarabati wa barabara zinazotarajiwa kugharamiwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Developmemnt Corridors Transport Project* barabara hizo ni pamoja na Rusumo – Lusahunga kilometa 92; Mtwara – Mingoyo - Masasi kilometa 200; Makambako - Songea kilometa 295 na Iringa – Msembe *(Ruaha National Park -* kilometa 104*).* Maelezo ya kina kuhusu miradi ya barabara na madaraja yapo kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 128 hadi 149.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege; katika mwaka wa fedha 2018/2019 miradi ya viwanja vya ndege imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 215. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha *JNIA*, kuendelea na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu katika kiwanja cha ndege cha Mwanza, ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Geita. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Tabora, Kigoma, Sumbawanga, Shinyanga, Mtwara, Musoma, Songea na Songwe. Serikali pia itakamilisha mapitio ya

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuendelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Msalato. Aidha, Serikali itaanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya Iringa, *Lake Manyara,* Lindi, Simiyu na Tanga. Maelezo zaidi kuhusu miradi hii inapatikana kwenye ukurasa wa 150 mpaka 156 kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Barabara; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Barabara unatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 908 zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, sekta ya ujenzi na taasisi zake imetengewa shilingi bilioni 636.166 na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na taasisi zake imetengewa shilingi bilioni 272.642 kama inavyooneshwa katika ukurasa 156 hadi 157 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uchukuzi; bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; katika mwaka wa fedha 2018/2019 bajeti ya matumizi ya kawaida kwa sekta ya uchukuzi ni shilingi bilioni 86.292. Aidha, jumla ya shilingi trilioni 2.3 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo kwa miradi kwa sekta ya Uchukuzi ni kama inavyooneshwa katika Kiambatisho namba 6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imetenga shilingi bilioni 449.143 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ifuatayo:

(i) Kuendelea na kazi ya kuboresha Gati Namba 1 hadi 7 na ujenzi wa Gati la magari na miundombinu yake katika Bandari ya Dar es Salaam.

(ii) Kuendelea na ujenzi wa Gati Namba 3 pamoja miundombinu yake katika Bandari ya Mtwara, kukamilisha ujenzi wa Gati la Lindi.

(iii) Kukamilisha ukarabati Gati Namba 2 katika Bandari ya Tanga na kukamilisha mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ujenzi wa Bandari mpya ya Mwambani huko Tanga.

(iv) Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Mbegani huko Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma ya uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa meli moja mpya ya kubebea abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika, ujenzi wa meli moja mpya ya kubebea abiria na mizigo katika Ziwa Victoria na ukarabati wa meli za MV Victoria, MV Butiama, MV Liemba, MV Umoja na MV Serengeti. Maelezo zaidi kuhusu miradi ya *TPA* na *MSCL* yanapatikana katika kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 168 hadi 170.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Kampuni ya *ATCL* imetengewa shilingi bilioni 495.6 kwa ajili ya kununua ndege mbili; ndege moja aina ya *Bombardier Q400* na ndege kubwa moja aina ya *Boeing 787-8 (Dreamliner)*. Aidha, fedha hizo zitatumika pia kulipia bima, gharama za uendeshaji wa ndege, mafunzo ya marubani, Wahandisi na watoa huduma pamoja na ulipaji wa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha miundombinu na huduma za reli, *TRC* imetengewa shilingi trilioni 1.506 fedha za ndani kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro (kilometa 300) na Morogoro hadi Makutopora (kilometa 422) kwa kiwango cha *Standard Gauge* ambapo shilingi trilioni 1.4 zimetengwa na shilingi bilioni 106 kwa ajili ya miradi mingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha

2018/2019 Shirika la Wakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* litaendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kudhibiti usafirishaji wa nyara za Serikali, madini na makinikia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga *(TCAA)* itaendelea kudhibiti huduma za usafiri wa anga; katika mwaka wa fedha 2018/2019 *TCAA* imetenga katika bajeti yake shilingi bilioni 9.29 ili kutekeleza miradi ya kuimarisha usalama wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Wizara kupitia *TAA* imetenga shilingi bilioni sita kwa ajili ya ununuzi wa mitambo mbalimbali. Aidha, *KIA* itaendelea kukamilisha ukarabati wa jengo la abiria, uhakiki wa mipaka ya kiwanja na kufanya tathmini ya fidia kwa wananchi walioko katika eneo la kiwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* imetenga shilingi bilioni 20.5 kutokana na mapato yake ili kuendelea kuboresha huduma. Maelezo zaidi kuhusu miradi hii inapatikana kutoka ukurasa wa 176 hadi 177.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ubora wa huduma za sekta ya hali ya hewa, katika mwaka wa fedha 2018/2019 *TMA* imetengewa shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya hali ya hewa. Miradi hiyo ni pamoja na ununuzi wa rada tatu za hali ya hewa na kubadilisha vifaa vinavyotumia zebaki *(mercury)*. Maelezo zaidi kuhusu miradi ya *TMA* imeoneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 177 hadi 178.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano; jumla ya shilingi bilioni 18.856 za sekta ya mawasiliano, zikijumlisha shilingi bilioni 3.856 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 1.93 ni za mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 1.925 ni za matumizi mengineyo; shilingi bilioni 15 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano, imepanga kutekeleza Mpango wa muda wa kati na muda mrefu ambao utazingatia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sekta ya TEHAMA. Kusimamia utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ujenzi wa Kituo cha *Data* hapa Dodoma na Zanzibar pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ya Mitandao *Public Key Infrastructure - (PKI)* na kusimamia utekelezaji wa mradi wa Kikanda wa dijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano; kukamilisha uhuishaji wa Sera na Sheria ya Shirika la Posta Tanzania ili iendane na mabadiliko ya teknolojia, na mbili, kuendelea kuratibu utekelezaji wa mpango wa anwani za makazi na misimbo ya posta katika Miji yote Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani; kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Elias J. Kwandikwa, Naibu Waziri (Ujenzi); Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye, Naibu Waziri (Uchukuzi na Mawasiliano); Makatibu Wakuu Mhandisi Joseph Nyamhanga (Ujenzi); Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho (Uchukuzi); Mhandisi Dkt. Maria Sasabo - Sekta ya Mawasiliano na Mhandisi Angelina Madete, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano). Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Vitengo, Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara, viongozi wa taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu mkubwa kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwatambua na kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo ambao wamekuwa bega kwa bega na Wizara katika utekelezaji wa programu na mipango yetu ya Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Washirika hao wa maendeleo ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, Benki ya Dunia *(WB)*,

Japan *(JICA)*, Korea Kusini *(KOICA)*, *Abu Dhabi Fund*, Ujerumani *(KfW)*, Uingereza *(DFID)*, Uholanzi *(ORIO)*, Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)*, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB)*, Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID)*, Kuwait *(KFAED)*, Uturuki, *OPEC Fund*, *BADEA*, *HSBC, TMEA*, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za *SADC*, taasisi za fedha za *CRDB*, *NSSF* na *TIB*, Asasi zisizokuwa za Serikali pamoja na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika. Hotuba hii inapatikana katika tovuti za Sekta ya Ujenzi (www.mow.go.tz), Sekta ya Uchukuzi (www.uchukuzi.go.tz) na Sekta ya Mawasiliano (www.mst.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa maombi ya fedha ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 4,270,879,381,704. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,864,991,280,426 ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi. Shilingi 2,387,031,678,278 kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na shilingi 18,856,423,000 ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano.

Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo; Sekta ya Ujenzi Fungu 98 - jumla ya shilingi 1,864,991,280,426 za Fungu 98 - Ujenzi zinajumuisha shilingi 42,898,011,066 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo shilingi bilioni 31,075,545,000 ni za mishahara ya watumishi na shilingi 11,822,466,066 ni za matumizi mengineyo. Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 1,822,093,269,360 ambazo zinajumuisha shilingi 1,386,165,670 ambazo ni fedha za ndani na shilingi 435,927,599,360 fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha shilingi 336 166,000,000 kutoka Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi - Fungu 62 - imetengewa shilingi 2,387,031,678,278. Fedha hizi zinajumuisha shilingi 86,292,678, 278 kwa ajili ya Matumizi ya

Kawaida ambapo shilingi 57, 828,541,000 ni za Mishahara ya Watumishi na shilingi 28,446,137,278 ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa ni shilingi 2,300,739,000,000 ambazo ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano - Fungu 68; jumla ya shilingi 18,856,423,000 za Sekta ya Mawasiliano, zinazojumuisha shilingi 3, 856,423,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo shilingi 1,930, 485,000 ni za Mishahara ya Watumishi na shilingi 1,925,938,000 ni za Matumizi Mengineyo. Shilingi 15,000,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 (Kiambatisho Namba 1-7) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba viambatanisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika***, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuweka mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na

kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

***2. Mheshimiwa Spika*,** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuijalia nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa 11 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***3. Mheshimiwa Spika*,** kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri unaoonesha nia ya dhati ya kuipeleka nchi yetu kwenye hatua kubwa zaidi ya maendeleo. Uzalendo uliotukuka na uthabiti wake katika kulinda rasilimali za taifa letu una manufaa makubwa kwa nchi yetu sasa na kwa vizazi vijavyo. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na kumpa nguvu na afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano waTanzaniana Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa(Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vema nchi yetu kwa hekima na busara.

***4. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwako binafsi, Bunge lako tukufu, familia ya marehemu na wananchi wa Jimbo la Songea mjini kwa kuondokewa na Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama. Kifo cha Mbunge huyu kimeleta majonzi makubwa kwa Bunge na Taifa kwa ujumla. Marehemu atakumbukwa kwa michango yake katika maendeleo ya nchi hii. Mungu amweke mahali pema peponi, Amina.

***5. Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati natoa pongezi kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hususan Mwenyekiti Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso (Mb.) pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma (Mb.) kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati hii. Aidha, nawapongeza Wajumbe wapya waliojiunga na Kamati

hii na Wajumbe wa zamani kwa kuchaguliwa kuendelea kuwepo kwenye Kamati hii. Wizara inathamini ushirikiano na ushauri wenu mnaotoa katika kuboresha utendaji wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

***6.Mheshimiwa Spika,*** niwapongeze pia Waheshimiwa Wabungewalioaminiwa na kuchaguliwa na wananchi katika chaguzi ndogo zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2017/ 2018. Wabunge hao ni Mheshimiwa Maulid Abdallah Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni; Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Ole Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha; Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini; Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini na Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa Mamasita, Mbunge wa Jimbo la Longido. Ushindi walioupata unaonesha imani waliyonayo Wananchi kwao, kwa Serikali yao na Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim (Mb.); Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba (Mb.); Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye (Mb.); Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir (Mb.); Mheshimiwa Sonia Juma Magogo (Mb.); Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi (Mb.) na Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***7. Mheshimiwa Spika,*** mwisho napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb) kwa hotuba zao. Hotuba hizo zimefafanua vizuri utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali yenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii nchini.

## B. MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

***8. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na Sekta ya Mawasiliano.

***9. Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya msingi ya Sekta ya Ujenzi ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi (2003) pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009); ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege; ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme; usimamizi wa shughuli za ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi; usimamizi wa maabara na vifaa vya ujenzi; usimamizi wa masuala ya usalama na mazingira katika Sekta; uboreshaji utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Sekta na usimamizi wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Sekta.

***10. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya reli na bandari; usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga, reli na bandari; utoaji wa leseni za usafirishaji; usalama katika usafirishaji; usimamizi wa huduma za hali ya hewa; kuendeleza rasilimali watu na kusimamia Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

***11. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano, majukumu yake ni pamoja na kusimamia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003; na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2016 na utekelezaji wake. Aidha, Sekta ya Mawasiliano ina dhamana ya kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inachangia katika maendeleo ya nchi yetu, pamoja na usimamizi wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

***12. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Malengo Endelevu ya Maendeleo, Ahadi na Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Sera nyinginezo za Kisekta, Kitaifa na Kimataifa.

***13. Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Mpango na Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kila sekta.

## C.1 UTENDAJI WA SEKTA ZILIZO CHINI YA WIZARA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### C.1.1 SEKTA YA UJENZI

#### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

***14. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha **Shilingi 36,032,513,782.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 33,977,384,800.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake na **Shilingi 2,055,128,982.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi Machi, 2018 **Shilingi 22,904,459,689.20** zilikuwa zimetolewa na HAZINA. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 21,080,142,689.20** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 1,824,317,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

#### Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

***15. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 2,411,026,062,496.20** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 1,865,443,630,496.20** na **Shilingi 545,582,432,000.00** zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 642,284,000,000.00** za Mfuko wa Barabara. Hadi Machi, 2018 fedha zilizotolewa ni **Shilingi 1,673,417,096,716.54.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,435,534,514,202.54** ni fedha za ndani na **Shilingi 237,882,582,514.00** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizotolewa zinajumuisha **Shilingi 424,702,386,374.00** za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara na madaraja. Kwa ujumla, kiasi kilichotolewa hadi Machi, 2018 ni sawa na asilimia **69** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa

ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### Miradi ya Barabara na Madaraja

***16. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilipanga kutekeleza kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kuu na za mikoa. Kwa upande wa barabara kuu, miradi ya barabara iliyokamilika hadi Machi, 2018 ni pamoja na barabara ya Mayamaya Mela – Bonga (km 188.15), Tabora – Puge – Nzega (km 113.90), Tabora – Nyahua (km 85) na Kaliua – Kazilambwa (km 58.9). Miradi mingine iliyokamilika katika kipindi hiki ni barabara ya Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Kyaka – Bugene (km 59.1), Magole – Turiani (km 45.2), Uyovu - Bwanga (km 45), KIA – Mererani (km 26), Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass – km 17) na Mwigumbi – Maswa (km 50.30) pamoja na madaraja ya Kilombero na Kavuu. Aidha, Wizara ilikamilisha ukarabati wa jumla ya kilometa **77** za barabara kuu kwa kiwango cha lami.

***17. Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara kuu iliyoendelea kutekelezwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami ni pamoja na barabara za Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112), Kidahwe – Kasulu (km 63), Kakonko – Nyakanazi (km 50), Mafinga – Igawa (km 137.9), barabara ya mchepuo wa Arusha (km 42.4), Makutano – Natta (km 50), Maswa – Bariadi (km 49.7), Bwanga – Biharamulo (km 67), Bulamba – Kisorya (km 51), Ushirombo – Lusahunga (km 110), Tabora – Koga – Mpanda (km 370), Nyahua – Chaya (km 85.4), Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Itoni – Ludewa – Manda sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50), Mpemba – Isongole (km 50.3), Njombe – Ndulamo – Makete (km 109), Mtwara Newala – Masasi (Mtwara – Mnivata – km 50), Mto wa Mbu Loliondo (Waso) – Sale (km 49), Urambo – Kaliua (km 28), Mpanda – Vikonge (km 35), Sanya Juu – Elerai (km 32.2) na Chunya – Makongolosi (km 43). Aidha, ujenzi wa madaraja ya Sibiti, Mto

Mara, Lukuledi, Ruhuhu, Momba, Mlalakuwa na Magara uliendelea kutekelezwa. Kwa ujumla utekelezaji wa miradi ya maendeleo hadi Machi, 2018 ulikuwa umefikia **asilimia 72** ya malengo ya mwaka wa fedha 2017/2018.

***18. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia TANROADS iliendelea kutekeleza mpango wa matengenezo katika barabara kuu na barabara za mikoa. Hadi Machi, 2018, jumla ya kilometa **17,055** zilifanyiwa matengenezo katika barabara kuu na barabara za mikoa. Aidha, jumla ya madaraja **996** ya barabara kuu na barabara za mikoa yalifanyiwa matengenezo. Kwa ujumla, utekelezaji wa matengenezo ya barabara hadi Machi, 2018 ulikuwa umefikia **asilimia 67** ya malengo ya mwaka wa fedha 2017/ 2018.

***19. Mheshimiwa Spika,*** kazi ya kudhibiti uzito wa magari iliendelea katika mwaka 2017/2018 kwa kutumia mizani **46** ya kudumu na **22** inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi kufikia Machi, 2018, magari yapatayo **2,311,005** yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari **692,483** yalikuwa yamezidisha uzito ikiwa ni sawa na asilimia **30** ya magari yote yaliyopimwa. Jumla ya **Shilingi 3,114,040,000.00** zimekusanywa kutokana na tozo ya kuzidisha uzito wa magari. Aidha, Wizara imekusanya mapato yatokanayo na ada za vibali vya kusafirisha mizigo isiyo ya kawaida barabarani *(fees for abnormal load permits)* jumla ya **Shilingi 4,908,533,123.00** na kuziwasilisha Bodi ya Mfuko wa Barabara.

***20. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa kila mradi wa barabara hadi Machi, 2018 ni kama ifuatavyo:

***21. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200)** sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze(km144) unatekelezwa kwa kiwango cha "Expressway". Hadi Machi, 2018, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali pamoja na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zilikuwa zimekamilika. Taratibu za kumpata Mwekezaji (Concessionaire) kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa njia ya PPP zinaendelea. Mradi huu pia unahusisha ukarabati

(overlay) kwa kiwango cha lami sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44) ambapo hadi Machi, 2018 jumla ya kilomita 12 zilikuwa zimekamilika.

***22. Mheshimiwa Spika***, kazi ya ujenzi wa barabara **Bagamoyo – Msata (km 64)** pamoja na **Daraja la Ruvu Chini** ilikuwa imekamilika. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kuwapata makandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **TAMCO – Vikawe – Mapinga** (km 24) na **Kisarawe – Maneromango** (km 54) kwa awamu zinaendelea. Vilevile, majadiliano kati ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa barabara ya **Bagamoyo – Saadani – Tanga** yanaendelea. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Tegeta – Bagamoyo (km 46.9), Mbegani – Bagamoyo (km 7.2) na Makofia – Mlandizi (km 36.7) ambazo ni sehemu ya mradi huu umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami.

***23. Mheshimiwa Spika***, mradi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya **Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa** (km 422) umegawanywa katika awamu tatu na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

***i. Kyamyorwa – Buzirayombo (km 120)*** Mkandarasi amemaliza kazi ya marekebisho (marudio) ya sehemu zilizoharibika katika mradi huu na mradi umepokelewa na Wizara kupitia TANROADS.

***ii. Uyovu – Bwaga – Biharamulo (km 112) Lot 1 na Lot 2)***

Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zimekamilika kwa sehemu ya **Uyovu – Bwanga (km 43).** Mradi huu ulikabidhiwa kwa Serikali kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) tarehe 23 Oktoba, 2017 na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 10 Machi, 2018. Kwa sasa mradi upo chini ya uangalizi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, kwa sehemu ya **Bwanga**

**– Biharamulo (km 67)** maendeleo ya mradi kwa ujumla yalikuwa ni asilimia 75 ambapo kilometa 45 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

***iii. Geita – Bulyanhulu Jct*** - ***Kahama (Lot 1 and Lot 2)*** Usanifu wa kina wa sehemu ya **Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3) na Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7)** umekamilika na maandalizi ya ujenzi yanaendelea.

***24. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 353.7),** ujenzi wa sehemu ya ***Uvinza – Kidahwe (km 76.6), Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi na Barabara Unganishi (km 48), Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52) na Kaliua – Kazilambwa (km 56)*** umekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi hiyo.

Kuhusu sehemu ya ***Uvinza – Malagarasi (km 51.1),*** hadi Machi, 2018, Serikali imesaini makubaliano ya mikopo na Mfuko wa OPEC pamoja na Mfuko wa ABU-DHABI (ABU-DHABI Fund) kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii. Aidha, kwa sehemu ya **Urambo – Kaliua (km 28)** Mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

***25. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara ya **Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga na Bomang'ombe – Sanya Juu (km 173)**, ujenzi umekamilika katika sehemu za Tarakea Rongai – Kamwanga (km 32); Tarakea – Rombo Mkuu (km 32) na Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika (km 32). Aidha, kwa sehemu ya Bomang'ombe – Sanya Juu – Kamwanga (km 100), hadi Machi, 2018 ujenzi kwa sehemu ya Sanya Juu - Elerai (km 32.2) kwa kiwango cha lami ulikuwa umekamilika kwa asilimia 43.

***26. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Arusha - Moshi – Holili Pamoja na Mchepuo wa Arusha (Arusha Bypass) - km 140 na Mizani ya Himo:** Hadi Machi, 2018, kazi za ujenzi wa sehemu ya Arusha - Tengeru (km 14.1) na barabara ya ***KIA – Mererani (km 26)*** zimekamilika. Aidha, kazi za ujenzi wa barabara ya

Mchepuo wa Arusha (Arusha Bypass - km 42.4) zimefikia asilimia 69.18. Kazi ya usanifu wa kina wa barabara ya Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia imekamilika na taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea. Kuhusu barabara ya ***Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km16)*** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa kilometa 3.5 kwa sehemu ya Masama – Machame *Junction*.

***27. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Dodoma – Manyoni (km 127)** unahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini (km 4.8), ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Muhalala (Manyoni) – (One Stop Inspection Station - OSIS) pamoja na ujenzi wa mizani inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) eneo la Nala Mkoani Dodoma. Hadi Machi, 2018, kazi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo kuingia Manyoni mjini ilikuwa imekamilika. Aidha, kazi ya ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (OSIS) unaendelea. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ufungaji wa mizani inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) eneo la Nala Mkoani Dodoma.

***28. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nelson Mandela (km 15.6)** ulitengewa fedha kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Dar es Salaam Port – TAZARA (km 6) chini ya awamu ya pili ya mradi wa *Dar es Salaam Maritime Gateway* utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Hadi Machi, 2018, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa haujaanza kwa kuwa utajumuishwa kwenye mradi wa Mabasi Yaendayo kwa Haraka awamu ya tano (5) ambao uko kwenye maandalizi.

***29. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara ya **Dumila – Kilosa (km 63),** kazi ya ujenzi kwa sehemu ya ***Dumila – Rudewa (km 45)*** imekamilika Desemba, 2013. Kwa sehemu ya ***Rudewa – Kilosa (km 18),*** hadi Machi, 2018 taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu hii zilikuwa zinaendelea. Aidha, kazi ya ujenzi wa mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion - WIM) eneo la Dakawa ilikuwa inaendelea.

***30. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)** ulikuwa umefikia asilimia 76.10 na kazi ya ujenzi inaendelea. Aidha, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Matai – Kasesya (km 50**), Serikali inaendelea na maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi huu.

***31. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa madaraja makubwa, hadi kufikia Machi, 2018 ujenzi wa madaraja ya Kilombero na Kavuu ulikuwa umekamilika. Madaraja ambayo ujenzi wake unaendelea ni pamoja na Mara (asilimia 81.3), Lukuledi (asilimia 70), Sibiti (asilimia 68.58) na Ruhuhu (asilimia 65). Madaraja mengine ni Mlalakuwa (asilimia 60), Momba (asilimia 7.5) na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa daraja la Magara. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa madaraja ya Selander, Wami, Simiyu, Kigongo/Busisi, Sukuma na Mtera na ununuzi wa vyuma vya madaraja ya dharura (Steel Bridge Emergency Parts 200 Compact Bridge Parts) yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

***32. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara ya **New Bagamoyo (Morocco JCT – Mwenge – Tegeta: km 17.2)** hadi Machi, 2018, maandalizi ya upanuzi wa barabara sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3) yalikuwa yanaendelea.

***33. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa barabara ya **Kyaka – Bugene (km 59.1)** umekamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 06 Novemba, 2017. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika kwa sehemu ya Bugene – Kasulo (km 124) na usanifu wa kina wa barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105) unaendelea.

***34. Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2018 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kuhusu barabara ya **Isaka – Lusahunga – Rusumo (km 392),** ni kama ifuatavyo:

***i) Sehemu ya Isaka – Lusahunga (km 242)***

Kazi ya ukarabati wa sehemu ya **Ushirombo – Lusahunga (km110)** imefikia asilimia 61 ambapo kilometa 67 zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami.

***ii) Sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na Nyakasanza – Kobero (km 59)***

Kazi ya ukarabati wa sehemu korofi kwenye barabara hii inaendelea. Aidha, kazi ya mapitio ya usanifu wa kina ili kukidhi viwango vinavyotakiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki iko katika hatua za mwisho za kukamilika. Benki ya Dunia imekubali kugharamia ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 91) kwa kiwango cha lami chini ya mradi wa *Development Corridors Transport Project (DCTP).*

***iii) Mizani ya Mwendakulima (Kahama)***

Mizani ya kupima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) iliyopangwa kujengwa katika eneo la Mwendakulima itajumuishwa kwenye mradi wa ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi. Hadi Machi, 2018, kazi za ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU) zilikuwa zinaendelea.

***35. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara ya **Manyoni– Itigi– Tabora (km 259.7),** hadi kufikia Machi, 2018 ujenzi wa sehemu za ***Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35)*** na ***Tabora – Nyahua (km 85)*** ulikuwa umekamilika. Aidha, kwa sehemu ya ***Chaya – Nyahua (km 85.4)*** mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

***36. Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa barabara ya **Korogwe – Handeni (km 65**) na barabara ya **Handeni – Mkata (km 54)** umekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 zilitumika kulipa madai ya Mkandarasi.

***37. Mheshimiwa Spika***, kuhusu mradi wa ukarabati wa barabara ya **Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza**, hadi Machi, 2018, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami zilikuwa zinaendelea.

***38. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami, upanuzi na ukarabati wa **barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam (km 156.66);** barabara ya **Mbezi (Morogoro Road) – Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14),** kazi za ujenzi sehemu ya Kifuru – Malamba Mawili – Msigani (km 4.0) zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, barabara ya **Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6)** imekamilika. Kuhusu barabara ya **Tegeta Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20),** sehemu ya Goba – Madale (km 5.0) ujenzi umefikia asilimia 15.

***39. Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2018, utekelezaji wa ujenzi wa barabara nyingine za kupunguza msongamano ni kama ifuatavyo: **Kibamba - Kisopwa (km 12.0),** kazi za ujenzi wa sehemu ya Kibamba hadi Mlongazila (km 4) zimekamilika; **Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7);** kazi za ujenzi wa sehemu ya Kitunda – Kivule (km 3.2) imefikia asilimia 15; **Ardhi – Makongo – Goba (km 4.0),** kazi za ujenzi zinaendelea ambapo km 3.5 sawa na asilimia 90 zimekamilika na kwa barabara ya **Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda (km 2.5),** zabuni za ujenzi zimetangazwa. Kuhusu barabara ya **Mwai Kibaki (km 9.1); Kawe round about – Garden Rd Junction (km 2.9)** zabuni za ujenzi zimetangazwa na taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara za **Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (km 25.1)** na **Mjimwema – Kimbiji (km 27.0)** zinaendelea.

***40. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa barabara ya **Ndundu – Somanga (km 60)** umekamilika. Fedha zilizotengwa mwaka 2017/2018 ni kwa ajili ya malipo ya sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi huu.

***41. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Ifakara – Lupiro – Mahenge/Malinyi – Londo – Songea (km 396),** mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) na Daraja la Ruaha Mkuu ulisainiwa tarehe 28 Julai, 2017 na kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea.

***42. Mheshimiwa Spika***, kuhusu mradi wa barabara ya **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 373),** hadi kufikia Machi, 2018, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Tabora – Sikonge (Usesula) (km 30) zilikuwa zimefikia asilimia 79.1 ambapo kilomita 22.6 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu ya **Sikonge (Usesula) – Ipole - Koga – Mpanda (km 340)** mikataba ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Usesula – Komanga (km 108.0) na barabara ya kuingia mji wa Sikonge, (km 7.5), Komanga – Kasinde (km 108.0) na barabara ya kuingia mji wa Inyonga (km 4.8) na Kasinde – Mpanda (km 108.0) na barabara ya kuingia mji wa Urwira (km 3.7) ilikuwa imesainiwa chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Maandalizi ya kazi za ujenzi yanaendelea.

***43. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo (km 239) na Loliondo – Mto wa Mbu (km 213)**, hadi kufikia Machi, 2018 ujenzi wa sehemu ya **Makutano - Sanzate (km 50)** ulikuwa umefikia asilimia 54. Kuhusu sehemu ya **Sanzate - Natta – Mugumu (km 85),** Serikali inaendelea na taratibu za kurudia kutangaza zabuni baada ya wazabuni wa awali wa sehemu ya Natta – Mugumu (km 41.6) kuwa na gharama za juu zaidi ya makisio ya gharama za mradi. Aidha, Mkandarasi wa barabara ya **Loliondo – Mto wa Mbu** (sehemu ya Waso – Sale: km 49) anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

***44. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Ibanda – Itungi/ Kiwira (km 26)**, hadi Machi, 2018 kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara Kajunjumele – Kiwira Port (km 6) na sehemu ya Ibanda – Itungi Port (km 26) kwa kiwango cha lami ilikuwa inaendelea. Kwa upande wa barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach, sehemu ya Tenende – Matema (km 34.6), kazi zimekamilika kwa asilimia

65.3. Aidha, ujenzi wa sehemu ya Bujesi – Mbambo (km 15.0), ujenzi wa kilometa 10.0 ulikamilika kwa kiwango cha lami. Serikali inaendelea na maandalizi kwa ajili ya kutangaza zabuni ili kuanza ujenzi wa sehemu ya Tukuyu – Mbambo (km 15).

***45. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Nzega – Tabora (km 115)** kwa kiwango cha lami umekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka 2017/2018 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri.

***46. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi (km 768),** hadi kufikia Machi, 2018 ujenzi wa sehemu ya ***Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi Kibaoni (km 76.6)*** na ***Sitalike – Mpanda (km 36.9)*** ulikuwa umekamilika. Kuhusu sehemu ya ***Mpanda – Mishamo (km 100): sehemu ya Mpanda - Ifukutwa – Vikonge (km 30),*** maendeleo ya mradi yamefikia asilimia 43. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Kibaoni – Sitalike (km 71.0).***

***47. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ukarabati wa barabara ya **Nyanguge – Musoma (km 185.5)** unahusisha pia ujenzi wa barabara ya Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass: km 17), Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55), Bulamba - Kisorya (km 51) na barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92). Mradi huu unahusisha pia ukarabati wa barabara ya Makutano – Sirari (km 83).

***48. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2018 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Kazi za ukarabati wa sehemu ya barabara ya ***Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5)*** zilikuwa zimekamilika. Maandalizi kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya ***Nyanguge – Simiyu/ Mara Border (km 80)*** yanaendelea ambapo mradi unatarajiwa kugharamiwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Lake Victoria Transport Project* (LVTP). Kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Usagara – Kisesa (km 17*****)** imekamilika.

Kuhusu barabara ya ***Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa; sehemu ya Bulamba –Kisorya (km 51),*** hadi Machi, 2018, kazi za ujenzi wa sehemu ya Bulamba – Kisorya (km 51) zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 37.58. Aidha, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea ambapo mradi unatarajiwa kugharamiwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Lake Victoria Transport Project* (LVTP).

Upanuzi wa ***barabara ya kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mwanza (km 12.0)*** unaendelea; ujenzi wa ***Daraja la Waenda kwa Miguu la Furahisha*** umekamilika; Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa ***Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)*** na kazi ya ukarabati wa barabara ya ***Makutano – Sirari (km 83)*** inaendelea.

***49. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara ya **Magole – Turiani - Mziha (km 83.8),** hadi Machi, 2018, ujenzi wa barabara ya Magole – Turiani (km 45.2) ulikuwa umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Turiani – Mziha – Handeni (km 104.0).

***50. Mheshimiwa Spika,*** hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi wa ujenzi **wa barabara za juu (flyovers/interchange) na maboresho ya makutano ya barabara katika jiji la Dar es Salaam** hadi Machi, 2018 ni kama ifuatavyo:

**i) Barabara ya Juu *(Flyover)* katika makutano ya TAZARA**

Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 70.1 na kazi za ujenzi zinaendelea.

**ii) Barabara za Juu *(Interchange)* katika makutano ya Ubungo**

Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo.

**iii) Barabara za Juu (Flyovers) katika makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA,**

**Uhasibu, Mbezi Mwisho, Selander (Kinondoni Makaburini), Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct na Morocco** Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika makutano hayo zinaendelea.

***51. Mheshimiwa Spika,*** barabara ya ***Mwigumbi – Maswa - Bariadi – Lamadi (km 171.8)*** na sehemu ya **Mwigumbi – Maswa (km 50.3)** zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Maswa – Bariadi (km 49.7).***

***52. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Tabora - Ipole – Rungwa (km 172)**, hadi kufikia Machi, 2018 kazi ya upembuzi yakinifu ilikuwa imekamilika na usanifu wa kina unaendelea.

***53. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Kidahwe – Kibondo – Nyakanazi (km 413)**, hadi kufikia Machi, 2018, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Kidahwe – Kasulu (km 63)** ulikuwa umefikia asilimia 56 na kwa sehemu ya **Nyakanazi – Kabingo (km 50)** ujenzi ulifikia asilimia 41. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa sehemu ya **Kabingo – Kibondo – Kasulu - Manyovu (km 300)** yanaendelea ambapo Serikali imeanza mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kugharamia ujenzi wa barabara hii. Aidha, wakati mazungumzo hayo yanaendelea, Serikali imeanza taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nduta – Kibondo – Kabingo na barabara ya kupitia Kibondo mjini (km 87.7).

***54. Mheshimiwa Spika,*** barabara ya kwenda **Uwanja wa Ndege wa Mafia (Mafia Airport Access Road - km 14)** ilikamilika Januari, 2015. Fedha zilizotengwa mwaka 2017/2018 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasina Mhandisi Mshauri.

***55. Mheshimiwa Spika***, kuhusu mradi wa barabara ya **Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12),** hadi Machi, 2018, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii zilikuwa zinaendelea na zimefikia asilimia 83.4.

***56. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni) (mita 680)** ulikamilika na ujenzi wa barabara unganishi yenye urefu wa kilometa 1.5 kutoka Daraja la Nyerere (Kigamboni) kuunganisha na barabara ya Tungi – Kibada katika eneo la Vijibweni unaendelea. Aidha, usanifu wa barabara za Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjimwema (km 1.6) unaendelea.

***57. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa **njia za magari mazito na maegesho ya dharura katika Ukanda wa Kati** una lengo la kuimarisha na kuboresha barabara pamoja na kuongeza usalama kwa watumiaji barabara katika ukanda huo. Mradi huu umepangwa kujumuishwa kwenye usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara za Ukanda wa Kati. Kazi hii itazingatiwa wakati wa kufanya usanifu wa kina wa barabara ya Morogoro hadi Dodoma.

***58. Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi wa barabara ya **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) hadi Pugu (km 8.0)** ni kuipanua barabara hii kuwa njia sita. Mradi huu utajumuishwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu *(BRT Phase III).* Hadi Machi, 2018, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa kina wa *BRT Phase III* zilikuwa katika hatua za mwisho.

***59. Mheshimiwa* Spika**, mradi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 25.7)** unahusisha upanuzi wa barabara hii kuwa njia sita ikijumuisha **upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**. Hadi Machi, 2018, taratibu za kumpata Mkandarasi wa upanuzi wa barabara kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga (*Design and Build*) kwa sehemu ya Kimara – Kiluvya (km 16.2) zilikuwa katika hatua ya mwisho.

***60. Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi wa barabara ya **Kisarawe - Maneromango – Mlandizi (km 119)** ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Hadi Machi, 2018, Serikali ilikuwa inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

***61. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu kuijenga kuwa njia sita barabara ya pete ya **Pugu – Kifuru - Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, hadi Machi, 2018, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa njia sita ilikuwa bado haijaanza. Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na Washirika wa Maendeleo mbalimbali kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji wa mradi huu.

***62. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa **mizani mpya karibu na bandari ya Dar es Salaam**, unatekelezwa ili magari makubwa yapime uzito kabla ya kuanza safari na hivyo kudhibiti uzidishaji wa uzito. Hadi Machi, 2018, mkataba wa ujenzi wa mizani mpya karibu na bandarini ulikuwa umesainiwa na kazi zilikuwa zinaendelea.

***63. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Tunduma – Sumbawanga (km 223.21),** ujenzi kwa sehemu ya Tunduma - Ikana (km 63.7), Ikana-Laela (64.2), Laela - Sumbawanga (km 95.31) na Tunduma – Ikana (eneo la Tunduma mjini - km 1.6) umekamilika. Aidha, mkataba wa ujenzi umesainiwa kwa upande wa barabara ya **Mpemba – Isongole (km 51.2)** na Mkandarasi ameanza kazi za ujenzi.

***64. Mheshimiwa* Spika,** kuhusu mradi wa barabara ya **Kagoma – Lusahunga (km 154)**, ujenzi ulikamilika Desemba, 2013. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

***65. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya **Arusha – Namanga (km 105)** ulikamilika Desemba, 2012. Aidha, kazi ya ujenzi wa Kituo cha Kutoa Huduma kwa Pamoja Mpakani (One Stop Border Post - OSBP) imekamilika. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri.

***66. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi na ukarabati wa **barabara ya Arusha – Minjingu – Babati – Singida** (km 327.5) umekamilika.

Fedha zilizotengwa kwenye mradi huu kwa mwaka 2017/2018 ni za kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi.

***67. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani,** upanuzi wa sehemu ya ***Bendera Tatu – KAMATA (km 1.3)*** utajumuishwa kwenye mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili. Aidha, Serikali inaendelea kufanya maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa sehemu ya **Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8)** pamoja na Daraja la Mzinga.

***68. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Msimba – Ruaha/ Ikokoto – Mafinga – Igawa (km 356.6),** hadi Machi, 2018, kazi za ukarabati kwa sehemu ya Mafinga – Nyigo (km 74.1) zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 86.34 ambapo kilometa 60.5 zimekamilika na kwa upande wa sehemu ya Nyigo – Igawa (km 63.8), kazi za ukarabati zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 87.7 ambapo kilometa 62 zimekamilika. Kuhusu barabara ya ***Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152)***, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

***69. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya ***Njombe – Ndulamo – Makete (km 109.4)***, mikataba ya ujenzi wa sehemu ya Njombe – Moronga (km 53.9) na Moronga – Makete (km 53.5) imesainiwa na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami yanaendelea. Aidha, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Njombe – Lupembe - Madeke (km 125)*** zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi; kazi za ujenzi wa barabara ya **Igawa – Mbarali – Ubaruku; sehemu ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9)** zinaendelea ambapo kilometa 2.3 zimekamilika kwa kiwango cha lami na ujenzi wa kilometa 6.6 unaendelea. Kuhusu barabara ya ***Iringa – Ruaha National Park (km 104.0)*** mradi huu umeainishwa katika miradi itakayofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Development Corridors Transport Project.* Tathimini ya athari za mazingira inaendelea katika barabara hiyo.

***70. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ukarabati wa barabara ya

**Korogwe – Mkumbara – Same (km 172)** umekamilika. Fedha zilizotengwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi.

***71. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Mbeya – Makongolosi (km 115),** mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya ***Chunya – Makongolosi (km 43)*** kwa kiwango cha lami umesainiwa na maandalizi ya ujenzi yanaendelea. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kumtafuta Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Mkiwa - Itigi - Noranga (km 56.9)***.

***72. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa barabara ya **Chalinze – *Segera* – Tanga (km 245),** Serikali inaendelea na taratibu za kumtafuta Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Amani – Muheza (km 36.0)***.

***73. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa barabara ya **Itoni – Ludewa – Manda (km 211)** unalenga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami na zege. Hadi Machi, 2018, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha zege wa sehemu ya ***Lusitu – Mawengi (km 50)*** inaendelea.

***74. Mheshimiwa Spika,*** barabara ya ***Handeni Kibereshi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijochini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba Kwa Mtoro – Singida (km 460)*** ambayo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi bandari ya Tanga usanifu wa kina umekamilika. Aidha, Serikali inatafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa awamu.

***75. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu barabara ya **Dodoma – Mtera – Iringa (km 260)**, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Iringa (km 7.3). Aidha, kuhusu barabara ya **Dodoma – Babati (km 251),** ujenzi wa barabara yote umekamilika kwa kiwango cha lami.

***76. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa barabara ya **Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 659.7)** na **Masasi – Newala – Mtwara (km 209)** mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Mbinga – Mbamba Bay (km 66)*** umesainiwa

ambapo mradi unagharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Kuhusu barabara ya ***Mtwara – Newala – Masasi (km 209.0),*** hadi Machi, 2018, ujenzi wa sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50.0) kwa kiwango cha lami ulikuwa umefikia asilimia 16. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Masasi – Nachingwea – Nanganga (km 91.0)*** imekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

***77. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye **Chuo cha Uongozi cha Bagamoyo** pamoja na barabara za ndani ya Chuo hicho, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo.

***78. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa ***Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi ya Nne,*** hadi Machi, 2018, ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili ulikuwa katika hatua ya kuwapata Makandarasi wa ujenzi. Aidha, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu wa kina na usimamizi wa mradi wa BRT Awamu ya Tatu zinaendelea.

***79. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Miradi hiyo inahusisha kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya barabara, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, ukarabati wa barabara kwa kiwango cha changarawe na kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Hadi Machi, 2018 utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

***i) Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/Benaco (km 183.1) – Sehemu ya Bugene – Kasulo/ Benaco (km 124)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***ii) Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwamtoro – Singida (km 460)***

Kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni imekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa awamu.

***iii) Kufanya Mapitio na Kuandaa Miongozo (Standards and Specifications)***

Wizara iliendelea na kazi ya kupitia na kuchambua mapungufu yaliyoko katika miongozo mbalimbali ujenzi wa barabara. Aidha, Wizara inaendelea kuandaa rasimu ya Hadidu za Rejea kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hiyo.

***iv) Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)***

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***v) Barabara za Juu (TAZARA na Ubungo)***

Hadi Machi, 2018, malipo ya fidia na uhamishaji wa miundombinu ya huduma iliyokuwepo kwenye eneo la mradi wa TAZARA *Flyover* yalikuwa yamekamilika. Aidha, kwa upande wa mradi wa Ubungo *Interchange,* malipo ya fidia yamekamilika na uhamishaji wa miundombinu ya umeme, maji, simu, gesi unaendelea.

***vi) Barabara ya Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala –Oldeani Jct (km 328)***

Upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

***vii) Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Mto Sibiti – Lalago – Maswa (km 389)***

Kazi ya upembuzi yakinifu wa barabara hii inaendelea chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ujerumani (KfW). Aidha,

Mhandisi Mshauri amewasilisha rasimu ya taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu.

***viii) Barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete (km 96.2)***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

***ix) Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)***
Rasimu ya taarifa ya usanifu wa kina imewasilishwa na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya mapitio. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2018.

***x) Daraja la Kigongo/Busisi katika Barabara ya Usagara – Geita***
Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Kazi ya usanifu wa kina inaendelea na inatarajiwa kukamilika Juni, 2018.

***xi) Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86)***
Kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea na rasimu ya taarifa ya awali imewasilishwa kwa ajili ya mapitio.

***xii) Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 457)***
Serikali inaendelea na maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

***xiii) Barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 96.7)***
Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zipo kwenye hatua za mwisho.

***xiv) Barabara ya Tegeta – Bagamoyo (km 43.2)*** Kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza upanuzi wa barabara hii kuwa ya njia nne.

***xv) Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)*** Kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***xvi) Barabara ya Mbegani – Bagamoyo (km 7.2)*** Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

***xvii) Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)***
Kazi ya usanifu wa kina inaendelea na rasimu ya taarifa imewasilishwa kwa ajili ya mapitio.

***xviii) Barabara ya Mtwara Pachani – Lusewa - Lingusenguse – Nalasi (km 211)***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

***xix) Barabara ya Kibondo – Mabamba (km 45)*** Kazi ya usanifu wa kina imekamilika. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

***xx) Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430)***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

***xxi) Barabara ya Kibada – Mwasonga – Kimbiji (km 19.2)***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea

***xxii) Barabara ya Kimbiji – Tundwisongani (km 30.5)***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

***xxiii) Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 91):***
Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Aidha, Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa kina.

***xxiv) Daraja la Mlalakuwa***
Kazi ya ujenzi inaendelea na imefikia asilimia 48 ambapo daraja la upande mmoja limekamilika na limeanza kutumika.

***xxv) Kuboresha Eneo la Mlima Kitonga (km 10)***
Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxvi) Barabara ya Shabiby – Arusha/Dodoma Round About (km 1.6)***

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxvii) Barabara ya Chimwaga – Chinyoya – Kikuyu (Dodoma Roundabout) (km 6.5)***

TaratibuzakumpataMhandisiMshauriwakufanya upembuzi yakinifunausanifu wakina zinaendelea.

***xxviii) Barabara ya Dar es Salaam Nanenane) – Miyuji (Arusha Road) – Mkonze (km 23)***

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxix) Barabara ya Emmaus – Mlimwa – Wajenzi (km 5)***

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxx) Dodoma Outer Ring Road / Dodoma Bypass (Mtumba - Veyula –Nala – Matumbulu – Mtumba – km 104)***

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

***xxxi) Barabara ya Ngaresh – Enguik (Monduli Juu) (km 104)***

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxxii) Daraja la Kitengule***

Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Aidha, kazi ya usanifu wa kina inaendelea na inatarajiwa kukamilika Julai, 2018.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho ya Vivuko na Matengenezo ya Magari**

***80. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/2018,

Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ilipanga kuendelea na kazi ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni, ujenzi wa maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli ya kivuko cha Chato – Nkome na ujenzi wa maegesho ya Lindi - Kitunda. Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa vivuko vipya vya Magogoni – Kigamboni na Kigongo - Busisi; ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa karakana za TEMESA; pamoja na ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II, MV Sengerema na MV Kigamboni. Aidha, Wizara kupitia TEMESA ilipanga kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi katika majengo ya Serikali. Kazi nyingine ni kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

***81. Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2018 ujenzi wa kivuko kinachotoa huduma ya usafiri kati ya Magogoni – Kigamboni (MV. Kazi) ulikuwa umekamilika na kimeanza kutoa huduma. Aidha, ujenzi wa kivuko cha Kigongo – Busisi unaendelea na unatarajiwa kukamilika Mei, 2018 na ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kayenze - Bezi upo katika hatua ya kusaini mkataba.

***82. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ujenzi wa maegesho ya vivuko, ujenzi wa maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome hatua inayoendelea ni kurudia zoezi la kumpata Mkandarasi baada ya Wazabuni walioomba awali kukosa sifa. Aidha, kazi ya ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda imekamilika. Kwa upande wa upanuzi wa maegesho ya Kigamboni, Wizara inaendelea na hatua za uthamini kwa ajili ya kulipa fidia ya nyumba ili kupisha upanuzi wa maegesho hayo. Aidha, zabuni zimetangazwa kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa maegesho ya Kikove katika Mto Kilombero kwa ajili ya kivuko kitakachotoa huduma kati ya eneo la Mlimba na upande wa Malinyi.

***83. Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa kivuko cha MV. Pangani

II umekamilika mwezi Desemba, 2017 na kivuko kinatoa huduma. Aidha, Mikataba kwa ajili ya ukarabati wa vivuko vya MV. Misungwi, MV. Sengerema na MV. Kigamboni ipo katika hatua za kusainiwa.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

***84. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilipanga kuendelea na ujenzi na ukarabati wa nyumba kwa ajili ya makazi ya Viongozi wakiwemo Majaji na Watumishi wa Serikali pamoja na majengo ya Serikali. Aidha, kipaumbele ni ujenzi wa nyumba za Viongozi katika makao makuu ya nchi mkoani Dodoma.

***85. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2018, miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa nyumba 16 za Viongozi mjini Dodoma; ujenzi wa nyumba za Majaji katika Mikoa ya Shinyanga (1), Kilimanjaro (1), Mtwara (1) na Dar es Salaam (1). Kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa nyumba za Makazi za Magomeni 'Quarters' Dar es Salaam pamoja na ukarabati wa Ikulu Ndogo katika Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa.

**Usalama Barabarani**

***86. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu shughuli za usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara. Kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi, uanzishwaji wa Mamlaka ya Usalama Barabarani nchini, ukaguzi wa usalama wa barabara pamoja na mapitio ya Sera na Sheria ya Usalama Barabarani. Kazi nyingine ni kutoa elimu ya usalama barabarani kwa umma, utoaji wa elimu ya usalama barabarani mashuleni pamoja na uendeshaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani.

***87. Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2018 kazi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (One Stop Inspection Station –

OSIS) katika maeneo ya Manyoni na Nyakanazi ilikuwa imeanza. Aidha, ujenzi wa mizani ya kisasa ya upimaji wa magari yakiwa kwenye mwendo mdogo mijini upo kwenye taratibu za kumpata Mkandarasi wa kujenga mizani ya aina hiyo kwa mkoa wa Dar es Salaam. Kuhusu kuanzisha Mamlaka ya Usalama Barabarani, jukumu hili limehamishiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, kazi ya Ukaguzi wa Usalama wa Barabara (Road Safety Audit) ipo katika hatua ya kumpata Mshauri Mwelekezi na kazi ya kuweka kamera za kudhibiti mwendo kasi kwa vyombo vya usafiri barabarani imeanza katika Ukanda wa Kati katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na inatarajiwa kukamilika Julai, 2018. Aidha, Wizara imekamilisha utoaji wa elimu juu ya miongozo ya matumizi ya Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani kwa askari wa usalama barabarani nchi nzima. Kuhusu mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani, 2009, taratibu za kumpata Mtaalam Mwelekezi wa kufanya mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani zinaendelea.

## MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018 malengo na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege hadi Machi, 2018 ni kama ifuatavyo:

i) Katika mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria, jengo la kuongozea ndege, maegesho ya ndege na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Wizara iko katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi wa kutekeleza mradi huu.

ii) Katika mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mpanda** kazi zilizopangwa ni kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri. Kwa sasa, Serikali inatafuta fedha za kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri waliofanya kazi ya ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya viungio pamoja na maegesho ya ndege katika kiwanja hicho.

iii) Kuhusu ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Tabora,** kazi zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni kumalizia kazi za awamu ya pili zinazohusu ukarabati wa barabara ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Kazi nyingine ni kuanza awamu ya tatu ya mradi inayohusu ujenzi wa jengo jipya la abiria, kituo cha uangalizi wa hali ya hewa, barabara ya kuingilia kiwanjani pamoja na maegesho ya magari. Kazi zote za awamu ya pili ya mradi zimekamilika. Aidha, mkataba kwa ajili ya kazi za awamu ya tatu ya mradi huu umesainiwa. Maandalizi kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradiyanaendelea.

iv) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Songwe,** kazi zilizopangwa zilikuwa ni kumalizia ujenzi wa jengo jipya la abiria, kusimika taa za kuongozea ndege, kukarabati tabaka la juu la barabara ya kuruka na kutua ndege na kukarabati eneo la usalama (Runway End Safety Area - RESA). Kazi za ujenzi wa jengo la abiria imekamilika kwa asilimia 57. Hata hivyo, Serikali inaangalia uwezekano wa kusitisha mkataba kutokana kasi ndogo ya mkandarasi anayetekeleza mradi huo. Aidha, mkataba wa kusimika taa za kuongozea ndege umesainiwa na taratibu za kuanza kazi zinaendelea.

v) Katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza,** kazi zilizopangwa ni umaliziaji wa ujenzi wa jengo jipya la kuongozea ndege, kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege na kupanua maegesho ya ndege. Kazi nyingine ni pamoja na ujenzi wa uzio, jengo la mizigo, jengo jipya la abiria, barabara ya kuingiakiwanjani,maegeshoyamagarinausimikaji wa taa za kuongozea ndege. Kazi zilizokamilika ni kuongeza urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita 500 na upanuzi wa maegesho ya ndege. Aidha, ujenzi wa jengo la mizigo pamoja na jengo la kuongozea ndege umefikia asilimia 65. Vilevile, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 2 kwa mwaka.

vi) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Arusha** kazi iliyopangwa ni kufanya usanifu wa kina ili kuboresha jengo la abiria. Kazi ya Usanifu wa Kina kwa ajili ya uboreshaji wa jengo la abiria imekamilika. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea.

vii) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara,** kazi zilizopangwa ni kuanza kazi ya ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege, kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani pamoja na maegesho ya magari. Mkataba umesainiwa na Mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya kuanza kazi.

viii) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga,** kazi zilizopangwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Kazi nyingine ni ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Mkataba kwa ajili kazi hizo umesainiwa na Serikali inaendelea na taratibu za kulipa fidia ili kazi hiyo iweze kuanza.

ix) Kuhusu mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga,** kazi zilizopangwa ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na mradi huu, ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa kiwanja cha ndege cha Shinyanga na mkataba kwa ajili ya kazi za ujenzi umesainiwa. Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi.

x) Kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro,** kazi zilizopangwa ni kukarabati barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara za viungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege, barabara ya kuingilia

kiwanjani pamoja na maegesho ya magari. Hadi Machi, 2018, kazi ya ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, ukarabati wa jengo la abiria na ukarabati wa jengo la mizigo ilikuwa imekamilika. Aidha, maandalizi ya kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya mradi wa ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio na usimikaji wa taa za kuongozea ndege yameanza.

xi) Kuhusu mradi wa **Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa** kazi zilizopangwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipya cha mkoa wa Geita. Kazi nyingine ni ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Musoma, Songea na Iringa na kufanya maandalizi kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja nane (8) vya mikoa ambavyo ni Njombe, Lindi, Lake Manyara, Kilwa Masoko, Singida, Moshi, Tanga na Simiyu. Aidha, kazi nyingine ni pamoja na kupanua na kukarabati jengo la abiria la kiwanja cha ndege cha Dodoma.

Hadi Machi, 2018, kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege kwa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Geita zilikuwa zimefikia asilimia 67. Aidha, mkataba kwa ajili ya ukarabati wa jengo la abiria la kiwanja cha ndege cha Dodoma ulikuwa umesainiwa na maandalizi ya kuanza ukarabati yalikuwa yanaendelea. Vilevile, taratibu za kuwapata makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa viwanja vya Songea na Musoma zilikuwa zinaendelea. Benki ya Dunia imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa, Lake Manyara na Tanga ambapo mazungumzo bado yanaendelea.

xii) Kwa upande wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Msalato**, hadi Machi, 2018, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea na zimefikia asilimia 60.

xiii) Kuhusu **Kiwanja cha Ndege cha Bukoba,** kazi zilizopangwa zilikuwa ni kulipa fidia eneo jipya la Omukajunguti na ujenzi wa jengo la watu mashuhuri (VIP). Serikali imesitisha mpango wa kuhamishia kiwanja cha ndege

cha Bukoba kwenda eneo la Omukajunguti kutokana na gharama kubwa za kulipa fidia. Aidha, Serikali imeanza taratibu za kumtafuta Mhandisi Mshauri ili kufanya utafiti na kuishauri Serikali kuhusu njia bora ya kurefusha njia ya kuruka na kutua ndege katika kiwanja hicho.

xiv) Kuhusu mradi wa ujenzi wa **Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III)** katika **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)** utekelezaji umefikia asilimia 72.

**UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI**

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mfuko wa Barabara ulitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 917,548,290,000.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 582,644,500,000.00** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na mikoa ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na **Shilingi 249,704,790,000.00** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Hadi Machi, 2018, Bodi ilikuwa imekusanya na kugawanya jumla ya **Shilingi 604,489,346,576.00** sawa na **asilimia 66** ya bajeti ya mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipokea **Shilingi 41,950,377,799.00,** TANROADS ilipokea **Shilingi 377,553,400,195.00**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilipokea **Shilingi 17,204,797,005.00,** TARURA ilipokea **Shilingi 162,582,163,197.00** na Bodi ya Mfuko wa Barabara ilipokea **Shilingi 5,198,608,380.00.**

***90. Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na TANROADS iko katika hatua za mwisho kuanza kutumia mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato yatokanayo na faini kwa magari yanayozidisha uzito (ePayment System for Overloading Fees). Aidha, ili kuimarisha usimamizi, uwajibikaji na kuongeza uwazi katika shughuli zinazofanyika kwenye vituo vya mizani, Bodi kwa kushirikiana na TANROADS na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uwekaji mfumo wa kielektroniki na kamera za CCTV kwenye vituo vya mizani vya kupimia uzito wa magari. Mfumo huo utawezesha taasisi husika kufuatilia moja kwa moja, kwa wakati husika namna upimaji wa magari unavyoendelea kwenye vituo vya mizani nchini. Bodi ya Mfuko wa Barabara itakuwa na uwezo wa kujua magari yaliyozidisha uzito na faini iliyotozwa muda huohuo kupitia mfumo wake wa taarifa (RFB Management Information System).

***91. Mheshimiwa Spika,*** Bodi iliajiri Mtaalam Mshauri wa kufanya utafiti juu ya vyanzo vipya vya mapato ya Mfuko na kuandaa ushauri kwa Serikali juu ya hatua za kuchukua ili kuongeza mapato ya fedha za matengenezo ya barabara. Bodi pia ilifanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote Tanzania Bara. Aidha, Bodi ilifanya ufuatiliaji wa mapato ya Mfuko na kutathmini juu ya ubora wa njia zinazotumiwa kukusanya mapato.

**Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**

***92. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wakala wa Majengo Tanzania ulipanga kuendelea kukamilisha ujenzi wa jengo lenye Ghorofa 6 (Mtaa Moshi Plot Na.5) – Dodoma; kununua viwanja mikoani na Makao Makuu; kufuatilia upatikanaji wa hati za viwanja vya Wakala mikoani na Makao Makuu; ununuzi wa samani za Jengo la Ubia lililopo barabara ya Chimala na Jengo lililopo barabara ya Chole; kufanya upembuzi yakinifu kwenye viwanja vitatu vya TBA kwa ajili ya miradi ya uwekezaji pamoja na kumalizia ujenzi wa jengo la TBA Makao Makuu kwa kuweka *lift*. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa maghorofa mawili ya *flats* 8 kila moja katika jengo la EX NMC Mbezi Beach - DSM na maghorofa mawili katika kiwanja Na. 176- Ukonga, DSM; upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuendeleza karakana za samani mikoani pamoja na ukarabati wa majengo mbalimbali Dar es Salaam na mikoa mingine.

Wakala pia ulipanga kuendelea na ujenzi wa nyumba 200 za watumishi wa Serikali kama sehemu ya programu ya ujenzi

wa nyumba 2,500 DSM; kukamilisha ujenzi wa jengo la X- Posta Dodoma na kufanya ununuzi wa jengo la ofisi katika kiwanja Na. 487 eneo la Kilimani, Dodoma.

***93. Mheshimiwa Spika*****,** hadi Machi, 2018, kazi zilizofanyika ni kukamilisha ujenzi wa jengo lenye Ghorofa 6 (Mtaa Moshi Plot Na.5) – Dodoma na ukarabati umefanyika kwenye jengo la TBA Makao Makuu. Aidha, upembuzi yakinifu kwa ajili ya uendelezaji kiwanja namba 176 Ukonga umekamilika na maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu kwa uwekezaji yameanza kwenye karakana za samani mikoani, mradi wa nyumba za kijamii na viwanja vitatu (3) vilivyopo ploti za EX THA, Mbezi Tangi Bovu na ploti namba 55 na 57 Mtaa wa Ngano, ploti namba 906 iliyopo barabara ya Ally Hassani Mwinyi na ploti namba 198 iliyopo barabara ya Ghuba.

Vilevile, TBA imeendelea kufuatilia hati miliki za viwanja vya Wakala Makao Makuu. Kuhusu ununuzi wa kiwanja namba 487 Kilimani Dodoma, Wizara ya Maji na Umwagiliaji imesitisha uuzaji wa kiwanja hiki kutokana na uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma.

***94. Mheshimiwa Spika*****,** majukumu mengine yaliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kukamilisha ujenzi wa mabweni ya wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu - Dodoma; ujenzi wa shule ya Sekondari Ihungo – Kagera; ujenzi wa nyumba za askari Magereza - Ukonga - DSM na ujenzi wa maabara ya *Tanzania Atomic Energy Commission* iliyopo Njiro- Arusha. Aidha, TBA imeendelea kutekeleza miradi ya ubunifu na ujenzi (Design and Build) ambayo inatekelezwa nje ya bajeti. Miradi hii ni kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (MDAs). Wakala una jumla ya miradi 90 ya *design & build* inayotekelezwa ambayo ina thamani ya jumla ya Shilingi 154,974,576,390.26.

**Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)**

***95. Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, TEMESA ilipanga kuendelea na kazi ya upanuzi wa maegesho

ya Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bwina ya kivuko cha Chato – Nkome na ujenzi wa maegesho ya Lindi – Kitunda. Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa vivuko vipya vya Magogoni – Kigamboni na Kigongo – Busisi; ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa karakana za TEMESA pamoja na ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II, MV Sengerema na MV Kigamboni. Aidha, TEMESA ilipanga kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali pamoja na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba za Serikali.

***96. Mheshimiwa Spika*****,** hadi Machi 2018, ujenzi wa Kivuko kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Magogoni – Kigamboni umekamilika na kivuko kimeanza kutoa huduma tangu mwezi Mei, 2017. Ujenzi wa Kivuko cha Kigongo – Busisi unaendelea huko mkoani Mwanza na umefikia asilimia 65 na ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kayenze – Bezi upo katika hatua ya kusaini mkataba.

***97. Mheshimiwa Spika***, kuhusu ujenzi wa maegesho ya vivuko, ujenzi wa maegesho ya Bwina katika kivuko cha Chato – Nkome upo katika hatua za kumpata mkandarasi; ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda umefikia asilimia 95 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2018; upanuzi wa maegesho ya Kigamboni upo katika hatua za uthamini wa nyumba kwa ajili ya kupisha upanuzi wa maegesho na zabuni imetangazwa kwa ajili ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya Kikove katika mto Kilombero. Kwa upande wa ukarabati wa vivuko, ukarabati wa kivuko cha MV. Pangani II umekamilika na kivuko kinatoa huduma; mkataba kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha MV. Misungwi upo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kusainiwa; ukarabati wa kivuko cha MV. Sengerema upo katika hatua ya kusaini mkataba na taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha MV. Kigamboni zinaendelea.

***98. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, TEMESA

imeendelea kutekeleza majukumu ya matengenezo ya magari ambapo jumla ya magari 11,197 yalifanyiwa matengenezo. Aidha, miradi 322 ya umeme, miradi 528 ya viyoyozi, miradi 510 ya kielektroniki imetekelezwa na TEMESA katika karakana zake.

Kuhusu ukarabati wa karakana, michoro kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa karakana ya mkoa wa Dar es Salaam (Vingunguti) imekamilika na hatua iliyopo sasa ni kumpata Mkandarasi. Aidha, ujenzi wa Karakana mpya ya mkoa wa Manyara awamu ya III umekamilika na Wakala kwa sasa unajipanga kuanza awamu ya IV.

## Bodi ya Usajili wa Wahandisi

***99. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) iliweka malengo ya kusajili wahandisi **1,500,** mafundi sanifu **150**, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **20;** kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri; kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu **1,303** pamoja na kukagua shughuli za kihandisi nchini. Lengo ni kuwezesha shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa.

***100. Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2018, Bodi imesajili wahandisi **2,018** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **17** na kufikisha jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **21,179** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi kuwa **322.** Kati ya jumla ya wahandisi waliosajiliwa, wahandisi **19,348** ni wazalendo na **1,831** ni wageni. Kampuni za ushauri wa kihandisi za kizalendo ni **227** na za kigeni ni **95.** Katika kipindi hicho, Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi wataalamu **407,** wahandisi washauri **27** na kampuni za ushauri wa kihandisi **39** kwa kukiuka Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya miradi **203** ilikaguliwa. Wahandisi wa kigeni **130** walibainika kufanya kazi bila usajili ambapo kati yao **109** walikuwa na sifa na hivyo walisajiliwa na **19** walikuwa hawana sifa hivyo walikataliwa usajili na hivyo kurejeshwa kwao.

***101. Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia iliandaa warsha **5** katika kanda **5** kwa wahandisi wataalam wanaosimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu. Aidha, Bodi iliendelea kuwaapisha wahandisi wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi **2,876** waliapishwa.

Bodi vilevile iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa wahandisi wahitimu **1,200.** Jumla ya wahandisi wahitimu **4,695** wameshapitia mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003. Aidha, wahandisi wahitimu zaidi ya **586** kutoka Serikali za Mitaa na Taasisi mbalimbali za Serikali wameshahitimu mafunzo hayo na kusajiliwa na Bodi kama wahandisi watalaam. Bodi pia iliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi 2017 (Annual Engineers' Day 2017) ambayo ilihudhuriwa na wahandisi zaidi ya **2,500.** Mada iliyojadiliwa katika siku ya wahandisi ilikuwa ni *Jukumu la Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati katika Ujenzi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi.*

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

***102. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilipanga kusajili Wataalamu **223** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo, ambapo wataalam **158** wamesajiliwa kufikia Machi, 2018, ikiwa ni asilimia **71** ya malengo. Aidha, Bodi ilipanga kusajili kampuni **15** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi ambapo kampuni **11** zimesajiliwa ikiwa ni asilimia **73** ya malengo. Bodi vilevile ilipanga kuwajengea uwezo wahitimu **110** katika fani za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani zinazoshabihiana nazo kupitia mafunzo kwa vitendo ambapo wahitimu **115** wamepatiwa mafunzo ikiwa ni ongezeko la asilimia **5** ya malengo.

***103. Mheshimiwa Spika,*** Bodi vilevile ilipanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,000** katika mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo miradi ya ujenzi **1,321** imekaguliwa kufikia Machi, 2018 ikiwa ni asilimia **66** ya lengo. Miradi **342** ilikutwa na kasoro

ambapo wataalam na waendelezaji wa miradi yenye mapungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini na kusimamishiwa ujenzi. Aidha, Bodi ilipanga kusajili miradi ya majengo **800** ambapo miradi ya majengo **630** imesajiliwa kufikia Machi, 2018 ikiwa ni asilimia **79** ya lengo.

Bodi pia iliendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa kidato cha pili na mashindano ya kubuni nyumba zenye gharama nafuu kwa wananchi wenye kipato cha chini ikiwa ni njia mojawapo ya kujitangaza.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/ 2018, Bodi ilisajili makandarasi wapya **599**, hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia **9,191**. Kulikuwa na ongezeko la makandarasi wapya **25** kwa mwaka 2017/ 2018 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo walisajiliwa makandarasi wapya **574**. Aidha, jumla ya makandarasi watatu **(3)** walifutwa kwa hiari yao.

***105. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, jumla ya miradi **2,374** ilikaguliwa. Miradi **666** sawa na asilimia **28** ilipatikana na mapungufu mbalimbali yakiwemo kutozingatia afya na usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa daraja husika. Makandarasi waliokutwa na mapungufu walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili.

Bodi iliendesha kozi mbili **(2)** za mafunzo kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Makandarasi (Sustainable Structured Training Programme – SSTP) katika mikoa ya Dodoma na Mara. Jumla ya makandarasi **72** walishiriki katika mafunzo hayo. Pia Bodi iliendesha warsha mbili **(2)** za mafunzo ya ushirikiano kupitia ubia (Joint Venture) zilizofanyika Dar es Salaam na Bukoba ambapo jumla ya makandarasi **231** walishiriki. Bodi pia iliendelea kuendesha

Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund - CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi wa ndani walio katika daraja la chini na la kati ili kuwezesha ushiriki wa makandarasi wazalendo katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mfuko huu ulifikisha mtaji wa **Shilingi bilioni 3.6** kwa mwaka 2017/2018. Aidha idadi ya wanachama wa Mfuko iliongezeka kutoka **1,510** mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia **1,667** mwaka 2017/2018.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018 Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) liliendelea na taratibu za kufanya mapitio ya Sheria iliyoanzisha Baraza hilo (Cap 162, Revised Edition (R.E.) 2008) kwa lengo la kulihuisha Baraza hilo. Mkutano wa wadau wa sekta ya ujenzi ulifanyika tarehe 22 Septemba, 2017 ili kupata maoni kwa lengo kuboresha Baraza hilo. Aidha, Baraza liliendelea na kuratibu mfumo wa utekelezaji wa majaribio wa kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma ujulikanao kwa jina la "Construction Sector Transparency Initiative (CoST)" ambapo Rasimu ya Mpango Mkakati wa kutekeleza mfumo huo kwa kipindi cha miaka mitatu (2017 – 2020) imeandaliwa.

***107. Mheshimiwa Spika,*** Baraza katika mwaka wa fedha 2017/2018 limeendelea kuratibu na kutekeleza mafunzo kwa wadau wa sekta ya ujenzi kuhusu usuluhishi wa migogoro ya ujenzi, usimamizi wa mikataba na ununuzi wa huduma ya ushauri wa kiutaalam. Aidha, Baraza limeendelea na tafiti kuhusu upimaji wa tija na ubora wa kazi katika Sekta ya Ujenzi na changamoto za ushindani wa makandarasi wa ndani katika kutekeleza miradi ya ujenzi ukilinganisha na makandarasi wa kigeni. Tafiti nyingine zilihusu kanuni za mikataba katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu na usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga (Design and Build). Vilevile, Baraza lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau mbalimbali wa sekta ya ujenzi katika maeneo yanayohusu mikataba ya ujenzi, madai, mabadiliko ya bei, manunuzi na

sheria zake kuhusiana na masuala ya ujenzi, usuluhishi wa migogoro, thamani ya mradi ikilinganishwa na gharama za ujenzi (value for money) na makadirio ya gharama za ujenzi.

***108. Mheshimiwa Spika,*** Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi **190** yenye thamani takribani **Shilingi bilioni 19** kwenye Halmashauri za wilaya zilizo kwenye mikoa ya Mbeya, Kigoma, Rukwa na Shinyanga. Baraza pia limeendelea na jukumu la kukusanya takwimu za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2017/2018 kwa matumizi ya wadau wa sekta ya ujenzi na kufuatilia ukuaji wa sekta. Aidha, Baraza liliendelea kukusanya na kuandaa bei za vifaa vya ujenzi na "indices" kwa ajili ya matumizi ya mabadiliko ya bei (Price Fluctuation Formula). Vilevile, Baraza limeendelea kukusanya taarifa muhimu ili kuwezesha uchapishaji wa jarida la "Construction Business Journal" na "Directory of Construction Materials".

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

***109. Mheshimiwa Spika,*** Kituo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha/kuboresha Sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa ujumla kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa wadau. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kituo kilifanya kazi zifuatazo:

i) Kushiriki katika mikutano **2** ya kimataifa na mikutano **2** ya ndani ya nchi inayohusu utafiti na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya Ujenzi na Usafirishaji.

ii) Kushiriki katika mradi unaotekelezwa na Umoja wa Mamlaka za Barabara katika nchi za SADC (Association of Southern African National Road Agencies – ASANRA) unaolenga kutambua mapungufu ya ujuzi na hivyo kutoa mapendekezo ya kujenga uwezo kwa watendaji wa Mamlaka za Barabara.

iii) Kuandaa mkutano wa kimataifa kuhusu Mikakati ya

Uwekezaji katika Miundombinu katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji.

iv) Kuendelea kutoa huduma za maktaba ya Kituo kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji na kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo na njia za utunzaji wa kumbukumbu na upashanaji wa habari za teknolojia.

v) Kuanza utekelezaji wa mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na uchukuzi hapa nchini Tanzania.

vi) Kuendeleza juhudi za kuhamasisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupenda masomo ya sayansi na uhandisi ujenzi na usafirishaji kwa kuwafundisha programu zinazohamasisha na kuvutia watoto kwa kushirikiana na Mamlaka ya Barabara ya Marekani (Federal Highway Administration).

## C.1.2. SEKTA YA UCHUKUZI

### Bajeti ya Sekta ya Uchukuzi kwa mwaka 2017/2018

***110. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 2,569,073,208,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,477,931,183,000.00** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi 91,142,025,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufi Machi, 2018, fedha za maendeleo **Shilingi 1,035,040,293,508.00** sawa na asilimia 41.7 ya bajeti ya Maendeleo zilikuwa zimetolewa na fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 61,170,031,880.00** sawa na asilimia 67 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa imetolewa.

### Marekebisho ya Muundo wa Taasisi

***111. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara iliendelea kuzifanyia marekebisho sheria za sekta ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa taasisi za umma. Mwezi Oktoba,

2017, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Shirika la Reli Na.10 ya mwaka 2017 (Tanzania Railways Corporation Act, No. 10 of 2017) kwa lengo la kuunganisha majukumu ya Kampuni Hodhi ya Raslimali za Reli (RAHCO) na Kampuni ya Reli (TRL) na kuunda Shirika jipya la Reli (Tanzania Railways Corporation – TRC). Shirika hili lilianzishwa rasmi tarehe 28 Februari, 2018. Aidha, ili kukabiliana na changamoto zilizoko katika usafiri kwa njia ya maji ikiwa ni pamoja na kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, Bunge lako pia lilitunga Sheria ya Wakala wa Meli Na.14 ya mwaka 2017 (Tanzania Shipping Agencies Act, No.14 of 2017). Sheria hii ilianzisha Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation - TASAC) ambalo limechukua majukumu ya udhibiti wa usafiri kwa njia ya maji yaliyokuwa yakitekelezwa na SUMATRA. Shirika hili lilianzishwa rasmi tarehe 23 Februari, 2018. Mapendekezo ya kutunga sheria kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini yapo katika hatua za mwisho.

## USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA BARABARA

***112. Mheshimiwa Spika,*** mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa sekta ya usafi na uchukuzi kwa njia ya barabara umeendelea kuongezeka. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Wizara kupitia SUMATRA ilitoa leseni za usafi 112,457 kwa magari ya abiria na mizigo ikilinganishwa na leseni 103,739 zilizotolewa kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Ongezeko hilo la leseni ni sawa na asilimia 8.

***113. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa ushiriki wa sekta binafsi katika kuboresha miundombinu ya uchukuzi na kutoahudumazausafiriwaabiriakatikamijinamajiji. Tunaishukurusektabinafsikwamwitikiomzurikatika utoaji wa huduma za usafiri kwa njia ya barabara.

***114. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kuboresha utoaji wa huduma za usafiri wa abiria katika majiji na miji mikubwa nchini. Kazi ya kufanya tathmini kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari barabarani (Road Traffic Congestion) katika majiji

ya Dar es Salaam na Mwanza ilikamilika Desemba, 2017. Tathmini hiyo ilipendekeza kuwe na Mfumo wa Mipango Miji wa muda mrefu unaoendana na mahitaji ya usafiri mijini; kuboresha miundombinu ya barabara; na kubuni mbinu za kupunguza matumizi ya magari binafsi, kutumia njia (mode) nyingine za usafiri na kuyaondoa mabasi yanayobeba abiria wachache. Mapendekezo ya taarifa hii yatawasilishwa kwa wadau kabla ya kuanza utekelezaji wake.

***115. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, SUMATRA imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuimarisha usalama na ubora wa huduma za uchukuzi kwa njia ya barabara. Hatua hizo ni pamoja na kukamilisha usimikaji wa mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa mabasi ya masafa marefu (Vehicle Tracking System- VTS). Usimikaji wa Mfumo huu ulikamilika Desemba, 2017. Aidha, mfumo huu wenye lengo la kuimarisha udhibiti wa mwendokasi wa mabasi ya abiria hadi sasa umeshafungwa katika mabasi 446. Taratibu za kupanua matumizi ya mfumo huu nchini zinaendelea.

***116. Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza idadi ya ajali za barabarani nchini, SUMATRA imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa magari ya abiria na mizigo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani. Kutokana na juhudi hizo, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, idadi ya malori ambayo yalihusika katika ajali ilishuka kwa asilimia 29.3 kutoka malori 669 hadi malori 473 sawa na asilimia 29.3. Aidha, katika kipindi hicho idadi ya mabasi yaliyohusika katika ajali ilishuka kutoka mabasi 893 hadi mabasi 599 sawa na asilimia 32.9.

## USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA RELI

***117. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, huduma za usafiri kwa njia ya reli zimeendelea kutolewa na Shirika la Reli Tanzania na Mamlaka ya Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA). Aidha, SUMATRA imeendelea kudhibiti na kusimamia usalama na ubora wa huduma za reli nchini kwa kufanya ukaguzi katika njia za reli za TRC na TAZARA pamoja na kugharamia mafunzo ya wafanyakazi 60 yanayohusu

usalama wa usafiri wa njia ya reli kutoka TRL na TAZARA. Lengo la mafunzo haya ni kuimarisha kiwango cha usalama wa huduma za usafiri wa reli nchini.

**Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam**

***118. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari barabarani. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya abiria 5,448,764 (sawa na dala dala 673 zinazochukua abiria 30 kwa siku katika kipindi hicho) walisafirishwa kwa njia ya reli kati ya katikati ya Jiji la Dar es Salaam na Mwakanga kwa kutumia reli za TAZARA na TRC. Aidha, jumla ya abiria 920,479 walisafirishwa kati ya stesheni ya Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa. Miundombinu ya reli iliyopo iliendelea kuboreshwa kwa kujenga mchepuo wa njia ya reli kutoka "Ilala block post" hadi Stesheni ili kuepusha mwingiliano wa treni ya abiria kutoka Stesheni kwenda Ubungo na ile ya mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam. Uboreshaji wa huduma za usafiri kwa njia ya treni umesaidia kupunguza tatizo la msongamano wa magari katika maeneo ambayo usafiri huo unapatikana.

***119. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TRC inaendelea kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/ Kibaha na Bunju/ Kerege. Upembuzi huu unatarajiwa kukamilika Desemba, 2018. Aidha, Japan kupitia Shirika lake la JICA inaendelea kuandaa Mpango Kabambe wa Usafiri Jijini Dar es Salaam (Dar es Salaam Urban Transport Masterplan) ambao unajumuisha usafiri kwa njia ya barabara, reli na maji. Mpango huo wa miaka 30 unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa 2018.

**SHIRIKA LA RELI TANZANIA (TRC)**

**Miundombinu ya Reli ya TRC**

***120. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali kupitia TRC imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Reli ya

*Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kuanza na sehemu ya Dar es Salaam – Morogoro (km 205) na Morogoro Makutupora (km 422). Kwa sehemu ya Dar es Salaam – Morogoro, utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2019. Kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na:

i. Ujenzi wa kambi ya Mkandarasi ya Dar es Salaam umekamilika kwa asilimia 99, Soga asilimia 89 na Ngerengere asilimia 67;

ii. Upimaji wa ardhi itakapopita njia ya reli (Topographical Survey) umekamilika kwa asilimia 95;

iii. Njia kwa ajili ya kuhudumia Mradi (kupitisha watu, mitambo na vifaa vya ujenzi) imekamilika kwa asilimia 83;

iv. Jumla ya vifaa kwa ajili ya ujenzi (mitambo na magari) 755 vimeshawasili kwa ajili ya kazi;

v. Kazi ya kusafisha eneo la mradi imekamilika kwa asilimia 59.1;

vi. Utafiti wa Ardhi itakayobeba misingi ya madaraja pamoja na makalvati ya kuvukia watu, wanyama na baiskeli umekamilika kwa asilimia 10; na

vii. Kazi ya ujenzi wa tuta la reli imekamilika kwa asilimia 15.

***121. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* kwa sehemu ya pili inayoanzia Morogoro hadi Makutupora yenye jumla ya urefu wa kilomita 422 (km 336 njia kuu na km 86 njia za kupishania treni) unaendelea vizuri. Mkataba wa ujenzi kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga (Design and Build) ulisainiwa Septemba, 2017 kati ya RAHCO na Kampuni ya Yapi Merkezi ya Uturuki. Mhandisi Mshauri wa mradi huu ni muungano (JV) wa makampuni manane unaoongozwa na Kampuni ya KORAIL ya Korea. Aidha, jiwe la msingi la ujenzi wa sehemu hii ya reli liliwekwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John

Pombe Joseph Magufuli tarehe 14 Machi, 2018. Mradi wa ujenzi wa reli ya Morogoro - Makutupora unatarajiwa kukamilika Desemba, 2020.

***122. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* kwa sehemu za Makutupora – Tabora (km 295), Tabora – Isaka (km 133), Isaka - Mwanza (km 250), Tabora – Uvinza – Kigoma na Kaliua – Mpanda - Karema, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha. Nchi kama vile China, Korea, Ujerumani, Ufaransa, India, Marekani, Nigeria, Ureno na Uingereza zimeonesha nia ya kushiriki katika ujenzi huo. Aidha, Zabuni kwa ajili ya kununua treni na mitambo itakayotumika kutoa huduma ya usafiri kwenye reli ya *Standard Gauge* ilifunguliwa Februari, 2018 na tathmini inaendelea.

***123. Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua umuhimu wa Reli ya Kati iliyopo sasa kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri kwa abiria na uchukuzi wa mizigo na kuendelea kusafirisha mitambo na vifaa kwa ajili ya ujenzi wa reli ya *standard gauge* inayojengwa sasa. Kwa kutambua umuhimu huo, maandalizi ya kuanza kazi ya kukarabati miundombinu ya Reli ya Kati kupitia mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Reli (Tanzania Intermodal and Rail Development Project - TIRP) unaogharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia yanaendelea. Mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ukarabati wa eneo la Dar es Salaam hadi Kilosa (km 283) na sehemu ya pili ni Kilosa hadi Isaka (km 687).
TaarifayaTathmini yazabuniya kumpata mkandarasi wa ukarabati kwa sehemu ya Dar es Salaam - Kilosa imekamilika na mkandarasi amepatikana ili kuanza ukarabati wa sehemu hiyo kwa kuondoa reli nyepesi ya ratili 60 kwa yadi na kutandika reli na mataruma mapya ya ratili 80 kwa yadi. Kuhusu sehemu ya Kilosa- Isaka, taarifa ya tathmini ya zabuni za kumpata mkandarasi imewasilishwa Benki ya Dunia Machi, 2018 ili kupata ridhaa.

***124. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa katika mwaka 2017/2018 ni pamoja na:

i. Kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Arusha hadi Musoma (km 600) kwa *standard gauge* pamoja na kuunganisha na reli ya Tabora-Mwanza (km 120), tawi kuelekea Engaruka (km 53), tawi kuelekea Minjingu (km 35) na tawi kuelekea Dutwa (km 2.8). Kazi hii inategemewa kukamilika Desemba, 2018;

ii. Kuendelea na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya Mpanda - Karema (km 150) kwa *Standard gauge.* Kazi hii inategemewa kukamilika Desemba, 2018;

iii. Kuendelea na usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora - Kigoma na Kaliua – Mpanda. Kazi hii inategemewa kukamilika Septemba, 2018;

iv. Kuendelea na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Uvinza - Musongati (Burundi) yenye urefu wa km 200 kwa *standard gauge.* Kazi hii inategemewa kukamilika Septemba, 2018; na

v. Kuendelea na uboreshaji wa eneo la treni la kupakia/ kupakua mizigo katika bandari ya Dar es Salaam, pamoja na kukarabati vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka. Kazi hii inategemewa kukamilika Desemba, 2018.

**Huduma za Usafiri wa Reli ya TRC**

***125. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya tani 276,769 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 217,331 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la asilimia 27. Kuhusu usafirishaji wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, abiria wa masafa marefu 380,578 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 469,922 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Huu ni upungufu wa asilimia 19. Sababu za upungufu huu ni pamoja na kusitisha huduma zinazoanzia Dar es salaam badala yake zilianzia Dodoma katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, 2018 kutokana na reli kuharibiwa na mafuriko katika maeneo ya Kilosa na Gulwe.

***126. Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizokamilika katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni pamoja na:

i. Ukarabati wa mabehewa ya mizigo 107 na mabehewa ya abiria 20;

ii. Ukarabati wa njia ya reli ya Korogwe – Mombo – Buiko (km 91). Kukamilika kwa ukarabati wa reli ya Tanga – Arusha kutasaidia kusafirisha shehena ya saruji kutoka Tanga Cement, mafuta kutoka kampuni ya GBP ya Tanga na mizigo mbalimbali toka bandari ya Tanga;

iii. Ukarabati wa injini moja ya treni (steam engine). Ufufuaji wa injini hii utasaidia kukuza shughuli za utalii wa ndani;

iv. Matengenezo makubwa ya daraja km 209/7 lililoko Mazimbu, Morogoro;

v. Ukarabati wa makalvati 2 katika njia ya reli maeneo ya Mnyusi na Muheza; na

vi. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kuelekea Bandari Kavu katika eneo la Kwala, Kibaha.

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

***127. Mheshimiwa Spika,*** Serikali za Tanzania na Zambia zimeendelea kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za reli ya TAZARA. Uboreshaji huo ulihusu kufanya matengenezo makubwa ya njia kwenye sehemu zilizowekewa katazo la mwendo kasi (Speed Restriction) ya treni kutoka maeneo 48 yenye jumla ya urefu wa kilometa 150 hadi maeneo 22 yenye jumla ya urefu wa kilometa 59.8. Lengo ni kutokuwa na maeneo kama hayo kabisa. Kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 ni pamoja na ukarabati wa vichwa vya treni 2; mabehewa ya mizigo 78; mabehewa ya abiria 5; mabehewa ya kokoto 84; mabehewa ya kusafirishia makasha 11 na kiberenge 1. Aidha, ukarabati wa madaraja matatu ya Ruipa, Mbalizi na Idiga pia ulikamilika.

***128. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali iliendelea kuboresha huduma za usafiri wa reli ya TAZARA. Hadi Machi, 2018, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa *Traction Motors* 42 pamoja na mitambo (Dumper Truck, Excavator and Drill Rig) kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo ilikuwa imetangazwa na mkandarasi kupatikana. Mkataba kati ya TAZARA na mkandarasi unapitiwa na unatarajiwa kusainiwa mwanzoni mwa Mei, 2018. Serikali imetoa Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

***129. Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa miundombinu, vitendea kazi na huduma za TAZARA umesaidia kupunguza muda wa kusafirisha mizigo kati ya Dar es Salaam na New Kapiri Mposhi kutoka wastani wa siku 8.5 mwaka 2016/2017 mpaka wastani wa siku 6.5 hadi kufikia Machi, 2018. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, TAZARA ilisafirisha tani 173,000 za mizigo ikilinganishwa na tani 124,393 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Utendaji huu ni ongezeko la asilimia 28. Kwa upande wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, TAZARA ilisafirisha abiria wa njia kuu 404,238 ikilinganishwa na abiria 372,060 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Utendaji huu ni ongezeko la asilimia 8.

Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, huduma za usafiri wa abiria wa treni ya TAZARA inayotoa huduma kati ya Kidatu na Makambako (km 365) (maarufu kama treni ya Udzungwa), ilisafirisha abiria 287,487 ikilinganishwa na abiria 196,370 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Utendaji huu ni ongezeko la asilimia 32.

***130. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na TAZARA imeendelea kuweka mikakati mbalimbali ili kuongeza umiliki wake katika soko (market share) la usafirishaji wa shehena na kuhimili ushindani. Mikakati hiyo ni pamoja na kuweka bei ya usafirishaji wa shehena ya mizigo yenye ushindani katika soko lakini yenye tija kwa TAZARA. Biashara ya sasa ni ya ushindani hivyo kwa kiwango kikubwa shehena ya mzigo husafirishwa kwa kuzingatia bei ya nguvu ya soko. TAZARA nayo imeanza kuzingatia nguvu ya

soko katika kupanga bei zake kusafirisha shehena ya mizigo. Mkakati huu umesaidia kuongezeka kwa shehena ya mzigo hususan shaba kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia. Aidha, TAZARA imeanza kurudisha imani kwa wateja wa mizigo iliyokuwa inasafirishwa kupitia bandari nyingine ambazo ni shindani za Bandari ya Dar es Salaam na wale waliokuwa wanasafirisha kwa kutumia malori kwa umbali mrefu.

***131. Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeanza kutekeleza mpango wa kuzalisha umeme katika Maporomoko ya Maji ya Mto Rufiji, yafahamikayo pia kama *Stiegler's Gorge*. Lengo la mradi huu ni kuzalisha umeme utakaotosheleza katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa umeme katika viwanda vilivyopo na vinavyotarajiwa kujengwa. Kwa kutambua umuhimu huo na wajibu wa sekta ya uchukuzi katika kuwezesha miradi mingine ya maendeleo kutekelezeka kirahisi, TAZARA imeanza taratibu za kuboresha kituo cha reli cha Fuga/Kisaki ili kiweze kutoa huduma za usafirishaji wa mizigo na mitambo ya ujenzi wa mradi huu.

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Majini**

***132. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kudhibiti huduma za usafiri wa majini nchini. Aidha, SUMATRA imeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Bahari Zanzibar (Zanzibar Maritime Authority - ZMA) katika ukaguzi na uhakiki wa ubora wa vyombo vya usafiri majini, taratibu za utafutaji na uokoaji, kubadilishana taarifa muhimu zinazohusu usalama wa vyombo vya usafiri majini na uhifadhi wa mazingira ya bahari. Ili kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri majini, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, SUMATRA imefanya ukaguzi wa vyombo vikubwa vya usafiri majini ambapo jumla ya kaguzi 97 zilifanyika. Vilevile, SUMATRA ilifanya ukaguzi wa vyombo vidogo vya usafiri majini, ambapo jumla ya vyombo 2,903 vilikaguliwa na vyombo 2,132 sawa na asilimia 73 vilipewa leseni ya kuendelea kutoa huduma. Wamiliki wa vyombo vilivyobakia walipewa maelekezo kuhusu marekebisho yanayopaswa kufanywa kabla ya leseni kutolewa. Upungufu ambao ulijitokeza zaidi katika kaguzi za

vyombo vidogo ni pamoja na kushindwa kushusha nanga, kukosekana kwa majaketi ya uokozi na vifaa vya mawasiliano kama *VHF Radio.*

***133. Mheshimiwa Spika,*** SUMATRA pia imekuwa ikifanya mikutano ya usalama wa usafiri majini kwa kujumuisha wadau katika maeneo mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya mikutano 144 ilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Baadhi ya maeneo ambayo mikutano hii ilifanyika ni pamoja na Dar es Salaam, Lindi, Pwani, Tanga, Mwanza, Ukerewe, Kagera, Mara, Rukwa na Geita.

## HUDUMA ZA USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI

***134. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, ubora, usalama na uendelezaji wa miundomiunu na huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji zimeendelea kutekelezwa na Wizara kupitia taasisi zake za Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP), Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) pamoja na sekta binafsi. Aidha, huduma za bandari zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na sekta binafsi.

### Huduma za Uchukuzi Baharini

***135. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, uchukuzi wa masafa marefu baharini umeendelea kutolewa na SINOTASHIP. Kampuni hii imeendelea kutoa huduma zake kwa kutumia meli kubwa moja yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa wakati mmoja. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, SINOTASHIP ilisafirisha tani 580,000 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na tani 490,000 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la asilimia 18 ya mizigo iliyosafirishwa. Ongezeko hili linatokana na Meli ya *Mv Changshun II* kukodishwa kwa mkataba wa miaka 8. Aidha, kuhusu ununuzi wa meli nyingine, SINOTASHIP inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kununua au kukodi meli za mizigo ili kushiriki kikamilifu katika

fursa zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na kusafirishia gesi (LNG) ya Tanzania kwa ajili ya soko la ndani au la nje.

***136. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, SINOTASHIP imeendelea kutoa huduma za uwakala wa kuondoa mizigo bandarini katika bandari za Dar es Salaam na Mombasa. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya makasha 20,880 yalihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na lengo la kuhudumia makasha 11,400.

**Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa**

***137. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imeendelea kutoa huduma za usafiri majini kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, huduma za Kampuni ya MSCL zilipungua kwa ajili ya uharibifu wa meli. Upungufu huo unatokana na kusimama kutoa huduma kwa meli za MV. Clarias, MV. Serengeti, MV. Liemba, MV.Umoja, MT. Sangara na MV. Songea.

***138. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi bilioni 24.496 kwa ajili ya kununua meli mpya mbili (2) na kukarabati meli tano (5). Hadi kufikia Desemba, 2017, Serikali ilikuwa imetoa fedha hizo kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Tanganyika zimefunguliwa tarehe 18 Aprili 2018 na kazi ya uchambuzi inaendelea. Matarajio ni kumpata mkandarasi mwaka huu wa 2018. Kuhusu ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria, taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea na mkataba utasainiwa mwaka huu wa 2018.

***139. Mheshimiwa Spika***, kuhusu ukarabati wa meli za MV. Victoria na MV. Butiama, Mkandarasi Kampuni ya *M/S KTMI in Joint Venture with Yuko's Enterprises Co. Ltd* kutoka Korea anatarajiwa kusaini mkataba mwaka huu wa 2018. Kwa upande wa ukarabati wa meli ya MV. Liemba, taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea baada ya Kampuni iliyokuwa imeshinda zabuni hiyo (M/S Leda shipyard kutoka Croatia) kushindwa kufaulu katika hatua ya upekuzi. Taratibu

za kufanya uchambuzi wa Kampuni ya pili kwa ushindi (M/S JGH Marine kutoka Denmark) zinaendelea.

***140. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia ujenzi wa meli moja mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa. Meli hii inajengwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kwa gharama ya Shilingi bilioni 9.119. Aidha, Wizara kupitia TPA na MSCL inaangalia utaratibu mzuri wa uendeshaji wa meli hii kwa lengo la kuboresha huduma za usafirishaji wa mizigo na abiria katika Ziwa Nyasa. Ujenzi wa meli hii unatarajiwa kukamilika Juni, 2018.

***141. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, MSCL ilikamilisha kazi zifuatazo:

i. Matengenezo ya meli ya abiria na mizigo ya MV. Clarias yalikamilika Desemba, 2017. Meli hiyo imeanza kutoa huduma ya usafiri kati ya miji ya Mwanza na Nansio-Ukerewe Desemba, 2017;

ii. Matengenezo ya meli ya kubeba mafuta ya MT. Sangara iliyoko Ziwa Tanganyika. Meli hiyo ilianza kufanya safari zake Novemba, 2017;

iii. Matengenezo ya meli ndogo ya mizigo ya ML. Wimbi iliyoko Ziwa Victoria; na

iv. Ufungaji wa mfumo wa kielektroniki wa kukata tiketi za abiria. Mfumo huu ambao umefungwa kwa ushirikiano kati ya MSCL na Wakala ya Serikali Mtandao umezinduliwa rasmi Februari, 2018.

**Huduma za Bandari**

***142. Mheshimiwa Spika,*** Bandari ni moja ya sekta muhimu nchini ambayo huchochea ukuaji wa biashara, uchumi, maendeleo ya sekta nyingine na ustawi wa Taifa kwa ujumla. Bandari ni lango kuu la biashara kati ya nchi yetu na nchi nyingine zikiwemo nchi jirani za Zambia, Malawi, Burundi,

Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda. Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya biashara zote nchini husafirishwa nje ya nchi na kuingizwa nchini kupitia bandari. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda na kutoka katika nchi hizo za jirani ilikuwa tani milioni 3.9 ikilinganishwa na tani milioni 3.1 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 23. Ongezeko hili la shehena kwa kiasi kikubwa limechangiwa na uboreshaji wa huduma, uimarishaji wa usalama wa mizigo na kufanya kazi kwa saa 24 siku saba kwa juma.

***143. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilihudumia jumla ya tani milioni 9.822 za shehena za mizigo ikilinganishwa na tani milioni 8.572 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Utendaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia 14.6. Katika shehena hiyo iliyohudumiwa, bandari ya Dar es Salaam ilihudumia tani milioni 8.988 za shehena na bandari nyingine tani milioni 0.834. Aidha, Kitengo cha Makasha cha Bandari ya Dar es Salaam kilihudumia makasha 84,309 ikilinganishwa na makasha 106,448 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Huu ni sawa na upungufu wa asilimia 21. Sababu za makasha yaliyohudumiwa na Mamlaka kupungua ni pamoja na baadhi ya wateja wenye meli kubwa na zinazohitaji kina kirefu cha maji (Kampuni za meli za PIL na MSC) kuhamishia huduma zao katika kitengo cha TICTS kutokana na magati ya kitengo cha shehena ya kawaida yanayohudumiwa na TPA kuwa na kina kifupi cha maji.

***144. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Kitengo cha Makasha (TICTS) kilihudumia makasha 351,344 ikilinganishwa na makasha 317,507 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Utendaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia 11. Ongezeko la shehena linatokana na kuondolewa kwa utaratibu wa mfumo wa forodha kati ya Tanzania na DRC (single customs territory), kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa shehena ya mizigo ya nchi jirani; mikakati ya TPA kujitangaza kimasoko

na biashara kwa wateja wa ndani na nje kutumia bandari za Tanzania, kuongezeka kwa meli kubwa na kuongezeka kwa ufanisi wa bandari katika kutoa huduma kwa wateja.

***145. Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari umeendelea kukua mwaka hadi mwaka licha ya ushindani kutoka bandari nyingine. Viashiria vya utendaji wa Mamlaka vimeendelea kuonesha kuwa muda wa makasha kukaa bandarini (dwell time) umepungua kutoka wastani wa siku 11.5 Desemba, 2016 hadi wastani wa siku 9.6 katika mwezi Februari, 2018. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini (shipturnround time) umepungua kutoka wastani wa siku 2.4 mwaka 2016/2017 hadi wastani wa siku 2 mwaka 2017/2018.

***146. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha miundombinu na huduma za bandari ili kuimarisha utendaji wake. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:

i. Kukamilisha ujenzi wa Jengo la kuwaweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam (One Stop Center). Jengo hili limeanza kutumika Machi, 2018;

ii. Kukamilisha kazi ya kuvunja na kujenga upya ghala Na. 2 na Na. 3 katika Bandari ya Dar es Salaam. Ujenzi wa ghala Na. 2 ulikamilika Januari, 2018 na ule wa ghala Na. 3 ulikamilika Julai, 2017;

iii. Kazi ya kumpata Mkandarasi atakayenunua na kufunga mita mpya za kupima mafuta wakati wa kupakua kutoka kwenye meli (flow meters) kwa ajili ya bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara imekamilika. Kazi inayoendelea sasa ni kumfanyia upekuzi (due deligence) mkandarasi aliyepatikana;

iv. Kuendelea na upanuzi wa Bandari ya Mtwara kwa kujenga gati moja lenye urefu wa mita 300. Ujenzi wa gati hili umekamilika kwa asilimia 20 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2019;

v. Kuanza ujenzi wa gati la Nyamisati. Ujenzi wa mradi huu utaanza baada ya kukamilisha majadiliano na Mkandarasi kuhusu uboreshaji wa baadhi ya vipengele vya Mkataba. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza Mei, 2018 na kukamilika Juni, 2020;

vi. Kukamilisha ujenzi wa gati la Pangani, ujenzi huu ulikamilika Septemba, 2017;

vii. Kuendelea na ukarabati wa gati la Lindi, ukarabati huo umekamilika kwa asilimia 90;

viii. Kuendelea na ujenzi wa gati la Ndumbi katika Ziwa Nyasa, ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 30;

ix. Kuendelea na ujenzi wa gati za Nyamirembe na Magarine katika Ziwa Victoria. Kazi za ujenzi zimeanza Februari, 2018 na zinatarajiwa kukamilika Juni, 2020;

x. Kukamilisha kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati la Karema, Kigoma ili kuunganishwa na Bandari ya Kalemie, DRC. Upembuzi huu ulikamilika Machi, 2018;

xi. Kuendelea na ujenzi wa gati la Kalya/Sibwesa katika Ziwa Tanganyika. Ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 90;
xii. Kuendelea na ujenzi wa gati la Kibirizi katika Ziwa Tanganyika. Ujenzi wa gati hili umekamilika kwa asilimia 20 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2020;

xiii. Kuendelea na ujenzi wa gati la Lagosa katika Ziwa Tanganyika. Ujenzi wa gati hili umekamilika kwa asilimia 75 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2018; na

xiv. Kuendelea na ujenzi wa gati la Kabwe katika Ziwa Tanganyika. Ujenzi wa gati hili umekamilika kwa asilimia 20 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2020.

***147. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa bandari ya Dar es Salaam wa kuboresha na kuongeza kina katika gati Na. 1 hadi 7, kujenga gati jipya la kushushia magari eneo la Gerezani Creek na kupanua na kuongeza kina cha lango la

kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli, Mkandarasi Kampuni ya *China Harbour Engineering and Construction Company* (CRCC) alipatikana Juni, 2017. Aidha, jiwe la msingi kuashiria kuanza kazi liliweka na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Julai, 2017. Kazi ya uboreshaji wa gati Na. 1-7 na ujenzi wa gati jipya la kushushia magariinatarajiwa kukamilika Juni, 2020.

***148. Mheshimiwa Spika,*** kazi za utekelezaji wa Mradi wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam zinaendelea vizuri. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kukamilisha ujenzi wa makazi ya wahandisi, maabara ya ujenzi na kuleta mashine za ujenzi;

(ii) Kuendelea na tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na tafiti za udongo (geotechnical surveys) kwa ajili ya kufanya usanifu wa mradi. Hadi sasa, tafiti na usanifu kwa gati la kuhudumia meli za magari (RoRo berth) zimekamilika na usanifu wa Gati Na. 1 – 3 unaendelea; na

(iii) Kazi ya ujenzi wa gati la kuhudumia meli za magari katika eneo la Gerezani Creek imeanza kwa kujaza kifusi.

***149. Mheshimiwa Spika,*** kazi ya kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Dar es Salaam inatarajiwa kuanza Januari, 2019. Kazi ya kufanya uchambuzi wa zabuni ya awali (Expression of Interest) imekamilika. Hatua ya pili ya zabuni (Request for proposal - RFP) itafanyika baada ya kukamilika kwa *geotechnical surveys, environmental and social impact assessment* na *detailed design*. Kazi hizi zimeanza Februari, 2018.

***150. Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa bandari ya Mbegani, Bagamoyo ni moja ya vipaumbele vya Serikali katika kuboresha huduma za bandari nchini. Majadiliano kati ya Serikali na wawekezaji (Kampuni ya *China Merchants Holdings International Limited* (CMHI) na Mfuko wa Uwekezaji wa Oman (State Reserve Fund) kuhusu Vipengele vya Mikataba

ya Mradi yapo katika hatua za mwisho. Majadiliano haya yamechukua muda mrefu kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. Majadiliano hayo yanatarajiwa kukamilika na mkataba kusainiwa Juni, 2018.

***151. Mheshimiwa Spika,*** kazi ya kuhuisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya Mwambani kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango (Kitengo cha PPP) ilianza Februari, 2018. Mara baada ya kazi hiyo kukamilika, Serikali itaendelea kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari hiyo. Aidha, kuhusu maandalizi kwa ajili ya kujenga gati la Chongoleani (Tanga) litakalopokea mafuta kutoka Uganda, majadiliano baina ya Tanzania na Uganda pamoja na kampuni inayohusika na ujenzi huo yapo katika hatua za mwisho.

## USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

### Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga

***152. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imeendelea kuhakikisha kuwa viwanja vya ndege nchini vinakidhi masharti na kanuni zilizowekwa ili kuimarisha na kuboresha huduma za usafiri wa anga. Katika mwaka 2017/2018, viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere (JNIA), Amani Abedi Karume na Kilimanjaro (KIA) vilikaguliwa na kupata vyeti vya ubora kulingana na matakwa ya vigezo vya kimataifa vya viwanja vya ndege. Aidha, viwanja vya ndege vya Nachingwea, Iringa, Tanga, Dodoma, Tabora, Mpanda, Sumbawanga, Songwe, Shinyanga, Mwanza, Musoma na Kigoma pia vilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora.

***153. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini imeendelea kuhakikisha kuwa matukio ya ajali katika usafiri wa anga yanapungua. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, matukio 3 na ajali 5 za ndege zilitokea. Ajali hizo zilisababisha vifo vya watu 12 ambapo ajali 3 kati ya 5 zilitokana na hali mbaya ya hewa. Aidha, Mamlaka ilitoa mafunzo elekezi kuhusu usalama wa usafiri wa anga kwa

wadau 239 kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), TANAPA, na sekta binafsi Lengo lilikuwa ni kuwakumbusha na kuwajengea uwezo na stadi zaidi katika kazi zao za kila siku. Mafunzo haya yalifanyika katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza na Zanzibar.

***154. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imesaini Mkataba wa kununua na kusimika rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia. Mkataba wa mradi huu wenye thamani ya Shilingi bilioni 67.3 ulisainiwa Agosti, 2017 ambapo Serikali inachangia asilimia 55 (Shilingi bilioni 35.1) na TCAA inachangia asilimia 45 (Shilingi bilioni 32.2) ya gharama hiyo. Rada hizi zitakazosaidia kudhibiti na kuimarisha usalama wa usafiri wa anga nchini zitafungwa katika viwanja vya ndege vya JNIA, Mwanza, Kilimanjaro na Songwe. Jiwe la msingi la ujenzi wa usimikaji wa mfumo wa rada hizo liliwekwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 2 Aprili, 2018. Mradi huu utakamilika Machi, 2019. Aidha, Mkataba wa kazi ya kufanya ukarabati wa mnara wa kuongozea ndege katika kituo cha Pemba ulisainiwa Oktoba, 2017 na kazi hii inatarajiwa kukamilika Mei, 2018.

***155. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga iliongezeka hadi kufikia abiria 4,950,994 kutoka abiria 4,725,094 waliotumia usafiri huo mwaka 2016/2017. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 4.8. Kwa abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi, katika kipindi hicho, jumla ya abiria 2,261,528 walisafiri ikilinganishwa na abiria 2,070,949 waliosafiri katika kipindi hicho mwaka 2016/2017. Aidha, abiria wa ndani wameongezeka kutoka abiria 2,786,852 mwaka 2016/2017 hadi kufikia abiria 2,926,195 mwaka 2017/2018. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Kwa upande wa safari za ndege (aircraft movements), kuna ongezeko la asilimia 3.2 kutoka safari 238,515 za mwaka 2016/2017 hadi safari 246,072 kwa mwaka 2017/2018. Sababu za ongezeko katika utoaji wa huduma hizi ni pamoja na kusainiwa kwa mikataba ya usafiri

wa anga kati ya Tanzania na nchi nyingine (Bilateral Air Services Agreements - BASA); uimarishaji wa miundombinu na huduma za viwanja vya ndege; uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Julius Nyerere (JNIA); kufufuliwa kwa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL); na ukuaji wa uchumi na shughuli za utalii nchini.

***156. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, mizigo iliyosafirishwa kwenda na kutoka nje ya nchi ilifikia tani 24,574.4 ikilinganishwa na tani 23,743.3 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hili ni ongezeko la asilimia 3.5. Ongezeko hili linatokana na kukua kwa shughuli za kibiashara na kiuchumi ndani na nje ya nchi.

***157. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupitia upya Mikataba ya Usafiri wa Anga kati ya Tanzania na nchi nyingine (Bilateral Air Services Agreements – BASA) ili kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya soko na hali halisi ya maendeleo na mabadiliko katika usafiri wa anga. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Tanzania ilisaini mikataba mipya na nchi za New Zealand, Finland na Japan. Aidha, mikataba ya nchi za India, Israel, Zambia, Uturuki, Oman, Sri Lanka, Marekani, Switzerland, Jordan, Qatar, Saudi Arabia na Italy ilipitiwa upya. Kusainiwa kwa mikataba kumeifanya Tanzania kuwa na mikataba ya usafiri wa anga (BASA) na nchi 70 ikilinganishwa na nchi 67 za mwaka 2016/2017. Hadi Machi, 2018, Mashirika ya ndege ya kimataifa ya ndani na nje ya nchi yapatayo 31 yalikuwa yanatoa huduma za usafiri wa anga kwa utaratibu wa BASA. Safari za ndege kati ya nchi hizo na Tanzania zilikuwa 176 kwa juma.

***158. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa Mfuko wa Mafunzo kwa marubani na wahandisi wa ndege. Pamoja na uhaba wa fedha za kutunisha Mfuko huu, marubani wa ndege watano (5) wamegharamiwa kupitia Mfuko huo. Aidha, uchambuzi wa majina ya wanafunzi waliotimiza vigezo vya ufadhili unaendelea ili kuwawezesha kuanza masomo Oktoba, 2018 nchini Ethiopia. Mamlaka ya Usafiri wa Anga inaendelea

kushirikiana na vyuo vya ndani ya nchi kama vile Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuhakikisha kuwa mafunzo zaidi yanatolewa nchini ili kuweza kupata wataalam wengi zaidi.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

***159. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea kuboresha miundombinu na huduma za viwanja vya ndege nchini kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na taratibu ili kuviwezesha viwanja hivyo kuvutia mashirika mengi ya ndege nchini. Lengo ni kuongeza ushindani na kupunguza gharama za usafiri wa Anga nchini.

***160. Mheshimiwa Spika,*** Kiwanja cha Ndege cha Songwe ni kitovu cha usafiri wa anga katika ukanda wa nyanda za juu kusini pamoja na nchi zilizo katika ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Mkandarasi wa kusimika mfumo wa taa za kuongozea ndege (Airfield Ground Lighting) ili kuboresha huduma za kiwanja hicho amepatikana na kazi inatarajiwa kuanza Juni, 2018.

***161. Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea na jitihada za kuimarisha na kuboresha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini, katika mwaka 2017/2018, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea kununua mitambo ya ukaguzi. Mitambo hiyo ni pamoja na mashine za X-Ray kwa ajili ya ukaguzi wa abiria na mizigo kwa viwanja vya ndege vya JNIA (3), Mwanza (2), Dodoma (1), na Songea (1). Aidha, ujenzi wa uzio wa usalama kwa viwanja vya ndege umefanyika kwa viwanja vya Dodoma, Moshi, Lake Manyara, Bukoba na Tabora.

***162. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilinunua gari la Zimamoto moja na ununuzi wa magari ya zimamoto mengine sita (6) kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha usalama na huduma za Uokoaji na Zimamoto viwanjani unaendelea. Uandaaji wa programu za usalama katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Songwe, Bukoba, Shinyanga, Musoma, Tanga, Arusha, Iringa, Dodoma, Songea,

Kigoma, Lake Manyara, Mafia na Tabora ulikamilika na kuanza kutumika. Lengo la programu hizi ni kuinua kiwango cha usalama katika viwanja vya ndege na kuongeza weledi wa watumishi waliopo katika viwanja hivyo ili kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya kiteknolojia, kiuchumi na kijamii Duniani.

## Huduma za Usafiri wa Anga

***163. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) pamoja na Kampuni za sekta binafsi kama *Precision Air, Fastjet, Auric* na Coastal zimeendelea kutoa huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi.

***164. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, ATCL imeendelea kuonesha mwelekeo chanya katika utekelezaji wa mpango wa kuifufua na kuendelea kuchangia uboreshaji wa huduma za usafiri wa anga nchini. Aidha, ATCL ilitoa huduma katika vituo vya Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Songea, Tabora, Zanzibar na Hahaya (Comoro). Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Kampuni ilisafirisha abiria 156,518 ikilinganishwa na abiria 107,207 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 46. Ongezeko hili limeiwezesha Kampuni kuongeza mapato kutoka Shilingi bilioni 34.4 yaliyokusanywa mwaka 2016/2017 hadi Shilingi bilioni 43.8 katika mwaka 2017/2018.

***165. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) imeendelea kuongeza tija katika utendaji wake ambapo wastani wa kuruka umefikia saa (kumi) 10 kwa siku kutoka saa nane (8) katika mwaka 2016/2017. Aidha, uhakika wa ndege kuruka na kutua kwa wakati (On Time Performance) umeboreshwa kutoka wastani wa asilimia 82 mwaka 2016/2017 hadi wastani wa asilimia 83 katika mwaka 2017/2018.

***166. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Serikali ilipanga kupokea ndege nne (4). Ndege moja aina ya *Bombardier Q400* yenye uwezo wa kubeba abiria 76 imepokelewa nchini

tarehe 2 Aprili, 2018. Aidha, ndege moja aina ya *Boeing 787 Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262 na ndege mbili (2) aina ya *Bombardier CS 300* zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja zinatarajiwa kuwasili nchini mwaka huu wa 2018.

***167. Mheshimiwa Spika,*** ili ujio na uwepo wa ndege hizo uweze kuwa na tija hususan katika safari za kikanda na kimataifa, ATCL imeendelea kuajiri na kutoa mafunzo kwa watumishi wake. Kwa mwaka huu wa 2018, ATCL inatarajia kuwa imefundisha marubani 10 kwa ajili ya kutoa huduma kwa kutumia ndege aina ya *Dreamliner Boeing 7*87. Marubani wengine wapya 12 wanatarajiwa kuwa wamemaliza mafunzo kwa ajili ya ndege aina ya *Bombardier Q400* kupitia mkataba wa mafunzo ya marubani na mafundi wa ndege ulioingiwa baina ya ATCL na Shirika la Ndege la Ethiopia. Aidha, hadi Machi, 2018, ATCL imetoa mafunzo kwa marubani 16, wahandisi wa ndege 20 na wahudumu wa ndani ya ndege 22 kwa kuzingatia matakwa ya sheria za usafiri wa anga. ATCL inatarajia kuajiri wahudumu wengine wa ndege 84 kwa lengo la kuboresha huduma.

***168. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imeanza maandalizi ya kuweka mifumo muhimu ya uendeshaji wa biashara ya ndege kwa safari za nje ikiwemo kufanya upembuzi yakinifu wa mifumo ya TEHAMA inayotakiwa kusimikwa, kuchambua mashirikiano ya kibiashara tutakayoingia, na kuwianisha vigezo vya kujiunga na Mamlaka za Kimataifa zinazosimamia usafiri wa anga zikiwemo za *IATA, IATA Billing and Payment System, Global Distribution System (GDS), IATA Clearing House (ICH)* na *SITA*. Aidha, Serikali imeanza kurudisha mali za ATCL zilizokuwa zimekabidhiwa kwenye Mamlaka nyingine wakati ATCL ilipokuwa chini ya uendeshaji wa sekta binafsi. Hivi sasa jengo la matengenezo ya ndege (hangar) la KIMAFA lililopo Kiwanja cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) limekabidhiwa kwa ATCL ili kuipunguzia gharama za uendeshaji.

***169. Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) umeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kutumia ndege nne kutoa huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Katika mwaka 2017/2018, Wakala uliendelea kuzifanyia matengenezo stahiki ndege zake kulingana na sheria za usalama wa usafiri wa anga. Aidha, Wakala uliwapeleka mafunzoni marubani 6 na wahandisi 3 ambapo marubani 2 walipata mafunzo ya kuendesha ndege aina ya *Fokker 50;* Marubani 4 walipatiwa mafunzo ya kuendesha ndege aina ya *Gulfstream G550*; na Wahandisi 3 walipatiwa mafunzo ya kutengeneza ndege aina za *Fokker 28* na *Fokker 50*.

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA

***170. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kuboresha huduma za hali ya hewa ili kukidhi mahitaji ya wananchi na sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2017/2018, Wakala umeendelea kupata cheti cha utoaji wa huduma bora za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga kwa mujibu wa matakwa mapya ya Shirika la Viwango Duniani (ISO 9001:2015). Mafanikio hayo yameifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi tatu (3) katika Afrika kutimiza makubaliano ya Kimataifa kwa kutumia mfumo mpya wa ukaguzi wa viwango kabla ya Septemba, 2018. Nchi nyingine ni Nigeria na Afrika Kusini. Aidha, Tanzania imekuwa ni nchi pekee katika Afrika iliyotumia Wataalam wake wa ndani katika kufikia viwango hivyo na hatimaye kupata cheti cha ubora.

***171. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, kazi zilizokamilika ni pamoja na:

i. Kufunga mitambo mipya mitatu (3) inayojiendesha yenyewe katika maeneo ya Morogoro, Tanga na Pwani (Kibaha);

ii. Kukamilisha ukarabati wa vituo vya hali ya hewa vya Kizimbani (Zanzibar), Matanguani (Pemba) na Kigoma;

iii. Kuanza kutoa huduma za hali ya hewa katika bandari za Pemba, Dar es Salaam, Kigoma na Mwanza. Utoaji huduma huu umeendelea kuimarisha usalama wa vyombo vinavyotoa huduma za usafiri kwa njia ya maji, pamoja na kuongeza

ufanisi kwenye shughuli za kiuchumi zinazofanyika kwenye maziwa na bahari zikiwemo uvuvi, usafiri, biashara, na utafiti wa mafuta na gesi; na

iv. Kufunga mkongo wa Taifa katika vituo 11 vya hali ya hewa. Hatua hii imeongeza ufanisi katika utumaji wa *data* na taarifa za hali ya hewa.

***172. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wakala wa Hali ya Hewa umeendelea kubadili vifaa vya hali ya hewa vinavyotumia Zebaki ili kuendana na matakwa ya kimataifa. Jumla ya vifaa vitano (5) vinavyotumika kupima hali joto (thermometers) vilibadilishwa. Aidha, huduma za hali ya hewa ziliendelea kuwafikia watumiaji wengi zaidi hususan wakulima kwa njia za Simu za Mkononi (Farm SMS). Ujumbe huu umesaidia kutoa elimu na taarifa kwa Wakulima kuhusu matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa na vipindi vya hali ya hewa kulingana na maeneo yao.

***173. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kununua rada ya hali ya hewa. Maandalizi ya ununuzi wa rada hiyo ya tatu ya hali ya hewa nchini yanaendelea vizuri. Eneo kwa ajili ya kufunga rada hiyo limepatikana Mikindani, Mtwara. Wakala pia umeendelea kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri katika Bahari ya Hindi kwa kuanza kutoa huduma za hali ya hewa katika Bandari ya Mkoani, Pemba. Aidha, katika kulinda usalama wa binadamu na mazingira kutokana na matumizi ya kemikali ya zebaki (mercury), Wakala umebadilisha vifaa vitano(5) vinavyopima hali ya hewa vyenye vimiminika vya zebaki.

### C.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO Ukusanyaji wa Mapato

***174. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/2018, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Wizara kupitia TCRA imekusanya Jumla ya **Shilingi 20,011,862,803.58** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,295,824,157** zinatokana na asilimia 15 ya pato ghafi la Mamlaka ambazo zimepelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 8,716,038,646.58** ni kutokana na Mfumo wa TTMS. Kati

ya fedha za TTMS, kiasi cha **Shilingi 6,226,168,895.52** zilipelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kiasi cha **Shilingi 2,489,869,751.06** zilielekezwa katika Mfuko wa Utafiti na Maendeleo uliopo COSTECH. Vilevile, Sekta kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imechangia kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Dola za Kimarekani **4,890,647** sawa na **Shilingi 11,303,996,943.45** zilikusanywa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na kuhifadhiwa katika akaunti maalum ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

***175. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi 4,104,139,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,267,001,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,837,138,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2018 **Shilingi 2,654,824,061.00** zilikuwa zimetolewa na Hazina. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,231,647,319.00** zimetolewa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,423,176,742.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Bajeti ya Maendeleo**

***176. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa jumla ya **Shilingi 14,000,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Sehemu ya fedha hizo inatarajiwa kutolewa kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha.

**Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano**

***177. Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kuwa moja ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 Sekta ya Mawasiliano ilikuwa ya pili katika kuchangia ukuaji wa uchumi ambapo ilikua kwa asilimia 13.1 ikilinganishwa na asilimia 10.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Aidha, kuna ongezeko kubwa la huduma kwa wananchi

zinazotolewa na Serikali na pia sekta binafsi kupitia mawasiliano ya simu za kiganjani kama vile kutuma/kupokea pesa, kununua umeme, kulipia huduma za maji na ving'amuzi. Ni wazi huduma za mawasiliano zimechangia kurahisisha utendaji kazi na kuboresha maisha ya wananchi kijamiii, kiuchumi kutokana na kupata huduma mbalimbali kwa uwazi, urahisi, haraka na pasipo na ubaguzi. Vilevile, ukuaji wa sekta ya mawasiliano umesaidia Serikali kuimarisha ukusanyaji wa kodi na maduhuli kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

***178. Mheshimiwa Spika,*** idadi ya watumiaji wa intaneti waliongezeka kutoka 19,862,525 mwaka 2016 hadi kufikia 22,995,109 mwaka 2017. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 148 mwaka 2016 hadi kufikia vituo 158 mwaka 2017 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga kwa kutumia mitambo iliyosimikwa ardhini vimeongezeka kutoka vituo 30 mwaka 2016 hadi kufikia vituo 34 mwaka 2017. Pia, watoa huduma za mawasiliano ya simu na posta wameongezeka na kuleta ushindani wenye tija na ufanisi nchini kwa sekta zote. Aidha, kutokana na kukua kwa sekta, bei ya jumla kwa maunganisho ya simu za mkononi imepungua kutoka Sh. 34.9 kwa dakika mwaka 2013 hadi kufikia Sh. 15.6 kwa dakika mwaka 2018.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

***179. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano inaratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchini, ambao kwa sasa upo katika Awamu ya III na IV ya utekelezaji. Awamu ya III imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusisha uunganishaji wa Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; ujenzi wa mtandao wa miundombinu ya Itifaki [Internet Protocol-Multilayer Label Switching (yaani IP-MPLS Network), na ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Data (National Internet Data Centre) Dar es Salaam ambapo kazi hizi zilikamilika mwaka wa fedha 2016/2017. Katika kipindi

cha mwaka 2017/2018 sehemu ya pili ya Awamu ya III imeanza kutekelezwa.

***180. Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya III Sehemu ya pili, Wizara imefanya tathmini ya miundombinu ya Mkongo kwa lengo la kuboresha matumizi ya miundombinu hiyo na kuwezesha upanuzi wa Mkongo hadi kwenye Halmashauri za Miji 190 na Makao Makuu ya Wilaya 133. Vilevile, Awamu ya IV ni ujenzi wa Mikongo ya Mijini (Metro Fibre Optic Networks) ambao unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Watoa Huduma za Mawasiliano. Hadi sasa ujenzi wa kilometa 3,040 umekamilika katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Moshi, Mbeya, Shinyanga, Musoma, Biharamulo, Morogoro na Dodoma.

***181. Mheshimiwa Spika,*** kuongezeka kwa kasi kwa matumizi ya miamala ya kielektroniki nchini kumeleta uhitaji mkubwa wa ujenzi wa Muundombinu wa Taifa wa Utambuzi wa Miamala ya Kielektroniki (National Public Key Infrastructure - NPKI). Mfumo huo utatumia teknolojia ya funguo maalum kuhakiki ukweli na usahihi wa miamala ya kielektroniki itakayotumwa, kuweka usiri wa taarifa na kuhifadhi taarifa za taasisi zinazojihusisha na shughuli zote zinazohusu miamala ya kielektroniki kama vile biashara mtandao, benki mtandao na barua pepe. Faida za kuwepo kwa mfumo huo ni kuwezesha utambuzi baina ya pande zinazowasiliana, usalama wa watumiaji wa miamala mbalimbali ya kieletroniki hapa nchini na kulinda taarifa zinazotumwa kwenye mitandao ya mawasiliano. Wizara imefanya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa Mpango wa Biashara unaolenga kukuza matumizi ya Mfumo wa Utambuzi wa Miamala ya Kielektroniki.

**Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kutunza Data**

***182. Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Taifa cha Kutunza Data cha Dar es Salaam (Internet Data Centre) kimeendelea kutoa huduma bora kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi ikiwemo kuongeza ukusanyaji wa mapato Serikalini na kubuni chachu

mbalimbali za kuihudumia Serikali na nchi kwa ujumla kupitia TEHAMA. Hadi kufikia Machi 2018 jumla ya wateja 52 wanatumia huduma hii. Kati ya wateja hao, 41 ni taasisi za Serikali na 11 ni kampuni binafsi. Taasisi 41 za Serikali ni kati ya Taasisi 90 zinazotarajiwa kupeleka taarifa zao kwenye *Data Centre*. Aidha, uhamasishaji unaendelea kufanyika kwa Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali na Kampuni binafsi kuhusu uwepo kituo hiki chenye uwezo mkubwa na hadhi ya Kimataifa kwa ajili ya kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na taarifa mbalimbali ili kuunganisha taasisi nyingi na kuendelea kukuza usalama na kupunguza gharama za uendeshaji wa miundombinu ya TEHAMA nchini.

***183. Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya III Sehemu ya pili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano inayohusisha ujenzi wa vituo viwili vya Data katika miji ya Dodoma na Zanzibar kama "back- up" ya Kituo cha Data cha Taifa cha Dar es Salaam, taratibu za kumpata mshauri mwelekezi (TBA) kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi wa *Data Centre* Dodoma zimekamilika. Kwa upande wa Zanzibar taratibu za kurasimisha eneo la ujenzi zimefanyika. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivi kutaongeza usalama, usiri wa data, kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali na mwingiliano wa mifumo (intergration) katika kituo cha Data cha Taifa pamoja na kujikinga na majanga.

**Juhudi za Serikali Kufikisha Huduma ya Mawasiliano Vijijini**

***184. Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliingia mkataba na Kampuni ya simu ya Viettel kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini mwaka 2014. Kupitia makubaliano hayo, kampuni ya simu ya Viettel ina wajibu wa kufikisha huduma ya mawasiliano kwenye vijiji 4,000. Hadi mwezi Machi, 2018 Viettel walijenga minara na kufikisha huduma ya mawasiliano katika vijiji 3,712 ambapo vijiji 288 vilivyosalia vinatarajiwa kupata huduma mwaka 2018/19.

***185. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na Watoa huduma za mawasiliano katika mwaka wa fedha 2017/2018,

imefikisha huduma ya mawasiliano vijijini katika kata 451 zenye vijiji 1954 na wakazi 3,158,628. Serikali inawahimiza Watoa huduma wote waendelee na jitihada hizo za kukamilisha miradi ya mawasiliano vijijini ili kuwaletea tija na maendeleo wananchi. Aidha, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, iliendelea na utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya TEHAMA kwa upande wa Zanzibar, ambapo ujenzi wa vituo vyote 10 umekamilika.

**Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi**

***186. Mheshimiwa Spika,*** Utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi unafanyika kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 kazi ya uwekaji wa nguzo zinazoonesha majina ya mitaa inaendelea katika Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino. Aidha, maandalizi ya uwekaji wa muundombinu wa Mfumo huu yameanza kufanyika katika Halmashauri zenye makao makuu ya Mikoa ya Morogoro, Mbeya, Kagera, Mwanza, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Shinyanga, Geita na Lindi.

***187. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeimarisha Hifadhi-data ya Anwani za Makazi na Postikodi kwa kuhuisha mifumo yake. Pia, Mamlaka imetoa elimu ya uwekaji wa miundombinu ya Anwani za makazi na kwa viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mikoa ya Songwe, Katavi, Mjini Magharibi, Wete, Kigoma, Tabora, Geita na Kagera. Aidha, Mamlaka imetengeneza mfumo wa kupata taarifa za Postikodi kutoka Hifadhi-data kwa njia ya simu ya mkononi kwa mwananchi kupiga *152*00#.

**Programu ya Miundombinu ya TEHAMA ya Kikanda (RCIP)**

***188. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano imetekeleza Awamu I ya Programu ya Miundombinu ya Kikanda (RCIP) ambayo imekamilika Desemba, 2017. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na mradi wa shule mtandao (e-school) uliohusisha ununuzi, usimikaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA

katika Shule za Sekondari 80 na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu. Vifaa vya TEHAMA vilivyonunuliwa na kusimikwa ni pamoja na *printers, scanners, projectors* na *cameras*. Pia, mradi wa *Video Conference* uliohusisha ununuzi, ufungaji na usimikaji wa mitambo ya *Video Conference* katika Makao Makuu ya Mikoa Tanzania Bara na baadhi ya Taasisi za Serikali. Kwa upande wa Zanzibar, ufungaji umefanyika katika Makao Makuu ya Mikoa 4 na Ofisi ya Rais – Ikulu. Pia, programu imewezesha kujenga Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (Government Communications Network – GovNet) ambapo taasisi za Serikali 72 na Halmashauri 77 zimeunganishwa kwenye mtandao mmoja wa Serikali.

***189. Mheshimiwa Spika,*** mifumo mingine iliyojengwa kupitia programu hii ni pamoja na: Mfumo wa Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo kupitia RITA. Mfumo huu umeweza kuongeza tija na ufanisi kwenye kuandikisha vizazi na vifo hapa nchini kwenye vituo sitini (60) katika mikoa ya Shinyanga, Geita na Dar es Salaam. Kwa kutumia mfumo huu vyeti vya kuzaliwa kwa sasa vinatolewa hospitalini pindi mzazi anapojifungua na tangu mwezi Novemba, 2017 jumla ya vyeti 11,331 vya vizazi na 467 vya vifo vimetolewa.

***190. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha uwekezaji hapa nchini, Mfumo wa Taarifa za Biashara (National Business Portal) kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara umejengwa. Mfumo huu utaboresha biashara kwa kuwa na tovuti kuu (portal) yenye taarifa muhimu na huduma kwa wafanya biashara na wawekezaji. Mfumo huu utasaidia kuongeza tija kwenye eneo la kuanzisha na kufanya biashara nchini na kukuza uchumi wa nchi ambapo mwombaji wa leseni ya biashara ataomba leseni kwa kupitia mtandao na kuondoa usumbufu kwa wananchi kusafiri ili kupata huduma hii. Tayari mfumo unatumika kuhuisha taarifa za Kampuni zenye usajili hapa nchini.

***191. Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa Taarifa za Kitabibu (Telemedicine System) kupitia Hospitali ya Taifa ya Muhimbili umeongeza ufanisi kwenye utoaji wa tiba kwenye vituo nane (8) vilivyopo katika mikoa ya Lindi, Morogoro na Pwani

ambapo madaktari bingwa wanaweza kutoa tiba na ushauri kwa kutumia mtandao. Aidha, umejengwa Mfumo wa taarifa za Ununuzi (E-Procurement system) ili kuongeza ufanisi na uwazi kwenye manunuzi mbalimbali yanayofanywa na taasisi za umma. Mfumo huu utaboresha ununuzi wa zabuni na kupunguza matumizi ya karatasi hivyo kulinda mazingira. Vile vile mfumo utaondoa gharama za kubeba vitabu vya zabuni na hivyo kupunguza gharama za utekelezaji miradi.

***192. Mheshimiwa Spika***, umewekwa mfumo wa "Electronic Records" kupitia Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa, ambao unatumika kuwezesha upatikanaji haraka wa kumbukumbu na kuhifadhi nyaraka mbalimbalizaSerikali. Taarifahizi zauhifadhi na upatikanaji wa kumbukumbu hizo kutumika kwa taasisi za Serikali, watafiti na wananchi kwa ujumla.

Sambamba na uwepo wa mfumo wa nyaraka umejengwa Mfumowa"Electronic Office" unaotumiwa katika utendaji wa Serikali kutunza shajala chini ya usimamizi wa Wakala ya Serikali Mtandao (eGA). Ofisi mtandao pamoja na mambo mengine itaongeza usahihi wa usalama na usiri wa nyaraka za Serikali.

***193. Mheshimiwa Spika,*** kupitia Programu ya Miundombinu ya Kikanda (RCIP), Tanzania imenufaika na Ununuzi wa Mkondo wa Mawasiliano (Internet Bandwidth) inayotumika na taasisi zaidi ya 200 za Serikali ambazo ni pamoja na taasisi za Elimu, Halmashauri, Serikali kuu, Mamlaka ya Mapato (TRA), Benki Kuu (BoT), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ambayo imesaidia kupunguza gharama za huduma ya internet kwa asilimia 50 na kuimarisha huduma ya intaneti katika taasisi hizo.

***194. Mheshimiwa Spika,*** lengo la Programu ni kuhakikisha mifumo iliyopo nchini inabadilishana taarifa (Information sharing) ili kuboresha ukusanyaji wa taarifa, kupunguza usumbufu kwa wananchi kuulizwa maswali ya utambuzi kila wakati na kutumia mfumo wa vitambulisho vya Taifa kwa maendeleo. Wizara imeendelea kuboresha mazingira

ambapo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hatua za kuandaa Waraka wa kuomba kutunga Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi (Personal Data Protection Act) upo katika ngazi ya kuomba kibali katika Baraza la Mawaziri.

## UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MAWASILIANO

### Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

### Mfumo wa Kuhakiki na Kusimamia Huduma za Mawasiliano (TTMS)

***195. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeendelea kusimamia mfumo wa TTMS kwa ufanisi ili kuhakikisha kuwa mapato ya TTMS yanayopatikana yanawasilishwa Hazina. Mapato ya TTMS yaliyotokana na idadi ya dakika za mawasiliano ya simu za kimataifa zilizoingia hapa nchini, kuanzia mwezi Oktoba, 2013 hadi mwezi Februari,2018 yaliyopelekwa Hazina ni **Sh. 69,199,471,928.99.**

***196. Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa TTMS umewezesha Kuhakiki ubora wa huduma za Mawasiliano; Kutoa takwimu za mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya nchi (international and local traffic); Kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao (mobile money transaction); Kugundua mawasiliano ya ulaghai (fraudulent traffic); Kubaini na kufungia simu zenye namba tambulishi zilizonakiliwa (Duplicate IMEIs) ambapo taarifa hii inapatikana kwenye rajisi ya namba tambulishi ya simu; Kutambua taarifa za laini ya simu (SIM Card profile) na namba tambulishi za kifaa cha mawasiliano, “Central Equipment Identification Register” (CEIR). Moduli ya Utambuzi wa mapato itakamilika kabla ya mwezi Juni, 2018.

***197. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TCRA inaendelea kusimamia kwa ufanisi uendeshaji wa Mfumo wa Rajisi wa Namba Tambulishi za simu za kiganjani (CEIR) hivyo kuwezesha kudhibiti matumizi ya simu ambazo hazina ubora

(bandia). Simu bandia haziwezi tena kuunganishwa na mtandao wowote wa simu hapa nchini. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2018 idadi ya namba tambulishi (IMEIs) zilizofungwa zilikuwa takribani **2,150,967**. Mfumo wa CEIR umepunguza kwa kiasi kikubwa wizi wa simu za mkononi kwani mara mteja anapoibiwa simu yake na kutoa taarifa simu hiyo inafungiwa mara moja.

***198. Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa matumizi mabaya ya mtandao kwa Taasisi za Ulinzi na Usalama, Serikali kupitia TCRA iliwafadhili watumishi wa Taasisi za Ulinzi na Usalama kwenye mafunzo ya tzNOG yaliyofanyika Dodoma Septemba 2017. Aidha, TCRA iliandaa na kuwashirikisha watumishi wa Taasisi za Ulinzi na Usalama katika mafunzo ya matumizi ya vifaa vya uchunguzi wa kina (Forensic Investigation) mwezi Novemba 2017. Kwa upande wa elimu kwa umma, TCRA imetoa Kitabu cha Mwongozo wa matumizi mazuri ya mawasiliano kilichozinduliwa tarehe 19 Januari, 2018.

**Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

***199. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Posta limeendelea kutoa huduma ya kusambaza barua, nyaraka, vipeto na vifurushi kwa kupitia mfumo wa kawaida wa masanduku na mifuko ya kupokelea barua iliyoko katika ofisi za posta nchini pamoja na mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi ambao huwafikia wateja hadi majumbani/ofisini kwao. Shirika limeendelea kuimarisha huduma ya "Posta Mlangoni" ambapo huduma zimetolewa katika kata ambazo miundombinu ya Anwani za Makazi imekamilika ambazo ni kata 8 mkoani Arusha, kata 32 jijini Dar es Salaam, kata 8 zilizoko Dodoma, na kwa upande wa Zanzibar, Unguja wadi 2 na Pemba wadi 4 zenye miundombinu husika. Mkakati wa kupanua miundombinu unaendelea kufanyika kwa kusimamiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Manispaa katika miji husika.

***200. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Posta lina mtandao wa Ofisi 120 zilizounganishwa katika mtandao wa kielekitroniki

wa Postglobal Netsmart. Ofisi hizi zinaweza kufuatilia (Track and Trace) nyaraka, vifurushi na vipeto vinavyotumwa kupitia mtandao wa Posta. Shirika pia linakamilisha uanzishwaji wa huduma za kifedha kupitia mtandao. Jitihada zinaendelea za kuunganisha Ofisi nyingine 30 kadri ya mtiririko wa fedha utakavyoruhusu. Biashara Mtandao italiwezesha Shirika kuuza bidhaa zake zikiwemo Stempu na bidhaa nyingine kupitia tovuti ya Duka Mtandao: (http://www.stamps.tz.post).

***201. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeboresha nembo yake na kuanza kuboresha muonekano wa vitendea kazi vyake ikiwemo Magari na Majengo ili kuweka mvuto mpya na kuongeza Imani kwa wateja. Aidha, Shirika limeanzisha dirisha la huduma jamii (One Stop Centre) ambapo huduma mtambuka hutolewa ikiwa ni pamoja na malipo ya pensheni za wastaafu na usajili wa watahiniwa katika Baraza la Mitihani.

**Shirika la Mawasiliano Tanzania**

***202. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeamua kuanzisha Shirika la Mawasiliano Tanzania ili kuimarisha mawasiliano nchini kwa maslahi mapana ya Taifa. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa 10, lilipitisha Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2017 ambayo ilianza kutumika tarehe 1 Februari, 2018 kama ilivyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Sheria hii itaiwezesha Shirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pamoja na majukumu mengine Shirika la Mawasiliano Tanzania limepewa jukumu la kuendesha na kusimamia Miundombinu ya Kimkakati kwa maslahi ya Taifa.

***203. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mawasiliano Tanzania linaendelea na utekelezaji wa mpango mahsusi wa kusimika mtandao wa simu za kiganjani kwa kutumia teknolojia ya GSM. Hadi sasa Shirika limesimika mtandao wa 3G na 4G LTE kwenye Mikoa 18 ambayo ni Dar-es Salaam, Dodoma, Pwani, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya, Morogoro, Iringa, Mtwara, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Unguja, Pemba, Singida,

Kagera, na Kilimanjaro. Kwa upande wa huduma za mawasiliano vijijini, Shirika limekamilisha usimikaji wa mtandao kwenye vituo 61 vipya na hivyo kufanya jumla ya vituo vyote vilivyojengwa na Shirika chini ya mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kufikia 142.

***204. Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeongeza idadi ya wateja hai (Active Customers) wa huduma mbalimbali za simu (voice na data) kutoka 293,495 mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 429,735 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 46.

**Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

***205. Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Tume ya TEHAMA imeanza mpango wa kusajili wataalam wa TEHAMA nchini. Mpango huu unalenga kunufaisha wataalam kutoka sekta ya umma na binafsi kutambulika, kulindwa na kuendelezwa kama ilivyo kwa wataalam wa uhasibu, udaktari na ugavi. Vile vile mpango huo una lengo la kutambua wataalam wa TEHAMA na kuwaendeleza bila kuathiri viwango na nidhamu ya taaluma husika. Aidha, Mfumo wa kutambua utaalam wa TEHAMA (ICT Professionals Accreditation Framework) unaandaliwa ili kuwezesha wataalam waliopo nchini kutumika kimataifa na hivyo kuongeza fursa za ajira na kupunguza utegemezi wa wataalam kutoka nje.

***206. Mheshimiwa Spika***, katika maandalizi ya utambuzi wa wataalam, Tume imetoa Semina kwa wanafunzi na jamii ya Vyuo vya elimu ya juu kuhusu utalaam na maadili ya TEHAMA na kuwahamasisha kujisajili na kutambuliwa. Hadi kufikia mwezi Desemba 2017, Jumla ya maombi 1,341 kutoka kwa wataalam wa TEHAMA katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali (MDA’s) yalikuwa yamepokelewa na kufanyiwa uchambuzi. Asilimia 85 ya waombaji wameonyesha kuwa na sifa za kutambulika katika madaraja mbalimbali ya utaalam katika mfumo huo.

***207. Mheshimiwa Spika,*** Tume imeweza pia kuwa na ushirikiano na taasisi za nje. Tume kwa kushirikiana na Kampuni ya Oracle

mwezi Agosti, 2017 iliandaa na kuwezesha warsha kwa Wataalam wa TEHAMA 44 kutoka taasisi mbalimbali za Serikali iliyohusu matumizi ya teknolojia Serikalini. Aidha, Tume iliandaa Kongamano la kwanza la mwaka la wataalam wa TEHAMA (Annual ICT Professionals Conference- AIPC) lililohudhuriwa na watalaam 405 kutoka sekta ya umma na sekta binafsi. Mwezi Februari 2018 Tume iliandaa Jukwaa la TEHAMA Salama Tanzania (Cybersecurity Tanzania Forum) ambalo lilihudhuriwa na wataalam 111 kutoka sekta ya umma na binafsi.

## C. 2 TAASISI ZA MAFUNZO

***208. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inasimamia vyuo vya mafunzo vifuatavyo:
**Chuo cha Ujenzi Morogoro**

***209. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Chuo cha Ujenzi kiliendelea kutoa mafunzo ya ufundi katika fani mbalimbali ikiwemo umeme, uashi, magari, bomba, barabara na madaraja, uchomeleaji na mitambo. Mafunzo mengine yaliyotolewa yalihusu uchoraji wa ramani za majengo na udereva wa magari na mitambo. Hadi Machi, 2018 Chuo kimetoa mafunzo kwa jumla ya wanafunzi **1,173** wa kozi mbalimbali ikilinganishwa na lengo la kufundisha jumla ya wanafunzi **1,050.** Kazi nyingine zilizotekelezwa ni ukarabati wa majengo ya Chuo, ununuzi wa vifaa vya kufundishia pamoja na ufufuaji wa mitambo mitatu ya ujenzi wa barabara kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo.

### Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATTI)

***210. Mheshimiwa Spika,*** Chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuratibu, kutoa na kuendeleza matumizi stahiki ya teknolojia ya nguvukazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara nchini.

***211. Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2018, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya ukarabati na matengenezo

ya barabara za changarawe kwa wasimamizi wa barabara kutoka taasisi na sekta binafsi; kufanya uhamasishaji juu ya matumizi ya teknolojia ya nguvukazi kwa viongozi wa tarafa, kata na vijiji pamoja na kutoa mafunzo ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa wasimamizi wa barabara vijijini katika Halmashauri Wilaya ya Rungwe. Kazi nyingine ni kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Mikoa 9 ya Njombe, Morogoro, Shinyanga, Mbeya, Rukwa, Katavi, Tabora, Singida na Dodoma; kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake katika kushiriki kazi za barabara nchini ambapo wanawake 25 walishiriki kutoka Mkoa wa Songwe pamoja na kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo kupitia barabara za mafunzo ambapo kilomita 0.7 zilikarabatiwa katika Halmashauri ya Rungwe na Halmashauri Mbeya Vijijini. Aidha kilomita 21 zilizopo chini ya TANROADS mkoani Mbeya zilifanyiwa matengenezo ya kawaida kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Jumla ya wananchi 180 wamenufaika kwa kupata ujuzi wa kukarabati na kutengeneza barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.

***212. Mheshimiwa Spika,*** Chuo pia kilishiriki katika makongamano na kufanya uhamasishaji wa kutangaza huduma na mafunzo yatolewayo na Chuo yaliyoandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), maonyesho ya nanenane Jijini Mbeya na kongamano la kimataifa la matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi lililoandaliwa na ILO lililofanyika nchini Ethiopia.

***213. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na taratibu za kuanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) ambayo inatambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Hadi Machi, 2018, Mtaalam Mshauri (Consultant) amewasilisha taarifa ya mwisho kuhusu mitaala na mahitaji ya rasilimali watu. Tayari NACTE imetoa usajili wa muda kwa Taasisi hiyo. Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATTI) vitakuwa chini ya ICoT na vyeti vyao vitakuwa vinatambuliwa na NACTE.

**Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

***214. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kilitoa huduma za mafunzo, utafiti, na ukarabati wa vifaa vya kuokolea maisha. Chuo kimeendelea kudahili wanafunzi wa kozi mbalimbali, ambapo katika mwaka huo, jumla ya wanafunzi 557 walidahiliwa katika kozi ndefu. Kati ya wadahiliwa hao, wanafunzi 48 ni wanawake na wanafunzi 51 walitoka nje ya Tanzania. Katika kozi fupi, jumla ya wanafunzi 1,575 walidahiliwa. Chuo pia kimeanza kutoa Stashahada ya juu katika uhandisi mitambo wa vyombo viendavyo majini, Sheria za masuala ya bahari, teknolojia ya nguvu ya umeme katika vyombo vya usafiri majini na sayansi ya Bahari. Aidha, Chuo kimepanua uwezo wa Maktaba; kuimarisha huduma za Maktaba ya kielektroniki; na kukarabati vifaa vya kufundishia na miundombinu ya Chuo.

***215. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Chuo kimekamilisha taratibu za manunuzi ya vifaa vya karakana ya mafunzo (Workshop), vifaa vya mafunzo ya Usalama katika sekta ya Uchimbaji Mafuta na Gesi baharini (offshore safety training) pamoja na uendelezaji wa eneo la Mkuranga. Aidha, Mkataba wa kukarabati meli kwa ajili ya mafunzo ya wanafunzi ulisainiwa Novemba, 2017.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

***216. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu katika kozi 20 ambapo jumla ya wanafunzi 6,813 walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 7,752 katika mwaka 2016/2017. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 12. Sababu za upungufu huu ni pamoja na kubadilika kwa mfumo wa udahili, hivyo maombi mengi kushindwa kukidhi vigezo vya udahili. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa kozi 13 za menejimenti ya usafirishaji na udereva mahiri. Mafunzo haya ni muhimu katika kukabiliana na changamoto ya ajali za barabarani na usalama katika usafirishaji na uchukuzi. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya washiriki 4,542 walihudhuria mafunzo haya ikilinganishwa na

washiriki 4,532 walioshiriki katika mafunzo haya katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Hii inaonesha mwitikio mzuri wa washiriki kuendelea kushiriki katika kozi hizi.

***217. Mheshimiwa Spika,*** Chuo kinaendelea kukamilisha taratibu za ithibati za utoaji wa mafunzo ya urubani na wahudumu wa ndege kutoka Mamlaka ya Uthibiti wa Usafiri wa Anga (TCAA). Kati ya hatua tano (5) za ithibati, hatua tatu (3) za *Pre-Application stage, Formal Application Stage na Document Compliance and Document Approval* zimekamilika. Hatua mbili (2) zilizobaki zinaendelea kufanyiwa kazi. Mafunzo haya yatafanyika katika viwanja vya Ndege vya Dodoma na Dar-es-Salaam.

***218. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha NIT kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeendelea kutoa elimu ya mazingira na kukagua magari yaliyotumika na kuingizwa nchini kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Magari haya hukaguliwa katika Kituo cha Kisasa cha Ukaguzi wa Magari kilichoko katika maeneo ya Chuo. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya magari 1,586 yalikaguliwa ikilinganishwa na magari 904 yaliyokaguliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 75 na limetokana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kutokuongeza muda wa mkataba na moja ya kampuni iliyokuwa ikitoa huduma hizo nje ya nchi baada ya kujiridhisha kuwa kazi hiyo inaweza kufanywa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kwa ufanisi.

### Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)

***219. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usafiri wa Anga (Civil Aviation Training Centre - CATC) imeendelea kutoa mafunzo yanayokidhi viwango vya Kimataifa katika sekta ya usafiri wa anga kwa Watanzania na nje ya nchi. Mafunzo yanayotolewa ni ya fani za uongozaji ndege, mawasiliano, usambazaji wa taarifa za safari za ndege, usalama wa viwanja vya ndege na utafiti na ushauri kuhusu usalama wa usafiri wa anga. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya wanafunzi 575 kutoka ndani na nje ya nchi walihitimu

mafunzo mbalimbali katika Chuo hiki. Aidha, mashine ya kufundishia wanafunzi (Simulator) imewasili nchini na kazi ya usimikaji ilianza Machi, 2018 na inatarajiwa kukamilika Juni, 2018.

**Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma**

***220. Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa kada mbalimbali kulingana na mpango wa mafunzo wa Wakala wa Hali ya Hewa. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya wanafunzi 46 walidahiliwa katika ngazi ya cheti na Diploma. Aidha, wanafunzi 13 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya cheti. Wanafunzi hawa wanaendelea kutoa huduma za hali ya hewa katika vituo vya hali ya hewa nchini.

## C.3 MASUALA MTAMBUKA

**Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara**

***221. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetekeleza mikakati mbalimbali katika mwaka wa fedha 2017/2018 ili kuhakikisha ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara unaongezeka. Hadi Machi, 2018 Wizara kupitia Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia ya Nguvu Kazi ilikuwa imeendesha mafunzo ya mwezi mmoja kwa wanawake wakandarasi 25 kutoka katika mkoa wa Songwe ili kuwapa ujuzi wa kushiriki katika kazi za barabara. Wizara imeendesha mafunzo kwa jumla ya waratibu 27 wanaosimamia shughuli za ukandarasi wa wanawake kutoka ofisi za TANROADS mikoani. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia kazi zinazofanywa na wanawake katika matengenezo na ukarabati wa barabara nchini na kubaini kuwa kazi zao zinaridhisha. Vilevile, Wizara imetembelea jumla ya shule za sekondari 39 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara na kuongea na wanafunzi wa kike zaidi ya 5000 kuwahamasisha kusoma masomo ya sayansi na hisabati.

**Ushiriki wa Wizara Katika Jumuiya Mbalimbali za Kimataifa**

***222. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imeendelea kushiriki katika masuala yanayohusu Sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda na hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Umoja wa Mawasiliano ya Afrika (ATU na PAPU).

***223. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara kupitia Sekta ya Ujenzi imeendelea na utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya barabara iliyoidhinishwa mwaka 2012 na Wakuu wa Nchi za EAC ambayo itawezesha kuboresha miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, bandari na reli zinazohudumia Tanzania na nchi jirani. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kazi (Retreat) wa Wakuu wa Nchi ambao umefanyika tarehe 14 – 23 Februari, 2018 mjini Kampala, Uganda. Kaulimbiu (Theme) ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za EAC ilikuwa ***"Development of Resilient Infrastructure to Accelerate Industrialization and Support Trade to Foster Socio-Economic Transformation in the EAC".***

***224. Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana kutokana na Mkutano wa Kazi (Retreat) wa Wakuu wa Nchi za EAC ni pamoja na baadhi ya miradi kupata fedha za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kutoka NEPAD-IPPF/AfDB. Miradi hiyo ni pamoja na: upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Lusahunga – Rusumo/Kayonza - Kigali inayounganisha Tanzania na Rwanda; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakanazi – Kasulu – Manyovu/ Rumonge – Rutunga - Bujumbura inayounganisha Tanzania na Burundi; upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kumnazi – Kasulo - Bugene - Kyaka – Mutukula - Masaka inayounganisha Tanzania na Uganda.

***225. Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo wa Kazi wa Wakuu wa Nchi za EAC, Benki ya Dunia imekubali kugharamia fedha za kutekeleza miradi ya barabara kupitia mradi wa *Development Corridors Transport Project (DCTP), Lake Victoria*

*Transport Programme (LVTP) and Lake Tanganyika Transport Programme (LTTP).* Miradi hiyo ni ukarabati wa barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200); ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo/Nyakasanza – Kobero (km 150); ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (km 295); ujenzi wa barabara ya Iringa – Msembe (Ruaha National Park) – km 104 na ujenzi wa Viwanja vya ndege vya Iringa, Lake Manyara na Tanga itakayotekelezwa chini ya programu ya **DCTP.** Miradi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Musoma Port Access; upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Nansio - Rugezi Port access; mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na ukarabati wa barabara ya Mara /Simiyu Border – Nyanguge (km 100.4); mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4) na upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Bukoba - Bukoba Port Access itatekelezwa chini ya programu ya **LVTP.** Aidha miradi itakayotekelezwa chini ya programu ya **LTTP** ni upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kagwira – Karema na ujenzi wa barabara ya Mpanda (Vikonge) – Uvinza.

***226. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Wizara pia imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano ya SADC kuhusu masuala ya mtangamano. Baadhi ya masuala muhimu yanayoendelea kujadiliwa ni:

(i) Uwianishaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango kuhusu usafirishaji wa mizigo mizito kwa magari makubwa kwa njia ya barabara. Majadiliano hayo yamepanuliwa na kuhusisha Jumuiya za Utatu (*COMESA, EAC and SADC Tripartite Free Trade Area*) ambapo lengo kuu ni kurahisisha ufanyaji wa biashara katika Jumuiya hizo tatu kwa kuwianisha viwango vya usafirishaji wa mizigo pamoja na ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi wa Magari.

(ii) Majadiliano ya Biashara ya Huduma (*Negotiations on*

*Trade in Services*) kwa Nchi Wanachama wa SADC ambayo yamelenga kufungua na kukuza fursa za utoaji huduma kwa Sekta ya Ujenzi zikiwemo kazi za ujenzi, huduma za kihandisi pamoja na huduma za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi.

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya barabara iliyojumuishwa katika Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Miundombinu kwa Nchi Wanachama wa SADC. Miradi hiyo ni Dar es Salaam – *Chalinze Expressway* (km 144); barabara ya Mtwara – Mbamba Bay sehemu ya barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) ambapo utekelezaji wa mradi huu umeanza chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); barabara ya Makambako – Songea (km 295); na barabara ya Manyoni – Tabora – Kigoma (km 718.9) na Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi (km 310).

***227. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mawasiliano, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa nchi katika Baraza la Uendeshaji la Umoja wa Posta Duniani (UPU) ambalo Tanzania ni mjumbe kwa miaka minne (2016-2020). Hatua hii inaiwezesha Tanzania kushiriki maamuzi yanayohusu maendeleo ya sekta ndogo ya Posta duniani ikiwemo mgawanyo wa faida zinazotokana na makusanyo ya Umoja (Quality of Service Fund – QSF) ambapo Tanzania kupitia Shirika la Posta imekuwa ikipokea vifaa mbalimbali vya kazi yakiwemo magari ya kubebea abiria na mizigo. Aidha, Tanzania ni mjumbe wa Baraza la Utawala la Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU Council) katika kipindi cha 2014 – 2018. Hatua hii inaiwezesha nchi yetu kushiriki maamuzi kuhusu maendeleo ya Mawasiliano na TEHAMA duniani.

## D. CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

***228. Mheshimiwa Spika,*** changamoto mojawapo ni **uwezo mdogo wa Mfuko wa Barabara kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara** ambapo kwa sasa Mfuko unatosheleza asilimia 45 tu ya mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara nchini. Mtandao mkubwa wa barabara

unaogharamiwa na Mfuko ni wa changarawe au udongo ambao huharibika mara kwa mara hususan kipindi cha mvua na hivyo kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara.

***229. Mheshimiwa Spika,*** mikakati inayotekelezwa na Serikali kutatua changamoto hii ni kushirikisha taasisi za ndani na za kimataifa kufanya tafiti za teknolojia rahisi ya matengenezo ya barabara kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika maeneo husika. Aidha, Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na TRA na EWURA zinafanya tafiti za kubaini na kupendekeza njia stahiki za kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya Mfuko.

***230. Mheshimiwa Spika,*** changamoto nyingine ni **uzidishaji wa uzito wa mizigo inayobebwa na magari makubwa barabarani** kinyume na ile inayokubalika kisheria ambayo inasababisha barabara kuharibika haraka na hivyo kuongeza gharama za matengenezo ya barabara. Aidha, uharibifu na wizi wa samani za barabara ikiwa ni pamoja na alama za barabarani hufanywa na baadhi ya watumiaji wa barabara na wananchi ambao huondoa alama za barabara na vyuma vya madaraja na kuuza kama chuma chakavu. Hii pia huchangia kuongeza gharama za matengenezo ya barabara nchini. Mkakati uliopo ni kuelimisha watumiaji wa barabara na wananchi kwa ujumla kupitia radio, runinga, magazeti, vipererushi na mitandao ya kijamii juu ya umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu ya barabara katika maeneo yao ili kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

***231. Mheshimiwa Spika,*** **uhaba wa fedha za maendeleo** kwa ajili ya kukarabati na kuendeleza miundombinu ya reli, bado ni changamoto kubwa inayoikabili Wizara. Hii ni kutokana na miradi hii kuhitaji fedha nyingi. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaendelea kutenga fedha katika bajeti yake ya kila mwaka. Juhudi mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kupata mikopo yenye masharti nafuu ili kukamilisha ujenzi wa Reli *standard gauge*. Serikali itaendelea kujadiliana na wawekezaji mbalimbali wenye lengo la kuwekeza katika sekta hii kwa kuzingatia Sheria na Sera ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi.

***232. Mheshimiwa Spika,*** changamoto nyingine ni **kutojitokeza kwa wingi kwa wazabuni wanaokidhi vigezo na sifa** zinazostahili kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli katika Maziwa. Mkakati uliopo ni pamoja na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kwa kushirikiana na Wizara na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutumia Balozi zetu zilizoko nje ya nchi kuelezea miradi hii ya maendeleo ili wazabuni wenye kukidhi vigezo waweze kujitokeza kwa wingi kushindania zabuni husika.

***233. Mheshimiwa Spika,*** changamoto ya **uchakavu wa miundombinu ya reli na bandari** kutokana na kukosa matengenezo kingamizi imeendelea kutatuliwa kwa kuandaa mpango wa biashara (business plan) kwa mashirika ya reli na bandari ili kusaidia ushawishi wa kutafutia fedha za kuboresha utendaji na kuleta tija ikiwa ni pamoja na kushirikisha sekta binafsi.

***234. Mheshimiwa Spika,*** kuhusu changamoto ya **uchakavu na uchache wa vitendea kazi** kama vichwa vya treni na mabehewa, Wizara imeendelea kujenga uelewa kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi ili kuona fursa zilizopo katika kuwekeza kwenye sekta ya Uchukuzi kupitia mpango wa ubia wa sekta ya umma na binafsi (PPP).

***235. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa changamoto inayokabili huduma za reli ya **uharibifu/hujuma zinazofanywa na wananchi katika miundombinu ya reli** pamoja na **mafuriko na wizi wa vyuma chakavu**, Wizara imeendelea kusimamia Sheria zilizopo kuhusu uharibifu huo pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutunza miundombinu ya uchukuzi kwa lengo la kupunguza uharibifu/hujuma ya miundombinu hiyo. Aidha, mikakati ya kukabiliana na mafuriko yanayoweza kuharibu miundombinu ya reli, Wizara kupitia TRC imeendelea kufanya matengenezo kingamizi (preventive maintenance).

***236. Mheshimiwa Spika,*** kuna changamoto ya **Madai ya fidia** katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara

imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia ya mali za wananchi wanaotakiwa kupisha utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya uchukuzi. Aidha, kwa wale waliovamia hifadhi ya reli na barabara, elimu imeendelea kutolewa na kuwataka wazingatie Sheria.

***237. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada za kutoa elimu na kusimamia makampuni ya simu, kuboresha mifumo ya udhibiti wa mianya ya matumizi mabaya katika mitandao ya simu ikiwemo ulaghai na wizi katika miamala ya kifedha (spoofing) bado changamoto hii inaendelea kutokea. Uchunguzi uliofanywa na TCRA umebainisha kuwepo kwa vithibiti visivyojitosheleza kwenye mifumo ya watoa huduma. Aidha, TCRA inaendelea na utaratibu wa kuhakiki mianya ya ulaghai kwa kutumia njia za kitaalam na kutoa elimu kwa umma. Vile vile, Serikali inaendelea kusimamia sheria ya makosa ya mtandao ya mwaka 2015 na kupendekeza kutungwa kwa sheria nyingine ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za mawasiliano.

## E. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

***238. Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka 2018/2019 ni miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo na miradi iliyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali.

## E.1 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA SEKTA ZA WIZARA

### E.1.1 SEKTA YA UJENZI

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

***239. Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni Shilingi

**42,898,011,066.00.** Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 1,822,093,269,360.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na.1.***

Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

**MRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL SUPPORT)**

***240. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 250.00** fedha za ndani. Fedha hizo zitatumika kuwapatia Watumishi wa Sekta ya Ujenzi mafunzo katika fani mbalimbali kwa lengo la kuwaimarisha kitaaluma. Fedha hizo pia zitatumika kununua vitendea kazi na vifaa vya ofisi.

**MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI**

**Ujenzi wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

***241. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,000.00** kwa ajili ya miradi ya vivuko kama ifuatavyo:

**i) Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**

***242. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu una lengo la kujenga maegesho kwa ajili ya kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko nyakati zote za mwaka. Katika mwaka wa fedha 2018/19, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 1,676.00** kwa ajili ya upanuzi wa maegesho ya Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia na ujenzi wa jengo la abiria na ofisi katika maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda.

**ii) Ununuzi wa Vivuko Vipya**

***243. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 9,064.00** kwa ajili

ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni (MV. Kazi); kuendelea na ujenzi wa kivuko kipya cha Kigongo – Busisi; ununuzi wa kivuko kipya cha Nyamisati – Mafia na ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA.

**iii) Ukarabati wa Vivuko**

***244. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,260.00** kwa ajili ya kukamilisha malipo ya kazi ya ukarabati wa kivuko MV. Pangani II (Tanga); ukarabati wa kivuko MV. Sengerema, MV. Kigamboni na MV. Misungwi.

**Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

***245. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 17,450.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatavyo:

**i) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi na Ofisi za Serikali**

***246. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya **Shilingi milioni 10,200.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za viongozi wa Serikali. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 9,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi pamoja na Ikulu ya Dodoma. Aidha, **Shilingi milioni 700** ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba za Majaji katika Mikoa ya Dar es Salaam (1), Kilimanjaro (1), Mtwara (1) na Shinyanga (1).

**ii) Ujenzi wa Kambi kwenye Mradi wa Kufua Umeme katika Mto Rufiji (Rufiji Hydropower Project)**

***247. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kambi katika mradi wa kufua umeme kwenye Maporomoko ya Mto Rufiji.

**iii) Ujenzi wa Nyumba za Makazi Eneo la Magomeni (Magomeni Quarters)**

***248. MheshimiwaSpika,***katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya **Shilingi milioni 200** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea

na ujenzi wa nyumba za Makazi eneo la Magomeni (Magomeni Quarters).

**iv) Ukarabati wa Nyumba na Ununuzi wa Samani Kwa Ajili ya Nyumba za Viongozi**

***249. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya **Shilingi milioni 1,550.00** zimetengwa kwa ajili ya kukarabati nyumba za viongozi na ununuzi wa samani. Kati ya fedha hizo **Shilingi milioni 900** ni kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za Viongozi, **Shilingi milioni 200** ni kwa ajili ya ununuzi wa samani za Viongozi na **Shilingi milioni 450** kwa ajili ya ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA).

**v) Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri**

***250. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 100.00** zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) kupitia Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Aidha, **Shilingi milioni 400.00** zimetengwa kwa ajili ya huduma za ushauri, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za Serikali.

**vi) Ujenzi wa Karakana za TEMESA**

***251. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya **Shilingi milioni 2,500** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Karakana mpya ya mkoa wa Dodoma na ukarabati wa karakana zilizopo mkoani Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya na M.T Depot Dar es Salaam. Aidha, **Shilingi milioni 500** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi.

**MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA**

***252. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizaraitaendelea kutekeleza ujenzi na ukarabati wa miradi

mbalimbali ya barabara ili kufikia maeneo mengi zaidi ya kiuchumi na kijamii. Maelezo ya miradi itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ni kama ifuatavyo:

**Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (km 367)**

***253. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10,000.00** kwa ajili ya ukarabati wa barabara za kuelekea kwenye mradi wa kufua umeme wa Mto Rufiji. Barabara hizo ni Ngerengere - Kisaki - Selous (km 166) na Kibiti - Mloka - Selous (km 201).

**Barabara ya Dar e Salaam – Chalinze – Morogoro – Dodoma (km 467.90)**

***254. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,300** kwa ajili ya kulipa madai ya Mshauri Mwelekezi aliyefanya upembuzi yakinifu wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze Expressway (km 144.00) na kuendelea na ukarabati wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44.00). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara za Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.60), Kwa Mathias (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3) na kufanya usanifu kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260).

**Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 410.8)**

***255. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,100.00** kwa ajili ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Bagamoyo – Msata (km 64) na kuendelea na ujenzi wa barabara za TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24) na Kisarawe – Maneromango (km 54). Aidha, kazi nyingine ni kufanya maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Bagamoyo (Makurunge) – Saadani – Pangani - Tanga (km 246) sehemu ya Tanga – Pangani (km 50), Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (sehemu ya Tegeta – Bagamoyo - km 46.9), Mbegani – Bagamoyo (km 7.2) na Makofia – Mlandizi (km 36.7).

**Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo - Kyamyorwa (km 230)**

***256. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 18,000.00** fedha za ndani kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Uyovu – Bwanga (km 43) ambayo imekamilika, kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bwanga – Biharamulo (km 67) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3) na Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7).

**Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7)**

***257. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 39,230.00** kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya malipo ya Makandarasi waliojenga miradi ya Daraja la Kikwete katika Mto Malagarasi na barabara za maingilio (km 48), barabara za Kidahwe - Uvinza (km 76.6), Ndono – Urambo (km 52), Tabora - Ndono (km 42) na Kaliua – Kazilambwa (km 56). Kazi zingine ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Urambo – Kaliua (km 28) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.10) na sehemu ya Kazilambwa - Chagu (km 42).

**Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai - Kamwanga/ Bomang'ombe – Sanya Juu ( km 330.31)**

***258. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 33,795.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi wa barabara za KIA – Mererani (km 26). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Arusha – Moshi – Holili (sehemu ya Sakina – Tengeru na mchepuo wa Arusha - km 56.51), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Alerai: km 32), Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16.0), Kiboroloni – Kikarara – Tsuduni - Kidia (km 10.8), Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST: km 20) na kuendelea na maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105) pamoja na ujenzi wa mizani ya Himo.

***259.*** **Barabara ya Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95.0)** katika mwaka wa fedha 2018/2019 imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 100.00** kwa ajili ya kukamilisha malipo ya Mkandarasi wa barabara hiyo.

**Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Mchepuo kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)**

***260. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,065.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni) na kununua na kufunga mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion – WIM) kwenye kituo cha Nala (Dodoma).

**Ukarabati wa Barabara ya Port Access (Nelson Mandela) - km 6**

***261. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 100.00**, kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuifanyia upanuzi sehemu ya kuanzia Bandarini hadi TAZARA yenye urefu wa kilometa 6 kutoka njia nne za sasa na kuwa njia sita.

**Barabara ya Dumila – Kilosa - Mikumi (km 69)**

***262. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,300.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyejenga sehemu ya Dumila – Rudewa (km 45) pamoja na kuendelea na ujenzi wa mizani inayopima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion - WIM) ya Dakawa. Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 24).

**Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 162)**

***263. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya **Shilingi milioni 8,500.00** zimetengwa kwa ajili

ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai Kasanga Port (km 112) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50).

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

***264. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 46,960.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa Daraja la Kilombero (Morogoro) na Daraja la Kavuu (Katavi) ambayo yamekamilika. Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa Daraja la Kirumi (Mara), kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Magara (Manyara), Sibiti (Singida), Ruhuhu (Ruvuma), Momba (Rukwa/Songwe), Mlalakuwa (Dar es Salaam), Lukuledi (Lindi), Mara (Mara) na Mkenda (Ruvuma).

Kazi zingine ni kuanza ujenzi wa madaraja ya *New* Wami (Pwani), Selander (Dar es Salaam), Msingi (Singida), Sukuma (Mwanza) na Simiyu (Mwanza) pamoja na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Kigongo/ Busisi (Mwanza). Aidha, kazi nyingine ni kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa madaraja ya Mtera (Dodoma) na Malagarasi Chini (Kigoma) pamoja na ununuzi wa vyuma vya ujenzi wa madaraja ya dharura (*Emergency Bridge Parts*).

**Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta: km 17.2)**

***265. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/ 2019 jumla ya **Shilingi milioni 19,905.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza upanuzi wa sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3) na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua kwenye barabara ya Mwenge – Tegeta (km 12.9).

**Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 288.10)**

***266. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya **Shilingi milioni 9,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1), kulipa sehemu ya fidia kwa barabara ya Bugene –

Kasulo (km 124) na Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105). Kazi nyingine ni kuanza mapitio ya usanifu wa kina kwa sehemu ya Bugene – Kasulo (km 124) ili kukidhi viwango vya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ndiyo inaratibu ufadhili wa mradi huu kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

**Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 533)**

***267. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya **Shilingi milioni 50,493.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya Mkandarasi wa barabara ya Isaka Ushirombo (km 132), kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110) na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station - OSIS) cha Nyakanazi. Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 91) na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakahura - Kumubuga – Murusagamba na Kumubuga - Rulenge – Kabanga Nickel (km 141).

**Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.75)**

***268. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya **Shilingi milioni 27,900.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35) na Tabora – Nyahua (km 85). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4) ambao unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka KUWAIT Fund.

**Barabara ya Korogwe – Handeni (km 65)**

***269. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya **Shilingi milioni 100.00** zimetengwa kwa ajili ya kumalizia malipo ya Mkandarasi.

**Barabara za Mikoa**

***270. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/

2019, jumla ya **Shilingi milioni 35,012.67** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya kilometa **606.12** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **36.51** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja **15**. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)**

***271. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya **Shilingi milioni 700.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuifanyia ukarabati barabara hii.

**Barabara ya Handeni – Mkata (km 54)**

***272. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 barabara ya Handeni – Mkata imetengewa **Shilingi milioni 100.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara hiyo.

**Mradi wa Kuondoa Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 169.66)**

***273. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 20,150.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za Kimara – Kilungule – External (km 9.0); Mbezi – Malambamawili - Kinyerezi – Banana (km 14.0) sehemu ya Kifuru – Malambamawili – Msigani (km 4.0); Tegeta – Kibaoni –Wazo Hill – Goba – Mbezi (Morogoro Road) sehemu ya Mbezi Mwisho – Goba (km 7.0); Tangi Bovu – Goba (km 9.0); Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.60); Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66), sehemu ya Kibamba – Mloganzila (km 4.0); Ardhi – Makongo – Goba (km 9.0), sehemu ya Goba - Makongo (km 4.0). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa

barabara za Kimara – Kilungule – External (km 9.0), sehemu ya Kimara – Kilungule – Majichumvi (km 6.0); Mbezi - Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14.0), sehemu ya Mbezi – Msigani (km 2.0) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba (km 13), sehemu ya Madale – Goba (km 5.0). Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itaendelea kwa barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7) na kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa - Kwembe – Makondeko (km 14.66), sehemu ya Mloganzila – Mloganzila Citizen (km 4.0); Maji Chumvi - Chang'ombe – Barakuda (km 2.5) na Mjimwema – Kimbiji (km 27.0). Kazi nyingine ni kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1) na Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (km 25.1).

**Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)**

***274. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii.

**Kidatu – Ifakara – Lupiro – Mahenge/Malinyi – Londo – Songea (km 499)**

***275. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 16,645.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Kidatu – Ifakara (km 68).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 370)**

***276. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 58,235.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Tabora - Sikonge (Usesula) (km 30), Usesula – Komanga (km 115.5), Komanga – Kasinde (km 112.8) na Kasinde – Mpanda (km 111.7).

**Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/ Loliondo – Mto wa Mbu (km 185)**

***277. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 23,800.00** kwa

ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Makutano – Sanzate (km 50) na Waso – Sale Jct (km 50). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Sanzate – Natta – Mugumu (km 85).

**Barabara ya Ibanda – Itungi/Kajunjumele – Kiwira Port (km 64.6)**

***278. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 17,000.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi wa barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (sehemu ya Bujesi – Mbambo km 15.0); kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (sehemu ya Tenende – Matema: km 34.6) pamoja na kuanza ujenzi wa sehemu ya Tukuyu – Mbambo (km 15.0).

**Barabara ya Nzega – Tabora (km 224.7)**

***279. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,800.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa sehemu za Nzega – Puge (km 58.6) na Puge – Tabora (km 56.10). Kazi nyingine ni kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110.0).

**Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 517.4)**

***280. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 24,850.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Sumbawanga - Kanazi (km 75.0), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6) na Sitalike – Mpanda (km 36.5). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 30.0). Aidha, kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Kibaoni – Sitalike (km 71.0) na Vikonge – Magunga – Uvinza (km 159.0) pamoja na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (km 64.8).

**Barabara ya Nyanguge – Musoma, Mchepuo wa Usagara – Kisesa na Bulamba - Kisorya (km 495.90)**

***281. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 22,150.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu za Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5), Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass: km 17.0). Aidha, fedha hizi zitatumika kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba: km 51), ukarabati *(overlay)* wa barabara ya Makutano – Sirari (km 83.0) na upanuzi wa barabara ya kwenda uwanja wa ndege wa Mwanza (km 12). Kazi nyingine ni kuanza kufanya mapitio ya usanifu wa kina kwa sehemu ya Nyamuswa – Bunda - Bulamba (km 55), kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92) na ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4).

**Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 149.0)**

***282. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Magole – Turiani (km 45.0) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Turiani – Mziha - Handeni (km 104.0).

**Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini Dar es Salaam na Barabara Unganishi**

***283. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50,852.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa 'Flyover' ya TAZARA; *Interchange* ya Ubungo pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/ Mandela, Morocco, Buguruni, makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Kenyatta na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct). Aidha, kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

**Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171.8)**

***284. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 20,000.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Bariadi – Lamadi (km 71.8) na Mwigumbi – Maswa (km 50.3). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Maswa – Bariadi (km 49.7).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa - km 172)**

***285. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina.

**Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 413)**

***286. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi *milioni* 25,200.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 63), Nyakanazi – Kakonko (km 50) pamoja na kuanza ujenzi wa sehemu ya Nduta – Kibondo – Kabingo (km 61.84) na barabara ya kupitia Kibondo mjini (km 25.85).

**Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road - km 16)**

***287. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 307.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara hii.

**Barabara ya Dodoma University na Barabara ya Mzunguko wa Dodoma (km 116.0)**

***288. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,500.00** katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na

Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12.0) na kuanza ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma (Mtumba – Veyula – Nala – Matumbulu – Mtumba - km 104.0).

**Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi**

***289. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,500.00** ikiwa ni sehemu ya mchango wa Serikali katika ujenzi wa daraja hilo na kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi za Kigamboni (Daraja la Nyerere) – Vijibweni (km 1.5). Kazi nyingine ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjimwema (km 1.6).

***290. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara pia itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

**Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu za Ukanda wa Kati:** Jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza kazi ya usanifu wa kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika barabara kuu ya Ukanda wa Kati.

**Upanuzi wa Barabara ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) – Pugu (km 8) kuwa njia sita:** mradi huu utajumuishwa kwenye mradi wa BRT awamu ya tatu. Jumla ya **Shilingi milioni 100.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kufanya maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu *(BRT Phase III).*

**Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji: Jumla ya Shilingi milioni 20,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza upanuzi wa barabara na madaraja tajwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (Design and Build).

**Ujenzi wa Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119):** Jumla ya **Shilingi milioni 100.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Upanuzi wa Barabara ya Bandari na Ujenzi wa Barabara ya Dockyard na Mivinjeni (km 2.9):** Jumla ya **Shilingi milioni 100.00** zimetengwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya upanuzi wa barabara hizo.

**Ujenzi wa Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34.0):** Jumla ya **Shilingi milioni 1,200.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho na Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34).

**Ujenzi wa Mizani Karibu na Bandari ya Dar es Salaam:** Jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/19 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mizani ya kupima uzito wa magari karibu na Bandari ya Dar es Salaam.

***291. Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ya maendeleo ya barabara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/ 2019 ni:

**Barabara ya Tunduma – Sumbawanga (km 276.01):** Jumla ya **Shilingi milioni 10,000.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2).

**Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 233.1):** Kiasi cha **Shilingi milioni 14,500.00** kimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Kagoma – Lusahunga (km154), kuendelea na ujenzi wa sehemu ya barabara ya Muhutwe – Kamachumu - Muleba (km 54) na kuanza ujenzi wa barabara ya Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5).

**Barabara ya Arusha – Namanga (km 105):** Jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyefanya kazi za ujenzi wa mradi huu.

**Barabara ya Singida – Babati – Minjingu (km 333.5):** Kiasi cha **Shilingi milioni 1,900.00** kimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa barabara za Singida – Kateshi (km 65.1) na kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Singida – Shelui (km 110.0).

**Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani** (sehemu ya KAMATA – Bendera Tatu, km 1.3): **Shilingi milioni 9,350.00** zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya KAMATA – Bendera Tatu na ujenzi wa Daraja la Gerezani na kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8) pamoja na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mzinga.

**Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 1,226.20): Shilingi milioni 81,459.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete (km 107.4), sehemu ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9) na kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Mafinga – Igawa (km 137.9). Kazi nyingine ni kufanya maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152.0), Njombe – Lupembe – Madeke (km 125.0) na Iringa – Ruaha National Park (km 104.0). Aidha, kazi nyingine ni kufanya mapitio ya usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (km 295.0), kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Mafinga – Mgololo (km 78.0) na Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) ikijumuisha barabara ya mchepuo ya Mbeya (Uyole – Songwe Bypass) (km 48.9).

**Barabara ya Korogwe – Mkumbara – Same (km 172): Shilingi milioni 100.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi aliyekarabati sehemu ya Korogwe – Mkumbara (km 76.0).

**Barabara ya Mbeya – Makongolosi - Mkiwa (km 171.9): Shilingi milioni 16,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 43) na kuanza ujenzi wa barabara ya Itigi - Noranga – Mkiwa (km 56.9).

**Barabara ya Chalinze – Segera – Tanga (km 248):** Jumla ya **Shilingi milioni 5,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Amani – Muheza (km 36.0).

**Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211):** Jumla ya **Shilingi 13,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50).

**Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kibaya - Singida (km 460): Shilingi milioni 1,000** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara hiyo.

**Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1): Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass: km 7.3).

**Barabara ya Dodoma – Babati (km 243.80): Shilingi milioni 5,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35) na Mela – Bonga (km 88.80). Kazi nyingine ni kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass: km 12.0).

**Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 1,470.9): Shilingi milioni 61,837.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa malipo ya mwisho ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2) na Kilimasera – Namtumbo (km 60). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi

wa barabara za Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Masasi – Newala – Mtwara (sehemu ya Mtwara – Mnivata: km 50.0). Aidha, kazi nyingine ni kufanya maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45), Nanganga - Ruangwa – Nachingwea (km 107), Likuyufusi – Mkenda (km 122.5), Kitai – Lituhi (km 90) na ukarabati wa barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200). Mradi huu pia unahusisha kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130).

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na Ofisi za Mikoa: Shilingi milioni 6,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

**Ujenzi wa Barabara ya Kwenda Chuo cha Uongozi (km 8.8):** Jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hizo.

**Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi ya Nne (km 69.8):** Jumla ya **Shilingi milioni 46,828.60** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Pili, Tatu na Nne.

**MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA**

***292. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu ya kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu.

***293. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,211.00** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi katika maeneo ya Nyakanazi na Manyoni, ukaguzi wa usalama wa barabara, mapitio ya Sera ya

Usalama Barabarani, ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo mdogo Dar es Salaam (Slow Weigh in Motion Weighbridge), ujenzi wa miundombinu na uwekaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani katika vyuo vya Polisi nchini pamoja na kuweka mfumo wa kudhibiti mwendokasi kwa vyombo vya usafiri barabarani katika barabara kuu nchini. Aidha, jumla ya **Shilingi milioni 141.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutoa elimu ya usalama barabarani kwa umma pamoja na utoaji wa elimu ya usalama barabarani mashuleni.

***294. Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Menejimenti ya Utunzaji wa Mazingira** katika mwaka wa fedha 2018/2019, umetengewa **Shilingi milioni 148.00** fedha za ndani kwa ajili ya kutoa mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira na hifadhi ya mazingira katika Sekta ya Ujenzi kwa wahandisi na mafundi sanifu kutoka TANROADS, TEMESA na TBA; kutoa elimu ya usimamizi wa mazingira pamoja na kuandaa mfumo wa kusimamia mazingira (Environmental Management System). Kazi nyingine ni kufanya ukaguzi wa mazingira katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuandaa mpango wa kukabili mabadiliko ya tabianchi na kuandaa programu za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta (Pollution Control Programme) ikihusisha kuandaa machapisho na matangazo yanayohusu utunzaji na kuhifadhi mazingira kwa umma kwa njia ya redio, luninga, vipeperushi na magazeti.

## MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE

***295. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, miradi ya viwanja vya ndege imetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 215,000.00** Kati ya hizo fedha za ndani ni **Shilingi milioni 115,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi milioni 100,000.00**. Miradi ifuatayo itatekelezwa:

### Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma

***296. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,370.75.** Fedha hizi

zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria, maegesho ya ndege, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Kazi nyingine ni pamoja na ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani pamoja na uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda**

***297. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi wa ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya viungio na maegesho ya ndege.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

***298. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10,386.43** kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi inayohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Fedha hizi zitatumika pia kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa awamu ya pili ya mradi iliyohusisha ukarabati wa barabara ya pili ya kuruka na kutua ndege. Kazi nyingine ni ujenzi wa barabara ya kiungio pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

***299. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,724.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Kazi nyingine ni ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya kiungio pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege (RESA).

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

***300. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019,

mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,550.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria. Kazi nyingine ni kuendelea na upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo, uzio wa kiwanja pamoja na maegesho ya ndege za mizigo. Aidha, kazi nyingine ni ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na ujenzi wa mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha**

***301. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,100.00** kwa ajili ya kuanza upanuzi wa jengo la abiria, kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa meta 200 na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pad). Kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama, barabara mpya ya kuingilia kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

***302. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 12,848.00** kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio pamoja na maegesho ya ndege. Kazi nyingine ni kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia kiwanjani na maegesho ya magari.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

***303. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,440.00.** Fedha hizi zitatumika kulipa fidia kwa mali zitakazoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu na kuanza ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

***304. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,215.00.** Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na kujenga uzio wa usalama.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro**

***305. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,530.00** kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina na kuanza ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa maegesho ya magari.

**Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

***306. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 62,437.50** kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya mikoa vya Geita, Iringa, Ruvuma, Lindi, Tanga, Mara, kiwanja kipya cha Mkoa wa Simiyu pamoja na kiwanja cha Lake Manyara. Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ukarabati wa viwanja vingine vya mikoa na kukarabati jengo la abiria pamoja na kumalizia ulipaji wa fidia kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato**

***307. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,518.50** kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina na kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanja kipya cha Msalato mkoani Dodoma. Aidha, kazi nyingine ni kulipa fidia kwa mali zitakazoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**

***308. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 2,200.00** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la watu mashuhuri (VIP Lounge), usanifu wa kina kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**

***309. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/ 2019, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 67,179.82** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) pamoja na kuanza ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria. Kazi nyingine ni kulipa fidia kwa wakazi wa Kipunguni na Kigilagila na ununuzi wa viwanja 537 vya makazi kwa ajili ya wananchi waliohamishwa kupisha utekelezaji wa mradi huu.

**FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA**

***310. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 908,808,000,000.00** zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake (TANROADS na Bodi ya Mfuko wa Barabara) imetengewa **Shilingi 636,166,000,000.00** na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi yake (TARURA) imetengewa **Shilingi 272,642,000,000.00.**

***311. Mheshimiwa Spika,*** kati ya **Shilingi 636,166,000,000.00** zilizotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), TANROADS imetengewa **Shilingi 567,625,475,000.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara (Sekta ya Ujenzi) imetengewa **Shilingi 63,069,497,240.00** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,471,027,760.00**

zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 3 - 5.**

**Miradi ya Barabara Kuu**

***312. Mheshimiwa Spika,*** fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa miradi ya barabara kuu ni **Shilingi 16,159,929,000.** Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Barabara Kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kilometa **3,586.80.** Orodha ya miradi ya barabara kuu itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3**.

**Miradi ya Barabara za Mikoa**

***313. Mheshimiwa Spika,*** fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa miradi ya barabara za mikoa ni **Shilingi 33,583,664,000.00** zitakazotumika kufanya ukarabati wa jumla ya **kilometa 478** kwa kiwango cha changarawe na kujenga **kilometa 24.67** kwa kiwango cha lami na kukarabati **madaraja 15** katika mikoa mbalimbali nchini. Orodha ya miradi ya barabara za mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4**.

**Miradi ya Vivuko**

***314. Mheshimiwa Spika,*** fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko ni **Shilingi 5,131,392,000.00.** Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 3.**

**Miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira**

***315. Mheshimiwa Spika,*** fedha za Mfuko wa Barabara

zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira ni **Shilingi 2,800,917,000.00.** Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.3.**

**Kazi Zinazohusu Shughuli za Barabara**

***316. Mheshimiwa Spika,*** kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara (Ujenzi) pamoja na kujenga uwezo wa watumishi zimetengewa **Shilingi 5,393,595,240.00** kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.3.**

**Matengenezo ya Barabara**

***317. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 567,625.475** fedha za Mfuko wa Barabara zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja, uendeshaji wa mizani, gharama za usimamizi wa Wakala wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2018/2019**.** Mchanganuo wa mpango huo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A hadi 5E.**

**MPANGO WA UTEKELEZAJI KAZI KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Wakala wa Barabara**

***318. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wakala umepanga kujenga barabara zenye urefu wa **kilometa 597.10** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **15** pamoja na ukarabati wa **kilometa 72.10** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Aidha, Wakala umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometa 32,653.92**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi ya **kilometa 6,292.95** na matengenezo ya madaraja **3,281**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi ya barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu (Performance Based Management and Maintanance of Roads).

***319. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala utajenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometa 61.18** ambapo **kilometa 36.51** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 24.67** zitajengwa kwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 1,084.12** zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo **kilometa 606.12** na madaraja **15** yatakarabatiwa kwa kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 478.00** pamoja na madaraja **15** yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

**Wakala wa Majengo (TBA)**

***320. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wakala wa Majengo utaendelea kutekeleza kazi zinazoendelea ikiwemo ujenzi wa nyumba za wakazi wa Magomeni Kota, ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Uchaguzi (NEC) Dodoma, ujenzi wa nyumba za Askari Magereza - Ukonga, Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa maabara ya *Tanzania Atomic Energy Commission* Njiro, Arusha.

***321. Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine itakayoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa Kituo cha Tiba cha Mwalimu Nyerere (Mwalimu Nyerere Medical Center) Musoma, ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Geita, ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Handeni, ujenzi wa jengo la ofisi ya mkoa wa Njombe (Block A Lunyanywi A), ujenzi wa wodi ya upasuaji (theatre na surgical) katika hospitali ya Mkoa wa Mbeya, ujenzi wa jengo la utawala/OPD Hospitali ya Sekou Toure Mwanza pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Chato.

Wakala pia umepanga kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri Butiama, ujenzi wa jengo la utawala/OPD la hospitali ya Mkoa wa Simiyu, ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Uvinza Kigoma, ujenzi wa jengo la utawala na mikutano Wilaya ya Kyerwa Kagera, ujenzi wa nyumba za makazi za Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Mkoa

wa Songwe (phase 1) pamoja na ujenzi wa Chuo cha Muhimbili Kampasi ya Mloganzila (MUHAS).

***322. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni ujenzi wa ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kasulu, ujenzi wa jengo la maktaba Chuo Kikuu cha Mbeya (MUST), ujenzi wa jengo la utawala la Mkurugenzi wa Wilaya ya Mlele, ujenzi wa jengo la *x-ray* katika Hospitali ya Rufaa, Mbeya na ujenzi wa ofisi ya mkoa wa Dodoma ya Wakala wa Misitu Tanzania. Vilevile, Wakala utaendelea na mradi wa ukarabati wa majengo ya shule kongwe za Tosamaganga, Azania na Malangali.

**Wakala wa Ufundi na Umeme**

***323. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wakala umepanga kuendelea na upanuzi wa maegesho ya Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni, ujenzi wa maegesho ya Bwina, Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome na ujenzi wa jengo la abiria na ofisi katika maegesho ya kivuko cha Lindi – Kitunda, ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Nyamisati – Mafia, ununuzi wa kivuko kipya cha Chato – Muharamba na Chato – Nkome pamoja na ununuzi wa kivuko kipya cha Nyamisati - Mafia.

Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa kivuko kipya cha Kigongo – Busisi; kukamilisha malipo ya kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni (MV. Kazi) na malipo ya ukarabati wa kivuko cha MV. Pangani II pamoja na ukarabati wa MV. Sengerema, MV. Misungwi na MV. Kigamboni. Aidha, TEMESA itafanya ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa karakana za TEMESA; matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali pamoja na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

***324. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019,

Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 908,808,000,000** zitakazotumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 636,166,000,000** zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na **Shilingi 272,642,000,000** zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za wilaya zilizo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

***325. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itagharamia na kufanya tathmini ya mtandao wa barabara (Road Inventory and Condition Survey) ili kubaini thamani, urefu na hali ya barabara nchini. Takwimu hizi zitasaidia kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini na kupendekeza mgawanyo mpya wa fedha za Mfuko wa Barabara. Bodi ya Mfuko wa Barabara itaendelea kugharamia tafiti za vyanzo vipya vya mapato kwa kuzingatiauzoefu wa kikanda na kimataifa. Aidha, Bodi itaimarisha ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato ya Mfuko na kufanya tafiti juu ya maeneo ambayo yanaweza kusababisha upotevu wa mapato na kuishauri Serikali ipasavyo. Bodi pia itaendelea kushirikiana na taasisi za kitafiti ili kupata teknolojia nafuu ya matengenezo ya barabara ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za Mfuko.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi**

***326. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Bodi imepanga kusajili wahandisi **1,700,** mafundi sanifu **170,** na kampuni za ushauri wa kihandisi **20.** Aidha, Bodi imepanga kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu **1,503.** Idadi hii inahusisha wahandisiwahitimu **1,103** wanaoendelea na mafunzo na **400** wapya wanaofadhiliwa na Serikali, Washirika wa Maendeleo na sekta binafsi. Vilevile, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi pamoja na kutembelea na

kukagua miradi yote ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara. Bodi pia itaendelea kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaam na washauri wote kwa ajili ya kuwaendeleza pamoja na kuwashawishi wahandisi wataalam ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani na hivyo kusogeza huduma hii muhimu karibu na watumiaji.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

***327. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Bodi imepanga kusajili Wataalam **267** katika fani za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani zinazoshabihiana nazo. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **17** za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani zinazoshabihiana nazo. Vilevile, Bodi imepanga kuendelea na mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu **132** katika fani za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani zinazoshabihiana nazo.

***328. Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,300** katika mikoa yote Tanzania Bara na kusajili miradi ya majengo **920.** Aidha, Bodi imepanga kuendesha mashindano ya kubuni mchoro wa jengo la zahanati la gharama nafuu ambao utatolewa kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao utatumika katika ujenzi wa zahanati katika maeneo mbalimbali nchini. Bodi pia itaendeleza mashindano ya insha kwa wanafunzi wa sekondari wa kidato cha pili, ikiwa ni njia ya kuwahamasisha kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na taaluma zinazoshabihiana nazo.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

***329. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Bodi imepanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya **900** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,100.** Aidha, Bodi inatarajia kuendesha kozi tatu (3) za mafunzo kwa makandarasi katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, na Arusha. Vilevile, Bodi imepanga kuendesha warsha mbili (2) za mafunzo ya ubia

(Joint Venture) katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Bodi itaendeleza Mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wa ndani. Aidha, Bodi itaendelea na jitihada za kuhamasisha makandarasi wazalendo kujiunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

***330. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Baraza limepanga kushirikiana na Wizara ili kukamilisha mapitio ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003. Baraza pia litaendelea na taratibu za kufanya mapitio ya sheria iliyoanzisha Baraza na kuandaa Kanuni za Utekelezaji. Lengo ni kuhuisha Baraza liwe Taasisi Kiongozi (Apex Organization) ya kusimamia maendeleo ya Sekta ya Ujenzi pamoja na kuwa na vyanzo endelevu vya mapato. Kazi nyingine ni kuratibu na kutoa mafunzo katika sekta, ushauri wa kiufundi na utatuzi wa migogoro; kufanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi; kuboresha ukusanyaji, uwekaji na utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi pamoja na kuandaa majarida ya kiufundi kuhusu Sekta.

***331. Mheshimiwa Spika,*** Baraza pia litaendelea na taratibu za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (Construction Industry Development Fund (CIDF) pamoja na kuendelea kuratibu mfumo wa majaribio wa kutoa taarifa muhimu za miradi ya ujenzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi [Construction Sector Transparency Initiative (CoST)]. Aidha, Baraza litaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi yenye lengo la kukuza vipato vya wananchi katika maeneo husika. Baraza pia limepanga kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa majengo yake ya uwekezaji katika viwanja vya Regent Estate, Mbezi Beach jijini Dar es Salaam na kiwanja cha Dodoma.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

***332. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019,

Kituo kimepanga kuendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika sekta ya ujenzi na usafirishaji hapa nchini. Kituo kitaandaa na kusambaza majarida yatakayoandaliwa kila robo mwaka kuhusu teknolojia mbalimbali katika sekta ya ujenzi na usafirishaji. Aidha, Kituo kitaendesha mafunzo, warsha na semina kwa wadau kwa lengo la kutatua changamoto zinazoikabili sekta hizi. Kazi nyingine ni kuendesha programu zinazohamasisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wapende masomo ya sayansi na hisabati ili baadaye wasomee fani za uhandisi. Aidha, Kituo kitaendelea kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo ya ujenzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya barabara na usafirishaji hapa nchini. Vilevile, Kituo kitaendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Morgan cha Marekani na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) katika kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya barabara na uchukuzi hapa nchini.

Kituo pia kitaratibu maandalizi ya Mkutano wa kimataifa unaohusu uwekezaji katika miundombinu ya barabara na usafirishaji utakaofanyika Arusha Novemba, 2018. Mkutano huo utaandaliwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirikisho la Barabara Duniani (World Road Association-PIARC) ili kwenda sambamba na kaulimbiu ya ***Tanzania ya Viwanda*** kwa kuboresha miundombinu katika nchi za Afrika Mashariki.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato, Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

***333. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Uchukuzi ni **Shilingi 86,292,678,278.** Aidha, Sekta hii imetengewa jumla ya **Shilingi 2,300,739,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na.6.*** Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

***334. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imetenga **Shilingi milioni 549,143.00**

kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali. Fedha hizi zinajumuisha Shilingi milioni 438,743.00 fedha za ndani na shilingi milioni 110.40 fedha za nje kutoka Benki ya Dunia (IDA) na DFID. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kuendelea na kazi ya kuboresha Gati Na. 1 hadi 7 katika Bandari ya Dar es Salaam;

(ii) Kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia na kutokea meli, pamoja na kuongeza kina cha sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Dar es Salaam;

(iii) Kujenga gati moja lenye urefu wa mita 300, kuboresha mfumo wa usalama, kukarabati barabara na maeneo ya kuhudumia shehena, kuboresha maegesho ya meli na kukarabati eneo la gati Na.3 katika Bandari ya Mtwara; kukamilisha ujenzi wa Gati la Lindi; na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa gati za Kilwa na Rushungi;

(iv) Kukamilisha ukarabati na kuongeza kina cha Gati Namba 2 katika Bandari ya Tanga, ukarabati wa barabara kuelekea lango Na.2 katika bandari ya Tanga na kukamilisha mapitio ya Upembuzi yakinifu wa ujenzi ya Bandari mpya Mwambani - Tanga;

(v) Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Mbegani (Bagamoyo);

(vi) Kukamilisha ujenzi na ukarabati wa magati katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na miundombinu ya usalama;

(vii) Kuendelea kuimarisha matumizi ya mfumo wa usalama bandarini (Port Integrated Security System - ISS);

(viii) Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu katika eneo la Ruvu (Ruvu Dry Port); na

(ix) Kununua mitambo na vifaa vya kuhudumia shehena katika bandari za Mamlaka.

***335. Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu, katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga **Shilingi milioni 20,000** kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi ifuatayo:

(i) Shilingi milioni 1,300 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa meli moja mpya ya kubeba abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika;

(ii) Shilingi milioni 8,000 ili kuendelea na ujenzi wa Meli moja mpya ya kubeba abiria na mizigo katika Ziwa Victoria;

(iii) Shilingi milioni 9,000, kuendelea na ukarabati wa meli ya MV.Victoria;

(iv) Shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa meli ya MV.Butiama;

(v) Shilingi milioni 600 ili kuendelea na ukarabati wa meli ya MV Liemba;

(vi) Shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa meli ya MV Umoja; na

(vii) Shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa meli ya MV Serengeti.

***336. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Kampuni ya Ndege (ATCL) imetengewa **Shilingi milioni 495,600** kwa ajili ya kununua ndege mbili (2), moja aina ya Q400 yenye uwezo wa kubeba abiria 76 na ndege kubwa moja (1) ya masafa marefu aina ya Boeing 787-8 (Dreamliner) yenye uwezo wa kubeba abiria 262. Aidha, fedha hizo zitatumika kulipia bima, gharama za uendeshaji wa ndege (start up cost), mafunzo ya marubani, wahandisi na wahudumu pamoja na ulipaji wa madeni.

***337. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu na huduma zinazotolewa na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Hivyo, Serikali

imetenga **Shilingi milioni 1,506,500** fedha za ndani ili kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kuendelea na ujenzi wa reli ya Kati kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) na Morogoro hadi Makutopora (km 422) kwa *Standard Gauge* ambapo **Shilingi milioni 1,400,000** zimetengwa;

**(ii) Shilingi milioni 100,000** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli ya Isaka- Rusumo (km 371) kwa *Standard gauge* kwa kushirikiana na Serikali ya Rwanda;

**(iii) Shilingi milioni 3,000** zimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kumwajiri mtaalam (transaction advisor) atakayeandaa nyaraka na kusaidia kutafuta fedha za ujenzi wa reli ya Mtwara – Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa *Standard Gauge*;

(iv) Kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam, zikiwemo zile za kwenda maeneo ya Pugu kupitia uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/ Bagamoyo; kumpata Transaction Advisor na kuboresha miundombinu katika stesheni za Ubungo na Pugu, **Shilingi milioni 1,500** zimetengwa; na

**(v) Shilingi milioni 2,000** zimetengwa kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli ya *standard gauge* kati ya Arusha – Musoma, pamoja na matawi ya kwenda Engaruka na Minjingu.

***338. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa reli ya Kati iliyopo inaendelea kutoa huduma, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TRC itaendelea kutekeleza mpango wa uboreshaji wa reli hiyo unaogharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kutandika reli nzito za ratili 80 kwa yadi kati ya Dar es Salaam na Isaka, kukarabati madaraja na makalavati, kuimarisha mitambo muhimu katika karakana za matengenezo ya vichwa vya treni na mabehewa, karakana ya kukarabati reli na

mataruma yake, kukarabati machimbo ya uzalishaji kokoto na matengenezo ya njia ya reli; kuboresha ulinzi na usalama wa mizigo ya wateja na kujenga uwezo wa rasilimali watu.

***339. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation-TASAC) litaendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Wakala wa Meli ya Namba 14 ya Mwaka 2017. Majukumu yatakayotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kudhibiti usafirishaji wa nyara za Serikali, Madini na Makinikia na mapato ya Serikali yatokanayo na kodi, ada na kamisheni ya utoaji wa huduma za uwakala wa meli;

(ii) Kusajili na kusimamia meli zote nchini;

(iii) Kufanya ukaguzi wa ubora na usalama wa meli zifanyazo kazi nchini na zinazotoka nje ya nchi;

(iv) Kusimamia ubora wa elimu ya mabaharia inayotolewa na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kulingana na Mkataba wa Kimataifa wa Ufundishaji na Utoaji vyeti vya mabaharia;

(v) Kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na meli katika bahari na maziwa;

(vi) Kusimamia ujenzi wa meli mpya na zenye kuhitaji marekebisho makubwa;

(vii) Kuweka mifumo mbalimbali ya kielektroniki itakayoiwezesha Shirika kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

(viii) Kuajiri watumishi wenye sifa hasa katika eneo la utoaji huduma za biashara za uwakala wa meli, uhakiki shehena na uondoshaji shehena bandarini; na

(ix) Kufungua ofisi katika mikoa ya Tanzania Bara yenye shughuli za usafiri majini.

***340. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) itaendelea kudhibiti huduma za usafiri wa anga. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, TCAA imetenga katika bajeti yake **Shilingi milioni 9,290** ili kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Shilingi bilioni 7 kwa ajili ya kukamilisha ununuzi na usimikaji wa rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia katika viwanja vya JNIA, KIA, Mwanza na Songwe;

ii. Shilingi milioni 641 kwa ajili ya kununua na kisimika vifaa vya mawasiliano ya sauti kati ya marubani na waongozaji ndege katika viwanja vya ndege vya Dodoma, Songwe na Pemba;

iii. Shilingi milioni 550 kwa ajili ya kununua mitambo ya kupeleka taarifa za hali ya hewa kwa marubani na waongozaji ndege (Automatic Terminal Information Services – ATIS na Automatic Weather observation System AWOS) kwenye Kiwanja cha ndege cha KIA;

iv. Shilingi milioni 559 kwa ajili ya kufanya uhakiki wa vifaa vya kuongozea mienendo ya ndege;

v. Shilingi milioni 400 kwa ajili ya kununua mfumo wa usambazaji taarifa za ndege kimtandao (AXIM - Aeronautical Information Exchange Modal); na

vi. Shilingi milioni 140 kwa ajili ya kuendelea na mchakato wa kufunga mtambo wa ILS huko Zanzibar.

***341. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Sekta ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetengewa **Shilingi milioni 6,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Ununuzi wa Magari ya Zimamoto kwa Viwanja vya Ndege vya Mpanda, Shinyanga na Iringa;

ii. Ununuzi wa mitambo ya ukaguzi wa abiria na mizigo (X-ray machines-13) kwa ajili ya Viwanja vya Ndege vya Mwanza,

Iringa, Songea, Kigoma, Dodoma, Musoma, Songwe, Mtwara, Kilwa - Masoko, Lindi, Nachingwea, Moshi na Bukoba;

iii. Ununuzi wa Kamera zenye mifumo ya kufuatilia matukio ya kiusalama (CCTV) katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma na Mtwara;

iv. Upembuzi Yakinifu na kuandaa Mpango Kabambe wa Mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kwa wafanyakazi;

v. Ununuzi wa Vifaa vya Mawasiliano katika Viwanja vya Ndege vya Arusha, Songea, Kahama, Mafia na Iringa;

vi. Kukamilisha Uandaaji wa Matumizi ya Ardhi katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Songwe, Arusha na Msalato;

vii. Mapitio ya Upembuzi Yakinifu wa Viwanja vya Ndege vya Arusha, Mafia na Mwanza;

viii. Kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Mkoa wa Manyara;

ix. Kukamilisha ujenzi wa uzio wa usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na kuanza ujenzi wa uzio wa usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe; na

x. Kukamilisha usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Songwe.

***342. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, shughuli zitakazotekelezwa katika KIA ni pamoja na:

i. Kuendelea kuboresha huduma katika uwanja wa ndege kwa kukamilisha ukarabati wa Jengo la abiria;

ii. Kuendelea kushughulikia suala la kuhakiki mipaka ya kiwanja, kuweka alama za mipaka, kufanya tathmini ya kulipa fidia wananchi walioko katika eneo la uwanja; na

iii. Kujengauwezo wa kitaasisi katika kutoa huduma kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuzingatia matakwa na viwango vya kitaifa na kimataifa.

***343. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali kupitia SUMATRA imetenga **Shilingi milioni 60,704** katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuongeza uwezo wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

ii. Kuimarisha ushindani na kuhakikisha huduma za usafiri wa nchi kavu zinakuwa endelevu;

iii. Kuimarisha usalama, ulinzi na ubora wa huduma za usafiri wa nchi kavu;

iv. Kuhakikisha mazingira endelevu sambamba na maendeleo ya huduma ya usafiri kwa jamii; na

v. Kuboresha sheria, kanuni na mahusiano ya kitaasisi katika sekta za usafiri wa nchi kavu.

***344. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) imetenga **Shilingi milioni 20,500** kutokana na mapato yake ili kuendelea kuboresha huduma. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(i) Ukarabati wa majengo ya karakana ya Dar es Salaam, mitambo, vifaa na mashine mbalimbali ikijumuisha Karakana ya Mbeya, kiwanda cha kokoto na uzalishaji wa mataruma ya zege cha Kongolo;

(ii) Kuimarisha stesheni ya Matambwe/Fuga ili kuongeza utalii katika mbuga ya Seluos na kusafirisha vifaa vya ujenzi wa Mradi wa Umeme wa *Stiegler's gorge*;

(iii) Kufanya upembuzi yakinifu wa tawi la reli Mlowo hadi Machimbo (km 20) kwa ajili ya kuhudumia Makaa ya Mawe ya Magamba, Songwe;

(iv) Kufanya upembuzi yakinifu wa tawi la reli kutoka Mbegani Bagamoyo hadi stesheni ya Mzenga (km 150);

(v) Kukarabati mabehewa ya abiria 21 kwa ajili ya treni ya kusafirisha abiria Jijini Dar es Salaam na Udzungwa;

(vi) Ununuzi wa mataruma ya mbao 11,000 na ukarabati wa njia ya reli kwa kilometa 100;

(vii) Ukarabati na uimarishaji wa miundombinu ya njia kuu ya reli iliyopo;

(viii) Matengenezo na ukarabati wa vichwa vya treni vilivyopo, mitambo, mabehewa ya mizigo na ya abiria; na

(ix) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kujenga uwezo wa rasilimali watu.

***345. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ubora wa huduma za sekta ya hali ya hewa, katika mwaka 2018/2019, TMA imetengewa **Shilingi milioni 20,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Shilingi milioni 13,590 kwa ajili ya ununuzi wa Rada tatu (3) za hali ya hewa;

ii. Shilingi milioni 1,800 kwa ajili ununuzi wa vifaa vya hali ya hewa ikiwemo kubadilisha vifaa vinavyotumia zebaki;

iii. Shilingi milioni 2,500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri, Dodoma;

iv. Shilingi Milioni 1,490 kwa ajili ya ujenzi wa hosteli na ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma; na

v. Shilingi milioni 620 kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa vituo vya hali ya hewa.

***346. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha huduma zinazotolewa za Wakala wa Ndege za Serikali, ili kuendelea

kuimarisha na kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Serikali.Katika mwaka 2018/2019, Wakala unatarajia kufanya matengenezo ya ndege zake kulingana na matakwa ya viwango vya ICAO na TCAA; kukarabati karakana ya ndege, kununua vipuli; na kutoa mafunzo kwa wanahewa na watumishi wa Wakala.

### E.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO

***347. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Mawasiliano ni **Shilingi 3,856,423,000.** Aidha, Sekta hii imetengewa jumla ya **Shilingi 15,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na.7.***

***348. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano imepanga kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

**TEHAMA**

i. Kusimamia utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufikisha huduma za Mkongo hadi Makao Makuu ya Wilaya na watumiaji wa mwisho, ujenzi wa kituo cha data Dodoma na Zanzibar pamoja na ujenzi wa Muundombinu wa Mawasiliano ya Mitandao “Public Key Infrastructure - (PKI)”;

ii. Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Kikanda wa dijitali (RCIP-Digital Tanzania Program);

iii. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao (National Cyber Security Strategy);

**MAWASILIANO**

i. Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Shirika la Posta Tanzania na maboresho ya kuhuisha Sheria ili iendane na mabadiliko ya Teknolojia;

ii. Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi katika miji yote Tanzania Bara na Zanzibar; na

iii. Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Posta (National Postal Strategy, 2017 - 2020) utakaoendana na viwango vya kimataifa.

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

***349. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2018/19, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itatekeleza masuala yafuatayo:

i. Kuendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu sheria, haki na wajibu wa watumiaji, kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa anwani za makazi na Postkodi, uhakiki wa usajili wa laini za simu za kiganjani, wajibu wa watumiaji katika masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kupitia mtandao;

ii. Kuendelea kutekeleza usimamizi wa usalama wa mitandao ya mawasiliano kupitia TZ-CERT;

iii. Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kumbukumbu za simu za kiganjani kwa kushirikiana na watoa huduma wa simu za kiganjani (CEIR);

iv. Kuendelea kuratibu uendelezaji wa viwango vya kitaalam ili viendane na viwango vya kikanda na kimataifa katika vifaa mbalimbali vya mawasiliano;

v. Kuendelea kutekeleza mfumo wa Mobile Number Portability (MNP) kwa kuhamasisha watumiaji wa simu waweze kuhama kwa hiyari kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine ili kuboresha ushindani na kuongeza ubora wa huduma;

vi. Kuendelea kutekeleza mifumo ya utendaji kazi (Quality Management System) ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa Mawasiliano ya simu, Posta na Utangazaji;

vii. Kuratibu uuzaji wa masafa kwa kutumia mnada kama njia mpya ya kuongeza mapato ya Serikali;

viii. Kufuatilia ujenzi wa mifumo na uratibu wa huduma za mawasiliano kwa kutumia mtambo wa TTMS na kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano;

ix. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) ya mwaka 2010 kupitia kanuni zake; na

x. Kuendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa matumizi mabaya ya mtandao kwa Taasisi za Ulinzi na Usalama.

**Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

***350. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 Shirika la Posta Tanzania litatekeleza masuala yafuatayo:

i. Shirika litaendelea kuimarisha huduma yake ya Posta Mlangoni katika usambazaji wa barua, nyaraka, vipeto na vifurushi kwa kupitia mfumo wa Postikodi na anwani za makazi.

ii. Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa kuongeza ofisi 10 zilizounganishwa katika mtandao wa kielektroniki wa *Postglobal Netsmart* hadi kufikia ofisi 150. Kuunganishwa kwa ofisi hizi kutaziwezesha kutoa huduma za kufuatilia (Track and Trace) nyaraka, vifurushi na vipeto vinavyotumwa kupitia mtandao wa Posta wa Postal Global Netsmart pia Shirika litaunganisha kompyuta zake zinazotumika kwa wateja katka mfumo wa kielekitroniki wa Kodi (EFD) ili kuboresha ukusanyaji wa kodi kwa kila Ofisi ya Posta;

iii. Kuimarisha huduma za Duka Mtandao zilizoanzishwa kupitia tovuti: **http://www. stamps.tz.post** ;

iv. Kupanua huduma ya vituo vya *Jamii Centre* kwa kuongeza eneo la kituo cha Azikiwe (GPO), na kuanzisha vipya katika miji ya Dodoma, Morogoro, Mwanza, Arusha na Zanzibar;

v. Kuanzisha ujenzi wa majengo mapya ya uendeshaji kwa awamu katika maeneo ya Dodoma, Bariadi - Simiyu na Ngara Kagera; na kuendelea kufanyia matengenezo majengo ya kutolea huduma za Posta ili yaweze kuendelea kuwa na mvuto kwa wateja; na

vi. Kuendelea kuimarisha utendaji kwa kutekeleza muundo mpya wa Shirika pamoja na kupata vitendea kazi kama vile kununua magari 25, pikipiki 30 za kusafirisha na kusambaza barua, kompyuta, mizani, mihuri na mifuko ya kubebea barua na vifurushi na vifaa vya usalama kama *CCTV* na *Baggage Scanner.*

**Shirika la Mawasiliano Tanzania**

***351. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2018/19 Shirika la Mawasiliano Tanzania litatekeleza yafuatayo:-

i. Kupanua Mtandao pamoja na kujenga, kusimamia na kuendesha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kituo mahiri cha kutunzia kumbukumbu (National Internet Data Centre);

ii. Kupanua mtandao wa mawasiliano wa Mikutano (Audio, Video and Web Conference) ili kuweza kuwafikia wateja wengi zaidi nchini.

iii. Kuongeza Tija na Ufanisi wa Shirika la Mawasiliano Tanzania kwa kuboresha mapato hadi Shilingi bilioni 345.2 mwaka wa fedha 2018/19;

iv. Kuongeza idadi ya wateja hai (Active Customers) wa huduma mbalimbali za simu (voice na data) kutoka 488,537 mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 1,704,627 kwa mwaka wa fedha 2018/19;

v. Kuendelea na uboreshaji wa makusanyo ya Mapato na

Madeni ya Kampuni yanayotokana na huduma za simu zinazotolewa kila mwezi kwa wateja wake, ikiwemo Serikali kuu na taasisi zake; na

vi. Shirika la Mawasiliano Tanzania litaendelea na jukumu la kuhakikisha kuwa mawasiliano ya kuaminika katika nyanja zote yanapatikana ili kuisadia Serikali kwenye ajenda ya maendeleo ya kiuchumi kuelekea Tanzania ya Viwanda.

**Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

***352. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/19, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) utatekeleza kazi zifuatazo:

i. Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini katika kata 156 ili kuhakikisha kuwa huduma zinawafikia wananchi;

ii. Mfuko unatarajia kutoa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule 120;

iii. Kutekeleza mradi wa kuanzisha vituo 10 vya TEHAMA nchini kwa kutumia ofisi za Posta;

iv. Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 360; na

v. Kuendeleza ushirikiano na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili katika uunganishwaji wa mtandao wa mawasiliano katika hospitali za Serikali ili kuleta ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo la uhaba wa madaktari bingwa.

**Tume ya TEHAMA (ICTC)**

***353. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/19, Tume ya TEHAMA itatekeleza mambo yafuatayo:

i. Kusajili na kuendeleza wataalam wa TEHAMA kupitia programu mbalimbali za mafunzo ili kujenga uwezo wa kitaalam wenye ushindani katika soko la ajira;

ii. Kukuza uwekezaji katika TEHAMA kwa kushirikiana na sekta binafsi ikiwemo kuendeleza wajasiriamali wadogo wadogo wa TEHAMA hapa nchini pamoja na kushirikiana na makampuni ya TEHAMA nchini na nje ya nchi; na

iii. Kuandaa majukwaa ya kitaalam na Biashara (ICT Professionals and Business Forums) kama mkakati wa kukuza ufahamu wa masuala ya TEHAMA kwa wataalam, kuvutia zaidi shughuli za ubunifu na biashara za TEHAMA kutoka nje ya nchi pamoja na kukuza zile za hapa nchini.

## E.2 TAASISI ZA MAFUNZO Chuo cha Ujenzi Morogoro

***354. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Chuo cha Ujenzi Morogoro kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,200** katika fani za ufundi sanifu na ufundi stadi wa fani za barabara, madaraja, majengo, magari na mitambo. Kozi nyingine zitahusu mafunzo ya kompyuta, udereva wa magari ya umma na magari ya abiria pamoja na uendeshaji wa mitambo. Aidha, Chuo kimepanga kuendelea kufanya ukarabati wa mitambo mitatu ya ujenzi wa barabara itakayotumika katika mafunzo kwa vitendo. Kazi nyingine ni kumalizia ujenzi wa karakana ya ufundi magari, kununua vifaa vya maabara ya barabara na majengo pamoja na kufanya tathmini ya mafunzo yanayotolewa na Chuo kwa Wilaya zote za Tanzania Bara na Visiwani.

## Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATTI) - Mbeya

***355. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Chuo kimepanga kuendesha mafunzo ya kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yatakayohusisha ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa mafundi sanifu 30 na wasimamizi wa barabara 30 pamoja na uwekaji wa tabaka la lami kwa washiriki 10. Chuo pia kimepanga kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake kushiriki katika kazi za barabara hapa nchini; kutoa mafunzo kwa viongozi wa vikundi mbalimbali vya ujenzi kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na kuhamasisha na

kusambaza matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa wadau wa sekta ya ujenzi katika mikoa 14 ambayo ni Mbeya, Njombe, Rukwa, Dodoma, Morogoro, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Kigoma.

Chuo kimepanga kufanya tathmini ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi nchini na kuwajengea uwezo watumishi wake hususan wakufunzi kwa kutembelea vyuo vinavyotoa mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi nje ya nchi ili kuleta ufanisi katika ufundishaji. Aidha, Chuo kimepanga kuendelea kushiriki kwenye mikutano na maonesho mbalimbali ya wadau wa sekta ya ujenzi ndani na nje ya nchi ili kuhamasisha Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika ujenzi wa barabara.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

***356. Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeendelea kukabiliwa na changamoto za uhaba na uchakavu wa miundombinu. Ili kukabiliana na changamoto hizo, katika mwaka 2018/2019, **Shilingi milioni 10,300** zimetengwa katika mapato ya ndani ya Chuo kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa Kituo Cha Raslimali Mafunzo (Jengo la Maktaba);

ii. Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Ukaguzi wa Magari;

iii. Kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa uzio; na

iv. Kupanua miundombinu ya Chuo kukidhi mahitaji ya wanafunzi.

**Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

***357. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kimetengewa **Shilingi milioni 5,590** katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kutafuta mbiakwaajiliyauendelezaji wamiundombinu ya chuo katika eneo la Mkuranga na lile la Sokoine Drive;

ii) Kununua vifaa vipya na kukarabati vifaa vilivyopo vya kufundishia;

iii) Kuimarisha huduma za Maktaba kielektroniki; na

iv) Kukarabati Majengo ya Chuo.

**Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma**

***358. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali imetenga Shilingi milioni 1,490 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hosteli za Chuo pamoja na kukarabati miundombinu ya Chuo na nyumba za walimu.

## E.3 MASUALA MTAMBUKA

**Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara**

***359. Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara imepanga kutoa mafunzo ya namna ya kufanya huduma za ununuzi wa miradi ya barabara kwa makandarasi wanawake; kutoa mafunzo kwa vikundi vya wanawake juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi pamoja na kufuatilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na makandarasi wanawake. Aidha, Wizara imepanga kutembelea vyuo vya elimu ya juu ili kufuatilia idadi ya wanawake wanaosoma masomo ya sayansi, uhandisi na hisabati kwa lengo la kutumia takwimu hizo katika mipango ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta ya ujenzi. Kazi nyingine ni kuendelea kusambaza nakala za miongozo ya ushirikishaji wa wanawake katika kazi za barabara.

## F. SHUKURANI

***360. Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati ninapenda

kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa **Elias John Kwandikwa, Naibu Waziri (Ujenzi);** Mheshimiwa **Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, Naibu Waziri (Uchukuzi na Mawasiliano);** Makatibu Wakuu **Mhandisi Joseph M. Nyamhanga** (Ujenzi); **Mhandisi Dkt. Leonard M. Chamuriho** (Uchukuzi); **Mhandisi Dkt. Maria L. Sasabo** (Mawasiliano) na **Mhandisi Angelina Madete**, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano). Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

***361. Mheshimiwa Spika,*** naomba kuwatambua nakuwashukuruwashirikambalimbali wamaendeleo ambao wamekuwa bega kwa bega na Wizara katika utekelezaji wa programu na mipango yetu ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Washirika wa Maendeleo wanajumuisha mashirika na taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu. Washirika hao wa maendeleo ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uholanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, OPEC Fund, BADEA, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF na TIB, Asasi Zisizokuwa za KiSerikali pamoja na sekta binafsi.

***362. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya sekta zetu. Shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa wabunge wenzangu kwa michango yenu ambayo imesaidia katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba muendelee na moyo huo ili tuweze kuendeleza sekta hizi ambazo ni kichocheo katika maendeleo ya Sekta nyingine za kiuchumi na kijamii.

***363. Mheshimiwa Spika,*** mwisho, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na Naibu Spika. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti za Sekta ya Ujenzi (www. mow.go.tz), Sekta ya Uchukuzi (www.uchukuzi.go.tz) na Sekta ya Mawasiliano (www.mst.go.tz).

## G. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

***364. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilianoinaombakuidhinishiwajumlaya**Shilingi 4,270,879,381,704.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,864,991,280,426.00** nikwaajiliya Sekta ya Ujenzi, **Shilingi2,387,031,678,278.00ni** kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na **Shilingi 18,856,423,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

### SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)

***365. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 1,864,991,280,426.00** za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha **Shilingi 42,898,011,066.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 31,075,545,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 11,822,466,066.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi **1,822,093,269,360.00** ambazo zinajumuisha **Shilingi 1,386,165,670,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 435,927,599,360.00** fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 636,166,000,000.00** kutoka Mfuko wa Barabara.

### SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)

***366. Mheshimiwa Spika,*** ili Sekta ya Uchukuzi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika mwaka 2018/2019, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,387,031,678,278.00** Fedha hizi zinajumuisha

**Shilingi 86,292,678,278.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 57,828,541,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na Shilingi **28,464,137,278.00** ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa ni **Shilingi 2,300,739,000,000.00** ambazo ni fedha za ndani.

**SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)**

***367. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 18,856,423,000.00** za Sekta ya Mawasiliano, zinajumuisha **Shilingi 3,856,423,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 1,930,485,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,925,938,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 15,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, zikiwa ni fedha za ndani.

***368. Mheshimiwa Spika***, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 (**Kiambatisho Na. 1-7)** ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

***369. Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yako nzuri. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Kakoso, karibu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni ya Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge

ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza inahusu utangulizi, sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa. Sehemu ya pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo; kwanza ni Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2017/2018; mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili; Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu manne ambayo ni makisio na ukusanyaji wa mapato ya mwaka wa fedha 2018/2019, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2018/2019 na mambo mengine yaliyojitokeza wakati wa kujadili, kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu imejielekeza katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyika ya uchambuzi katika Fungu 62 - Sekta ya Uchukuzi, Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi na Fungu 68 - Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya mapato; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Fungu 68, Sekta ya Mawasiliano ilikusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 2,200,000,000 na shilingi 10,907,180,261.25 kutoka huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Februari, 2018. Aidha, makusanyo mengine ya Sekta

ya Mawasiliano ni kutokana na mfumo wa *TTMS* ambao ilikusanya kiasi cha shilingi 8,716,083,646.58.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 62,002,000,000.00 kupitia idara zenye vyanzo vya mapato. Hadi kufika mwezi Machi, 2018 jumla ya shilingi 26,120,000,000.00 zilikusanywa sawa na asilimia 42.13 ya kiwango kilichokadiriwa na kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa hali ya fedha; Sehemu hii inabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo na sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Jedwali limeonesha. Mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa sekta ya ujenzi ni wa kuridhisha kwani hadi mwezi Machi, 2018 asilimia 74 ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo ilikuwa imeshatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tofauti na ilivyo kwenye Sekta ya Uchukuzi ambako utolewaji wa fedha siyo wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 fedha zilizotolewa hazizidi asilimia 45. Hali hii ni mbaya zaidi kwa Sekta ya Mawasiliano ambayo katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni kumi na nne na hadi kufikiwa mwezi Machi, 2018 hakuna fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokutolewa kwa wakati kwa fedha za miradi ya maendeleo katika Sekta ya Uchukuzi na Mawasiliano imekuwa ni changamoto kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 baadhi ya miradi haikuwa imepata fedha yoyote. Miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kati ya Mtwara-M/bay, Mchuchuma, Liganga, ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tanga - Arusha hadi Musoma, kuboresha miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji - *NIT* na mradi wa usafiri wa treni ya Dar es Salaam. Miradi mingine ni pamoja na mradi wa Anuani ya Makazi na Misimbo za Posta, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, mradi wa kituo cha kutengenezea vifaa vya TEHAMA na mawasiliano, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya miradi kwa mwaka 2017/2018; Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 21 Machi, 2018, ambapo Kamati iliweza kutembelea baadhi ya miradi ya sekta ya ujenzi na uchukuzi katika Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali lifuatalo linaonesha miradi iliyokaguliwa ikihusisha fedha zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 na fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Kamati ilipotembelea miradi hiyo. Jedwali limeonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyobainika katika ziara hiyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza; hadi Kamati ilipotembelea mradi huu, kati ya shilingi 9,300,820,927 fedha za ndani kwa ajili ya kumalizia kazi ya ujenzi wa jengo jipya la kuongozea ndege, kurefusha barabara ya kutua na kuruka ndege, upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa uzio, ujenzi wa jengo la mizigo, usimikaji wa taa za kuongozea ndege, kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na miundombinu yake pamoja na barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho yake. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huu ni shilingi 15,000,000 tu zilikuwa zimetolewa. Hali hii si nzuri katika kuendeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili ni Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Mwanza. Mradi huu uliidhinishiwa shilingi bilioni 6,295,000,000 mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bandari katika Ziwa Victoria. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huu hakuna fedha yoyote iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria ambao una lengo la kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu (Ziwa Victoria,

Tanganyika na Nyasa) kwa kununua meli mpya na kukarabati zilizopo. Kamati inaipongeza Serikali kwani imetoa kiasi chote cha fedha kilichokuwa kimeidhinishwa cha shilingi 24,496,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa miradi hasa ya sekta ya uchukuzi ni kutokupatikana fedha za miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati; wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo ulihusu masuala muhimu kama vile bandari, reli, viwanja vya ndege, barabara na mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na:-

Kwanza, ushauri wa kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam ili iweze kuvutia wateja wengi na kushindana na bandari nyingine. Kamati imejulishwa kuwa baadhi ya tozo zilizokuwa kikwazo kwa wafanyabiashara zimeangaliwa na kufutwa. Mfano, Serikali imefuta tozo ya ongezeko la thamani kwa huduma zitolewazo na mawakala kwa wenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani *(VAT on transit goods)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Himaya ya Forodha kwa Pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mzigo wa Congo. Mpango huu umesitishwa kuanzia tangu tarehe 28 Februari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wote wa bandari sasa hufanya kazi saa 24 kwa siku zote za juma, hii imesaidia kupunguza muda wa mzigo kukaa bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mradi wa upanuzi na uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam; shughuli mbalimbali zimeendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na tafiti na usanifu wa mradi Gati Namba 1-7 ambapo tafiti na usanifu kwa Gati Namba 1-3 umekamilika. Aidha, ujenzi wa gati la kuhudumia meli za magari *(RoRo berth)* umeanza kwa kujaza kifusi na kuondoa maji;

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu upanuzi wa lango la kuingia bandarini, tathmini ya zabuni ya awali imekamilika na ripoti imewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya idhini. Aidha, tathmini ya zabuni ya kumpata mtaalam mwelekezi imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Gati Namba 13 na14, kamati imejulishwa kuwa mradi huu utatekelezwa katika awamu ya pili ya mradi wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuondolewa kwa baadhi ya tozo kumeongeza shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda na kutoka katika nchi jirani za Burundi, Jumhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia ambapo katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda kwenye nchi hizo ilikuwa ni tani milioni tatu mia nane sitini na nne zikilinganishwa na tani milioni milioni tatu mia moja arobaini na tatu zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya ushauri ni juu ya ujenzi wa reli ya kati na matawi yake yote. Kamati imefamishwa kuwa ujenzi wa reli hii ya kati kwa kiwango cha kimataifa unaendelea kwa awamu. Awamu ya kwanza utekelezaji wake umefikia asilimia tisa kutoka Dar es Salaam - Morogoro (kilometa 205) na unatarajia kukamilika Novemba, 2019.

Aidha, Awamu ya pili ya kutoka Morogoro-Makutopora (kilometa 336), Mkataba umesainiwa tarehe 29

Septemba, 2017 na jiwe la Msingi kuwekwa tarehe 14 Machi, 2018 ambapo unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuunganisha *RAHCO* na *TRL* ushauri umezingatiwa ambapo mnamo tarehe 28 Februari, 2018 Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* lilianzishwa rasmi ikiwa ni matokeo ya kuunganishwa kwa makampuni hayo na ikiwa ni sehemu ya ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ni kuhusu Serikali kulipa madeni ya wafanyakazi wa *TAZARA;* Kamati imejulishwa kuwa kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha Julai, 2017 hadi Desemba, 2017 jumla ya shilingi 550, 708,500 zimelipwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuhusu ushauri wa kurekebisha gharama za usafirishaji ili kwavutia wafanyabiashara wengi kutumia *TAZARA;* suala hili limezingatiwa ambapo bei ya kusafirisha shaba inayotoka *DRC* kuja Dar es Salaam imepungua kutoka dola za Marekani 110 hadi 90 kwa tani. Aidha, kusafirisha shaba kutoka Ndola, Zambia kuja Bandari ya Dar es Salaam bei imepungua kutoka dola za Marekani 90 hadi 80 kwa tani. Punguzo hili limefanyika hata kwa mizigo ya ndani kama vile mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ushauri huo wa Kamati, *TAZARA* imeweza kuwa na ufanisi ambapo katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Februari, 2018 ilisafirisha shehena ya tani 146,474 ambapo lengo lilikuwa ni kusafirisha tani 200,000 kwa mwaka 2017/2018. Utendaji huu ni sawa na asilimia 73.2 ya lengo lililokuwa limewekwa ukilinganishwa na kipindi cha mwaka 2016/2017 kilichoanzia Julai, 2016 hadi Januari, 2017 ambapo shehena ya tani 93,688 zilisafirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha viwanja vyote vinapatiwa hati miliki, hati miliki zimeendelea kutolewa kwa viwanja vya vya *KIA,* Kigoma, Bukoba na Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganisha makao makuu ya mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwa barabara za lami; baadhi ya barabara hizo zimeanza kufanyiwa kazi mfano, barabara ya Mpanda-Uvinza-Kasulu-Kibondo hadi Nyakanazi inayounganisha Mikoa ya Kagera – Kigoma na Katavi – Tabora. Ujenzi wa barabara ya Njombe- Ndulamo-Makete kilometa 107.4 ambapo inaunganisha Mkoa ya Njombe na Mbeya, barabara ya Mbinga- Mbamba Bay kilometa 67 na Mpemba-Isongole kilometa 51.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupunguza athari za matuta ya barabarani; baadhi ya matuta yameendelea kuondolewa na kupunguzwa ili yawe katika vipimo sahihi kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa usanifu wa barabara wa mwaka ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza mizani za kisasa zinazopima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo; Kamati imejulishwa mizani hiyo ya kisasa zinaendelea kujengwa katika maeneo mengine kama vile Nala (Dodoma), Njuki (Singida), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA)* kuharakisha kupata ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya simu kwa kutumia mtambo wa *Telecommunication Traffic Monitoring System (TTMS)* ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia simu za mkononi. Kamati imejulishwa kuwa uboreshaji Mfumo wa *TTMS* wa *module* ya kuhakiki mapato ya huduma za mawasiliano umefanyika na tayari takwimu za huduma za mawasiliano zinatolewa na Kampuni za Vodacom, Tigo na Airtel. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangilio wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, hususan sekta ya ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni arobaini na tano na milioni mbili

kutoka Idara zenye vyanzo vya mapato kama vile Idara ya Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Kiufundi, Kitengo cha Menejimenti ya Huduma za Ununuzi na Ugavi.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 4.2 ambazo ni sawa na shilingi 4,270,879,381,344. Jedwali linaonesha mchanganuo wa fedha zilizotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka 2018/2019 ambayo ni trilioni 4.2 imeshuka kwa asilimia saba ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha uliopita wa 2017/2018 ambayo ilikuwa ni trilioni 4.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yaliyojitokeza wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi; sekta ya uchukuzi; uimarishwaji wa mtandao wa reli nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya sekta ya uchukuzi ya mwaka 2018/2019 miongoni mwa malengo yaliyowekwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha miundombinu ya reli nchini hususan reli ya kati kwa kiwango cha kisasa *(Standard Gauge).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za ujenzi wa reli ya kati kutoka shilingi bilioni mia tisa zilizoidhinishwa 2017/2018 hadi shilingi trilioni 1.4 zilizotengwa kwa mwaka 2018/2019. Ongezeko hili la asilimia 64 ni kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (kilometa 300) na Morogoro hadi Makutopora kilometa 336. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini mkataba wa awamu ya pili ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Morogoro hadi Makutopora ambapo

mkataba ulisainiwa tarehe 29 Septemba, 2017 na Kampuni ya Yapi Merkezi ya Uturuki. Aidha jiwe la msingi liliwekwa tarehe 14 Machi 2018 ambapo gharama za mradi ni shilingi trilioni 4.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwani, ujenzi wa reli hiyo yenye kasi ya kilometa 160 kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria na malighafi hatimaye kuchochea ukuaji wa viwanda na hata kuongeza pato la taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Kamati kuwa reli hii itajengwa na matawi yake kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika maeneo ambayo yana malighafi nyingi ili reli hii iweze kufanya kazi ipasavyo na kuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, ni matarajio ya Kamati kuwa reli itajengwa na matawi yake kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika maeneo ambayo yana malighafi nyingi ili reli hii iweze kufanya kazi iapasavyo na kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati imejulishwa kuwa zimetengwa shilingi bilioni 6.5 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia ya reli ya kisasa kati ya Mtwara-Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga; Tanga–Arusha–Musoma, pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ikijumuisha njia mpya ya reli katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, zimetengwa shilingi 252,639,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA);* Mamlaka ya Bandari Tanzania ina majukumu ya kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika kuendeleza bandari. Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na Bagamoyo.

Vilevile Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki bandari kadhaa za Maziwa Makuu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na zile zilizopo Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Bandari licha ya kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi pia inahudumia nchi za Burundi, Rwanda, DRC Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nia na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuwa na uchumi wa Viwanda. Ni rai ya kamati kuwa wakati Mamlaka ya Bandari inaendelea kuboresha, kukarabati na kujenga Bandari ya Dar es Salaam pia ianze ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile Bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Bandari zilizopo Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Ndege *(ATCL);* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha dhamira ya dhati ya kufufua Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* ambapo mnamo mwezi Machi, 2018 imepokelewa ndege mpya ya tatu aina ya Bombadier D8-Q400*.* Ujio wa ndege hii umeifanya nchi yetu kuwa na ndege nne. Katika kuendeleza juhudi hizo mwaka wa fedha 2018/2019 imetengwa shilingi bilioni 495,600,000,000 kwa ajili ya kuboresha Kampuni ya Ndege ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, wakati tunaendelea kuongeza idadi ya ndege zilizosalia, ni vyema kuendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazolikabili shirika letu kama vile:-

(i) Uhaba wa rasilimali fedha;

(ii)Upungufu wa wataalam hasa marubani na wahandisi ambao wengi wao wamefikisha umri wa kustaafu;

(iii) Kuchelewa kurejea katika Chama cha Mashirika ya Ndege Duniani *(IATA);* na

(iv)Kushindwa kuanza baadhi ya safari kwa wakati kwenye baadhi ya mikoa kama vile Katavi kutokana na mapungufu katika viwanja hivyo ikiwemo ukosefu wa magari ya zima moto na namba ya usajili wa kiwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa jumla ya kilometa 35,000 ambapo kati ya hizo kilometa 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara zetu ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mipango Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na mikakati ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri zinazoendelea kutekelezwa na sekta ya ujenzi hasa kwenye ujenzi wa barabara nchini changamoto kubwa imekuwa ni rasilimali fedha ambapo kuchelewa kwake mara nyingine kumesababisha gharama za miradi kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujenga barabara kuu ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu na mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwishoni mwa 2017/2018 bado kuna mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara za lami hususan mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya - Makete - Njombe, Lindi - Morogoro,Lindi-Ruvuma, Arusha - Musoma. Aidha, baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ndio imepewa jukumu la kusimamia utendaji kazi za udhibiti wa uzito wa magari barabarani ambapo hadi sasa Wakala huu unamiliki jumla ya mizani 60 ambapo 38 ni ya kudumu, 22 inahamishika na mizani mitatu zinazopima

magari huku yakiwa kwenye mwendo. Pamoja na kuwa na vituo vingi vya kudhibiti uzito wa magari, bado changamoto ya uharibifu wa barabara kutokana na uzito uliopitiliza wa magari imeendelea kuwepo na kuligharimu taifa fedha za kufanya ukarabati wa barabara hizi mara kwa mara. Kamati inaona kuna umuhimu sasa wa kutafuta suluhu ya changamoto hii ili kunusuru barabara zetu na hatimaye ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara; Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mijini na vijijini kwa uwiano wa asilimia 20 kwa barabara za vijijini na asilimia 80 kwa barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa malengo hayo hayo mazuri ambapo mwaka 2017 Serikali ilianzisha Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA)* chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ajili ya kuhudumia barabara zote zilizoko vijijini kwa mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara ambapo sasa *TARURA* inapata mgao wa asilimia 30 na *TANROADS* inapata mgao wa asilimia 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ya viwanda haitowezekana ikiwa barabara hizi za vijijini ambazo nyingi zipo katika hali mbaya na hazipitiki hazitoangaliwa kwa jicho la pekee na kwa haraka ili kurahisisha usafirishaji wa mali ghafi na binadamu. Hii ndiyo sababu kamati inaona kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia na kuangalia upya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo na madai ya wakandarasi; Kamati inatambua kazi kubwa ambayo imefanywa na wakandarasi na wahandisi washauri katika ujenzi hususan kwenye miradi ya barabara. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2018 deni la wakandarasi washauri wa miradi ya barabara ni shilingi bilioni 711.13. Madeni yaliyolipwa ni yale yaliyohakikiwa hadi mwezi Juni, 2017. Aidha, kazi ya uhakik madeni hadi mwezi Juni,

2017 imekamilika na fedha zinaendelea kutolewa kwa ajili ya malipo na madai ya miradi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha wakandarasi wa ndani katika ujenzi wa miradi ya barabara. Kamati ilipokuwa katika ziara yake ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo mwezi Machi, 2018 ikiwa Mkoani Tabora ilifarijika kukuta wakandarasi watatu walioungana ambao wamepewa kazi ya ujenzi wa barabara kwa kipande cha barabara ya lami yenye kilometa 28 kutoka Urambo kwenda Kaliua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taarifa yangu ni kubwa, ninaomba sasa nijikite kwenye sehemu ya maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu wa Kamati umezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo nchini na matarajio ya Kamati kama fedha zilivyotengwa na zilizowakilishwa kwa mwaka 2018/2019. Kamati inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuhusu ujenzi wa reli; Kamati bado inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kati kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimetumika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika tawi la Tabora – Kigoma – Uvinza – Msongati; Kaliua – Mpanda – Kalema na Tabora – Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa, licha ya kuwa reli hii itakuwa ikihudumia na kunufaisha takribani mikoa 15 Tanzania Bara kwa kusafirisha mizigo na abiria, pia itasaidia sana kusafirisha mizigo mingi kwenda nchi jirani kama vile DRC Congo, Burundi na Rwanda. Aidha ujenzi wa reli hii uende sambamba na kudhibiti maeneo korofi kama vile Gulwe na Godegode – Kilosa. Vilevile kuimarisha karakana

za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli, ni vyema sasa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* kuweka alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu unaojitokeza mara kwa mara kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bandari; Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kubakisha angalau asilimia 40 ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza upanuzi na ukarabati wa Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kukamilisha kituo cha pamoja cha huduma kwa wateja *(one stop centre).* Hata hivyo, ili kuongeza ufanisi na mapato katika Bandari ya Dar es Salaam, Kamati bado inasisitiza kufanyika juhudi za makusudi ili kuweza kuhamisha Gati la Mafuta lililopo Kurasini *(KOJ)* na kujenga Gati Namba 13 na 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wote wa bandari waunganishwe kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia Mkuu, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*, Wizara ya Nishati na Madini na wengine kutokuwemo kwenye mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli Kamati inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Huduma za Meli kupanga mipango ya kujiendesha kisasa kwa kuimarisha njia za ukusanyaji mapato kwa njia kielektroniki, kuweka teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli *(flow scanner)* na kuweka mfumo wa kuweza kufatilia mahali meli ilipo kila wakati *(trucking system).* Kwa kufanya haya kutasaidia kuweza kuziba mianya ya upotevu wa fedha za kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Meli Tanzania kufanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na reli kwani kufanya hivyo kutawezesha kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara kuweza kusafirisha mizigo yao kutoka Dar es Salaam mpaka Uganda na hatimaye kupunguza gharama kwa wafanyabiashara na kuongeza pato na hata kampuni hii kuweza kutoa gawio kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kujipanga kutengeneza meli zote 14 zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inalipa deni la mishahara ya miezi 23 kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka kampuni hii itakapoweza kujiendesha, kwani uwekezaji unaofanyika kwa sasa wa kukarabati na kujenga meli mpya katika Maziwa Makuu hautakuwa na tija ikiwa maslahi ya wafanyakazi, hususani mishahara, haitopewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kurasimisha bandari bubu zilizozagaa katika mwambao wa Ziwa Victoria ili kuongeza mapato katika halmashauri na bandari kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAZARA;* Kamati inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wabia wa reli ya *TAZARA* kuendelea na mazungumzo ya kuimarisha reli hii ambapo mahitaji yake ni makubwa kwa uchumi. Kamati inaamini kwa takwimu zilizopo za shehena inayotoka bandarini peke yake na kusafirishwa na reli ya *TAZARA* inatosha kabisa mamlaka hii kuweza kupata uwezo wa kujiendesha kibiashara kwani zipo zaidi ya tani 1,500,000 ambazo zinahitaji kusafirishwa kupitia reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iajiri wafanyakazi wenye ujuzi na weledi wa kutosha ili kuweza kuliongezea

shirika uwezo, kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye Mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe, kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia *TAZARA* mapato makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA);* ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza tija na ufanisi katika viwanja vya ndege nchini, Kamati inashauri Serikali kuipatia mamlaka hii angalau asilimia 50 ya maduhuli *(retention)* yatokanayo na viwanja vya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa yapo mashirika mengi kama *Etihad, Fly Dubai, RwandAir, Jambo Jet* ya Kenya yanayofanya safari za kimataifa na yameonesha nia ya kufanya safari zake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, Kamati inashauri kuwahi kukamilishwa kwa jengo la kuongozea ndege *(tower),* jengo la mizigo, pamoja na kuondoa mapungufu mengine yanayokikabili kiwanja hiki ili kiweze kutumiwa na ndege za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya ujenzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako ndiyo huo.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na naomba tu *Hansard* iwe na kumbukumbu sahihi kwa sababu taarifa hii ni kubwa ukilinganisha taasisi tunazozisimamia ni nyingi ambazo kimsingi zinahitaji gharama kubwa ya uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuongeza kasi ya zoezi la usajili wa namba; sekta hii ni ngumu na sasa katika kuharakisha na kuchochea maendeleo ya nchi, miradi hii iliyo ndani ya sekta hii ni mikubwa, inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha sekta binafsi katika kutekeleza miradi mikubwa kama ile ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, kwa namna ya kipekee, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa akishirikiana na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa *Eng.* Nditiye na Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambao wameipa ushirikiano mkubwa sana Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vilevile inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii, *Eng.* Joseph Nyamuhanga wa Sekta ya Ujenzi, *Eng.* Dkt. Leonard Chamuliho, Sekta ya Uchukuzi, *Eng.* Dkt. Maria Sasabo, Sekta ya Mawasiliano, pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Angelina Madete. Kamati inawashukuru wakuu wote wa taasisi na wakurugenzi, wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa kwa kutoa ushauri na utaalam uliyoiwezesha kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa ambayo waliifanya ya kuchambua na kuangalia taratibu zote za Kamati hii na kuichambua Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge, Ndugu Athuman

Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Richard Masuke pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo:-

i. Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;

ii. Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu manne ambayo ni Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Mambo mengine yaliyojitokeza wakati wa kujadili, kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

c) Sehemu ya Tatu imejielekeza katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyiwa uchambuzi katika Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi), Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi) na Fungu 68 (Sekta ya Mawasiliano).

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.

### 2.1 Makusanyo ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, fungu 68- Sekta ya Mawasiliano ilikusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 2,200,000.00**; na **shilingi 10, 907,180,261.25** kutoka huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Februari, 2018. Aidha, makusanyo mengine ya Sekta

ya Mawasiliano ni kutokana na mfumo wa *TTMS* ambapo ilikusanywa kiasi cha **shilingi 8,716,083,646.58.**

**Mheshimiwa Spika**, fungu 98- Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 62,002,000.00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato. Hadi kufika mwezi Machi, 2018 jumla ya **Shilingi 26,120,000.00** zilikusanywa sawa na **asilimia 42.13** ya kiwango kilichokadiriwa kukusanywa.

## 2.2 **Upatikanaji** wa Fedha kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018.

**Jedwali Na. 1, Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi Kufikia Machi, 2018**

| SEKTA | Fedha zilizoidhinishwa 2017/18 | | | Fedha zilizotolewa hadi Machi, 2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mshahara na Matumizi Mengineyo | Fedha za Ndani za Mradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Mradi ya Maendeleo | Mshahara na Matumizi Mengineyo | Fedha za Ndani za Mradi ya Maendeleo | Fedha za Nje za Mradi ya Maendeleo |
| **Uchukuzi** | 91,142,025,000 | 2,227,646,000,000 | 250,285,182,000 | 53,591,490,874.54(58%) | 974,444,280,000 (44%) | 4,365,400,000(1.74%) |
| **Ujenzi** | 36,032,513,782 | 1,865,443,630,496.20 | 545,582,432,000 | 22,904,459,689.2(0 (63.57%) | 1,375,064,099,005.54 (74%) | 237,882,582,514 (44%) |
| **Mawasiliano** | 4,104,139,000 | 14,000,000,000 | 0 | 2,340,691,977 (57.03%) | 0 | 0 |

*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2017/2018*

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa sekta ya Ujenzi ni wakuridhisha kwani hadi mwezi Machi, 2018 **asilimia 74** ya fedha za ndani za Miradi ya Maendeleo ilikuwa imeshatolewa.

**Mheshimiwa Spika**, hii ni tofauti na ilivyo katika Sekta ya Uchukuzi ambako utolewaji wa fedha siyo wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 fedha zilizotolewa hazizidi **asilimia**

**45**. Hali ni mbaya zaidi kwa Sekta ya Mawasiliano ambayo katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilitengewa **shilingi bilioni 14** na hadi mwezi Machi, 2018 **hakuna** fedha zilizotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokutolewa kwa wakati kwa fedha za miradi ya maendeleo katika sekta ya Uchukuzi na Mawasiliano imekuwa ni changamoto kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 baadhi ya miradi haikuwa imepata fedha yoyote. Miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kati ya Mtwara-M/bay, Mchuchuma & Liganga (Km 1092), ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tanga-Arusha hadi Musoma (Km 1,108), kuboresha miundombinu ya Chuo cha Taifa cha usafirishaji-NIT na mradi wa usafiri wa treni Dar es Salaam. Miradi mingine ni pamoja na mradi wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mradi wa Kituo cha Kutengeneza Vifaa vya TEHAMa na Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

## 2.3 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 21 Machi, 2018 ambapo Kamati iliweza kutembelea baadhi ya miradi ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi katika Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Simiyu.

**Mheshimiwa Spika,** jedwali lifuatalo linaonesha miradi iliyokaguliwa ikihusisha fedha zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 na fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Kamati ilipotembelea miradi hiyo.

**Jedwali Na. 2, Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa na Kamati, Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2018**

| Na | Fungu | Jina la Mradi | Fedha za Miradi zilizoidhinishwa 2017/18 | | Fedha za Miradi zilizotolewa hadi Machi, 2018 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ndani | Nje | Ndani | Nje |
| 1 | 98-Ujenzi | 4130- Barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora | 75,317,746,662.55 | 15,081,250,000.00 | 69,143,212,564.55 | 10,083,713,857.00 |
| | | 4112- Ujenzi wa barabara ya Kigoma-Kidawa-Uvinza-Kaliua | 52,782,816,149.45 | 20,000,000,000.00 | 43,849,958,886.55 | - |
| | | 4152-Barabara ya Tabora - Nzega | 90,801,263,059.75 | - | 81,851,312,608.17 | - |
| | | 4162- Ujenzi wa barabara ya Mwigumbi-Maswa-Bariadi-Lamadi | 59,192,389,350.41 | - | 58,642,889,350.41 | - |
| | | 4155- barabara ya Nyanguge – Musoma-Kisesa bypass | 49,948,407,289.23 | - | 40,594,497,841.23 | - |
| | | 4209- Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza | 4,300,820,927.00 | 5,000,000,000.00 | 15,000,000 | - |
| | | 4118 barabara ya Dodoma - Manyoni | 145,466,784,269 | - | 145,451,780,000 | - |
| 2 | 62 - Uchukuzi | 4230-Mradi wa ukarabati wa Bandari ya Mwanza | 6,295,000,000 | - | - | - |
| | | 4295- Ukarabati wa Meli katika Ziwa Victoria | 24,496,000,000 | - | 24,496,000,000 | - |

*Chanzo; Taarifa ya Kamati ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2017/2018*

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyobainika katika ziara hiyo:-

a) Mradi wa ujenzi na upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Mwanza, hadi Kamati ilipotembelea mradi huu, kati ya **shilingi bilioni 9, 300, 820, 927** fedha za ndani kwa ajili ya kumalizia kazi ya ujenzi wa jengo jipya la kuongezea ndege, kurefusha barabara ya kutua na kuruka ndege, upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa uzio, ujenzi wa jengo la mizigo, usimikaji wa taa za kuongozea ndege, kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na miundombinu yake pamoja na barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho yake. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huu, **shilingi milioni 15,000,000** tu zilikuwa zimetolewa.

b) Mradi wa uboreshaji wa bandari ya Mwanza, uliidhinishiwa **shilingi bilioni 6, 295,000,000** mwaka wa Fedha 2017/18 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bandari katika Ziwa Victoria. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huu hakuna fedha yoyote iliyotolewa.

c) Mradi wa Ukarabati wa Meli katika ziwa Victoria ambao una lengo la kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu yaani (Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa) kwa kununua meli mpya na kukarabati zilizopo. Kamati inaipongeza Serikali kwani imetoa kiasi chote cha fedha kilichokuwa kimeidhinishwa cha **shilingi bilioni 24,496,000,000**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa miradi hasa ya sekta ya Uchukuzi ni kutokupatikana fedha za miradi kwa wakati.

### 2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/18, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri

huo uligusa masuala muhimu kama vile Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege, Barabara na Mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na:-

a) Ushauri wa kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam ili iweze kuvutia wateja wengi na kushindana na bandari zingine.

i) Kamati imejulishwa kuwa baadhi ya tozo zilizokuwa kikwazo kwa wafanyabiashara zimeangaliwa na kufutwa. Mfano, Serikali imefuta tozo ya ongezeko la thamani kwa huduma zitolewazo na mawakala kwa wenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani *(VAT on transit goods);*

ii) Himaya ya Forodha kwa Pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mzigo wa Congo, Mpango huu umesitishwa kuanzia tangu tarehe 28 Februari 2018;

iii) Wadau wote wa bandari sasa hufanya kazi saa 24 kwa siku zote za juma, hii imesaidia kupunguza muda wa mzigo kukaa bandarini;

iv) Mradi wa upanuzi na uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam; shughuli mbalimbali zimeendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na tafiti na usanifu wa mradi Gati Na. 1-7 ambapo tafiti na usanifu kwa Gati Na. 1-3 umekamilika;

Aidha, ujenzi wa gati la kuhudumia meli za magari (RoRo berth) umeanza kwa kujaza kifusi na kuondoa maji;

Vilevile kuhusu upanuzi wa lango la kuingia bandarini, tathmini ya zabuni ya awali imekamilika na ripoti imewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya idhini. Aidha, tathmini ya zabuni ya kumpata Mtaalam Mwelekezi imekamilika;

Kuhusu ujenzi wa Gati Na. 13&14, Kamati imejulishwa kuwa mradi huu utatekelezwa katika awamu ya pili ya mradi wa kuboresha bandari ya Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya kuondolewa kwa baadhi ya tozo kumeongeza shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda na kutoka katika nchi jirani za Burundi, Jumhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia ambapo katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 shehena ya mizigo iliyohudumiwa kwenda kwenye nchi hizo ilikuwa ni tani milioni 3.864 zikilinganishwa na tani milioni 3.143 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/ 2017.

b) Ushauri wa kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake yote;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefamishwa kuwa ujenzi wa reli hii ya kati kwa kiwango cha Kimataifa unaendelea kwa awamu. Awamu ya kwanza utekelezaji wake umefikia asilimia tisa (9%) kutoka Dar es Salaam-Morogoro (km 205) na unatarajia kukamilika Novemba, 2019;

Aidha, Awamu ya pili ya kutoka Morogoro-Makutopora (km 336), Mkataba umesainiwa tarehe 29 Septemba, 2017 na jiwe la Msingi kuwekwa tarehe 14 Machi, 2018 ambapo unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2020;

c) Kuunganisha RAHCO na TRL, ushauri umezingatiwa ambapo mnamo tarehe 28 Februari 2018 Shirika la Reli Tanzania-TRC lilianzishwa rasmi ikiwa ni matokeo ya kuunganishwa kwa Makampuni hayo mawili;

d) Serikali kulipa madeni ya wafanyakazi wa TAZARA; Kamati imejulishwa kuwa kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha Julai, 2017 hadi Desemba, 2017 jumla ya **milioni shilingi 550, 708,500** zimelipwa;

Aidha, kuhusu ushauri wa kurekebisha gharama za usafirishaji ili kwavutia wafanyabiashara wengi kutumia TAZARA; Suala

hili limezingatiwa ambapo bei ya kusafirisha Shaba inayotoka DRC kuja Dar es Salaam imepungua kutoka **Dola za Marekani 110** hadi **90** kwa tani. Aidha, kusafirisha shaba kutoka Ndola Zambia kuja Bandari ya Dar es Salaam bei imepungua kutoka **Dola za Marekani 90** hadi **80** kwa tani. Punguzo hili limefanyika hata kwa mizigo ya ndani kama vile mbao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia ushauri huo wa Kamati, TAZARA imeweza kuwa na ufanisi ambapo katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Februari 2018 ilisafirisha shehena ya **tani 146, 474** ambapo lengo lilikuwa ni kusafirisha **tani 200,000** kwa mwaka 2017/18. Utendaji huu ni sawa na **asilimia 73.2** ya lengo lililokuwa limewekwa ukilinganishwa na kipindi cha mwaka 2016/17 kilichoanzia Julai 2016 hadi Januari ,2017 ambapo shehena ya **tani 93,688** zilisafirishwa.

e) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha viwanja vyote vinapatiwa hati miliki, hati miliki zimeendelea kutolewa kwa viwanja vya vya KIA, Kigoma, Bukoba na Songwe;

f) Kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwa barabara za lami; baadhi ya barabara hizo zimeanza kufanyiwa kazi Mfano, barabara ya Mpanda-Uvinza-Kasulu-Kibondo hadi Nyakanazi inayounganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma na Katavi, ujenzi wa barabara ya Njombe-Ndulamo-Makete (km 107.4)ambapo inaunganisha Mkoa ya Njombe na Mbeya, barabara ya Mbinga- Mbamba Bay (km 67) na Mpemba-Isongole (km 51.2);

g) Kupunguza athari za matuta ya barabarani, baadhi ya matuta yameendelea kuondolewa na kupunguzwa ili yawe katika vipimo sahihi kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa usanifu wa barabara wa mwaka 2011 (*Road Geometric Design Manual*) ya Mwaka 2011;

h) Kuongeza mizani za kisasa zinazopima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo; Kamati imejulishwa mizani hizo za kisasa zinaendelea kujengwa katika maeneo mengine

kama vile Nala (Dodoma), Njuki (Singida), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe);

i) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA kuharakisha kupata ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya simu kwa kutumia mtambo wa *Telecommunication Traffic Monitoring System-TTMS* ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia simu za mkononi; Kamati imejulishwa kuwa uboreshaji Mfumo wa *TTMS* wa *''Module''* ya kuhakiki mapato ya huduma za mawasiliano umefanyika na tayari takwimu za huduma za mawasiliano zinatolewa na Kampuni za Vodacom, Tigo na Airtel.

## 2.5 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/19

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hususan Sekta ya Ujenzi inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi milioni 45,002,000.00** kutoka Idara zenye vyanzo vya mapato kama vile Idara ya Rasilimali Watu, Idara ya Huduma za Kiufundi, Kitengo cha Menejimenti ya Huduma za Ununuzi na Ugavi.

### 2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 4.2 (4,270,879,381,344)**. Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa:-

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2018/2019 ambayo ni **trilioni 4.2** imeshuka kwa **asilimia 7** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha uliopita wa 2017/2018 ambayo ilikuwa **trilioni 4.5.**

### 2.5.3 Mambo Mengine yaliyojitokeza wakati wa Kuchambua na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2018/2019

a) **Sekta ya Uchukuzi**

i. **Uimarishwaji wa Mtandao wa Reli Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** katika mipango ya Sekta ya Uchukuzi ya Mwaka 2018/2019, miongoni mwa malengo yaliyowekwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha miundombinu ya reli nchini hususan reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (*Standard Gauge).*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za ujenzi wa reli ya kati kutoka **shilingi bilioni 900** zilizoidhinishwa 2017/2018 hadi **shilingi trilioni 1.4** zilizotengwa kwa mwaka 2018/19. Ongezeko hili la **asilimia**

**64** ni kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) na Morogoro hadi Makutopora (km 336).

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini mkataba wa awamu ya pili ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Morogoro hadi Makutopora ambapo mkataba ulisainiwa tarehe 29 Septemba, 2017 na Kampuni ya **Yapi Merkezi ya Uturuki**. Aidha, jiwe la msingi liliwekwa tarehe 14 Machi 2018 ambapo gharama za mradi ni **shilingi trilioni 4.3.**

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwani, ujenzi wa reli hiyo yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria na mali ghafi hatimaye kuchochea ukuaji wa viwanda, na hata kuongeza Pato la Taifa.

Ni matarajio ya Kamati kuwa reli hii itajengwa na matawi yake kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika maeneo ambayo yana mali ghafi nyingi ili reli hii iweze kufanya kazi ipasavyo na kuwa na tija.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati imejulishwa kuwa zimetengwa **shilingi bilioni 6.5 (6, 500,000,000.00)** kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia ya reli ya kisasa kati ya Mtwara- Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga; Tanga-Arusha-Musoma, pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu ikijumuisha njia mpya ya reli katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, zimetengwa **shilingi bilion 252,639,000,000** kwa ajili ya Mfuko wa reli.

ii. **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Bandari Tanzania ina majukumu ya kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia Sekta binafsi katika kuendeleza bandari. Mamlaka hii inamiliki na kusimamia Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Kwale, Lindi, Mikindani, Mafia, Pangani na

Bagamoyo. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania inamiliki bandari kadhaa za Maziwa makuu kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Bandari licha ya kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi; pia inahudumia nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa nia na dhamira ya Serikali ya awamu ya tano ni kuwa na uchumi wa Viwanda; ni rai ya Kamati kuwa wakati Mamlaka ya Bandari inaendelea kuboresha, kukarabati na kujenga Bandari ya Dar es Salaam; pia ianze ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na bandari ya Ziwa Nyasa.

iii. **Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha dhamira ya dhati ya kufufua Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ambapo mnamo Mwezi Machi, 2018 imepokelewa ndege mpya ya tatu aina ya Bombadia D8-Q400. Ujio wa ndege hii umeifanya nchi yetu kuwa na ndege nne. Katika kuendeleza juhudi hizo mwaka wa fedha 2018/ 2019 imetengwa **shilingi bilioni 495,600,000,000** kwa ajili ya kuboresha Kampuni ya Ndege ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, wakati tunaendelea kuongeza idadi ya ndege zilizosalia, ni vyema kuendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinazolikabili shirika letu kama vile;-

a) Uhaba wa rasilimali fedha;

b) Upungufu wa wataalam hasa marubani na wahandisi ambao wengi wao wamefikisha umri wa kustaafu;

c) Kuchelewa kurejea katika Chama cha Mashirika ya Ndege Duniani (IATA); na

d) Kushindwa kuanza baadhi ya safari kwa wakati kwenye baadhi ya mikoa kama vile Katavi kutokana na mapungufu katika viwanja hivyo ikiwemo ukosefu wa magari ya zima moto na namba ya usajili wa Kiwanja.

b) **Sekta ya Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa jumla ya kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara zetu ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mipango Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

i. **Miradi ya ujenzi wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri zinazoendelea kutekelezwa za ujenzi wa barabara nchini, changamoto kubwa imekuwa ni rasilimali fedha ambapo kuchelewa kwake mara nyingine kumesababisha gharama za miradi kuongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kujenga barabara kuu ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu na mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwishoni mwa 2017/18 bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara za lami hususan mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya – Makete- Njombe, Lindi- Morogoro,Lindi-Ruvuma n.k. Aidha, baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

ii. **Mizani za Barabarani**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara (TANROADS) ndio imepewa jukumu la kusimamia utendaji kazi za udhibiti wa

uzito wa magari barabarani ambapo hadi sasa Wakala huu unamiliki jumla ya mizani 60 ambapo 38 ni ya kudumu, 22 inahamishika na mizani 3 zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo. Pamoja na kuwa na vituo vingi vya kudhibiti uzito wa magari, bado changamoto ya uharibifu wa barabara kutokana na uzito uliopitiliza wa magari imeendelea kuwepo na kuligharimu Taifa fedha za kufanya ukarabati wa barabara hizi mara kwa mara. Kamati inaona kuna umuhimu sasa wa kutafuta suluhu ya changamoto hii ili kunusuru barabara zetu na hatimae ziweze kudumu kwa muda mrefu.

iii. **Fedha za Mfuko wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mijini na vijijini kwa uwiano wa asilimia 20 kwa barabara za vijijini na asilimia 80 kwa barabara kuu.

**Mheshimiwa Spika,** ni kwa malengo hayo hayo mazuri ambapo Mwaka, 2017, Serikali ilianzisha Wakala wa Barabara Vijijini -TARURA chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI kwa ajili ya kuhudumia barabara zote zilizoko vijijini kwa mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara ambapo sasa TARURA inapata mgao wa asilimia 30 na TANROADS inapata mgao wa asilimia 70.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ya Viwanda haitowezekana ikiwa barabara hizi za vijijini ambazo nyingi zipo katika hali mbaya na hazipitiki hazitoangaliwa kwa jicho la pekee na kwa haraka ili kurahisisha usafirishaji wa mali ghafi na binadamu. Hii ndio sababu Kamati inaona kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia na kuangalia upya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa barabara.

iv. **Malipo ya Madai ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wakandarasi na Wahandisi Washauri katika

ujenzi hususan kwenye miradi ya barabara. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Machi, 2018 deni la Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara ni **shilingi bilioni 711.13**. Madeni yaliyolipwa ni yale yaliyohakikiwa hadi mwezi Juni, 2017. Aidha kazi ya kuhakiki madeni ya hadi mwezi Juni, 2017 imekamilika na fedha zinaendelea kutolewa kwa ajili ya malipo ya madai ya miradi ya barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha wakandarasi wa ndani katika ujenzi wa miradi ya barabara. Kamati ilipokuwa katika ziara yake ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo mwezi Machi, 2018 ikiwa Mkoani Tabora, ilifarijika kukuta Wakandarasi watatu walioungana ambao wamepewa kazi ya ujenzi wa barabara kwa kipande cha barabara ya lami yenye kilometa 28 kutoka Urambo kwenda Kaliua. Hili ni jambo la kujivunia kwani imezoeleka kuwa miradi hii mikubwa yenye kuhitaji fedha nyingi inafanywa na wageni kutoka nje huku wazawa wakisaidia kazi ndogo ndogo tu.

Ni imani ya Kamati kuwa wakandarasi hao watafanya kazi yenye ubora na hatimae kuongeza imani kwa Serikali ili waweze kupewa kazi zingine.

### v. Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (*The Tanzania Electrical Machanical and Electronics Services Agency-TEMESA*) ni Wakala muhimu sana kwani unatoa huduma ya matengenezo ya magari, mitambo, pikipiki, mifumo ya umeme, majokofu na viyoyozi. Vilevile Wakala huu unasimamia ukodishaji wa magari na mitambo ya kusaga kokoto pamoja na kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali za kihandisi Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala huu unachangamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa rasilimali watu wenye ueledi wa kwenda samabamba na mabadiliko ya teknolojia, vifaa vya kisasa vinavyoweza kuendana na magari, mitambo ya kisasa

ambayo inahitaji kutumia mashine ili kugungua tatizo wakati wa ukarabati na sio kufanya kazi kwa kubahatisha ambako kunatumia muda mwingi na gharama kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo magari ya Serikali yanakwenda kutengenezwa kwa waagizaji wakubwa *(dealer)* ambao gharama zao zinatozwa kulingana na muda ambao umetumika kutengeneza gari husika na hivyo kusababisha gharama kuwa kubwa.

vi. **Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa viwanja vya ndege ni muhimu sana hasa ukuzingatia wakati huu ambapo tunajivunia kuwa na ndege zetu wenyewe. Hata hivyo, miradi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya kutokutolewa fedha kwa wakati. Mfano; katika mwaka wa fedha 2017/18 viwanja vya ndege vifuatavyo viliidhinishiwa fedha ambapo hadi kufika mwezi Machi, 2018 baadhi vilikuwa vimepata fedha kidogo na vingine vilikuwa hajijapata fedha kabisa. (Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kiliidhinishiwa **shilingi mioni 7,250** zimetolewa **shilingi 215,105,663)**, (Songwe- kati ya **shilingi milioni 230** zimetolewa **shilingi milioni 10** tu), (Mtwara- kati ya **shilingi milioni 1,150** zimetolewa **shilingi milioni 576**), (Sumbawanga -kati ya **shilingi milioni 13, 700** hakuna fedha zilizotolewa, (Kilimanjaro kati ya **shilingi milioni 27,868** hakuna fedha zilizotolewa) (Mpanda- kati ya **shilingi milioni 300)** na (Mwanza- kati ya **milioni 9,300** zimetolewa **milioni 15** tu).

**Mheshimiwa Spika**, kutokutolewa fedha za miradi hii kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ujenzi kwani kumekuwa na ongezeko la gharama kutokana na riba, mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi na mabadiliko viwango vya kubadilisha fedha.

c) **Sekta ya Mawasiliano**

i. **Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta**

**Mheshimiwa Spika**, bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu umeendelea kuwa changamoto.

Mfano, katika Mwaka wa Fedha uliopita 2016/2017 Mradi huu uliidhinishiwa **shilingi bilioni 3** ambapo kiasi kilichotolewa kilikuwa **milioni 95, 154, 500** sawa na **asilimia 3**. Na katika mwaka wa fedha wa 2017/18 mradi huu uliidhinishiwa **shilingi billion 3** ambapo hadi kufikia Machi 2018, hakuna kiasi chochote kilichotolewa.

Ni matarajio ya Kamati kwamba mradi huu sasa utapewa kipaumbele na fedha zilizoidhinishwa zitatolewa ili kkuharakisha maendeleo katika taifa letu.

ii. **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF)**

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Oktoba, 2017, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea maeneo mbalimbali ili kuona hali ya huduma za mawasiliano zinavyopatikana kwa sehemu ambazo minara ilijengwa na makampuni ya simu kwa kutumia ruzuku kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-*UCSAF*. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea takribani Mikoa 20 ya Tanzania Bara, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo;-

a) Serikali za Mikoa, Wilaya pamoja na wananchi hawatambui uwepo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; na kwamba, miradi hiyo ya ujenzi wa minara ni kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Dhana iliyoko maeneo mengi ni kuwa minara inajengwa na Makampuni ya simu yenyewe; hivyo mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano hautambuliki kabisa;

b) Upungufu wa rasilimali watu kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili kuweza kufuatilia kwa karibu ujenzi wa minara unaofanywa na Makampuni ya Simu;

c) Makampuni ya simu kutokutoa huduma za kijamii katika maeneo yanayofanya shughuli zake za kibiashara;

d) Migogoro dhidi ya umiliki wa maeneo husika;

e) Wizi wa vifaa vya minara kama vile mafuta, betri na nyaya aina ya ‘’*fiber*’’;

f) Minara mingi iliyojengwa inatumia umeme wa jua (*solar power*), hii inasababisha nyakati za usiku hasa kipindi cha mvua maeneo mengi kuwa na mawasiliano hafifu kwa sababu jua haliwaki kipidi kirefu;na

g) Makampuni kujenga minara pasipo kuweka huduma za kijamii kama vyoo, kibanda cha mlinzi na huduma zingine za msingi kwenye maeneo la mnara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa rai ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijijini. Pamoja na juhudi za Serikali kutoa ruzuku kwa kampuni za simu ili ziweze kufikia maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara, Kamati imebaini kuwa Makampuni makubwa ya simu bado hayajahimizwa vya kutosha kupanua huduma zao katika maeneo hayo.

iii. **Kampuni ya Simu Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha kituo cha kisasa cha Kanzi Data ya Taifa kwa njia ya mtandao (*Internet Data Center*) ambacho kilianza kufanya kazi tangu mwezi Agosti, 2016. Hiki ni kituo chenye uwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu kwa Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, Mashirika Binafsi na hata Watu Binafsi. Kamati imebaini kutokuwepo kwa hamasa kwa Serikali na Taasisi/Mashirika yake kwani mpaka sasa ni taasisi 41 tu ndizo zinazotumia kituo hiki.

Hofu ya Kamati ni Taasisi na Mashirika ya Umma kuendelea kujenga vituo vingine kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake wakati kituo hiki kipo na kinauwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu hizo. Taasisi kama vile Bunge inaweza kutunza taarifa rasmi za Bunge *(Hansard),* vilevile Mahakama inaweza kutumia kituo hiki kwa kutunza na mashauri yaliyokwisha tolewa uamuzi kwa mahakama *(Judgement*).

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Ushauri huu wa Kamati umezingatia umuhimu wa kuharakisha maendeleo nchini. Ni matarajio ya Kamati kuwa, fedha zilizotengwa kwa Sekta zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka 2018/ 2019, zitatolewa kwa wakati ili kuharakisha maendeleo.

### 3.1 Sekta ya Uchukuzi

1) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu ujenzi wa reli nchini;

a) Kamati bado inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kipaumbele kiwe kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zitakazokuwa zimetumika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba reli hii ijengwe kwa kuzingatia faida za kiuchumi na kipaumbele zaidi kiwekwe katika tawi la Tabora – kigoma -Uvinza- Msongati; Kaliua – Mpanda –Kalema; na Tabora- Mwanza;

Ikumbukwe kuwa, licha ya kuwa reli hii itakuwa ikihudumia na kunufaisha takribani Mikoa 15 ya Tanzania Bara kwa kusafirisha mizigo na abiria, pia itasaidia sana kusafirisha mizigo mingi kwenda nchi jirani kama vile DR Congo, Burundi na Rwanda.

Aidha, ujenzi wa reli hii uende sambamba na kudhibiti maeneo korofi kama vile Gulwe na Godegode- Kilosa. Vilevile kuimarisha karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu;

b) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli, ni vema sasa Shirika la Reli Tanzania-TRC kuweka alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi;

c) Shirika la reli kuanza kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatiliaji wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kujiendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji;

d) Kwa kuwa ujenzi wa reli ya kisasa ni wa gharama kubwa, na kwa kuwa pamoja na ujenzi wa reli ya kati unaoendelea sasa, pia tunatarajia kuanza kujenga reli zingine za Tanga –Arusha –Musoma (1108 km), Mtwara- Mbambabei na Mchuchuma Liganga (1092 km) na Isaka –Rusumo (371). Kamati inashauri Serikali kujenga reli hizi kwa awamu kwa kufuata kipaumbele; na

e) Ili kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini, Serikali iangalie uwezekano wa kushirikisha sekta binafsi au kupata mikopo yenye gharama nafuu. Kwa kufanya hivyo, Serikali itaweza kuendelea kutoa huduma zingine muhimu kwa kutumia fedha zake za ndani.

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari;

a) Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kubakisha angalau **asilimia 40** ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake;

b) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza upanuzi na ukarabati wa bandari ya Dara es Salaam pamoja na kukamilisha kituo cha pamoja cha huduma kwa wateja (*one stop centre)*, hata hivyo, ili kuongeza ufanisi na mapato katika bandari ya Dar es Salaam, Kamati bado inasisitiza kufanyika juhudi za makusudi ili kuweza kuhamisha gati la mafuta lililopo kurasini (KOJ) na kujenga gati namba 13 na 14;

c) Wadau wote wa bandari kuunganishwa kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati

mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia mkuu, Shirika la Viwango Tanzania-TBS ,Wizara ya Nishati na Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo;

d) Mchakato wa kuwa na eneo Kurasini-Shimo la Udongo ambalo litatumika kuegesha magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyabishara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika;

e) Serikali kuendelea kuondoa vikwazo visivyo vya lazima katika Bandari nchini ili kuzidi kuvutia na kujenga mazingira ya wafanyabiashara wengi kutumia Bandari zetu;

f) Serikali kuharakisha ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar se salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda mrefu sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Katosho-Kigoma na Misungwi –Mwanza;

g) Kamati inashauri Serikali kuharakisha majadiliano na wabia ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwani kukamilika kwa bandari hii kutatoa fursa nyingi za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali kulipa fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza.

3) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kampuni ya Huduma za Meli kupanga mipango ya kujiendesha kisasa kwa kuimarisha njia za ukusanyaji mapato kwa njia kielektroniki, kuweka teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli (*Flow Scanner)* na kuweka mfumo wa kuweza kufatilia mahali meli ilipo kila wakati (*trucking*

*system)*. Kufanya haya kutasaidia kuweza kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Kampuni;

b) Kampuni ya Meli Tanzania kufanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na Reli kwani kufanya hivyo kutawezesha kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara kuweza kusafirisha mizigo toka Dar es salaam mpaka Uganda na hatimaye kupunguza gharama kwa wafanyabiashara na kuongeza pato na hata Kampuni hii kuweza kutoa gawio la faida kwa Serikali;

c) Serikali kujipanga kutengeneza Meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara na hata kuweza kulipa madeni yote inayodaiwa;

d) Serikali ihakikishe inalipa deni la mishahara ya miezi 23 kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka Kampuni hii itakapoweza kujiendesha kwani uwekezaji unaofanyika kwa sasa wa kukarabati na kujenga meli mpya katika Maziwa Makuu hautakuwa na tija ikiwa maslahi ya wafanyakazi hususani mishahara haitopewa kipaumbele; na

e) Serikali kurasimisha bandari bubu zilizozagaa katika mwambao wa Ziwa Victoria ili kuongeza mapato katika halmashauri na bandari kwa ujumla.

4) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Nchi wabia wa reli ya TAZARA kuendelea na mazungumzo ya kuimarisha reli hii kwani bado mahitaji yake ni makubwa kwa uchumi. Kamati inaamini kwa takwimu zilizopo za shehena inayotoka Bandarini peke yake na kusafirishwa na reli ya TAZARA inatosha kabisa Mamlaka hii kuweza kupata uwezo wa kujiendesha kibiashara kwani zipo zaidi ya tani 1,500,000 ambazo zinahitaji kusafirishwa kupitia reli hii;

b) Serikali kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi na weledi wa kutosha ili kuweza kuliongezea Shirika uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu;

c) Serikali ijenge kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha kujiendesha; na

d) Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kendelea kulipa deni lote linalodaiwa na TAZARA.

5) **Mheshimiwa Spika,** kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA:-

a) Ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- TAA iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza tija na ufanisi katika viwanja vya ndege nchini; Kamati inashauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau asilimia 50 ya maduhuli (*retention)* yatokanayo na viwanja vya ndege;

b) Kwa kuwa yapo mashirika mengi kama Ethad, Fly Dubai, Rwanda Air,Jambo Jet ya Kenya yanayofanya safari za kimataifa na yameonyesha nia ya kufanya safari zake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza; Kamati inashauri kuwahi kukamilishwa kwa jengo la kuongozea ndege *(tower),* jengo la mizigo, pamoja na kuondoa mapungufu mengine yanayokikabili kiwanja hiki ili kiweze kutumiwa na ndege za kimataifa na kuweza kuongeza mapato; na

c) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kulipa fidia ili kumaliza migogoro na wanachi walio kwenye maeneo ya viwanja vya ndege. Vile vile kuharakisha zoezi la kupata Hati Miliki kwa viwanja vyote vya ndege na kuondokana kabisa migogoro hiyo katika siku za mbele.

6) **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL,

a) Kampuni ya ndege ya Tanzania kuingia kwenye mfumo wa (*International Air Transport Assoacition) IATA* ili kuweza kufanya ‘’*booking*’’ za abiria wanaotoka nje ya nchi wanapotaka kuunganisha ndege ndani ya Tanzania, jambo ambalo kwa sasa halifanyiki;

b) Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja mara kwa mara ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote; Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga; na

c) ATCL ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja na kuwa na bei nafuu ili kuhakikisha abiria wengi wanatumia ndege hizi.

7) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini-SUMATRA:-

a) Mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa nchi kavu na majini kuimarisha usalama na ubora katika kutoa huduma za usafiri kwani wimbi kubwa la ajali zinazotokea ni dalili tosha kuwa kuna mapungufu kwenye usimamizi wa sheria za usalama barabarani;na

b) Serikali kupitia SUMATRA kuhakikisha inaweka mikakati ya kupunguza msongamano ya magari kwenye miji inayokua kwa kasi kama vile Mbeya, Mwanza, Arusha na hivi sasa Dodoma. Miji hii imekuwa ikikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari na kusababisha kutumia muda mwingi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

## 3.2 Sekta ya Ujenzi

1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Barabara-TANROADS, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Serikali kutekeleza Sera yake ya kuunganisha Mikoa kwa barabara za lami (*Trunk Roads)* kama vile Lindi – Morogoro, Morogoro-Mlimba-Madeke Njombe, Lindi – Songea, Kigoma –Katavi-Tabora-Kigoma, Mbeya-Makete-Njombe, Arusha –Mara Aidha, miradi ya barabara hizi ambayo inaendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu. Vilevile, Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine *(Boarder Roads)* hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara;

b) Serikali iangalie upya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara na kuongeza asilimia ya fedha zitolewazo kwa TARURA kufikia asilimia 40 na Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS kupewa asilimia 60. Hii ni kutokana na ukweli kuwa barabara nyingi za vijijini hazipitiki katika misimu yote, na kwa kuwa Serikali inatekeleza Sera yake ya Viwanda ni vema kuongeza fedha kwa ajili ya barabara za vijijini ili ziweze kujengwa na kusafirisha mali ghafi zinazotoka vijijini kuja kwenye viwanda ambavyo vilivyo vingi viko mijini;

c) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuchukulia hatua kali kwa makandarasi wanaofanya kazi chini ya kiwango kwani yapo majengo na barabara nyingi zilizojengwa chini ya viwango kwani Serikali inatumia fedha nyingi za walipa kodi kuweza kugharamia miradi hii; Mfano, barabara ya Dodoma –Iringa imeanza kuharika huku haina muda mrefu tangu ijengwa.

d) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Makandarasi wa Ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu. Aidha, kuhamasisha Makandarasi wazalendo kujiunga na kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia na kupata dhamana kupitia Mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia Makandarasi wadogo na wa kati;

e) Wakati Serikali inajenga barabara pamoja na mambo mengine kuzingatia vigezo muhimu kiuchumi, kijamii (hasa

huduma za afya na elimu) pamoja na ahadi za Marais waliostaafu na Rais aliye madarakani;

f) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama Runinga, Magazeti, Redio na Simu za Mkononi. Pia vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara ili kuepusha usumbufu wakati maeneo hayo yanapohitajika;

g) Serikali kuharakisha kuleta Sheria bungeni ya Vyuma Chakavu ili kuweza kusaidia kupambana na watu wachache waliokosa uzalendo ambao wanaiba vyuma zenye alama za barabarani na kuviuza kama vyuma chakavu. Vilevile, kuchukuwa hatua kali za kulipa faini kwa magari ambayo yanagonga vibao vya alama barabarani;

h) Serikali iendelee na juhudi kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji;

i) Serikali kuongeza kasi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (*One Stop Inspection Stations*) ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa pamoja na kuokoa muda wa mizigo kukaa barabarani;

j) Wakati wa ujenzi wa barabara ni vema wakala wa barabara kuhakikisha wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo kwani maeneo mengi ambayo mifugo inatumia kuvuka kumekuwa na uhalibifu mkubwa sana wa barabara;

k) Wakati wa ujenzi wa barabara zipo taasisi nyingi za Serikali zinapeleka madai kwa makandarasi wa barabara kwa ajili ya ulipiaji malighafi zinazotumika kwenye ujenzi, kama vile Wizara ya Madini (kokoto, mawe, kifusi), Wizara ya Maji na umwagiliaji (vima vya maji), Wizara ya Viwanda na Mazingira (uharibifu wa mazingira) pamoja na ushuru unaotozwa na Halmashauri za miji;

Gharama hizi zinaongeza gharama za ujenzi wa barabara hivyo Kamati inaishauri Serikali kusamehe kodi hizo kwani zinalipwa na Serikali na si wakandarasi; na

l) Serikali kuendelea kutoa kazi za ujenzi wa barabara kwa wakandarasi wazawa ilikuweza kuongeza ujuzi na uzoefu katika shughuli za ujenzi.

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na hasa jengo la abiria ni jambo la kimkakati katika kuchochea uchumi wa nchi hivyo; Kamati inashauri Serikali kuweka kipaumbele na kuchukuwa hatua za makusudi kutekeleza azma yake ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ikiwa ni pamoja na kuharakisha ujenzi wa jengo la abiria ili kuweza kuendana na viwango vya Kimataifa ambavyo vimeainishwa na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga- ICAO kuwa sharti moja wapo ni kuwa abiria wa ndani na wa nje hawaruhusiwi kuchanganyika katika eneo moja;

b) Serikali kukamilisha kwa haraka ujenzi wa Jengo la Tatu (*Terminal III*) la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika katika muda uliopangwa. Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi;

c) Serikali kutoa fedha zote zilizoidhiniwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuepuka riba ambazo hutokana na miradi kutokamilika kwa wakati;

d) Serikali kuhakikisha inapata Hati Miliki za mali zake zote hususan viwanja vya ndege. Hii iambatane na kuweka mipaka, uzio au nguzo kuepusha uvamizi na migogoro kwa wananchi wanaoishi kandokando ya viwanja vya ndege; na

e) Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Viwanja vya ndege hasa mifereji ili kuzuia maji/ mafuriko kutuhama katika viwanja vya ndege hasa wakati wa mvua na kusababisha ndege kushindwa kuruka ama kutua.

3) **Mhesimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Majengo –TBA, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Serikali kuimarisha uwezo wa Wakala wa Majengo Tanzania-TBA ili iweze kuzalisha fedha na kuchangia Pato la Serikali. Ni vyema Wakala huu pamoja na kujenga nyumba za gharama nafuu, kuhakikisha zinakuwa katika hali ya ubora na viwango vinavyostaili;

b) Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa majengo ya Serikali, ni vema sasa Wakala wa Majengo Tanzania kuanza kushirikiana na taasisi zingine za Serikali zinazohusika na ujenzi kama Suma JKT, Shirika la Nyumba la Taifa na zingine ili kuongeza kasi ya ujenzi na kuleta tija;

c) Wakala wa Majengo nchini kufanya ukarabati wa nyumba zake zilizo maeneo mbalimbali ya nchi kwani nyingi ziko katika hali isiyoridhisha hasa kwenye mifumo ya umeme na maji machafu na hivyo kuhatarisha maisha ya wapangaji;

d) Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye majengo ya Ikulu ndogo zilizopo kwenye Wilaya mbalimbali nchini kote; na

e) Serikali kuajiri wafanyakazi wa kutosha ili kuongeza usimamizi wa miradi mingi na mikubwa inayosimamiwa na Wakala huu;

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme-TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Wakala wa Ufundi na Umeme kuharakisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo kwani kuna Wilaya zingine ziko umbali mrefu kwenda Makao Makuu ya Mkoa;

b) Wakala kuchukuwa hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo kwa kiasi kikubwa inazidai taasisi za Serikal ili Wakala huu uweze kijiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na

c) Serikali kuajiri wataalaum waliobobea kwenye fani ya ufundi wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nyingi magari ya Serikali yamekuwa yakitengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

## 3.3 Sekta ya Mawasiliano

1) **Mheshimiwa Spika,** ufuatao ni ushauri wa Kamati kuhusu Sekta ya Mawasiliano;

a) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wake kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania kwa kufunga ‘’moduli’’ ya uhakiki mapato ya huduma za mawasiliano ijulikanayo kama (*Telecom Revenue Assurance System* (*TRAS*). Hii itasaidia Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya kodi stahiki kutoka kwa makampuni ya simu kwa miamala inayofanyika;

b) Serikali kutoa fedha zote zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwani sekta hii inachangia kiasi kikubwa cha fedha kwenye mfuko mkuu ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha **shilingi bilioni 10.9** zilikusanywa kutoka kwenye mkongo na **shilingi bilioni 8.7** zilikusanywa kutoka Mamlaka ya mawasiliano;

c) Kwa kuwa Serikali inamiliki asilimia 40 ya hisa za Kampuni ya Airtel Tanzania; na kwa kuwa tangu ilipoingia ubia Serikali haijawahi kupata gawio; Kamati inasisitiza suala hili kuangaliwa kwa umakini;

d) Serikali kuipa kipaumbele mradi wa anwani za makazi na misimbo ya posta kwani mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;

e) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao;

f) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, kama vile, uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya uhalifu wa kimtandao na kuwabana wahalifu; na

g) Kamati inaendelea kusisitiza kuongezwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze

kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, sekta hii ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa.

## 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, (Mb) akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Eng. Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias Kwandikwa, (Mb).

Vile vile, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph Nyamuhanga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Angelina Madete. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalam wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - Mwenyekiti

2. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb- ‘’
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb - ‘’
6. Mhe. Joyce John Mukya, Mb - ‘’
7. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb - ‘’
8. Mhe. Susan Chogisasi Mgonukulima, Mb - ‘’
9. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb - ‘’
10. Mhe. Nuru Awadh Bafadhil, Mb - ‘’
11. Mhe. James Francis Mbatia, Mb - ‘’
12. Mhe. Saul Henry Amon, Mb - ‘’
13. Mhe. Ahmed Makhbuty Shabiby - ‘’
14. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb - ‘’
15. Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb ‘’
16. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfed Kikwembe, Mb‘’
17. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb- ‘’
18. Mhe. Dua William Nkurua, Mb - ‘’
19. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb - ‘’
20. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb - ‘’
21. Mhe. Charles Kitwanga, Mb - ‘’
22. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb- ‘’
23. Mhe. Rukia Kassim, Mb - ‘’
24. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - ‘’

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson M. Bisile, Makatibu wa Kamati Ndg. Hosiana John na Ndg. Richard Masuke pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, (Mb)
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**

23 Aprili, 2017

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa taarifa yako nzuri, imesheheni ushauri mzuri kwa Serikali.

Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaanza kuichangia hotuba hii, nina orodha ndefu ya wachangiaji kwa uwiano wa vyama vinavyowakilishwa humu Bungeni; tutumie muda wetu vizuri. Kwa upande wa CCM kila mmoja kuanzia leo mpaka huko ni dakika tano/tano, wale wenzangu ambao ntakuwa nawaambia kama ana dakika tano au kumi ntawaeleza kwa upande wa Chadema na CUF.

Tunaanza; mnasema mimi huwa siwapendi, nawapenda sana wote, Mheshimiwa Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza kwenye Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wa Ta'ala* ambaye ameweza kunipa afya njema na leo hii niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ili tuweze na sisi kunufaika na rasilimali za Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja suala hili; hotuba ya Mheshimiwa Waziri imezungumza kwa kiasi kikubwa sana ujenzi wa barabara, na nichukue fursa hii kushukuru na kuishukuru Wizara kwa kuanza utekelezaji wa

ujenzi wa Barabara ya Uchumi ambayo inajengwa kuanzia Mtwara Mjini mpaka Mnivata kule kwenye Jimbo la Nanyamba na baadaye itafika mpaka Masasi. Nichukue fursa hii kuishukuru Wizara kwa kuanza kutekeleza kilometa hizi 50 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumze kwamba wakati barabara hii inazinduliwa na Mheshimiwa Rais alivyokuja Mtwara mwaka jana kuja kuzindua ujenzi wa barabara hii na miundombinu mingine, alitoa wasiwasi wake juu ya mkandarasi ambaye amepewa ujenzi wa barabara hii; kwamba kuna wakati fulani akiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi aliwahi kumsimamisha kazi, akawa amemuagiza Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwamba awe makini sana; pale Mtwara tukiwa bandarini tunazindua ujenzi wa lile gati, na akasema kwamba atakuwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisikitike tu, yule mkandarasi bado yuko *slow* sana. Nimuombe Waziri, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, akaze buti huyu mkandarasi aendane na kasi ya ujenzi lakini pia aendane na muda ambao umewekwa; yuko *slow* sana yule mkandarasi anayejenga barabara ya Uchumi kutoka Mtwara Mjini mpaka Mnivata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze suala zima la barabara ya ulinzi; tulikuwa tumezungumza hapa kwa muda wa miaka miwili na huu ni mwaka wa tatu hivi sasa, kwamba kuna barabara ya ulinzi ambayo ilitumika kulinda mpaka wetu wa kusini, barabara inayoanzia Mtwara Mjini, inapita Jimbo la Mtwara Vijijini, inafika kule Kitaya Jimbo la Nanyamba, inafika Tandahimba, Newala mpaka kule Ruvuma. Hii ni barabara muhimu sana, ni barabara ambayo makamanda wetu walikuwa wanaitumia kumdhibiti Mreno ambaye alikuwa anakuja kutuchokoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwaka 1972 ndege ya Mreno ambayo ilikuja kuvamia Tanzania iliweza kudunguliwa Kijiji cha Kitaya pale Jimbo la Nanyamba, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini. Lakini baada ya kuidondosha ile

ndege ya Mreno yule kamanda wetu aliuawa pale, pamejengwa mnara mdogo sana. Mimi naomba sana na naishauri Wizara hii, hii barabara ijengwe na pale pajengwe mnara wa kumbukumbu ambao utaonesha kweli kwamba shujaa wetu pale Kijiji cha Kitaya ndipo alipouawa akiwa analinda mpaka wa Tanzania ambao uko huku maeneo ya kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa ikizungumza sana, imekuwa ikiongea sana kwamba tutatenga bajeti, niombe sana kwamba mwaka huu barabara hii ya ulinzi ambayo inalinda mpaka wa kusini itengewe pesa ili iweze kuanza kutengenezwa, kwa sababu hatuwezi jua huko mbeleni kwamba kitu gani kinakuja juu ya mipaka yetu ya Tanzania. Mpaka huu ni mpaka muhimu sana, barabara hii ni barabara muhimu sana, inaanzia Mtwara mpaka Ruvuma kule. Ninaomba sana Wizara iangalie kwa jicho la kipekee mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili ambalo tumekuwa tunazungumza la maendeleo ya Ukanda wa Kusini *(Southern Development Corridor)* ambalo limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu hivi sasa na maendeleo ya Ukanda wa Kusini inaanzia katika ujenzi wa bandari. Tunashukuru kwamba Gati la Bandari la Mtwara linajengwa kwa mita 350, lakini ujenzi wa gati ya bandari unaendana sambamba na barabara ya reli. Miaka ya 1963 huko Mtwara, kule kusini kulikuwa na reli na ile reli ikaondolewa, hatujui ilipelekwa wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili kuweza kufungua uchumi wa Kanda ya Kusini kuna ulazima Serikali ihakikishe kwamba huu ujenzi wa reli ambao umekuwa ukizungumzwa kila mwaka kwamba reli inayotoka Mtwara kuelekea Liganga na Mchuchuma kule kupitia kule Mbambabay ni muhimu mwaka huu sasa tuweze kutengewa pesa ile pesa iweze kupelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana ilizungumzwa hapa kwamba imetengwa pesa kwa ajili ya upembuzi

yakinifu karibu shilingi bilioni mbili, sijaona upembuzi yakinifu uliofanyika mpaka leo hii. Kwa hiyo tunaomba sana, ili tuweze kufufua uchumi wa kusini *(Southern Corridor)* ambapo itaunganisha Mikoa ya Kusini – Mtwara, Lindi, Ruvuma lakini kule maeneo ya Malawi na nchi nyingine za Kusini, tujenge hii barabara ya reli ya Ukanda wa Kusini. Itengewe pesa mwaka huu na pesa ziweze kutolewa kwa ajili ya upembuzi yakinifu lakini na ujenzi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la utanuzi wa bandari; lengo la kujenga bandari hizi; Bandari ya Mtwara, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mafia, Bandari ya Kilwa ni kuhakikisha ya kwamba tunafanya *decentralization of the economy,* hatuwezi kutegemea Bandari moja ya Dar es Salaam. Leo hii ukifika Bandari ya Dar es Salaam, mizigo yote ambayo inatakiwa kushuka Tanzania inashukia Bandari ya Dar es Salaam wakati Bandari za Mtwara, Tanga pamoja na Kilwa ni bandari zenye vina virefu, meli ya aina yoyote inaweza ikagati katika maeneo haya. Bandari ya Mtwara Wazungu wanasema ni *natural habour,* ni bandari ambayo ina kina kirefu kuliko bandari zote za Afrika Mashariki na Kati. Kuna meli nyingine, kama sio ukarabati wa Bandari ya Dar es Salaam, haziwezi kugati Dar es Salaam, lakini Mtwara zinaweza kugati kwa sababu ya kina kirefu cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana kwamba tunatumia Bandari ya Dar es Salaam tu. Leo hii ukiamua kuagiza gari kutoka Japan/kutoka nje ya nchi, katika *East Africa* kwa nchi yetu ya Tanzania iko Bandari ya Dar es Salaam pekee na Bandari ya Mombasa, wakati tungeweza kuongeza Bandari za Mtwara na Tanga ili tuweze kuuondoa msongamano Dar es Salaam. Mimi naiomba sana Wizara hii kwamba upanuzi wa bandari ambao tayari gati limeanza kujengwa pale Mtwara, kwanza uweze kukamilika kwa wakati, lijengwe kwa kasi lakini pia tuitumie Bandari ya Mtwara ili kuondoa msongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini Bandari ya Mtwara ikitumika sawasawa hii barabara yetu ya Morogoro haitaharibika hivi kwa sababu barabara inayotengenezwa

Tanzania kila siku ni barabara ya Morogoro kwa sababu mizigo inakuwa mingi sana. Magari ya Zambia, magari ya Burundi, magari ya Tanzania, *on transit* zote zinatokea Dar es Salaam. Tupanue Bandari ya Mtwara, tutumie Bandari ya Mtwara ili kuondoa uharibifu wa barabara moja hii ambayo inatengenezwa kila wakati.

Jambo lingine ni suala hili la meli; usafiri wa meli wakati fulani hivi nilitembelea Comoro pale, ukifika Comoro, Comoro ilipigwa *volcano,* yaani Comoro hata nyanya hazistawi, kila kitu wananunua kutoka nje, wanategemea kutoka Tanzania. Sasa hatuna usafiri wa meli ambapo wafanyabiashara wa Tanzania wangeweza kutokea Mtwara; Mtwara na Comoro karibu sana; wangeweza kutokea Dar es Salaam kwa kutumia meli, wangeweza kutokea Pemba kuelekea Comoro kupeleka mizigo kule na Watanzania tungekuwa na manufaa, wafanyabiashara wetu wangeweza kuinuka kiuchumi kwa usafiri wa meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale Mtwara tuna Kiwanda cha Dangote ambacho ana magari zaidi ya 1,000 yanayosafirisha *cement* kutoka Mtwara kuelekea kwenye soko kuu ambako ni huku Dar es Salaam na maeneo mengine. Kama tungeweza kumruhusu huyu Dangote akajenga ile bandari yake ndogo, lakini pia akalazimishwa kununua meli ili simenti yake aweze kusafirisha kwa njia ya meli, barabara hii isingeharibika, angeweza kuleta mzigo wake Dar es Salaam kupitia kwenye Bahari ya Hindi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri, unga mkono hoja. Tunaendelea; Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab na Mheshimiwa Dkt. Chegeni ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma hotuba hii yote kwa ujumla imeonesha kama vile yaani Tanzania kwenye mambo ya barabara na nini hakutakuwa na tatizo lolote, ndiyo hotuba nzima ilivyokuwa imeonesha. Lakini nitatumia kama dakika mbili kuelezea Jimbo langu la Momba halafu mengine ntayazungumza ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza swali hapa Bungeni miaka yote kuhusu kupandishwa hadhi kwa barabara ya Jimboni kwangu Momba kutoka Kakozi – Kapele kwenda Ilonga, Sumbawanga na Serikali ikaniahdi hapa kwamba tutaipandisha hadhi, wakakiri imekidhi vigezo na nini, lakini mpaka leo ile barabara huu ni mwaka wa nne tangu ahadi ya Serikali ndani ya Bunge, haijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna barabara ya kutoka Mlowo kwenda Kamsamba mpaka Kiliamatundu, barabara ile imekuwa kwenye ahadi ya kila mwaka ukosoma kwenye hotuba hii kila mwaka iko mle ndani kwamba tutaijenga kwa kiwango kinachoridhisha itakuwa na uhakika wa kiwango cha lami, lakini ile barabara imebaki kuwa *story* ambayo haikamiliki. Kwa hiyo, sasa ukiangalia haya mambo ndiyo inashindwa kuelewa kwa nini Serikali inashindwa kutekeleza kile inachokizungumza kila mwaka kwa sababu imekuwa ikichukua miaka mingi. Sasa hayo ndiyo maeneo makubwa ambayo sisi jimboni kwangu wakati wa sasa ndiyo yanayotusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nizungumzie mambo ya kitaifa. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ina *deal* na Shirika letu la Ndege la Taifa. Hivi karibuni ndege yetu ya tatu ya *Bombadier* imewasili nchini na baada ya kuwasili kulikuwa na taarifa za kukamatwa kwa ile ndege ya tatu, ilikuwa inadaiwa. Hata hivyo pamoja na kwamba imewasili Serikali haijatueleza imelipa kiasi gani kwenye kuikomboa ile ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka majibu kwa sababu zile fedha ni kodi za Watanzania. Masuala kama haya yanapoachwa kimya sisi Watanzania tutaendelea kuyauliza bila kupatiwa majibu kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata taarifa, Mamlaka ya Anga Tanzania pamoja na Shirika la Ndege Tanzania limeondolewa kwenye yale mashirika ya anga *(IATA)* umesikia hiyo taarifa hivi karibuni, kwa sababu ya madeni na inashindwa kujiendeleza. Sasa haya tunahitaji majibu ili tujue hili shirika letu ni kweli linajiendesha vile inavyotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisikia taarifa zinazotoka Serikali zinaeleza Shirika la Ndege la Taifa kwamba linapata faida; wao wanasema tumepata faida. Nakumbuka mara ya mwisho waliainisha kwamba wamekusanya karibu shilingi bilioni 20, lakini hawatuelezi *running cost* za ili shirika; hawaelezi wanaendeshaji; maana unatajiwa tu mapato ghafi. Atueleze kuhusu faida iliyopatikana baada ya kuondoa gharama za uendehaji wa shirika. Kwa hiyo tunahitaji kufahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *report* ya Kamati ya wakati uliopita ilikuwa inaonesha kabisa kwamba Shirika la Ndege lina madeni makubwa, kuliendesha ni gharama kubwa. Sasa kumekuwa na *contradiction* kati ya kinachotolewa na Serikali na maelezo yanayokuwa yanatoka kwenye Kamati. Kwa hiyo, jambo hili tunahitaji kupatiwa ufafanuzi ili tuweze kufahamu hivi shirika letu lipo katika kile kiwango tunachohitaji, yaani ili liweze kuendelea na kulishauri vizuri. Kwa hiyo, tulikuwa tunahitaji kupata ufafanuzi kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu kwenye shirika hili la ndege, hatujawahi kuona taarifa ya ukaguzi ya *CAG* juu ya hili shirika la ndege. Sasa tunahitaji majibu; kuna usiri gani wa kushindwa kuleta taarifa ya *CAG* ya ukaguzi wa Shirika la Ndege ndani ya Bunge? Tunahitaji hayo ili tuweze kujua namna gani tunaweza tukawashauri, lakini pia tunahitaji kujua hizi kodi za Watanzania zisingekuwa zinapigwa huko kimya kimya halafu sisi watu hatujui; kama ambavyo leo Watanzania wote wanahoji kuhusu zilipo shilingi trilioni 1.5 hatutaki kufika huko na ndiyo maana, Mheshimiwa Waziri atakuja kutueleza hapo kwenye ku-*wind up,* atueleze kwa nini taarifa zake hazionekani? Yaani

zinakuwa ni siri ilihali mradi huu ni kwa maslahi ya Taifa? Tunahitaji majibu juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka yote upande wa barabara *(TANROADS).* Wakala wa Barabara kwa miaka ya hivi karibuni tumeshindwa kupata ripoti ya ukaguzi ya *TANROADS* (Wakala wa Barabara wa Taifa). Tunazitaka hizo taarifa kwa sababu kuu mbili; kumekuwa na maneno uko mtaani watu wananon'gona nong'ona kwamba kulikuwepo na barabara hewa zenye thamani ya shilingi bilioni 252. Sasa unapoelezwa hizi taarifa halafu Serikali inakaa kimya; sisi kama Wabunge jukumu letu kuhoji tunahitaji kupata ufafanuzi ili tujue kweli hiki wanachokizungumza ni kweli ama ni uongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini *CAG* haruhusiwi ama taarifa zake haziletwi kwa Wakala wa Barabara wa Taifa? Kwa sababu tunaziona barabara zetu, tunataka kujua *value for money* ya hizi barabara. Je, barabara inayojengwa thamani yake inalingana na pesa iliyokuwa imetolewa? (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo majibu ambayo Serikali inapaswa kutuletea sisi Wabunge ili tuweze kuishauri namna ya kuliendesha hili taifa. Kwa hiyo, hilo tunahitaji kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; sasa hivi kuna *TARURA.* Najua *TARURA* inategemea Mfuko wa Barabara fedha zake nyingi zote, niseme fedha zote zinatoka kwenye Mfuko wa Barabara. Hata hivyo bado kumekuwa na mkanganyiko, fedha kule kwenye *TARURA* hazipelekwi. Kuna barabara ambazo kwa sasa *TARURA* haiwezi kuziendesha. Nataka kujua namna gani ambavyo watu wa *TANROADS* wanaweza yaani tunatafuta yaani kama ule ushirikiano wa namna kupandisha hadhi zile barabara ambazo *TARURA* hawawezi, lakini fedha nyingi zimekuwa zikipelekwa upande wa *TANROADS* kuliko upande wa fedha za miradi ya barabara vijijijini hususani kupitia *TARURA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimeona nilizungumzie, najua liko kwenye upande wa TAMISEMI zaidi, lakini wana *deal* na barabara kwa hiyo unazungumzia barabara lazima kuwepo na *connections,* kwamba huyu anakuleta kwenye ngazi ya Wilaya na Mkoa huyu anakupeleka kwenye ngazi ya kitaifa zaidi. Kwa hiyo, na hili nilikuwa nataka tupate ufafanuzi kutoka kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Simu la Taifa *(TTCL),* shirika hili lina miaka mingi lakini ukuaji wake, yaani linakua katika tunasema in *a negative growth.* Sasa hivi wanasema rudi nyumbani, lakini rudi nyumbani hawana uwezo wa kujiendesha, yaani kwenye Taifa hili wapo kwenye Mikoa kumi tu peke yake. Tuliwauliza hapa siku moja, *Halotel* amekuja ana muda usiopungua miaka miwili, lakini ndani ya muda mfupi *Halotel* ana wateja zaidi ya milioni moja. Lakini *TTCL* lenye miaka na miaka lina wateja hawafiki hata laki mbili, ukiwauliza Serikali wanakwambia hiki ndicho kitu cha kujivunia, hiyo ndiyo changamoto iliyopo kwenye Serikali yetu. Tunataka kuanzisha mambo mengi lakini hatuwezi ku-*compete.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaambia hapa kwa nini Serikali isikubali kushiriki kwenye ubia wa *PPP* juu ya namna ya ku-*run* hizi kampuni. Amekuja Waziri hapa anasema kwenye miradi ya *PPP* Serikali ya Awamu ya Tano haioni kama ni kipaumbele. Sasa unajiuliza, mtawezaje kuendesha kila kitu kwa gharama ya fedha za ndani? Sasa haya dunia ya sasa huwezi ku-*run* miradi mikubwa bila kuingia katika mfumo *PPP* haiwezekani, na bahati mbaya sana Awamu hii ya Tano inafiiri kila jambo linaweze kutekelezeka kwa fedha za ndani, kitu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, ahsante sana, lakini nikuulize Mheshimiwa Silinde, wewe hudaiwidaiwi? Haya tunaendelea Mheshimiwa Balozi Adadi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda sana kuusifu uongozi wa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Profesa Mbarawa na wasaidizi wake wote, kwa sababu Wizara hii ni Wizara mojawapo ambayo imeonesha kwa kweli ni kitu gani Awamu ya Tano inataka. Miradi mikubwa mingi sana imeanza kutekelezwa, tukianzia kwenye barabara, *SGR,* madaraja, bomba la mafuta la Tanga, *flyovers*, vivuko na mengineyo mengi. Hata hivyo nimefurahishwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri hasa hasa kwenye miradi hii mikubwa. Isipokuwa nimesikitika sana baada ya kuona kwamba reli ya Tanga imeachwa kabisa. Nimeangalia nimesoma kwa haraka haraka, lakini sijaona reli ya Tanga ikizungumziwa. Najua upembuzi yakinifu umemalizika kati ya Tanga mpaka Arusha na sasa hivi unafanyika upembuzi yakinifu wa Arusha mpaka Musoma. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeshauri kwamba hii reli ya Tanga ambayo upembuzi yakinifu umeshafanyika wa Arusha mpaka Tanga basi ingeanza kutangazwa kwa njia ya *PPP* ili wawekezaji waanze kufanya kazi hiyo. Naamini kabisa wawekezaji wa *PPP* watakapoarifiwa mradi huu unaweza kuanza mara moja. Nafahamu wapo na wanategemea Serikali itaanza kuutanga hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tunategemea bandari. Nimeona kwenye ratiba hapa Bandari ya Tanga ambayo ni bandari kubwa na sasa hivi kutokana na bomba la mafuta ambalo linategemewa kuanza tunategemea kwamba kazi itaanza. Mwaka uliopita ilitengewa fedha lakini naona kazi inakwenda kwa kusuasua, sasa nategemea kwamba basi wakati huu itatengenezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwenye jimbo. Barabara yangu ya Amani - Muheza kilometa 36 mwaka 2017

tulitengewa shilingi bilioni tatu. Nilitegemea kwamba kazi ingeanza lakini naona kwenye maandiko ya Mheshimiwa Waziri kwamba anatafutwa mkandarasi na kila nikimuuliza Meneja wa *TANROADS* Tanga vipi umefikia wapi ananiambia tunashughulikia. Sasa tutashughulikia huyu mkandarasi sijui atapatikana lini na fedha hizi zinaweza kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwamba nimetengewa tena shilingi bilioni tano, sasa naamini kabisa shilingi bilioni tatu zangu zile na shilingi bilioni tano hizi nikijumulisha pamoja ni shilingi bilioni nane naamini nitapata karibu kilometa 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakuomba sana fedha hizi zije ili hii kazi iweze kuanza. Nashukuru sana kwamba barabara ya Tanga mpaka Pangani mtaanza kuitengeneza na nimeona hapa mmeitengea hela kwa hiyo, nakushukuru sana na nategemea kwamba barabara hiyo yenyewe itaanza kutengenezwa kwa sababu barabara hiyo inapita pia kwenye jimbo langu. Namshukuru sana Mheshimiwa Elias Kwandikwa, alikuja na aliiona barabara hii na aliona matatizo yake. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba kazi itaanza mara kwa sababu waliwapa matumaini wanachi wa Amani kwamba kazi hii itafanyika na sasa hivi wanategemea kwamba kazi hiyo itaanza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawasiliano ya eneo hilo hilo la Amani, tuna tatizo kubwa sana la mawasialiano. Nafikiri sasa hivi imefika wakati kwamba kukimbilia kwenye mapaa ya nyumba au kupanda kwenye miti kwa ajili ya mawasiliano iwe imekwisha. Sasa naamini kwamba nimempa *list* Naibu Waziri ambaye aliuliza maeneo ambayo mawasiliano hakuna; na nimempa *list* ya Tarafa yote ya Amani, Muheza; Tarafa yote ya Bwembwera ambako mawasiliano yanakuwa ni tabu sana kwenye baadhi ya vijiji. Kwa hiyo, nategemea kwamba katika kipindi hiki basi atazituma hizi kampuni za simu kuja kusaidia kwenye haya mawasiliano, vinginevyo suala la *TARURA* bado hatujaona matunda yake. Muheza hawajaletewa hela kabisa na hii

*TARURA,* hata shilingi moja; sasa inakuwa taabu na kuwa-*control* hawa *TARURA,* najua ni TAMISEMI lakini inakuwa taabu sana kwa sisi kuweza kupata mawasiliano ya kujua kama wamepewa hela au hawakupewa hela, wao wapo wapo tu. Sasa naomba wapewe hela ili waweze kuonesha hiyo kazi ambayo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Balozi, tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Chegeni atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Magige na Mheshimiwa Abdallah Bulembo wajiandae.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni nzuri, nina *issues* za kuzungumza.

Kwanza napenda nipongeze sana miradi ya kimikakati ambayo inafanywa na Wizara hii; kwa mfano barabara, ujenzi wa reli, vivuko pamoja na ndege, ni miradi ya kimkakati na ni ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu dakika ni chache naomba niingie moja kwa moja kwenye hoja zifuatazo; kwanza tunahitaji kuwa na viwanja vya ndege ambavyo vya kimkakati vilevile. Uwanja wa Ndege wa Mwanza naomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unajibu hapo utuambie lini jengo la abilia linajengwa Mwanza. Imekuwa ni hadithi ya muda mrefu, lakini bado uwanja wa Mwanza ni uwanja wa mkakati hata kiuchumi. Nakuomba sana tupate majibu kwa sababu hatuwezi tukawa tunaenda tunarudi, tufike mahali tuwe na uamuzi ambao ni sahihi. Kama ni fedha tenga fedha za ndani zianze kujenga Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Vivyo hivyo uwekaji wa taa za kurukia ndege kwa Uwanja wa Songwe wa Mbeya nao ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile kuhusiana na suala la barabara ya Nyanguge - Busega - *Mara Border;*

ukitoka Mwanza mpaka Nyanguge barabara ni nzuri, ukifika *border* pale ya Mara na Simiyu kwenda mpaka Musoma barabara ni mzuri, kipande cha Nyanguge mpaka *Mara Border* ni kibovu sana na kila mwaka ukarabati unafanyiake fedha nyingi inatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kujua ni kwamba ni lini sasa barabara hii itarekebishwa kwa kiwango ambacho haitakuwa na usumbufu? Kwamba kila mwaka unaona wakandarasi wako barabarani? Inasababisha ajali na ni kipande ambacho ni muhimu sana; kwa hiyo ningepenga sana kujua hilo, pamoja na daraja la pale Simiyu, ukiwa pale Magu lile la chuma, ni barabara ya miaka nenda rudi mpaka leo hii ni *single lane,* yaani huwezi ukapishana pale na bado ni chakavu naomba lilekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja suala la barabara ya Nyashimo - Ngasamo mpaka Dutwa kwa Mheshimiwa Mwenyekiti Chenge. Barabara hii Mheshimiwa Rais alihaidi kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami, mpaka leo sijaona mkakati wowote wa kujenga kiwango cha lami. Nataka kujua Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* ni lini barabara hii ya Nyashimo-Ngasamo-Dutwa itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, aliwaahidi wananchi wa Wilaya ya Busega na Wilaya ya Bariadi, tena wakamshangilia sana na kura zikawa nyingi sana. Naomba hili suala tusimwagushe Mheshimiwa Rais. Kauli ya Mheshimiwa Rais ni maelekezo tosha kabisa. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa nataka kujua ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la *TTCL.* Tunazungumza kuhusu kuboresha mashirika yetu, lakini taasisi za Serikali hazitaki kujiunga na mfumo wa kanzidata wa *TTCL;* Mheshimiwa Waziri umesema ni makampuni 52 tu, kwa nini ni makampuni 52 peke yake? Naomba kampuni zote na taasisi ya Serikali zitimize maelekezo ya Serikali na walipe madeni. Hizi taasisi au mashirika yasipolipa madeni ya Serikai inakuwa tunakwamisha shughuli za uendelezaji wa mashirika

haya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana mashirika haya ya weze kulipa pesa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia la mwisho kabisa nakupongeza wewe, lakini naomba hivi barabara ya Nyasimo - Ngasamo - Dutwa nipate majibu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mhehsimiwa Chegeni, Mheshimiwa Catherine Magige, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajiandae.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa naomba nianze kwa kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayofanywa ya kuendeleza miundombinu ikiwemo ya barabara. Naomba nitoe shukrani zangu kwa kuwa tumeona Arusha inazidi kukua, tumeona barabara ya Tengeru mpaka Sakina kilometa 15, tumeona *by-pass* ndani ya Jiji la Arusha ambayo inaendelea kupunguza msongamano katika jiji la Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote naomba niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa barabara ya Ngorongoro. Tumeona barabara ya lami ya kilometa 50 inayofika mpaka Waso ambayo ni kiwango cha lami. Barabara hii itawasaidia sana akina mama wa Arusha katika kufanya biashara zao hasa Ngorongoro kwa ajili kusafirisha bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja katika masuala ya anga. Tumekuwa tukidhiakiwa na kupata aibu kuambiwa tunazidiwa na nchi ndogo kwa ajili ya ndege, lakini tumeona kazi aliyoifanya aliyofanya Mheshimiwa Rais kwa kutuletea ndege. Tumeona upande wa pili walikuwa wanasema shirika limekufa, likafufuliwa, tumeletewa ndege wakawa wanasema ndege hazijaja, sasa hivi ndege zimekuja wameingia wanansema kuna ufisadi katika manunuzi, jamani hivi hawa watu wanataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunamwambia Mheshimiwa Rais wetu afanye kazi kwa sababu kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji. Vilevile tunajua kabisa mwanaume wa kisukuma amewashika pabaya, na bado, itakapofika mwaka 2020 wataendelea kulialia kwa Watanzania na ndipo Watanzania watakapoamua, kwamba watafuata machozi au watamrudisha mwanaume wa Kisukuma? Amewashika pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja nielekeze mchango wangu katika Uwanja wa Ndege wa Arusha. Bajeti iliyopita walisema watakarabati Uwanja wa Ndege wa Arusha kwa kuongeza sehemu ya kugeuzia ndege na ya kurukia, lakini mpaka sasa hivi bado haujaongezwa; tumesahau kuwa Arusha ni Jiji la kitalii na watalii wengi wanatumia ndege zetu kwa ajili ya kuingia na kutokea Arusha. Kwa hiyo tumekuwa tukikosa mapato mengi kutokana na watalii wetu ambao wanaanzia Dar es Salaam au wanaanzia *KIA,* watalii ambao wanakwenda Kanda ya Kaskazini ikiwemo na Arusha.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri aniambie kwa sababu mwaka wa jana kulikuwa na uwanja wa Ndege wa Arusha...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** ... lakini sasa hivi sijaona kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja nijielekeze kwenye......

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimueleze mzungumzaji kwamba, wanaume wa Kisukuma katika nchi hii wako wengi, kabila la Kisukuma wananchi wake ni theluthi moja ya Watanzania wote. Kwa hiyo, kama alikuwa anamaanisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli amu-*address* hivyo ili ieleweke, kwa sababu hata wewe Mwenyekiti ni mwanaume wa Kisukuma. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza taarifa yake siitaki, anaelewa kabisa mwanaume wa Kisukuma anayewasumbua ni Rais John Pombe Magufuli, sina haja ya kumwambia, anatafuta kiki, Magufuli anawasumbua sana na bado...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Kwa hiyo wanaume wengine wa Kisukuma hawana maana?

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** ...kwa kazi kubwa anayofanya ya kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tunajua hamlali kwa ajili yake, mnamchafua halafu mnakuja kumuomba barabara, hebu tulieni huko. *(Makofi)*

**MBUGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wasinipotezee muda wangu.

**MBUGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye Shirika la Posta ambalo...

**MBUGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** ...limekuwa likiwalipa waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Posta ya Afrika Mashariki ambao wanalipwa kwa niaba ya Serikali...

**MBUGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaomba Serikali iwalipe zile pesa ambazo walikuwa wanawalipa Shirika la Posta, shilingi bilioni nne wawalipe ili na wenyewe waendelee...

**MBUGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** ...kujiendesha vizuri.

**MBUGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MWENYEKITI:** Kaa chini, Mheshimiwa nakuomba ukae chini, kaa chini.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wasinipotezee muda wangu. Tumeona reli ya *standard gauge* inakuja, ambayo itatusaidi sana wamekuwa wakiikashifu lakini hiyo italeta maendeleo kwa wananchi na hatimaye wananchi wanatuuliza maendeleo. Tunajua, tunaposema mwanaume wa kisukuma linawauma sana kwa sababu mwanaume wa kisukuma ambaye ni kiongozi wetu Tanzania nzima ni mmoja...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** ...na anafanyakazi na ni Rais wetu John Pombe Magufuli, anatekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, anaendelea kuleta maendeleo na Watanzania wote wanajua hata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. ABADALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa kwa sababu dakika tano ni chache, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mbarawa na wasaidizi wake, Katibu Mkuu, wasaidizi wake wengi wa taasisi mbalimbali, kazi mnayofanya inapendeza, tunawaona kila siku mnavyochapakazi, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwanza kwenye eneo la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kiwanja cha Ndege cha Musoma nimeona mmeweka pesa fulani hapa, lakini shughuli yake haitakuwa nzuri, lipeni wale watu fidia basi; kwa sababu tusipate hela halafu fidia ikawa shida. Muanze fidia twende kwenye uwanja, lakini tukianza uwanja watu watakwenda Mahakamani itaonekana kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, Kiwanja cha Ndege cha Bukoba; mmefuta ile Mkajunguti ambayo ilikuwepo kuanzia karibu miaka 43, tumesema tunakwenda pale Bukoba, basi tulipeni fidia tupanue uwanja ule, kwa sababu ndege chache zinatatua pale kama uwanja huo hautaweza kupanuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja mwingine ni Sumbawanga pale, mimi naongea Kitaifa kidogo. Pale Sumbawanga nao walipeni fidia uwanja uwepo. Sasa kwa sabbau eneo hili sehemu fulani imekwenda *TANROADS* ni vizuri sana mkasimamia zaidi angalau viwanja na ndege *Bombadier* zinakuja nyingi tunawapongeza ili ndege zifike kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze *standard gauge,* kwa maana ya *TRC.* Hawa watu wanafanyakazi kubwa sana ambayo ilikuwa haijafanyika siku zote, na ni kitu cha historia. Lakini naomba wale wanaokwamisha kuzuia kubomoa Serikali ifanye kazi yake kwa sababu Serikali inatakiwa kutenda. Huwezi kubomoa kuanzia Dar es Salaam ukifika pale katikati ya Tabora mtu anakataa, *standard gauge* itafikaje? Tuwape ushirikiano na

Wizara yako Mheshimiwa Mbarawa endeleeni kufanya ukali, haki ipatikane sisi tunataka maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kuhusiana na minara ya simu. Sisi tunatoka kwenye mikoa ya mbali kule. Ukianda pale Musoma, Sirari ukisogea kidogo inainga *Safaricom,* ukienda maeneo ya pale Bukoba karibu na Mutukura inakuja tena inaonekana unaanza kutumia *roaming,* wale wananchi mnawatesa, ni Watanzania, lakini nguvu ya upande wa pili inakuwa kubwa zaidi katika kutumia mawasiliano, kule tatizo lake naomba mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye *TTCL,* naomba niwapongeze Mwenyekiti Nundu na kijana Kindamba, kazi yenu ni kubwa mnayoifanya. Leo nilishawishi Bunge hili, kwa nini Wabunge mnakwenda Vodacom, Tigo hamtaki *TTCL?* Ndiyo yetu hii, ndiyo mali yetu. Mimi naomba tutumie hoja yangu kwamba kila mmoja akitoka nje ajiunge na *TTCL,* ni muda mfupi ujao miaka miwili *TTCL* itakuwa imepanda kuliko kampuni nyingine. Lakini unaweza kukuta hata ninyi Mawaziri *TTCL* hampo. Ninyi ni Mawaziri mnatumia pesa ya Serikali, *TTCL* hamjajiunga. Kwa kupitia hoja hii Waziri Mkuu, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uwaulize Mawaziri wako wangapi wako ndani ya *TTCL,* ndiyo kwa sababu wanatumia hela yetu ya kodi lakini hawajiungi na *TTCL. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Bandari ya Dar es Salaam; nichukue fursa hii kuupongeza utawala ulioko Dar es Salaam, mambo yanatoka pale, mizigo inaondoka haraka. Tunaomba nguvu hiyo isirudi nyuma kwa sababu wako wachache wanaokwamisha kwamisha juhudi zile. Wachukulieni hatua sisi tuendelee kupiga maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu *TANROADS.* Hivi *TANROADS* Mheshimiwa Mbarawa, *TARURA* mmewapa asilimia 30 si mkae mapema muongezee hata wapate 40, barabara ni nyingi za vijijini kuliko hizi barabara kuu? Kwa nini mnajipendelea? Maendeleo ni yetu wote, kwa sababu *TARURA* wana safari ndefu zaidi na ndiyo wanaanza.

Nasikia kwenye bajeti ya juzi nao viwango vya mishahara hamtaki kuwapa, hapana, tuwe *fair*, *TANROADS* wanaopata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea.

**MHE. ABADALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere na kama muda utaruhusu, Mheshimiwa Albert Obama ajiandae.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa rejea ya muda niseme tu kwamba pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na Waziri, Profesa Mbarawa na Mawaziri wake wote naomba Serikali itambue kwamba siasa za Rufiji ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa za Rufiji ni ngumu sana kwa sababu wananchi wetu wengi wanaamini kwamba serikali imewaacha mkono. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri ukisimama hapa utambue kwamba boma la Rufiji lilijengwa mwaka 1800. Hii inamaanisha kwamba Rufiji ilikuwepo nyakati za mkoloni, ni Wilaya ya sita nyakati za mkoloni na ni Wilaya ya 21 nyakati za uhuru (tulivyopata uhuru). Historia yetu inamuweka Bibi Titi Mohamed kuwa ni Mbunge wa kwanza Rufiji aliyepigania barabara ya kutoka Dar es Salaam kuja Kibiti na barabara hii ilijengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Warufiji hawaamini ahadi aliyoiweka Mheshimiwa Rais ya tarehe 2 Machi, 2017 kwamba barabara ya Nyamwage - Utete sasa inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami. Nimuombe Waziri ukisimama hapa waambie Warufiji kwamba sasa barabara hii inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa bahati mbaya

nimekagua kwenye kitabu chako sijaona ukurasa wowote unaozungumzia barabara ya Nyamwage - Utete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana, ukisoma ukurasa wa 228 imetengwa kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya upembuzi yakinifu barabara ya Nyamwage - Utete. Nikuombe Mheshimiwa Waziri ukisimama hapa waeleze wananchi wa Rufiji namna ambavyo Serikali sasa inakwenda kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itambue kuwa akina mama wengi wanafariki wakiwa wanalekea Utete kupata huduma za hospitali. Barabara hii ina kilometa 32 tu lakini inatumia masaa manne mpaka masaa matano kutembea kwenda Halmashauri ya Wilaya. Tangu mkoloni na baada ya uhuru, Rufiji ndiyo Wilaya pekee ambayo haiunganishwi na lami katika Halmashauri zote za awali, tangu nyakati za mkoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri, Warufiji sasa wamechoka, miaka 57 wamechoka, wamenituma niseme kwamba wamechoka. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri utakaposimama hapa uwaambie ahadi ya Dkt. John Pombe Magufuli ya tarehe 2 Machi, 2017; alisema mwenyewe pale Ikwiriri kwamba ataijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kabla ya mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, siasa za Rufiji ni ngumu sana, Warufiji wanabadilisha Wabunge kila baada ya miaka mitano. Nataka niiambie Serikali kwmaba iwapo barabara hii haitajengwa basi wajue na mimi watanikosa mwaka 2020. Niiombe Serikali, lazima niseme, niiombe Serikali hiki ni kilio cha muda mrefu Mheshimiwa Waziri, nikuombe sana utuambie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukurasa wa 212 Mheshimiwa Waziri umezungumzia ukaratabati mdogo, nikuombe tupe ufafanuzi wa ukarabati mdogo wa barabara Nyamwage - Utete. Kama barabara hii tayari Mheshimiwa

Rais aliashaahidi na ameeridhia ujengwe, sasa je, ni kwa nini ni kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ukarabati? Ni kwa nini fedha hizi zisiende kwenye mambo mengine na barabara hii ikajengwa kwa kiwango cha lami? Tumechoka Mheshimiwa Waziri. Nikuombe sana ukisimama hapa utueleze. Tumebakiza miaka miwili tu kwenda kwenye uchanguzi, sina sababu ya kukaa kimya, dhamira yangu ni kuizungumzia barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti. lakini pia tunaomba Mheshimiwa Waziri tumeridhia ukurasa wa 196, ujenzi wa barabara ya kutoka Kibiti kuelekea Mwaseni - Mloka ambako inajegwa kwa kiwango cha lami, nikuombe Mheshimiwa Waziri ukisimama hapa sasa utuelezee kuhusu Daraja la Utete kwa sababu halimo kwenye orodha ya mipango ya Serikali, na kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa nishati yeye alikwambia kwamba daraja hili litajengwa ili kuweza kuwaunganisha wananchi wa Rufiji na wananchi wa Kusini, tukuombe sasa utuelezee daraja hili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Obama

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze tu kwa kuwashukuru na niseme tu kwamba Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, wanafanya vizuri. Nimefuatilia mambo mengi wanayoyafanya na nchi nyingi zinazofanya mambo ya barabara, wanafanya vizuri sana, tunatakiwa kuwashukuru sana. Tumpongeze Waziri Mbarawa, Katibu wake, Naibu Waziri na wote wanaohusika na Wizara hii kwa kweli wanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nianze tu na barabara za Mkoa wa Mara na niseme wakati fulani huwa najiuliza sijui kwa sababu mtangulizi wa Taifa hili alitoka Mkoa wa Mara na kwa sababu alikuwa anajumuisha Taifa

hili kwa kuliona kama mtoto wa nyumbani kwake na akahusika kufanya maendeleo kwa kila eneo la nchi hii, lakini sasa Mkoa wa Mara kwa maeneo mengi hayaendi vizuri kwa kweli. Ukitazama barabara zetu barabara ya Nyamswa - Bunda tumeahidiwa toka mwaka juzi na iliwekewa shilingi bilioni nane mpaka leo iko kwenye utafiti tu hakuna kinachoendelea hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Buramba inatengenezwa haiendi, barabra ya Makutano - Sanzati haiendi, barabara ya Sanzati - Makutano - Mugumu haiendi, reli ya Arusha - Tanga - Musoma haiendi na Uwanja wa Ndege Musoma hauendi. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli Mheshimiwa Waziri uutakapokuja hapa uje na majibu kamili kwamba hizi barabara tulizozitaja hapa zinakwenda vizuri na unaandaa namna gani unaweza kusaidia vinginevyo tunaweza kung'anga'ania shilingi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mawasiliano, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuzungumzia masuala ya mawasiliano, niliomba kata tano, kwa maaa ya mawasiliano, nimepata kata moja kwa mtandao wa *Halotel.* Kuna vijiji vya Nyangere, Tingirima, Nyabuzume, Marambeka, Nyagurundu vyote havina mawasiliano. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri mnapokuja hapa muone ni namna gani ya kutusaidia, na ndugu yangu Nditiye uko hapo nadhani utanisaidia katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema mambo mengine madogo madogo haya lakini ni makubwa kwangu, nashangaa kuona vitu vingi vinazungumzwa hapa, sijui kuna shilingi trilioni 1.5, kuna ngapi, lakini sisi ambao tumeingia humu bado ni wageni kwenye Bunge hili tunajua utaratibu wa *CAG* unafuata kanuni ya kwenda kwenye Kamati ya *PAC* ambayo ndiyo inaita watu wote wanaohusika na ile mijadala kule ndani na kuona kile kinachohusika na kama uthibitisho utakuwa haupo ndipo tunajua kwamba hizi hela zimepotea au hazijapotea. Sasa naona watu hapa mishipa imewatoka, trilioni zimepotea, wapi sasa? Nani amekwenda kuthibitisha kwamba hela zimepotea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *report* ya *CAG* tumeona mengi, tumeona kuna vyama hapa vimepoteza hela nyingi, tumeona kuna vyama vingine vimeshindwa kupeleka hela hatusemi wameiba, tunasema ni vitu vimo ndani, kwa nini watu wameshupaa? Lakini mbaya zaidi inaonekana ni kama kwamba hizi hela ni kama vile zimechukuliwa na Rais wakati Rais si mtu wa masuhuli sasa ni maneno gani haya? Yaani kuna vitu vingine vinanga'ang'aniwa kiasi kwamba wakati mwingine huwezi kujua kama vina maana gani hivi. Jamani katika mtu ambae atakuwa wa mwisho kuhukumiwa katika Taifa hili kwamba ni mdhulumati, kwamba ni mwizi, kwamba ni mtu anayekula rushwa ni Rais John Pombe Magufuli, wananchi wanamjua ndiye namba moja kwa uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Albert Obama.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii nzuri ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kipekee kabisa kwanza nimpongeze Waziri na timu yake ya Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wote kwenye sekta hizi, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, niipongeze Serikali kwa miradi mikubwa ambayo inatekeleza, hii ya *standard gauge,* mambo ya ndege, upanuzi wa viwanda, viwanja vya ndege na kuboresha mawasiliano kwa ujumla mnafanyakazi nzuri. Kwa kuwa dakika tano ni chache basi naomba tu niipongeze Serikali kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, mimi ninatokea Buhigwe, mawasiliano kwenye vijiji vyangu viwili yanahitajika. Tumeshaleta maombi kwa Naibu Waziri na ndani ya ofisi ya mawasiliano, Kijiji cha Katundu na Kijiji cha Kajana mawasiliano ni hafifu na kule wamenituma muweze kupeleka mnara ili waweze kwenda vizuri.

La pili, niipongeze Wizara kwa kuipandisha hadhi barabara zangu miaka iliyopita, ya Buhigwe, Muyama, Mgera na Katundu, mmeanza kuitengeneza vizuri. Nimpongeze kwa dhati kabisa Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Kigoma anafanyakazi nzuri sana. Miongoni mwa mameneja ambao wanatakiwa uwapandishe na uwape mshahara mkubwa ni meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Kigoma, anafanyakazi nzuri sana, ni debe kwa sababu anafanyakazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe meneja wa *TANROADS* pale kwenye mto Mlangilizi pale kutokea Kijiji cha Migongo kwenda Mgera, tuna mto mkubwa ambao wameanza kuweka maandalizi ya kujenga lile daraja. Kwa hiyo naomba waweze kulimalizia kwasbabu bado ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna daraja lingine kwenye barabara hiyo, Mlela yeye anajua, ukitokea Buhigwe kwenda Muyama kuna daraja bovu sana pale tunalo; kwa sababu ile barabara imepanda hadhi; tungependa aweze kuimalizia. Vile vile barabara ile ya Mnanila - Mwayaya - Mbanga mpaka Janda ambayo ni ya *TANROADS* nayo tungeomba kwa safari hii iwekewe fedha ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha *TANROADS* kwa sababu Wilaya wana uwezo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sijaona ahadi ya kilometa tano za lami kwenye kitabu chako, kwa sababu Mheshimiwa Rais alishaahidi kwamba atazitengeneza, sasa sioni kama iko kwako na kama kwenye kitabu chako hatuoona kilomita tano zinatengenezwa kwa namna gani, tungependa utupe ufafanuzi utakapokuwa una-*wind up. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni ushauri. Shirika letu la *TRC* linafanya kazi nzuri na limeanza kwenda vizuri. Tunachokiomba wanapoahirisha watoe taarifa kwa wasafiri kwa sababu wanasumbuka sana, hawajui *reporting* yao na hamja-*improve* vizuri. Hata mnapofika Dodoma hamwendi Dar es Salaam basi muwataarifu, wanakaa waka-*hang*, wanatupigia simu, muwe mnawataarifu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; ningeomba muweze kumalizia jengo la abiria kwenye uwanja wa ndege wa Kigoma, kwa sababu uwanja umeshakuwa mzuri basi muweze kumalizia jengo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengine, nawashukuru, endeleeni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri mliyoanza nayo, tutaendelea mchana.

Kabla sijawataja ambao tutaanza nao nina tangazo hapa. Katibu wa Bunge ameomba niwatangazie waheshimiwa Wabunge kwamba tunaalikwa kuhudhuria katika maadhimisho ya sherehe za kutimiza miaka 54 ya Muungano wa kati ya iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar yatakayofanyika tarehe 26 Aprili, 2018 katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, Mgeni rasmi katika sherehe hizo atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wote wenye nia ya kuhudhuria; na tunaombwa wote tuhudhurie; sherehe hizo kujiandikisha tujiandikishe kwenye maokezi yaliyopo lango kuu la kuingia katika ukumbi wa Bunge pale. Ni tangazo muhimu sana hili, miaka 54 ya Muungano siyo haba, kuna nchi nyingine hazikufika hata 1/8 ya hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukaoanza nao mchana huu, Mheshimiwa John Kadutu, Mheshimiwa Mbaraka Dau (Mbunge wa Mafia huyu), Mheshimiwa George Lubeleje, heshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa na Mheshimiwa Omari Kigua, tutaanza na hawa halafu tutajipanga tena.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 7:00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Ahsante nilitaja Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao nianze na Mheshimiwa Chifu John Kadutu atafuatiwa na Mheshimiwa Baraka Dau na Mheshimiwa Lubeleje ajiandae, hawa dakika tano tano tu.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chifu wetu nikushukuru kwa kunipa fursa hii ambayo naitafuta muda mrefu, mambo yanakuwa magumu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sikuwahi kuzungumza toka tumeanza Bunge hili la bajeti, naomba nitoe maneno ya utangulizi juu ya amani kwa Watanzania wote. Suala la amani Waheshimiwa Wabunge si jambo la kikundi fulani au si jambo la Wabunge peke yake amani, dhamana ya amani ni ya wananchi na Watanzania wote. Tunafanya makosa sana kudhani sisi wanasiasa ndiyo wenye dhamana ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niseme wazi mimi sikufurahishwa na mjadala wa kuwajadili viongozi wa dini. Sisi ni sehemu yake na wao ni sehemu yetu. Kila wakati viongozi wa dini wanatuhubiri tuache mambo mabaya, mnaambiwa muache kuzini, wizi, rushwa mnashangilia lakini mkiambiwa jambo linalogusa mambo yenu mengine mnakuja juu. Tumerogwa na nani Watanzania kudhani kwamba viongozi wa dini wanachokisema ni cha uongo? Leo hii unakwenda unanyenyekea kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, lakini ukiambiwa jambo hili halifai, unakuja juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tuache kwani wao ni sehemu yetu. Mbona sisi tukifanya humu tunakuwa wakali na kupelekana Kamati ya Maadili, wapi sasa wao watajadili, wao hawana Kamati ya Maadili, wao kupitia

majukwaa ya Makanisa na Misikiti ndiyo uongozi tulionao. Kila siku tukipata mafanikio tunakwenda kunyenyekea kuombewa. Hakuna mtu humu hajaombewa baada ya kupata Ubunge hapa, lakini leo viongozi wetu wa dini tunawabeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili sijalifurahia kabisa na mimi niko tayari kutokuelewana na wengine. Najua 2020 tutakutana huko tukiwaombeeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, kwanza hii habari ya dakika tano mimi niseme tu sikubaliani nayo, muda mdogo sana huu kueleza mambo mbalimbali ya majimbo yetu na nianze na ujenzi wa barabara ya Urambo – Kaliua. Barabara hii ina kilomita 28 na inajengwa na mkandarasi mzalendo. Mimi nasema huyu mkandarasi mzalendo hana uzalendo. Haiwezekani karibu miezi nane anashughulika na usafi tu kama wa kilomita mbili. Mimi ningekuwa mwamuzi leo tunamnyanga'anya kazi hii. Hatuwezi kukaa na mtu ambaye uzalendo wake una mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia njema tu kwamba kilomita chini ya 30 tuwape wazawa wafanye kazi lakini kazi zenyewe hawafanyi. Magari kutoka Kigoma na sehemu nyingine yanazama eneo la tukio mkandarasi yupo pale wala hajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi gani hana uwezo hata wa kujenga kambi? Mvua zinanyesha za kwao, kila jambo baya wao, wapo pale. Mheshimiwa Waziri alikuja hawajali kabisa habari ya Waziri, wana kiburi kutoka wapi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri, wananchi wa Wilaya ya Kaliua wamechoshwa na jambo hili. Hatuwezi kukubali, tutafanya utaratibu tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema tofauti mnanielewa, kama hawezi sisi tutatafuta njia ya kumfanya asifanye kazi na tuko tayari kwa lolote hatuwezi kuvumilia. Kwa hiyo, tunataka sasa baada ya bajeti hii tuone mabadiliko

pale na mimi kila siku napita pale pamoja na kwamba njia siyo nzuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani suala la amani kila mmoja alizingatie, wote tuwe na dhamana ya amani. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Ezekiel Maige wajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nami nianze pale alipoishia Chifu Kadutu kwanza kumpongeza mtoa hoja wetu, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na timu yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mapema tu kwamba Wizara hii imepata bahati ya kupata Mawaziri ambao ni wapole, lakini watendaji sana kuliko kuongea. Naamini wanaitendea haki nafasi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda wenyewe ni mfupi, nitakwenda kwa haraka kidogo, nianze na ujenzi wa gati la Nyamisati. Tunashukuru kwenye kitabu tumeiona humu na mkandarasi ameshafika pale na kama alivyosema kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri kwamba kazi itaanza mwezi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wasiwasi wangu ni mdogo tu kwamba anaonekana mkandarasi huyu katika kuji-*mobilize* pale ameanza kwa kusuasua, anakuja na magari na vifaa vichache sana. Ningeomba aongeze spidi kwa sababu hali ya bandari ya Nyamisati ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni shukurani vilevile tena kwa Serikali angalau kwenye kitabu tumeona kwamba meli ya Nyamisati - Kilindoni sasa inaelekea kujengwa. Tunaishukuru sana Serikali wametenga shilingi bilioni tatu ingawa tunaambiwa itagharimu shilingi bilioni saba, tutamalizia mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni mdogo tu kwenye hili. Mheshimiwa Waziri hali ya usafiri baina ya Kilindoni na Nyamisati ni mbaya sana. Tunafahamu nia ya dhati na nia nzuri ya Serikali katika kujenga kivuko hiki kipya lakini kitachukua zaidi ya mwaka mmoja kuwa tayari. Katika kipindi hiki cha mpito, tunaiomba kwa namna ya kipekee kabisa Serikali iangalie namna gani tunaweza tukaishi ndani ya mwaka mmoja na nusu huu tukisubiri kivuko ambacho kinatengenezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanaweza wakatupatia hata vivuko vya jeshi au sehemu zozote ambazo tayari wana vivuko vya ziada watuletee Mafia angalau tuanze kwa kipindi hiki ambacho kivuko chetu kinatengenezwa tuweze kutumia mpaka hapo kivuko chetu kitakapokuwa tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi ya *TEMESA* anayoiongoza Mheshimiwa Waziri nashangaa sana, nia yake ya dhati na nia ya Serikali tunaiona lakini inaonekana limekuwa kama ni jeshi la watu watatu katika Wizara hii. Hawa *TEMESA* ni watu wa aina gani mbona hatuwajui? Jambo hili la kujenga meli kwa ajili ya Mafia tulitarajia watakuja Mafia wakae na wadau tuwaambie aina gani ya chombo ambacho kitatufaa watu wa Mafia kwa sababu kuna changamoto tofauti ya kutoka kwenye bahari na kuingia kwenye mto, kina kinaweza kikawa kinapungua, aina ya *cargo,* aina gani ya meli itakayotengenezwa, itabeba abiria wangapi, itabeba mizigo tani ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama Waziri anapambana peke yake lakini taasisi yake ya *TEMESA* haimuungi mkono, hawajafika Mafia, kwa *DC,* kwa Mbunge

wala kwa *DED,* hatujui hii meli mtaitengeneza katika *specification* zipi bila ya kuwashirika watu wa Mafia wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka sana na *TEMESA* kama kweli wana nia ya dhati ya kusaidia katika jambo hili. Kwa taarifa katika magari yanayotengenezwa pale Wilayani Mafia yamepelekwa *TEMESA* huu mwaka sasa wa nne, magari yale yako kule, hayajatengenezwa, yalikwenda kule kwa matatizo ya kama Sh.10,000,000 sasa hivi tunaambiwa yanagharimu zaidi ya Sh.40,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari yale yametushinda yako *TEMESA*, vifaa vimeibiwa, *spare parts* zimenyofolewa, tunaambiwa chukueni gari lenu, lipieni gharama za ku-*maintain* ile gari pale mkatengeneze wenyewe. Kwa hiyo, nina wasiwasi sana na utendaji wa kazi wa hii taasisi ya *TEMESA*, Mheshimiwa Waziri atupie macho hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu taasisi hii ya *SUMATRA*. Mafia nadhani ndiyo itakuwa ni Wilaya pekee au eneo pekee katika nchi hii ambapo ukitaka kusafiri kwa boti lazima ufanye *booking* wiki moja kabla. Kwa sababu wameweka masharti pale ya kupakia mwisho abiria 50 na katika *population* ya watu karibu 70,000 kusafiri watu 50 kwa siku moja ni changamoto kubwa, watu wako foleni wanasubiri kusafiri zaidi ya wiki. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dau, Mafia hiyo. Tunaendelea na Mheshimiwa George Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ujenzi wa barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa. Nashukuru kwamba Mbande - Kongwa imeshaanza kujengwa, wasiwasi wangu tukisubiri barabara hii ikamilike kuanzia Mbande - Kongwa *junction* ndiyo waanze kujenga barabara ya Mpwapwa kwa kweli itachukua miaka 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba barabara hii ianzie kujengwa Mpwapwa kuja huku Kongwa, nadhani hii itakuwa rahisi zaidi. Mwaka jana nilisema sana, nadhani Wizara hii ni sikivu, wamenisikia, mwaka huu watanisaidia. Wananchi wa Mpwapwa wameikosea nini Serikali ya CCM? Tangu nimeingia Bungeni mwaka 1990 kila hoja naiunga mkono, sijapinga hoja yoyote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Mstaafu Mheshimiwa Mwinyi aliniahidi haikujengwa, Rais Mstaafu Mheshimiwa Mkapa aliniahidi haikujengwa, Rais Mstaafu Mheshimiwa Kikwete aliniahidi haikujengwa na Rais Magufuli ameniahidi. Kwa hiyo, nina hakika kabisa Profesa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi mwaka huu asikilize kilio za wananchi wa Mpwapwa. Namwomba sana kwa unyenyekevu kabisa wanisikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimeona hapa Mheshimiwa Waziri *starting construction* Gulwe *brigde.* Daraja la Gulwe linajengwa sasa sijui linajengwa daraja lipi lingine? Daraja ambalo limebomoka kwa kuchukuliwa na mafuriko ni daraja la Godegode. Sasa hivi wananchi wanapata shida sana, wanavushwa kwa Sh.2000 kama ni pikipiki Sh.5000. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hii ni dharura wajenge daraja hilo ambalo ni kiungo kati ya Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa. Kwa hiyo, na,womba sana Mheshimiwa Waziri ashughulikie daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba barabara ya kutoka Gulwe – Berege – Chitemo - Mima mpaka Seruka ichukuliwe na Serikali. Kwa sababu wakati huo ilikuwa chini ya halmashauri wakasema hapana kwa kuwa tumeanzisha chombo *TARURA,* itajenga ile barabara. Ombi langu ni

kwamba *TARURA* wasigawane fedha na *TANROAD*, *TARURA* itengewe fedha zake za kutosha hizi za *TANROAD* ziachwe ili *TANROAD* ijenge barabara ya lami ya Mpwapwa – Mbande - Kongwa na barabara zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Tunaendelea na Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa na Mheshimiwa Omary Kigua wajiandae.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nishukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. Kazi kubwa ambazo zinafanyika kwa sasa katika sekta hii ya ujenzi Watanzania wote tunaona. Hakuna ubishi kwamba katika kipindi cha miaka 10 cha Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tutakuwa na Tanzania tofauti sana na Tanzania ambayo tumekuwa nayo kwa zaidi ya miaka 50 ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, nina mambo machache yafuatayo ambayo kimsingi ni maswali tu ambayo nataka Mheshimiwa Waziri au Naibu wake wakati wa kuja kutoa majumuisho anisaidie. Nafahamu na kwenye vitabu nimeona lakini wananchi wanauliza na mimi pia nauliza, mwaka jana kwenye bajeti ya 2017/2018 tulipitisha shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kahama – Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazungumzo ambayo nimekuwa nikiyafanya na Wizara hii toka muda huo ni kwamba baada ya bajeti kuwa imepitishwa kilichokuwa kinafuata ni utaratibu wa kumpata mkandarasi. Leo ni mwezi wa nne, mimi na wananchi hatuna taarifa zozote kuhusu utaratibu wa kumpata mkandarasi wa kujenga barabara ya Kahama - Bulyanhulu - Geita umefikia hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye bajeti ya mwaka huu tumeongeza tena fedha zingine, tumetenga shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa barabara hiyo, lakini kwa sababu wananchi hawaoni chochote kinachofanyika *on the ground* inakuwa siyo rahisi kuamini kwamba kweli barabara hii itakwenda kujengwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni nini hasa kilichofikiwa katika ujenzi, kupitisha bajeti hata mwaka jana tulipitisha lakini haitoshi wananchi wanataka kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tulikusudia kufanya Kahama iwe makao makuu ya kiuchumi kwa kanda hiyo. Ili kufikia azma hiyo tulisema ni muhimu sana kufungua barabara zinazounganisha Kahama au Shinyanga na maeneo mengine. Kuna barabara kama tatu ambazo zinaunga Kahama na Mkoa wa Mwanza kupitia Jimbo la Msalala ambazo sijaziona zimefikia hatua gani angalau kuanza kufanyiwa upembuzi yakinifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutoka Kahama - Nywang'wale - Busisi - Sengerema - Mwanza. Nimeona upande wa Mwanza kuna upembuzi yakinifu umeanza kwa ajili ya kutengeneza daraja la Busisi. lakini barabara inayounganisha sasa daraja la Busisi hadi Kahama haijawekwa katika mpango wa kufanyiwa upembuzi yakinifu. Napenda sana jambo hili nalo nisikie limefikia hatua gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutoka Kahama – Mhongolo - Burige - Solwa – Mwanangwa – Mwanza. Barabara hii ilikuwa ijengwe kwa *MCC* lakini kwa bahati mbaya fedha zile zilipoondoka ikawa imeingizwa kwenye mipango ya Serikali lakini sioni kama imewekwa katika mpango wa kufanyiwa upembuzi yakinifu. Nataka barabara hizi mbili niweze kuambiwa kitu gani kinaendelea au ni hatua gani imefanyika hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilimsikia Rais wa Rwanda Mheshimiwa Paul Kagame akiwaelekeza

viongozi wa Wizara ya Tanzania na Rwanda waanze kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga reli kutoka Isaka - Kigali. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijasikia lolote kwamba hatua gani imefikiwa sasa kwanza katika kufanya *feasibility study* na *detail design* ya reli hii lakini pia hata kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Mheshimiwa Rais niliyasikia vizuri kabisa alisema ifikapo mwaka 2020 angalau hatua fulani ya ujenzi iwe imeanza. Wananchi wa Msalala hasa Isaka na wananchi wa Tanzania kwa ujumla wanapenda kujua hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa agizo hilo la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo nataka kumalizia ni suala la mawasiliano. Nashukuru Serikali imefanya kazi kubwa sana kupitia wawekezaji wa *private sector* kuweka minara mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tatizo tulilonalo ni kwamba maeneo ambayo yamejengwa minara hii wenye minara hawalipi ushuru kwenye halmashauri (*service levy)* na vilevile hawalipi tozo yoyote ya ardhi kwenye kijiji na hata kwa wananchi ambao ardhi yao imechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwa ni jambo ambalo wamekuwa wakiliulizia na mara kadhaa tumekuwa tukiongea na Naibu Waziri, Mheshimiwa Atashasta Nditiye kuhusu suala hili, lakini kwa sababu tumekuwa tukiongea binafsi, wakati mwingine tunaongea tukiwa nje ya ukumbi huu ambao ni rasmi, napenda sana angalau leo awatangazie Watanzania kwamba ni utaratibu gani hasa ambao unapaswa kutumika kwa wananchi ili waweze kupata *appropriate share* ya *service levy* inayotoka kwenye makampuni ya simu yaliyoweka minara yao vijijini lakini vilevile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa. Mheshimiwa Omari Kigua na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi wajiandae.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza napenda nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa miradi mikubwa ambayo inaendelea ikiwemo kwenye Mkoa wangu wa Dar es Salaam na mikoa mingine. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote ambao wanatoka katika Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, nataka niongelee kuhusiana na *TARURA.* Asilimia 80 ya barabara ziko *TARURA,* lakini Mfuko wa Barabara unaipa *TARURA* asilimia 30. Tumekuwa na barabara mbovu ambazo haziwezi kutengenezwa, zinaishia tu kwenye kuandikwa na kuwekewa bajeti, matokeo yake hazitengenezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima waangalie ni jinsi gani watakavyoisaidia *TARURA* kwa sababu, wanavyoipa asilimia 30 hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea. Kwa mfano, barabara zangu, barabara ya *Airport,* Mheshimiwa Waziri anajua kabisa ndege nyingi zinaletwa, tunaenda tunazindua na kila kitu lakini barabara ni mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa unatoka *Airport* unaingia pale *opposite* na *Airport* barabara ambayo inakwenda Karakata Kipawa ni mbovu sana na kule watu wamejenga hoteli na vitu vingine ambavyo vingeweza kuongeza uchumi kwa wananchi wetu, lakini watu hawawezi kwenda kulala kule kwa sababu barabara zetu ni mbovu. Kwa hiyo, naomba sehemu ambazo wanaona kwamba zinaleta maendeleo *at least* zile sehemu ambazo wanaona ziko karibu na *Airport* basi mngeweza kuzifanyia mpango

au *strategy* maalum kwa ajili ya kuzipendezesha ili watu wanaokuja hapa nchini kwetu wakitoka tu *Airport* sio wanakutana na barabara mbovu, wakutane na barabara nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kuongelea wananchi wangu wa Kata ya Kipawa, Mtaa wa Kipunguni na Magharibi. Nimeshafanya mikutano tofauti na Waheshimiwa Mawaziri wawili au watatu juu ya madai yao ya mwaka 1992, mimi bado niko shule, lakini mpaka sasa hivi hao wananchi hawajalipwa. Mheshimiwa Waziri kila siku namwambia kwamba wale wananchi wanaendelea kuwa maskini kwa sababu tangu wamefanyiwa tathmini mwaka 1992 mpaka leo hawajalipwa, wanakuja wanawalipa watatu, wanaondoka, wanakuja wanawalipa wanne wanaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, wakati anakuja ku-*wind up* naomba aseme kwamba hao watu atawalipa au waendelee na shughuli zao zingine, kwa sababu kuwaweka wanavyowaweka, hawawaambii kama wanawalipa, hawawaambii kwamba waondoke, wapo tu kwenye njia panda hawajui kinachoendelea. Naomba sasa awaambie waendelee na shughuli zao kwa sababu mpaka sasa hivi kuna wengine wamekufa na wengine bado wanaendelea na wao wamesema kwamba watu wasijenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu nataka niongelee kuhusiana na wananchi wangu aliowabomolea wale waliokuwa kandokando ya reli. Sheria inasema kwamba mjini ni mita 15, kijijini ni mita 30, lakini cha ajabu wananchi wa Kata za Kipawa, Buguruni na Ilala kwa Mheshimiwa Zungu wote wamekwenda kuwabomolea mita 60. Tunajua kwamba wanafanya maendeleo, wanataka treni ipite lakini sasa hawa wananchi wamebaki maskini. Hilo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anielezee hawa wananchi wangu watalipwa au hawalipwi ili sasa tujue kama tunaenda sehemu nyingine ili tuweze kupata msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine niongelee kuhusiana na madaraja. Kuna madaraja ambayo yako mpaka kwa mpaka. Naongelea daraja la seminari yaani daraja linalounganisha Segerea pamoja na Kipawa. Hili daraja tangu mwaka 2012 baada ya mafuriko yale Mbunge akiwa Makongoro Mahanga mpaka leo halijawahi kutengenezwa. Kila siku namwambia Mheshimiwa Waziri hili daraja inaonekana utengenezaji wake kiwango chake cha pesa ni kikubwa, naomba walichukue *TARURA* kwa sababu Manispaa ya Ilala haiwezi kulitengeneza, haina uwezo. Sasa Mheshimiwa Waziri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma wajiandae.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi jioni ya leo niweze kusema machache juu ya hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Naibu Waziri wote wawili; ndugu yangu Mheshimiwa Nditiye pale na Mheshimiwa Kwandikwa wanafanya kazi kubwa sana. Namini kabisa Mheshimiwa Rais amechagua watu sahihi kwa ajili ya kumsaidia kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali hususan Wizara hii nimeona wametukumbuka juu ya barabara ya kutoka Handeni – Kibirashi – Kijungu - Nchemba

- Singida, ina kilometa 460. Barabara hii mara nyingi nimekuwa nikiizungumzia sana kwamba ina umuhimu mkubwa sana. Bahati nzuri kwamba barabara hii ndipo ambapo bomba la mafuta linalotoka Uganda hadi Tanga linapita. Nimeona wametutengea shilingi bilioni moja hapa, lakini niombe Waziri mwenye dhamana na uongozi mzima wa Wizara hii watutafutie pesa kwa sababu wanasema wanatafuta pesa lakini nasema watutafutie pesa wajenge barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ukiacha suala la mafuta ina shughuli nyingi sana za kiuchumi kwa sababu inaunganisha mikoa minne kwa maana ya Mkoa wa Tanga, Manyara, Dodoma na Singida. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, afanye atakachoweza ahakikishe kwamba anatupatia pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni kwamba barabara hii itakuwa na umuhimu kwa sababu upanuzi wa Bandari ya Tanga unakwenda sambamba na hilo. Kwa hiyo, mizigo ambayo itakwenda bandarini pale itatumia barabara hiyo, kwa hiyo, barabara hii ina umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naomba nizungumzie sana suala la reli ya kutoka Tanga – Moshi - Arusha - Musoma. Reli hii ni muhimu sana kwa sababu pia inalenga kuinua kipato cha nchi hii. Naamini kabisa hata mafuta yale yatakayokuwa yanakuja Bandari ya Tanga yataweza kutumia reli hii. Nimwombe Waziri mwenye dhamana ahakikishe kwamba wanaitengea kiasi cha pesa cha kutosha reli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwa ndugu yangu Waziri mwenye dhamana. Nimeona Wabunge wengi wakisimama hapa kila mmoja anazungumzia kuhusu barabara, lakini naamini kabisa nchi hii ni kubwa sana kwa maana kwamba siyo rahisi kwa Serikali kutenga pesa kwa kila barabara. Najiuliza kwa nini tusitumie sekta binafsi kwa maana ya *PPP (Public Private Partnership)?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweke mpango maalum ikiwezekana i-*train* watu wetu waje na taarifa hapa Bungeni namna gani hii *PPP* inaweza ikafanya kazi na siyo katika barabara peke yake, tunaweza kwenda pia katika maeneo mengine. Tumeona nchi nyingi duniani wametumia *PPP* katika kufanikisha maendeleo hususan katika sekta ya barabara. Naomba Waziri mwenye dhamana alichukue hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la pongezi. Nimeona barabara zangu nyingi sana za Wilaya ya Kilindi zimetengewa pesa. Kwa niaba ya Wanakilindi nawapongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa sababu naamini kabisa mazingira ya Jimbo langu la Kilindi kwa kweli yana changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina ushauri, wale wakandarasi ambao huwa wanapewa tenda za kutengeneza barabara, kwa mfano barabara hii ambayo nimeizungumzia kipindi cha wiki nzima iliyopita magari hayakupita kwa sababu wakandarasi hawa wanapotengeneza barabara hawatengenezi mitaro, magari yanakwama. Kwa hiyo, naomba Wizara iwasimamie wakandarasi hawa wanapowapa tenda hizi wahakikishe kwamba wanatengeneza katika viwango vinavyokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mawasiliano. Mara nyingi nimewasiliana sana na ndugu yangu Mheshimiwa Nditiye pale kwamba Wilaya ya Kilindi hususan katika Kata za Sauji, Kilwa, Lwande, hazina mawasiliano kabisa. Nimeona kuna taarifa imepita hapa kwamba kupitia Mfuko wa Mawasiliano wataweza kutujengea minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili walichukue kwa sababu kuna maeneo ambayo kabisa wananchi hawana mawasiliano. Jambo hili ni muhimu na ni haki ya Watanzania Wanakilindi kuhakikisha kwamba wanapata mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Mfuko huu wa Barabara. Mfuko wa Barabara ni muhimu sana, najua nilizungumzia kwenye *TARURA* lakini bado napenda nizungumzie kwamba Waziri mwenye dhamana lazima ahakikishe barabara hizi zinapitiwa mara kwa mara kwa sababu utengenezaji huu haukidhi viwango. Hili tumeona hata katika maeneo ya Mkoa huu wa Dodoma hapa, barabara nyingi haziko katika viwango vinavyotakiwa. Serikali inatenga pesa, ni lazima pesa hizo ziwe na thamani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Unaunga mkono hoja?

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Richard Mbogo wajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenijaalia kusimama hapa siku hii ya leo ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda moja kwa moja kwenye suala linalohusu usafiri wa anga. Usafiri wa anga kutoka Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya Songea, Mtwara kwenda Dar es Salaam. Tulikuwa tuna usafiri wa anga kwa maana ya *ATCL* lakini kwa masikitiko makubwa, usafiri huu umeondolewa kwa maelekezo ambayo tumepata kutoka kwenye Wizara kwamba uwanja unafanyiwa ukarabati lakini uwanja huo umetengewa karibu miezi 18 kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hizi ni siku nyingi sana kwa ajili ya ukarabati na isitoshe usafiri huu umekuwa ukichochea uchumi wa Mkoa wa Ruvuma na Mtwara kwa ujumla. Kwa hiyo, niombe huu ukarabati badala ya kufanyika kwa kipindi cha miezi 18 basi ufanyike kwa kipindi cha miezi sita ili uweze kurahisisha shughuli za wafanyabaishara na wananchi wote kwa ujumla kwenda kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii sasa niende kwenye barabara ambazo ziko ndani ya Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya wilaya mbalimbali zilizoko katika Mkoa wa Ruvuma. Kuna barabara ya Madaba – Ludewa inayounganisha Madaba na Ludewa ambayo tayari inaonekana imetengewa pesa na mwaka jana ilionekana hivyo hivyo, lakini bado utekelezaji haujaanza. Niiombe Serikali yangu iweze kufanya hima ili huduma hizi ziweze kufanyika kwa wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambayo iko Wilaya ya Namtumbo, ya Mtwara – Pachani – Lusewa kwenda mpaka Nalasi. Ahadi hii ilikuwa ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne lakini mpaka sasa hivi naona mpango mkakati unaendelea, mchakato unaendelea bado haijaingia kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mheshimiwa Mbarawa akaze misuli ili hii barabara iweze kutengemaa na wananchi waanze kuitumia kwa sababu inaunganisha wilaya mbili; Wilaya ya Namtumbo na Wilaya ya Tunduru ikipitia kule Nalasi, naomba atusaidie sana. Mwaka jana nilisimama hapa nilisema nitatoa shilingi na kweli nilitoa shilingi, sasa mwaka huu nitaondoka nayo kabisa niende nayo Ruvuma kama hatakuja na muafaka juu ya barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Namabengo - Mbimbi – Nalwehu yenye urefu wa kilometa 11. Naomba nayo pia iweze kuanza kutekelezwa kwa kipindi hiki cha mwaka 2018/2019. Hizi barabara zote zinapatikana katika hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ukurasa 220. Kuna barabara ya Lumecha – Kitanda – Londo

– Kilosa – Kwampepo, hii barabara nimekuwa nikiimba sana, inaunganisa Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Morogoro. Tunaomba sana barabara hii iunganishwe itakuwa ni *shortcut* na itarahisisha sana uchumi kati ya mikoa hii miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niende kwenye barabara ambayo iko katika Manispaa ya Songea, hii ni *bypass,* ina urefu wa kilometa 11 ambayo ilikuwa katika *package* ya *Mtwara Corridor* na inatoka katika Kata ya Sidifamu - Msamala – Ruhiko, ni kilometa 11 tu. Namwomba Mheshimiwa Mbarawa, atupie jicho hapo ili tuweze kupata ile *bypass.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kumekuwa na msongamano mkubwa sana katika Halmashauri ile ya Manispaa ya Songea. Malori yanapita hapo hapo, pikipiki na magari madogo, kwa hiyo, imekuwa ni tafrani, hapakaliki, hapaeleweki. Kwa hiyo, tunaomba tupate hiyo *bypass* ambayo itasaidia kupumua yale magari angalau hata mjini pale pakaweza kutazamika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende Songea Vijijini kwenye barabara yenye urefu wa kilometa 32 ambayo inatoka Mletele - Matimila - Mkongo. Naomba barabara hii iweze kufanyiwa matengenezo ili iweze kurahisisha pia shughuli za wakulima waweze kusafirisha mazao yao vizuri ipasavyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi wajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naanza kwa kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano na Awamu zilizopita kwani tayari tumepata daraja la Kilombero. Wananchi wa Morogoro tunashukuru sana na hivi karibuni daraja letu la Kilombero litafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuongelea ni barabara ya Kidatu – Ifakara – Kitanda – Namtumbo. Hii barabara imetengewa fedha kidogo, lakini tunashukuru Serikali hata kwa kutengewa fedha hiyo. Fedha iliyotengwa ni ya kutoka Kidatu – Ifakara, tunaishukuru sana Serikali kwa sababu hivi karibuni itawekewa jiwe la msingi. Hata hivyo, kwa upande wa kutokea hapo Ifakara - Namtumbo bado haieleweki. Ni muda mrefu tumeisemea tunaomba sana iweze kutengewa hela kwa bajeti zinazokuja au hata sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuongelea ni usafiri wa anga hasa nikimaanisha viwanja vya ndege vya mkoa. Mkoa wa Morogoro ni mkoa unaokua, una mbuga za wanyama ambazo ni Mikumi pamoja na Selous ambapo unapata watalii wengi na pia kuna ajali zinatokea. Juzi ajali ya ndege ilitokea kwenye kiwanja cha tumbaku ilibidi isukumwe kwa sababu ya kutokuwa na kiwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri tufikirie kiwanja cha abiria ambacho kitajengwa Mvomero au Kisaki. Morogoro huwezi kujenga hovyo ovyo kwa sababu ya mambo mengine yanayoeleweka, lakini kwa upande wa Mvomero na Kisaki kinaweza kikajengwa kikatumiwa na watalii wanaokuja kwenye mbuga zetu na kwa abiria pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Bigwa – Mvuha - Kisaki. Barabara hii tunaiongelea mara kwa mara ambayo ikijengwa kwa lami itasaidia watalii pia na kusafirisha mazao mengi ambayo yanaweza kulisha viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TARURA* pamoja na *TANROADS,* naungana na wenzangu kusema kwamba *TARURA* iangaliwe kwa sababu bila kupata malighafi kutoka vijijini ambako barabara zake ni mbovu hatutaweza kwa kweli kufanikiwa vizuri sana. Naomba sana itengewe fedha zaidi ili kusudi tuweze kujengewa hizi barabara zetu kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ifakara – Mahenge - Mwaya - Ketaketa sijaisikia. Hii ndiyo barabara ya kwenda Selous ambako kuna watalii na malighafi. Kwa hiyo, naomba wakati wanatenga bajeti na yenyewe waifikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile barabara ya kutoka Ifakara - Mbingu - Chita na yenyewe sijaisikia. Naomba na yenyewe waiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye mitandao ya simu, kuna sehemu mbalimbali ambazo Wabunge tumempatia Mheshimiwa Waziri ambazo hazina mitandao. Naomba sana waziangalie kusudi na zenyewe ziweze kupata minara ya simu tuweze kupata usikivu kwa upande wa Mkoa wetu wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee barabara ya Magole – Dumila - Kilosa – Mikumi – Mziha – Turiani, naishukuru Serikali imeanza kujengwa kwa lami, lakini kuna sehemu ambayo bado haijajengwa kwa lami. Naamini imetengewa fedha lakini fedha hiyo kidogo iliyotengewa ni kwa sababu ya fidia na hela za kuwalipa wakandarasi. Kwa hiyo, hiyo sehemu ya Ludewa - Kilosa - Mikumi - Mziha - Turiani naomba itengewe fedha kusudi iweze kupitika. Wakati wa mvua barabara ya Kilosa - Mikumi mawasiliano yanakatika kabisa ambapo huko ndiyo mahali ambapo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa wajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mbogo hayupo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Manyinyi na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na Mheshimiwa Daniel Nsazugwako wajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Waziri wa Ujenzi. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, lakini na kwa namna ambavyo ameweza kujipambanua katika kitabu hiki maana miradi yote inaonekana na iko wazi, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nitaenda kwa haraka sana. Namba moja, nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri alikuja Musoma na kama alivyokuwa ametuahidi Mheshimiwa Rais kujengewa uwanja wa ndege zoezi hilo limeanza na nimeona kwenye kitabu chetu hiki ziko kama shilingi bilioni 11, hongera kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu moja tu kwamba, kama Mheshimiwa Waziri alivyokuja tukazunguka katika maeneo yale kuna nyumba kama 106 ambazo zinahitaji fidia. Naomba atuambie lini tutawalipa hawa watu fidia ili waweze kuanzisha maisha yao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya hizi nyumba 106 tulikuwa na mpango wa kuchukua eneo kubwa zaidi ambalo lilichukua zaidi ya nyumba 300. Zile nyumba zote ziliwekewa X na kwa sababu sasa tulipunguza tukarudi

nyumba 106, naomba Mheshimiwa Waziri awaambie watendaji wake waende kufuta zile X kwa sababu nyumba zile watu wamehama na hawawezi kupanga tena wakiamini kwamba wakati wowote zitabomolewa. Mbaya zaidi hata benki sasa, wale wenye zile nyumba zingine hawakopi kwa sababu mabenki yanaamini kwamba nyumba zile nazo ziko katika mpango wa kuondolewa. Kwa hiyo, hilo nadhani ni vizuri likafanyika kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni barabara ya Nata – Mugumu – Klein’s Gate - Mto wa Mbu. Barabara hii tumekuwa tukiizungumza kwa kipindi kirefu lakini safari hii hata kuonyeshwa kwenye kitabu hiki Mheshimiwa Waziri hajaonyesha. Kwa hiyo, naomba tufahamu kama barabara hii imeondolewa maana ilikuwa inajengwa katika kiwango cha lami, kama imeondolewa basi ni vizuri tukajua kuliko kukaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la muhimu kwetu ni ile barabara inayotoka Musoma Mjini – Makojo. Barabara hii tunashukuru kwamba angalau safari hii imepata kama shilingi bilioni tatu lakini ina zaidi ya miaka 10 kila leo ni upembuzi yakinifu sijui fedha hizi ndiyo zitaanza lami au bado tuko kwenye upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, hilo nalo ningependa kupata maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la reli ya kutoka Tanga – Moshi - Arusha - Musoma. Mimi ile naingia hapa Bungeni mwaka 2005 kulikuwa na mpango huu wa hii reli ya kuja Musoma, lakini mpaka leo hivi tunavyozungumza kila siku inapewa tu fedha ndogo mfano kama safari hii nimeona kuna shilingi bilioni mbili. Sasa ni zaidi ya miaka 15 suala la upembuzi yakinifu bado linaendelea. Napenda Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina kuhusiana na hiyo reli ya Tanga – Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho linahusiana na hawa wakandarasi wetu wa ndani. Kwa kweli wazo na mipango ya Serikali ni mizuri kuwawezesha wakandarasi wa ndani, lakini hawa wakandarasi wa ndani kwa utaratibu

tunaoenda ni kweli kwamba hawawezi kukomaa. Mfano, ukiangalia barabara ya Makutano - Nata ni zaidi ya miaka mitano inajengwa katika kiwango cha lami lakini haisogei. Kwa hiyo, wakati mwingine tunakuwa na mashaka kwamba wale wakandarasi ndiyo hawana uwezo kwa maana kwamba ndiyo hawajengi lakini ukiangalia kwa kiasi kikubwa inachangiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachangia kwa sababu gani? Kama kweli tumedhamiria kwamba tunahitaji kuwa-*empower* ni lazima hata pale wanapoomba zile *advance payment* tuwe tunawapa kwa wakati. Kwa hiyo, anapojikuta kwamba akiomba *advance payment* hatuwezi kuwapa na inachukua muda mrefu na tunatambua kwamba hawana uwezo hayo ndiyo matokeo kwamba mradi mmoja unachukua muda mrefu na matokeo yake badala ya kumsaidia mkandarasi yule tunaendelea kumdhoofisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliangalie sana suala la namna ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii, lakini vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kushukuru Wizara, Waziri husika, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na wasaidizi wake wote. Kazi tunaiona na tunaendelea kuwa-*support,* tupo nyuma yenu, endeleeni kufanya kazi na tunaamini Tanzania itaendelea kubadilika kwa muda tunaotarajia kuweza kufika huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kwamba Wizara ya Ujenzi ni muhimu sana katika Taifa letu lakini hatuwezi tukasonga mbele kama tutakuwa hatuangalii au tuka-*review* bajeti zetu ambazo tunazipitisha mwaka baada ya mwaka. Kuna mambo mengi ambayo yameelezwa bajeti iliyopita mwaka 2017/2018 na 2018/2019 kuna baadhi ya mambo ambayo nimeangalia kwenye hotuba na nimeona yanakwenda vizuri lakini bila kuangalia tulichokifanya mwaka jana na mwaka juzi tunaweza tusiweze kufika tunakoenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kubwa ambalo tunaliangalia la *TARURA* na *TANROARDS* ambako tunakuta asilimia 30 kwa asilimia 70 ya maendeleo. Sasa tuangalie uwezekano kwa sababu *TARURA* tuna barabara nyingi, zaidi ya 100,000 ambazo tunatarajia kuzitengeneza lakini asilimia ambayo imetengwa ni ndogo sana. *TARURA* inaangalia vijijini ambako ndiko kwenye watu wengi na ndiko kwenye tija. Napenda kuishauri Serikali namna gani ambavyo tunaweza tuka-*balance* sasa *at least* tupeleke kwenye 40% kwa 60%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba viwanja vya ndege vimeendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali lakini niseme mahsusi kwa Kiwanja cha Nduli ambacho kipo Iringa. Kiwanja hiki cha ndege ni cha muhimu sana. Upande wa Nyanda za Juu Kusini ndiyo tuna Kiwanja cha Songwe ambacho Serikali imeshatenga fedha lakini naamini kabisa Kiwanja cha Nduli ambacho kipo Iringa kitakuwa ni sehemu ya ukuaji wa uchumi katika Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Nimshukuru sana Makamu wa Rais alikuja Jimboni na alikuja Mkoani Iringa na akaangalia maendeleo ya mkoa.

Kupitia Benki ya Dunia tumepata ufadhili wa kujenga ile barabara ya kutoka Iringa Mjini kuelekea *Ruaha National Park* kwa kiwango cha lami. Hiyo peke yake ni maendeleo ya makubwa sana kwa Taifa letu na watu wa Iringa tunajivunia sana kwa sababu tunaamini sasa tutaenda kupata uchumi ambao tunautarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba maendeleo bila barabara au bila kuhakikisha kwamba masuala mazima ya usafiri wa anga yanakaa vizuri bado tunaweza tukawa nyuma tukijilinganisha na nchi zingine za Afrika Mashariki. Niseme tu kwamba Tanzania tumejipanga vizuri na naamini kabisa kwa Awamu hii ya Tano tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali katika eneo moja, kuna mikataba mbalimbali ya usafiri wa anga ambayo Serikali inaingia inaitwa *Bilateral Air Service Agreement*, Tanzania bado tuko nyuma kidogo, tuingie mikataba mingi na mashirika mbalimbali ya kimataifa ili ndege mbalimbali ziendelee kufika Tanzania na sisi tuweze kurusha ndege zetu katika viwanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya wenzetu wameshasogea sana, Uganda nao wanakwenda sisi Tanzania mpaka mwaka 2017 tulikuwa tumeingia mikataba mingine mipya 10, hiyo haitoshi. Napenda kushauri Serikali kwamba bila kuingia mikataba mikubwa ya namna hii tunaweza tukabaki nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ni la *PPP*. Naamini kabisa maendeleo yetu Watanzania bila *PPP* tunaweza tukawa nyuma, tunaweza tusifanikiwe. Ni lazima tufanye utaratibu wa kuji-*engage* sisi wenyewe katika miradi ya *PPP*. Wenzetu wa Rwanda wamejenga uwanja wa Busegera ambao ni asilimia 25 kwa asilimia 75, utakuwa ni uwanja mmoja mzuri sana katika ukanda wa Afrika Mashariki. Naamini kwa sababu wameamua kufanya hivyo sio lazima watumie fedha zao zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bado tuko nyuma kimaendeleo. Afrika tunahitaji tuweze kujilinganisha na nchi zingine lakini tutafikaje huko tunakotaka kwenda kama tutakuwa tunatumia nguvu zetu nyingi bila kushiriki katika uchumi unaostahili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Yahaya Massare ajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kuwapa hongera Profesa na timu yake, Makatibu wake Wakuu, *Engineer* Nyamuhanga, Injinia Chamuriho na Injinia Sasabo kwa kazi nzuri. Vilevile niwape hongera Naibu wake wawili, *Engineer* Nditiye na Mhasibu na mbobezi ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu kwa sababu hii ni Kamati yangu, mambo mengi tumeshazungumza kwenye Kamati. Nianze na barabara ya Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi. Nimkumbushe Mheshimiwa Waziri tu kwamba barabara hii ina miaka 26 tangu imefanyiwa upembuzi yakinifu na *detail design,* barabara haijengwi. Kwa taarifa tu ni kwamba ndiyo barabara ndefu ambayo haijawa *paved for the last 26 years,* ni barabara sasa ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Kabingo - Nyakanazi. Najua ziko juhudi zinazofanyika lakini *quick match* ndiyo tunayoitaka kuliko hii *slow match.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa barabara hizi mbili za Kabingo -Nyakanazi na Kidahwe - Kasulu kwa kweli tunaomba zimekaa sana, zina miaka tisa sasa, hawa wakandarasi wanadai fedha wamalize zile barabara. Mheshimiwa Waziri haiingi akilini mkandarasi anadai shilingi

bilioni 11 analipwa shilingi bilioni moja analipa *diesel* tu basi kazi inasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *on a serious note* nimshauri Mheshimiwa Waziri na timu yake, wafanye *inventory* ya barabara hizi, zile barabara ambazo zilianza na zina wakandarasi zikamilike kwanza kuliko barabara zilizoanza hazikamiliki, zinakuja barabara za katikati zinakamilika, hatuna sababu ya kuzitaja hapa kwa sababu kila mmoja anahitaji barabara. Naomba sana Mawaziri wapo hapo wafanye *inventory* ya barabara hizi, barabara zilizoanza zenye wakandarasi zikamilike ili tupige hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 227 unazungumzia habari ya kitu kinachoitwa *Lake Tanganyika Roads under Lake Tanganyika Transport Program.* Sasa *Lake* Tanganyika ni mikoa mitatu tu Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Rukwa. Napenda watakapokuja kuhitimisha tujue ni barabara zipi hizi ambazo zimetengewa shilingi milioni 200 kwenye bajeti hii, ukurasa 227. Tusije tukawa tunazungumza barabara kumbe ni ya kwenda Chaguru au barabara ya Ilagala kwenda Kalya kumbe iko chini ya programu nyingine ambayo wanaita *Lake Tanganyika Roads Program*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda niliseme na hili limenishangaza kidogo, nadhani wenzangu kwenye Kamati watakubaliana na mimi tulijadili sana, ujenzi wa hii reli ya *standard gauge.* Naona zimetengwa shilingi bilioni 100 kuanzia Isaka kwenda Rusumo, hiyo inatoka wapi? Nilidhani hoja ya sasa ingekuwa ni kuanzia Makotopora kwenda Tabora ili hatimaye reli hiyo iwe na maana ya kiuchumi uliokusudiwa. Sasa hii hoja ya kuanzia Isaka kwenda Rusumo eti kwa sababu mnajenga na Rwanda maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie vipaumbele vyetu na kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati yetu tunataka reli hii iwe na manufaa zaidi kwa Watanzania kuliko majirani. Majirani watanufaika baada ya kuwa Watanzania tumeanza kunufaika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweke msisitizo, reli hii jina lake ni Dar es Salaam – Kigoma, ndiyo reli ya kati na ndiyo tafsiri yake. Sijui kwa nini tafsiri hii imekuwa ikipotoshwa na nashangaa sasa hiki kipande cha kutoka Isaka kwenda Rusumo wanakipa kipaumbele shilingi bilioni 100 wakati kipande cha Tabora – Dodoma bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nishukuru ujenzi wa uwanja wa ndege, jengo la abiria, nimeona shilingi bilioni mbili kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri. Napenda atakapokuja kuhitimisha hoja yake maeneo mengine ameeleza *status* mkandarasi amepatikana, lakini sisi imetengwa shilingi bilioni 2.3 lakini hawaelezi *status* ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma ambao naona ni jengo la abiria na maingiliano yake. Kwa hiyo, napenda atakapokuja kuhitimisha Waziri atueleze *status* ya ujenzi wa kiwanja hicho umefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni mawasiliano. Tumeshapeleka kwa Mheshimiwa Waziri orodha ya vijiji ambavyo havina minara, sasa huu mwezi wa nne. Tunataka tuone minara inajengwa, nadhani ndiyo hoja ya sasa. Hatuwezi kuzungumzia habari ya mawasiliano wakati maeneo mengine hayana mawasiliano.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Mwalongo ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya na kwa kweli wanaombeza labda hao ni wanga tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na Naibu wake wote

kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya katika Wizara hii. Wamezindua miradi mingi sana ukiwepo ununuzi wa ndege na ujenzi wa reli ya umeme, niwapongeze sana. Kutokana na kazi nzuri ambayo reli imekuwa ikifanya kuna ule mfuko wake pengine wangeachiwa maana unachukua muda mrefu na wao wana kazi nyingi na tunajua kwamba tunataka reli hii ikamilike mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze Serikali kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege, mwenzangu amepongeza na mimi napongeza. Kupitia *World Bank* Kiwanja chetu cha Nduli kitajengwa ikiwa *package* mojawapo na ile barabara inayokwenda mbuga za wanyama. Kwa kweli naamini kabisa Mkoa wetu wa Iringa sasa tutapata uchumi wa kutosha na utafunguka kiutalii kwa sababu tukishajenga uwanja na tukishapeleka barabara ya lami *Ruaha National Park* najua kwamba Nyanda za Juu Kusini na Mkoa wa Iringa pia utafunguka kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kupongeza Serikali kuhusiana na ujenzi wa mtandao wa barabara nchini ikiwepo barabara ya Dodoma - Mtera - Iringa kilometa 260. Kwa kweli barabara hii imekuwa mkombozi sana kwetu, inatufanya dakika dakika mbili tumefika Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ipo changamoto kubwa pale, ningeomba Mheshimiwa Waziri aangalie na ikiwezekana labda twende akaiangalie vizuri zaidi pamoja na wataalam wake. Wakati wa mvua ile barabara mawe yanadondoka kiasi kwamba kuna wakati magari hayapiti kabisa. Kwa hiyo, tumemwona hata Meneja wa *TANROARDS,* Ndugu Kindole, karibu siku tatu amefanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, naomba kabisa barabara hiyo iangaliwe kwa sababu kuna wakati itakuja kuleta ajali kubwa sana na ikiwezekana bajeti ya mkoa iongezwe kutokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali itoe kipaumbele kwa barabara zetu za kiuchumi zilizopo katika

Mkoa wa Iringa. Kwa sababu tumeona barabara hizi mara nyingi zimekuwa hazipitiki wakati wa mvua na kusababisha karibu siku mbili au tatu magari hayapiti, kwa hiyo, hilo ni tatizo kubwa. Barabara za Mafinga – Mgololo; Kilolo – Idete – Ipalamwa; Kinyanambwa – Saadani – Madibira na Kalenga – Kiponzelo, hizi ni barabara za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna barabara nyingine za kiuchumi ambazo ziko *TARURA,* pengine kwa sababu *TANROADS* huwa inachukua barabara za msongamano wa Dar-es-Salaam ingejaribu kuchukua hata barabara ambazo ni za kiuchumi zilizopo katika mkoa wetu ili huu uchumi wa viwanda sasa kwa sababu malighafi ziko huko, itakuwa matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka nichangie kuhusiana na *TAZARA.* Ni lini Serikali itarekebisha Sheria ile ya *TAZARA* kwa sababu imeshapitwa sana na wakati na utaona inawa-*favour* sana Wazambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TAZARA* ina madeni, Serikali ililipa milioni 550 lakini bado wanadai milioni 745. Hivyo, tungetaka tujue lini watawalipa hawa wafanyakazi ili waendelee kuwa na moyo wa kuitumikia Serikali yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee kuzungumza kuhusu *USCAF,* Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, niwapongeze wamefanya kazi nzuri, hata mimi nilishawahi kwenda katika ziara zao kwa kweli wamepeleka mawasiliano vizuri. Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo katika Mkoa wetu wa Iringa bado ni matatizo. Kuna Lyamungo, Mfukulembe, Kalenga, Mpanga *TAZARA,* Lulanda, Mlafu, Mahenge, Ilindi, Magana, Iramba, kote huko bado kuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu naona iongeze kasi ya usambazaji wa mawasiliano sehemu ambazo hazina mvuto wa kibiashara, lakini pia iongeze rasilimali watu ili hii kazi iweze kwenda kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, unga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Mwalongo atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa na Mheshimiwa Zainabu Mndolwa ajiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mpaji wa yote kwa kutujalia Wabunge wote kuwemo humu ndani na tunaendelea na kazi yetu vizuri. Pia nawapongeza sana watendaji wote wa Serikali, akiwemo Rais wetu na Mawaziri na wote wanaowasaidia kutimiza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala la ujenzi kwanza kabisa niseme kwamba kwa kweli nasikitishwa sana na jinsi bajeti ilivyowekwa katika Mkoa wa Njombe na hasa katika barabara ya Itoni – Manda. Barabara hii ni miaka mingi sana imekuwa ikiahidiwa itawekewa lami na kipande cha kilometa 50 kimeshaanza kuwekewa lami ndani ya Wilaya ya Ludewa lakini hakisongi mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayotolewa ni ndogo sana kiasi ambacho kazi haiendi na maeneo yale ni ya uzalishaji mkubwa na ndiyo ghala la chakula kwa ajili ya wananchi wa nchi hii. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali, hebu iwe *serious,* tunaposema tunataka kutengeneza barabara ya lami kwa ajili ya kuleta maendeleo katika maeneo yetu,

basi iwekwe fedha ya kutosha na kazi iweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuliongelea ni barabara za mijini ambazo *TANROADS* huwa inajenga. Njombe Mjini ni Makao Makuu ya Mkoa, tumetengenezewa barabara ya lami mita 150. Sasa ukiangalia *mobilisation* ya vifaa vya lami kwenda wilayani au mkoani kama Njombe halafu vinakuja kufanya kazi ya mita 150 ni upotevu wa fedha. Siyo kwamba tunakataa tusitengenezewe, lakini hebu wabadilishe utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya Mkoa barabara haziridhishi kabisa lakini zinakuja kutengenezwa mita 150, mkandarasi anakuja pale kwa ajili ya barabara ya mita 150, anasafirisha *grader, roller, escalator,* malori na mashine za kumimina lami, anakuja kufanya kazi ya mita 150, hii inasababisha barabara iwe ya ghali sana. Kwa hiyo, niombe sana Njombe tutengenezewe barabara za mjini kwa sababu ni Makao Makuu ya Mkoa na hali ya barabara za mjini ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uwanja wa ndege. Nimeona wanasema kwenye viwanja vya ndege ambavyo vimo na Njombe imo. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa nataka asema mipaka ya uwanja wa ndege iko wapi? Wananchi wale wanaozunguka uwanja wa ndege wa Njombe wanastahili nini? Wahame, waendelee kuwepo, watawalipwa fidia au wapime nyumba zao zile waendelee kuishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu siku zote wananchi wale wa Njombe wamekuwa hawaelewi, wanaishi kwenye sintofahamu. Wanashindwa kuendeleza maeneo yao, hawapimiwi na uwanja wa ndege hawatoi taarifa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ule uwanja wa ndege ni pori na unatusababishia vibaka pale mjini.

Niwaombe sana wakija hapa keshokutwa kuhitimisha bajeti yao waseme uwanja wa ndege wameshafyeka majani yote ndani ya uwanja hayapo. Kwanza uwanja wenyewe uko mjini, hawausafishi, wanatusababishia mji uwe mchafu. Vibaka wanatoka pale wanasumbua watu mtaani lakini vilevile wamefanya kama ndiyo *dampo* kwa ajili ya kutupa uchafu mbalimbali katika uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri anajitahidi sana kujenga barabara, lakini nimefanya utafiti mdogo, Jeshi la Polisi, Idara ya Trafiki wanabomoa barabara. Wanasimamisha malori mahali ambapo sio mahali maalum pa kusimamisha lori, matokeo yake barabara inamegeka mabega kidogo kidogo, wakiona pameshakuwa na mashimo pamemegeka sana wanahama wanaenda kuanzisha kituo mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ya Ujenzi wakae na Wizara ya Mambo ya Ndani wakubaliane *Police Traffic* watasimama wapi na watasimamisha magari wapi kwa sababu hii ni hasara kwa nchi. Kama sehemu za vivuko vya ng'ombe tumeandaa mazingira maalum kwamba ng'ombe wavuke mahali fulani, kwa nini malori yasiandaliwe mahali pa kusimamishwa? Wanaamua tu kwamba leo tusimame hapa, leo tusimame hapa, malori yanasimamishwa yanakwenda kandokando ya barabara yanaharibu barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo, lakini naomba sana barabara za Mji wa Njombe ziangaliwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kujadili hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Kwanza, nipende kumpongeza Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Profesa

Mbarawa, niwapongeze Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Injinia Nditiye na ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema Wizara inafanya kazi yake ipasavyo japo kuna upungufu kwenye maeneo mbalimbali. Nianze na barabara ya Itoni – Ludewa – Manda. Tukumbuke kwamba barabara hii inaenda kwenye ile miradi yetu ya kimkakati ya Liganga na Mchuchuma na ina kilometa 211 lakini mpaka sasa inajengwa kilometa 50 na ujenzi wake unaenda kwa kusuasua sana. Kwa hiyo, niwaombe Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla wake waongeze nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna barabara ya Mkiu – Madaba na Mchuchuma – Liganga. Barabara hizi sasa hivi zinafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa hiyo, nimwombe sasa Mheshimiwa Waziri na timu yake waanze kuiweka kwenye ule mpango sasa wa kujengwa kwa lami kwa sababu inaenda kwenye ile miradi kielelezo, miradi ya makaa ya mawe Mchuchuma na chuma Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara kupitia chombo chao kinachoitwa *Tanzania Road Fund.* Kwa kweli, kinafanya kazi nzuri na tumejaribu kuwa tunawasiliana nao kwa kina na hivi ninavyozungumza kule kwetu Ludewa tuna vijiji 15 ambavyo havijawahi kuona gari wala baiskeli lakini Wizara imekuwa sikivu kupitia mfuko huu. Leo hii tumeshapata fedha kidogo ambapo tunaanza kufungua angalau vijiji viwili, vitatu katika kipindi kijacho kifupi. Kwa hiyo, napenda kuwapongeza lakini tuendelee kuitia moyo Wizara iwakumbuke sana watu wa kule Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara inayotoka Lupingu - Matema. Barabara hi inapita mpakani mwa nchi na ina kilometa zipatazo 139 lakini haipitiki. Ndiyo maana sasa tunasema ifike mahali eneo la mpaka ni lazima tuwe na barabara na tuiombe sasa Wizara iingize kwenye mpango ili angalau mwisho wa siku tuweze kuwahakikishia

usalama, ulinzi na kuongeza utalii kwenye lile eneo. Tuna ziwa letu zuri linalopita kwenye Bonde la Ufa, kwa hiyo, kuna haja sasa ifike wakati tutengeneze barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Injinia Nditiye, kwa mara ya kwanza amefika Ludewa na amezungukia vijiji 15. Moja kati ya vijiji ni hivyo ambavyo havijawahi kupata barabara. Ziara yake imekuwa na tija, leo hii tunajengewa minara nane ya mawasiliano kupitia *effectiveness* ya ile ziara yake. Leo hii tunapata angalau vituo vya kupakia na kushusha abiria vipatavyo vitano kupitia ile ziara yake. Kwa hiyo, nimshukuru na ikiwezekana aendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nipende kukwambia wewe na Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Nditiye amepewa Uchifu kule kwa sababu ya ile ziara tu iliyopita. Watu wameona jitihada za Serikali hii na wameona kwamba Naibu Waziri anafanya kazi zake nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuipongeza Serikali kwa ajili ya barabara ambayo tumeipata ya Makonde – Mawenji. Barabara hii ilikuwa haipitiki kabisa lakini leo hii angalau tunaona zinakuja hela kwa ajili ya kuitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ujenzi wa meli mbili za mizigo ambapo tayari umeshakamilika katika Ziwa Nyasa na kuna ujenzi ambao sasa hivi unakaribia kwisha wa meli za abiria. Kwa hiyo, tuiombe Serikali ifanye jitihada za haraka kwa sababu wale watu wanasumbuka sana usafiri umekuwa haupo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hawa ninaowataja sasa hivi ni dakika 10, Mheshimiwa Zainabu Mndolwa na Mheshimiwa Ali Salim Khamis na Mheshimiwa Saed Kubenea wajiandae.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi yake nzuri anayoifanya pamoja na Naibu Mawaziri wake na wafanyakazi wa Wizara wote kwa ujumla. Nampongeza kwa sababu tunaona msongamano Mkoani Dar-es-Salaam umepungua kwa kupata mwendokasi na sasa hivi katika bajeti hii nimeona barabara mbalimbali zimetengewa bajeti ya matengenezo ili kuepuka msongamano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna changamoto nyingi zinajitokeza. Bajeti hii imepangwa na kwenye vitabu inaridhisha na inaonekana ni nzuri sana, Dar-es-Salaam ni uso wa nchi yetu kwa sababu watu mbalimbali wanavyotoka nchi za nje hufikia Dar-es-Salaam na baadaye ndio wanakuja mikoani, kwa hiyo, naomba bajeti iliyotengwa ifike kwa wakati. Vilevile tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri atutafutie wakandarasi ambao wana kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona barabara yetu ya Kilwa ilitengenezwa chini ya kiwango baada ya muda mfupi imeharibika na hapa tumeona pia itatengenezwa kwa mwendokasi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri mkandarasi atakayempata aiboreshe ile Barabara ya Kilwa iwe yenye ubora kwa sababu ilitengenezwa mara ya mwanzo lakini haikuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia kuhusu Kivuko cha Magogoni. Ni muda mrefu sana wananchi

wa Dar es Salaam, hususan waishio Kigamboni walikuwa na tatizo la kivuko na msongamano wa magari lakini tunashukuru Serikali ikatujengea Daraja la Nyerere. Napenda kueleza Bunge lako Tukufu, wananchi wa Kigamboni bado wana changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uvuke katika daraja lile kwa gari ndogo tu ni shilingi 2,000 ukizingatia wananchi wake wengi shughuli zao zote ziko ng'ambo ya bahari, lazima wavuke asubuhi wawapeleke watoto shule, ofisi nyingi ziko ng'ambo ya bahari, hospitali pia, changamoto ni nyingi na kwamba ni ghali mno kuvuka katika daraja lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa gari ndogo ni Sh.2,000, mtu akivuka tu kwenda na kurudi Sh.4,000. Wakati mwingine watu pia wanakuwa na wagonjwa hospitalini wanaenda mara tatu kwa siku, gharama ya kivuko ni kubwa mno Mheshimiwa Waziri. Namwomba pamoja na Wizara ya TAMISEMI, ingawa nilishauliza swali hili kwamba *NSSF* nao walijenga lakini ninachokiona kwa Daraja la Kigamboni, wananchi wa Kigamboni wamepewa mzigo mkubwa sana. Hawana faraja na lile daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijua kwamba wananchi wa Kigamboni wamepata faraja kwa uwepo wa daraja lile angalau watavuka labda kwa bei nafuu, lakini kwa bei ya Sh.2,000 kwa gari ndogo na gari kubwa mpaka Sh.7,000 mpaka Sh.15,000 ni ghali mno. Naiomba Wizara hii kwa kushirikiana na TAMISEMI waliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi imefikia wakati wananchi wa Kigamboni ambao wanatumia vyombo vya moto, magari yao hawavuki nayo. Ukienda katika Kata ya Kigamboni utakuta watu wengi wameweka *parking* za magari, anaweka gari lake anavuka kwa *panton* kwa shilingi 200, anaenda kufanya shughuli zake mjini kisha anarudi analipa shilingi 1,000. Kwa hiyo, anakwepa kuvuka kwenye daraja kwa sababu ni ghali mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wafanye utaratibu kabisa, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile analifahamu hili, wananchi wa Kigamboni wanafurahia daraja, lakini daraja lile halina neema kwao. Wanasema maisha bora kwa watu wa Kigamboni kwenye daraja lile hayapo ni ghali mno. Kwa sababu, hata kama ni mshahara Sh. 4,000 mtu anavuka kila siku kwenda na kurudi, mwisho wa mwezi aki-*calculate* ina maana unaishia kwenye usafiri. Nadhani katika madaraja yote Tanzania ni Daraja la Kigamboni tu ambalo watu hutozwa nauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea kwamba watu wa Kigamboni watapata neema kwa sababu madaraja ni huduma kama huduma nyingine. Kama ni masuala ya kukusanya kodi basi lile daraja lingejengwa Ruvu au Wami kwa sababu ni magari mengi sana yanapita maeneo hayo na Serikali ingekusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiomba Mheshimiwa Waziri, naona ananitazama lakini naomba aandike haya ninayozungumza na ayazingatie akishirikiana na TAMISEMI, wawaonee huruma wananchi wanaoishi Kigamboni kwa sababu daraja lile halina manufaa kwao, ni ghali mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wapunguze na ikiwezekana wavuke hata kwa kutumia *smart card,* hata kama wakiambiwa shilingi 10,000 kwa mwezi au shilingi 20,000 hata mtu akivuka mara tano mara kumi lakini ana kadi maalum ili kupunguza gharama ile. Wakati mwingine wanashindwa kabisa magari yao huacha ng'ambo na kwenda kwa kutumia *panton. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia kuhusu barabara zetu. Tumeona Serikali imejitahidi kwa kiwango kikubwa na imeona jambo la muhimu barabara ya Dar es Salaam – Morogoro na sisi ni mashahidi tunapita kila siku katika barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niliuliza hapa kwamba ni lini Serikali itafanya mkakati wa kukarabati barabara zetu na mojawapo ni eneo korofi sana la Chalinze hadi Mlandizi. Nikajibiwa kwamba eneo lile ni korofi kwa sababu inapita mizigo mizito lakini mimi ninachosema siyo mizigo mizito tu pia kiwango cha barabara ni cha hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mkandarasi aliyejenga maeneo yale hakuzingatia eneo lenyewe husika labda lina maji ya aina gani ili atumie *material* husika. Kwa sababu kama ni mzigo mzito umetokea Kurasini bandarini, ukapita barabarani ukafika mpaka Mlandizi pale barabara angalau ni nzuri, lakini kutoka Mlandizi mpaka Chalinze ile barabara ni mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo suala la mzigo mzito kwa sababu mzigo ni uleule uliotoka bandarini na ndiyo uleule uliopita katika eneo lile na ndio uliofika Chalinze na kwenda Chalinze ukaenda Morogoro au Tanga na barabara kule ni nzuri. Kwa hiyo, hapa tatizo ni wakandarasi wetu, wanajenga barabara chini ya viwango. Namwomba Mheshimiwa Waziri pindi atakapoanza kutengeneza hizi barabara atafute wakandarasi wenye viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwawekee masharti hawa wakandarasi, ikiwa watajenga barabara chini ya kiwango na ikifikia muda fulani na tumewalipa pesa, kwa pesa zao wenyewe waweze kugharamia barabara zile kwa maana kwamba wazitengeneze kwa fedha zao kwa sababu wanapewa fedha lakini barabara ziko chini ya kiwango na kuipa Serikali hasara kila mara kwenda kukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika taarifa hii kwamba barabara ya Chalinze mpaka Mlandizi kuna kilometa kama 12 zimeshaanza kukarabatiwa toka Machi lakini mimi napita mara kwa mara, ukarabati unaofanyika pale ni kuziba viraka. Kuziba viraka siyo kwamba ndiyo unatengeneza barabara, barabara ile ina mabonde kama matuta ya viazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa ile barabara ijengwe kwa kiwango hata kama ni cha zege ili kuhimili mizigo mizito inayopita. Kwa sababu wanakarabati kwa kuweka viraka kusema ukweli bado tutapiga *mark time,* bado hatujatengeneza barabara zetu. Naiomba Serikali, kama mnavyosema Serikali hii ni sikivu, iwe sikivu kweli, haya yaliyoandikwa yatekelezwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi zina matatizo pia. Kuna barabara ya kutoka Magole - Gairo ni mbovu. Mnaona maeneo ya Magubike tukipita barabara ni mbovu, naomba Serikali yetu pia itengeneze barabara hizo. Barabara nyingine ziko kwenye kingo za milima angalau Serikali wakati wanajenga zile barabara kuu zile waweke *pavements* ili wakati wa mvua kubwa mmomonyoko usiathiri barabara zetu na kuleta matatizo.

Kwa hiyo, haya aliyoyaandika Mheshimiwa Waziri katika kitabu hiki ni mazuri lakini changamoto zinakuja utekelezaji upo? Serikali itoe fedha kwa wakati na wakandarasi wanaoomba nawaomba wazingatie ubora na viwango vyao ili waweze kutengeneza barabara zetu ziwe za viwango na siyo kutengeneza barabara ili mradi barabara tu na kuipa Serikali hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri haya yote yaliyoandikwa yawe yanatekelezeka maana nimeona Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengi hapa wamechangia wakisema kwamba mambo mengi yalikuwepo bajeti zilizopita lakini mpaka leo ni ahadi tu kwenye vitabu lakini utekelezaji wake ni wa chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, kama ni Serikali sikivu aishauri iweze kukarabati na kujenga barabara zetu kwenye kiwango kinachohitajika ili kuepuka ukarabati wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mbarawa, kama ni Serikali sikivu naomba aishauri iweze kukarabati na kujenga barabara zetu kwenye kiwango kinachohitajika ili kuepuka ukarabati wa mara kwa mara. Ukarabati huu wa mara kwa mara huipa Serikali hasara pia na badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma. Badala ya kujenga barabara nyingine, tunarudi kujenga barabara ambazo zilishajengwa na zimejengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nashukuru sana kwa mchango huu namwomba Mheshimiwa Waziri yatekelezwe kwa wakati na Serikali itoe fedha kwa wakati kama ilivyoahidi na kama ilivyoandika ili barabara zetu ziwe za kiwango. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea Mheshimiwa Ali Hamisi Salim, Mheshimiwa Saed Kubenea na Mheshimiwa Lucy Magereli wajiandae.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na leo hii kuweza kupata fursa ya kuweza kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa na maswali zaidi kwa Mheshimiwa Waziri ili atakapokuja hapa aweze kutupa ufafanuzi. Kwanza ukiangalia kitabu cha Waziri cha mwaka 2017/2018 kinasema kwamba Waziri aliomba bilioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu za *Bombardier; Q400*, tatu; pamoja na *CS300,* mbili; na ndege kubwa ya 787.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Mpango ambao tumewasilishiwa Machi mwaka huu na Waziri wa Fedha pia anasema kwamba amelipa bilioni 7.8 kwa ajili ya kutekeleza mkataba wa ununuzi wa ndege, lakini pia ameomba bilioni 495.6 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ndege mbili za *CS300* kwa malipo ya asilimia 30 na ndege kubwa ya 787 kwa malipo ya asilimia 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwaka jana amesema Waziri kwamba ameomba hizi fedha kwa ajili ya kufanya malipo ya ndege hizi, lakini mwaka huu huu tena ameomba tena karibu bilioni zile zile 500 anaenda kulipia tena ndege hizi hizi ambazo ziliombewa fedha wakati ule. Sasa namwomba Waziri atakapokuja hapa atufafanulie ni ndege zipi nyingine ambazo zinazoenda kulipiwa na kule mwanzo katika kitabu cha mwaka 2017/2018 hakueleza kwamba analipia asilimia 30 ya hizi ndege mbili *CS300. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye Waziri wa Fedha amesema kwamba ameomba fedha kwa ajili ya kulipia tena ndege ya *Bombardier Q400,* sasa naomba Waziri kujua haya maelezo ambayo ameyatoa Waziri wa Fedha je, kuna *Q400* nyingine ya nne ama ni zile zile tatu za nyuma ambazo zilinunuliwa hapo kabla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza mwaka juzi na mwaka jana tulitoa ushauri hapa kwa Waziri kwamba hakuna anayekataa shirika la ndege kuanzishwa ili lilete tija katika Taifa letu, lakini tulisema kwamba biashara ya ndege ni biashara ya ushindani na tunahitaji wataalam wa biashara za ndege wapewe shirika hili ili waweze kulianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa haraka haraka limeanzishwa shirika lakini hadi hivi leo Kamati hapa imesema kwamba shirika hili limeshindwa kuungwa katika hii Taasisi ya Mashirika ya Ndege ya *IATA* ili kuweza kujiendesha shirika hili na badala yake tunatafuta kampuni nyingine ili ifanye kazi hii kwa niaba yetu ambayo ina uwezo wa kufanya kazi na *IATA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii inaonesha wazi kwamba yale tuliyokuwa tunayasema ndiyo ambayo yanayojitokeza sasa hivi. Ukiangalia ripoti hii ya *CAG. CAG* anasema kwamba ununuzi wa ndege umekiuka taratibu za manunuzi. Hatusemi hivi kwamba tunaipinga Serikali, sio kwa sababu ya kuipinga Serikali lakini tunaisaidia Serikali ifanye kazi zake na iwe ni tija kwa wananchi; lakini leo shirika hili linakwenda kuwa mzigo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano mmoja, kabla shirika hili halijarejeshwa hapa kuwa marehemu na *South African Airways* yalijitokeza mashirika matatu kulifufua hili shirika. Shirika la kwanza ni *British Airways* pamoja na *Emirates* na la tatu ni hili *South Africa. British Airways* walikuwa na lengo la kuifanya *Air* Tanzania iwe ndiyo kama *career* yao kwa *East Africa* pamoja na *Africa* kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *Emirate* walitoa *offer* kwa *Air Tanzania* kwamba wakipewa hili shirika wakilitumia kwa ajili ya *East Africa* hii liweze kufanya kazi kupitia *Emirate* kwa pamoja, pamoja na shirika la *Emirate* wangefanya matengenezo ya viwanja vyote vya ndege ambavyo leo tunavipigia kelele hapa ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana kutokana na kwamba hatuna viongozi ambao wanauzalendo na nchi hii wakatanguliza maslahi yao binafsi na *British Airways* na *Emirates* wakajiondoa na shirika likachukuliwa na *South African Airways* likarudi hapa shirika likawa marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *Emirates* kukosana na *Air* Tanzania walikwenda kuingia makubaliano na shirika la Srilanka na wakafanya nao kazi kwa muda mrefu na wakawajengea kiwanja cha ndege cha kimataifa chenye *shape* kama ile ambayo imetengenezwa *Dubai International Airport*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tunapozungumza utaratibu kwa sababu jambo lolote bila ya sera na utaratibu maalum Serikali haiwezi kufanya biashara ya ndege. Leo tuangalie Shirika la *Air* Rwanda, Serikali hiyo ilijitwika kifua kulichukua shirika wakawa wanaliendesha. Sasa hivi wanatafuta wawekezaji waliendeshe kwa sababu Serikali imeshaona kwamba ina mzigo mkubwa wa kulihudumia shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri tunayasema haya kwa maslahi ya Taifa la Tanzania. Tuliposema kwamba waje wataalam, mtaalam unapompa kazi anaangalia mpaka *liability* ya taasisi husika.

Kwani kulikuwa na ulazima lazima tuseme hii inaitwa *ATCL*. Leo hapa tukiangalia *Emirates* kuna mashirika matatu sasa hivi, kuna *Emirates* yenyewe, kuna *Fly Dubai* kuna *Etihad.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote yanafanya kazi na mashirika yote matatu haya yanakuja hapa Tanzania, yanafanya kazi zake yote matatu kila siku na yanafanya kazi kwa mafanikio makubwa. Sasa na sisi ilikuwa lazima tukae tutafakari ili kumsaidia Rais wa nchi hii aweze kufikia yale malengo ambayo anayakusudia, lakini naona sasa kwamba upande wa Mawaziri wanamwangusha Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ikiwa Rais alikuwa na nia ambayo ya kuonesha kabisa kunyanyua uchumi kupitia shirika la ndege lakini leo badala ya kufuata zile taratibu za kuonyesha kwamba shirika hili lingeweza kuleta tija na maslahi kwa Watanzania matokeo yake linakwenda kuwa mzigo. Hapa leo ukiangalia kwenye kitabu hiki hapa cha Waziri ambacho amekitoa tulisema hapa kwamba unapochukua *career* tofauti za ndege lazima na *base* ya matengenezo zinakuwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo Waziri kakubali maneno yangu na ndiyo maana kaingia mkataba na *Ethiopian Airline* kuzifanyia *service* ndege hizi za *Air Tanzania*. Tuliyasema haya katika Bajeti ambayo ilipita kuonesha kwamba lazima kutakuwa na *cost* za kuendesha shirika, sasa leo kwa sababu hatuwezi kujiendesha wenyewe ilibidi tutafute sasa shirika lingine liweze kutusaidia katika kufanyia *maintenance* ndege hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Waziri hii nchi ni yetu sote, tukiharibikiwa tumeharibikiwa sote. Sasa wasianze kulitoboa jahazi halafu tuzame sote. Ikiwa kuna uwezekano wa kuweka kalavati, tuweke hilo kalavati ili tusizame tufike safari yetu; lakini haiwezekani kwenda katika namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ukija katika suala la reli ya kati. Mheshimiwa Rais alimwomba aliyekuwa

Rais wa *South Africa,* Jacob Zuma kwamba atusaidie kujenga reli ya kati, lakini haikuwezekana. Hata hivyo, tukapata bahati nyingine akaja Rais wa Uturuki na Rais akamweleza nia ya kujenga reli ya kati kwa *standard gauge* na Rais wa Uturuki alikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapata mkanganyiko, tunasema Rais alivyomaliza kuzungumza na Rais wa Uturuki anasema tumefanikiwa tumezungumza na Serikali ya Uturuki, tumeweza kupata reli ya kati ya *standard gauge,* lakini huku tunaambiwa kwamba fedha ambazo zinatumika kujenga hii reli ni fedha za ndani. *Sasa part* yao hao Waturuki ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba akija hapa Waziri atueleze inakuwaje kwa sababu inawezekana pengine watu wakawa hawana uelewa wa kutosha halafu taarifa zikatoka vingine. Hebu leo waje watueleze hapa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Unga mkono hoja. Unga mkono.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ajibu maswali.

**MWENYEKITI:** Haya. Tunaendelea na Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Lucy Magereli ajiandae dakika kumi, kumi.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia. Kwanza nieleze masikitiko yangu kwenye Wizara hii juu ya uamuzi wa Serikali wa kuvunja nyumba za wananchi wa Ubungo, Kimara na maeneo mengine ya Dar es Salaam hasa baada ya Mahakama kutoa amri ya kuzuia ubomoji ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubomoaji umefanyika kinyume cha taratibu na namwomba Waziri kwa kuwa nyumba za wananchi wa Dar es Salaam zimevunjwa na tayari Benki ya Dunia imesimamisha msaada kwa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa hizo barabara, kwa kuwa ujenzi umekiuka taratibu, kanuni na haki za binadamu zimevunjwa, nataka Serikali iwafidie wananchi wa Ubungo ambao nyumba zao zimevunjwa bila kufanya tathmini ya kile kilichovunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi uliopo ni kwamba sasa Serikali italazimika kulipa fidia ili mradi uendelee, lakini fidia hii ilinalipwaje kwa nyumba ambazo tayari zimevunjwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie utaratibu mzuri kabisa wa wananchi wa Ubungo kufidiwa nyumba zao zilizovunjwa. Nyumba hizi zimejengwa katika mazingira magumu, watu hao wengine walikuwa watumishi wa umma, wamejitolea katika Taifa hili wamelipwa kiinua mgongo chao, wamejenga mabanda yao, nyumba zimevunjwa kinyume na sheria ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza tumeona barabara inakatwa kutoka mita 121.5 katikati ya barabara. Wataalam wanasema mita 121 ni uwanja wa mpira. Kwa hiyo, hivyo ni viwanja vya mpira viwili ndiyo inajengwa barabara ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni juu ya barabara ambazo zimetajwa katika kitabu cha Waziri, katika ukurasa wa 203 imetajwa barabara ya Nzega, Tuge hadi Tabora. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, barabara hii ilishakamika miaka miwili iliyopita leo inatengewa fedha na Wabunge hapa wapo hapa ambao wana barabara zao hazijajengwa. Kule Rufiji barabara haijajengwa tokea wakati wa Bibi Titi Mohamed, Mbunge anasimama hapa analia asubuhi, anaomba ijengwe barabara, lakini barabara inapelekwa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *watu wanasema inawezekana inapelekwa Tabora kwa sababu kuna*

*upendeleo maalum katika mikoa hiyo hiyo ya Kanda ya Ziwa kupeleka vitu vyote vya maendeleo. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Kubenea. Naomba twende vizuri na mchango wako. Hayo maneno uliyotumia, nakuomba kabisa, uyafute, naomba uyafute.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nimeyafuta.

**MWENYEKITI:** Maneno yapi umefuta.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekeze.

**MWENYEKITI:** Pesa hiyo inaenda kujenga huko kwa sababu ni...

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba fedha inaenda kujenga eneo la Kanda ya Ziwa na kwamba ni upendeleo, nimeyafuta. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL.* Wabunge wamezungumza na watu wengi wamezungumza kwenye nchi hii juu ya mchakato mzima wa ubinafsishaji wa Shirika la Ndege la Taifa *(ATCL)*. Mchakato ulitawaliwa na viriba, ulitawaliwa na udanganyifu na haukufuata taratibu zozote za ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shirika likabinafsishwa lakini baadaye Serikali ikalazimika kununua hisa zake ilizouza katika Shirika la Ndege la Afrika Kusini, Shirika likarudi Tanzania,

Serikali ikamiliki hisa za *ATCL,* leo tunafufua shirika ni kazi nzuri nawapongeza kwa kufufua shirika mmefanya kazi nzuri. Sisi wazalendo wa nchi hii tulikuwa tunalililia shirika hili liwe shirika letu la umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wameingiza nchi hii hasara kubwa kwenye *ATCL*. Tarehe 9 Oktoba, 2007, *ATC* ilisaini mkataba wa ukodishaji wa ndege aina ya *Air bus* na Kampuni ya *Wallis Trading Company*. Taarifa zilizopo ukaguzi wa ndani haukufanyika kujua ubora wa ndege wala Shirika la Anga la Tanzania halikushirikishwa. Matokeo yake baada ya muda mfupi ndege ile ikafa na ikawa *ATC* inalipa kati ya dola 3,700 kwa kila mwezi hadi kufikia deni la shilingi bilioni mia mbili na milioni mia tano tisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege hii ambayo ilikodishwa na Serikali ya Tanzania ilifanya kazi muda mfupi sana hapa nchini. Hadi mwezi Juni mwaka 2009 ndege hii ilipelekwa matengenezo nje ya nchi na baadaye ikapelekwa Ufaransa. Makadirio ya matengenezo ya ndege yalifikia dola za Marekani milioni 593.6 na deni liliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 3.039.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa, hebu subiri kidogo Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kaka yangu Kubenea *sometime* huwa anaweza akawa na hoja nzuri sana; lakini shida ni namna ya kuijenga hoja. Hajui namna ya kuijenga hoja, lakini pia nataka niseme kwamba tunachokizungumzia ni jambo la leo sio habari ya mwaka arobaini na saba.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Wewe acha shule, acha kufundisha watu.

**MWENYEKITI:** Polepole Waheshimiwa Wabunge, hapana hapana tuheshimiane tu. Mheshimiwa Kubenea taarifa hiyo.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajui analolifanya kwa hiyo nimemsamehe tu. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza historia na bila kuzungumza historia katika nchi hii, hatuwezi kujenga nchi, hakuna nchi isiyo na historia duniani, tunazungumzia *ATC* jinsi ilivyokufa, jinsi ilivyouawa na jinsi inavyofufuliwa. Kama hatujaangalia tulikotoka, tulikojikwaa, tutakwama mbele. Shirika hili huyo Mbunge haelewi kwamba tayari *ATC* imefunguliwa kesi nyingine London. Waziri wa Katiba na Sheria anajua, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anajua, Balozi Migiro anajua, viongozi wa Serikali wanajua kwamba tuna kesi mpya imefunguliwa London mwaka huu tunadaiwa zaidi ya dola milioni 38 zaidi ya bilioni 80, anazungumza nini huyu? Anazungumza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza *ATC* na tayari Serikali ya Tanzania imelipa *pound* elfu15 kwa malipo ya awali ya Mawakili, London. Tunazungumza *ATC* ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati huo alishauri mkataba usifungwe lakini ulisainiwa mkataba wa hii ndege na Kampuni ya *Wallis* bila kufuata taratibu. Leo watu wameenda *London* wamefungua kesi wanatudai kuna hatari ya *Bombardier* zetu zikakamatwa tena ndiyo kitu tunachokizungumza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza hatari ya ndege zinazonunuliwa na fedha za walipa kodi kukamatwa tena, kukamatwa kama ilivyokamatwa ile *Q400* kule Canada. Tunazungumza anakwambia tujenge hoja, hizo ndiyo hoja. Tuna nia ya kujenga Taifa letu, tuna nia ya kujenga *ATC* mpya, lakini hatuwezi kujenga *ATC* mpya bila kusaidia shirika hili likaondokana na huu mzigo wa madeni ambao linao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika hili linadaiwa zaidi ya bilioni 100 kwa mujibu wa taarifa za Serikali yenyewe na Serikali imebeba huo mzigo wa madeni, ni vizuri, ni jambo zuri. Hata hivyo, ni lazima tuhakikishe *ATC* inakwenda vizuri,

watendaji waliopo *ATC* wanapewa uwezo, wanapewa uhuru wa kuendesha ndege zao. Ni bahati wamepata Mkurugenzi mpya ambaye alikuwa *Boss* kule katika Mashirika ya Ndege ya Afrika, amerudi hapa amekuja kuongoza *ATC* alikuwa *Engineer* wa *ATC* kabla *ATC* haijabinafsishwa, amerudi kwa uzalendo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ina utaratibu mbaya wa kutumia watu wanaotoka nje, lazima waambiwe wasifanye mchezo huo. Wamemchukua Tido Mhando *London BBC* wakamleta *TBC*, amekaa mwaka mmoja wamemfukuza. Wamechukua mtaalam kutoka *South Africa* amekuja *TIC* amekuja hapa wamemu-*harass* ameondoka. Amekuja mtu Profesa Waziri wangu...

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo Mheshimiwa, subiri kidogo tu. Muda unalindwa, mimi ndiyo niko kwenye kiti hapa, *please!* Taarifa.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda tu kumpa taarifa Mheshimiwa Kubenea kwamba Tido Muhando hakukaa mwaka mmoja katika Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* bali alikaa miaka minne.

**MWENYEKITI:** Ahsante, taarifa hiyo Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tido Muhando aliajiriwa *BBC* alikuwa Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili labda Mheshimiwa Amina alikuwa hajui wakati huo kwamba Tido alikuwa Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili. Amerudi hapa Tanzania akawa Mkuu wa *TBC,* ameondolewa bila mkataba wake kuelezwa. Mtu ambaye alikuja *TIC* ameondoka, Profesa. Kwa hiyo, ninachozungumza ni kwamba wataalam wetu wanaoletwa Tanzania ambao walikuwa wanafanya kazi nje ya nchi, wameacha kazi yenye mishahara mkubwa, wenye marupurupu mazuri, yenye usalama yakinifu,

wakarudi Tanzania kuja kufanya kazi, ni lazima walindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomuomba mtu aje kufanya kazi huwezi kumleta mtu halafu ukawa unambabaisha babaisha. Kwa hiyo, ili *ATCL* iendelee ni lazima wafanyakazi wapewe vipaumbele na Menejimenti iachiwe ifanye kazi yake bila kuingiliwa na wanasiasa. Ndege zinachelewa kwa sababu ya Wabunge sisi baadhi yetu tunachelewa *Airport*. Kwa hiyo, *route* ya ndege ya kutoka Mwanza ...(*Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea Mheshimiwa Lucy Magereli, dakika 10.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya kuchangia ndani ya Bunge hili Tukufu katika hii hoja ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Ningetaka nianze na kuendelea hapo hapo alipoishia Mheshimiwa Kubenea kuhusu *ATCL* kwa sababu hili ni suala muhimu sana ambalo lazima tuendelee kukumbushana, lazima tuambiane ukweli, lazima tuwe wakweli juu ya nini tunataka kuhusu kuifufua *ATCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona ni kwamba nadhani wataalam wa Tanzania hawajapewa fursa kabisa na wala nadhani hawakushirikishwa wakati ulipokuja mjadala wa kutaka kuifufua *ATCL*. Naamini wangeshirikishwa maamuzi haya yaliyofanywa leo yasingefanywa. Hivi jamani ni nani aliyemshauri Mheshimiwa Rais kwamba anunue ndege? Kulikuwa kuna uwezekano mkubwa kabisa wa kuifufua *ATCL* kwa kutumia ndege za kukodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hatukuhitaji ndege kubwa Tanzania kwa wakati huu kwa sasa. Hivi

tunatakaje kwenda kushindana na mashirika makubwa ya kimataifa ya ndege ambayo yameshajiimarisha kwa muda mrefu, ambayo pamoja na yenyewe yanafanya biashara ya hasara. Badala ya kufikiri ya kwamba tunahitaji kwanza kuimarisha mtandao wa ndani wa ndege kabla ya kuanza kushindana kimataifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo, hizi taarifa zinaanza kunisumbua haya, taarifa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa mzungumzaji amesema Watanzania hawakuhitaji ndege, sisi Wabunge kipindi chote cha mwaka 2011 mpaka 2015 tulikuwa tunalalamika nchi yetu haina ndege na tulikuwa tunasema tunashindwa hata na Rwanda. Rwanda leo wamepata ndege sisi Tanzania hatuna ndege. Kwa hiyo, tulikuwa tunaiomba Serikali kila siku wakiwepo Wabunge wa Upinzani tununue ndege, kwa hiyo Watanzania walitaka ndege kupitia kwa sisi Wabunge wao ambao ni wawakilishi wa Watanzania.

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na mchango wangu kwa kusema suala siyo kuhitaji ndege. Ndege gani, kwa utaratibu upi, kwa malengo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri na ningeomba nisikilizwe kwa sababu hivi tunavyozungumza yaani hata viwanja vya ndani ya nchi vya ndege havifai kwa matumizi yetu. Mtalii leo akitua pale JK Nyerere anataka kwenda Ruaha, anataka kwenda Rubondo, anataka kwenda kisiwani Lake Victoria anapata tabu ya kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunadhani ukweli halisi ni kwamba Tanzania inao uwezo wa kununua ndege kubwa wakati *network* ya ndani bado haijakuwa imara? Ambacho

kingefanywa sahihi ni kwamba tulihitaji kuimarisha *network* yetu ya ndani kwanza halafu baadaye tutapiga hatua hiyo kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize, hivi ni nani aliyemshauri Mheshimiwa Rais kwamba tununue ndege kutoka makampuni tofauti tofauti? Tunaongelea habari ya *Bombardier,* tunaongelea habari ya *Boeing,* tunaongelea habari ya *Air bus*. Haya yote ni mzigo kwa nchi hii. Ndege za *Bombardier* zitahitaji kuwa na *service centre* yake yenyewe, ndege za *Boeing* tutahitaji kuwa na *service centre*, ndege ya *Air bus* itahitaji *service centre*. Unatengeneza *service centre* Tanzania kwa ndege moja ya *Air bus*? Unatengeneza *service centre* kwa ndege moja, mbili za *Boeing*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tukubaliane kwamba kesho na keshokutwa Bunge hili litakaa tena tupeane taarifa, tulaumiane kwamba tumechezea kiasi kikubwa sana cha pesa za walipa kodi katika kuifufua *ATCL* ambayo mwisho wa siku imegeuka kuwa msiba kwa Taifa. Nawaambieni huu ndiyo ukweli, *ATCL* miaka mitano ijayo tutakaa ndani ya Bunge hili tutajadili jinsi ambavyo imekuwa tatizo kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwamba hili suala la *ATCL* warudi kwenye mikono ya wataalam, watafute menejimenti nzuri, washauriane, waone namna ambavyo *ATCL* itafufuliwa. Hizo ndege mnazozisubiria huko kwa sababu hebu kwa mfano tumetumia bilioni 130 ku-*sort* ile kesi ya Mahakama ya *Bombardier* zile bilioni 130 ni ndege nne zingine za *Bombardier*. Jamani mnataka mseme hata hapo mlifanya *rational decision*? Hizo pesa bilioni 130 ziliidhinishwa na Bunge gani? Nani aliyeidhinisha pesa zika-*sort* hiyo tatizo la Mahakama Canada? Hasara ambayo *ATCL* itatutengenezea ni kubwa na itaenda ku-*bust*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie kwenye suala la Daraja la Kigamboni. Naomba nishukuru na nipongeze mchango wa Mheshimiwa Zainabu Mndolwa. Daraja la Kigamboni ni mzigo kwa Watanzania wa

Kigamboni. Sisi tulikuwa tunatumia vivuko vya Magogoni, MV Kigamboni na *Alhamdullaah* wametuongezea kivuko kingine cha *MV* Kazi. Vile vivuko vyote tunalipia, awali nyuma kabla ya daraja tukaambiwa daraja litakuja kuwa suluhisho na kutupunguzia gharama kama *optional way* ya kupita kama huhitaji kulipia au huna huo uwezo wa kulipia. Lile daraja limefanywa la kulipia, tena basi tulifikiri ni kwa muda fulani *specific* lakini *it's a life time business*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, kwa hili kwa kweli wamewadanganya na wamewadhulumu wananchi wa Kigamboni. Walikuwa na sehemu yao ya kulipia kwenye ule mkataba na *NSSF*, Serikali wameingia mitini, wamegoma kulipia sehemu yao ya mkataba, badala yake wamewaangushia wananchi wa Kigamboni kulipia zile gharama na hata hawaja-*specify* kwamba ni kwa muda gani. Maana yake sasa sisi tumeshakuwa *commodities of trade.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa Kigamboni ukitaka kuvuka kwenye daraja unalipa, kwenye kivuko unalipa na basi si gharama kidogo ni gharama kubwa sana. Gari ya daladala ambayo inatoka Mnazi Mmoja kuja Kigamboni kuvuka pale darajani inalipia Sh.7,500 kila inapopita.

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeh!

**MHE. LUCY S. MAGERELI** Sasa fikiria kweli wananchi wa Kigamboni kama tulifikiri tukipata daraja basi tutapata na namna rahisi ambayo tutakuwa tunavuka kutoka Kigamboni kuja Dar es Salaam badala yake mpaka leo tuna…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo Mheshimiwa. Taarifa!

**MHE. MAULIDI S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri namheshimu sana Mzungumzaji dada yangu

mtu makini sana, lakini taarifa ninayompa kwamba miongoni mwetu humu tunasema Serikali isifanye miradi wenyewe, ifanye *PPP.* Sasa hayo yanayotokea ndiyo malipo na ndiyo stahili ya *PPP,* kwa hiyo asishangae. Kama tunavyosema tusitoe pesa zetu tutumie *PPP* basi tuwe tayari kuchangia gharama hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa taarifa hiyo.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ningeweze kuafikiana nalo kama tungekuwa tuna mbadala mwingine, lakini sisi tunalipa kote kwenye kivuko unalipa na kwenye daraja unalipa. Kwa hiyo sikubaliani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja nyingine ya barabara ya Kibada - Mwasonga – Tundwi – Kimbiji. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake ametaja barabara hii ambayo tangu bajeti ya mwaka wa 2016/2017, 2017/2018 imetajwa na imetengewa fedha. Ile barabara ni muhimu sana kwa eneo hilo la Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara inapita katika kata nne ambazo bahati nzuri tunashukuru ni katika kata ambazo zina maeneo mengi ya uwekezaji. Ile barabara hata leo hii ukipita hali yake ni mbaya mno na tumekuwa tunaitengea fedha inatajwa, inatengwa, inatajwa lakini haipewi fedha na wala haijawahi kufanyiwa kulingana ambavyo taarifa zimekuwa zimetolewa katika kitabu cha Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata taarifa zilizotolewa hapa kwenye kitabu ukurasa wa 34 sijaelewa kilichomaanishwa kwa sababu kwenye sehemu ya 21 inasema barabara ya Kibada – Mwasonga – Kimbiji kilometa 19 lakini sehemu ya 22 inasema barabara ya Kimbiji – Tundusongani kilometa 30.5 sijaelewa kwa sababu sidhani kama barabara hii inafika kilomita 49 *point something* nadhani kuna jambo hapa halikuwekwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ile barabara haipitiki hasa wakati wa mvua. Nimeona wanasema upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea, tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie hata itengenezwe kwa kiwango cha moram na ishindiliwe vizuri, iwekewe mitaro ya barabara kwa sababu yale malori ya *cement* yanapita kutoka Nyati *Cement* Kimbiji yanapata shida sana kupita kwenye ile njia na mara nyingi yanakwama na yakishakwama maisha yetu ya Watanzania wa eneo lile yanakuwa magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia mtandao wa barabara katika Manispaa ya Dodoma. Naamini tunakubaliana wote tuliokaa ndani ya nyumba hii kwamba uamuzi wa kuhamia Dodoma nadhani kuna *step* ilirukwa ya kuandaa miundombinu. Barabara za Dodoma sasa hivi mji huu asubuhi unasimama msongamano ni mkubwa sana na barabara ya Dodoma ni nyembamba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi barabara ya Dar es Salaam hii kwa maana ya kutokea maeneo ya Ilazo kuja Kisasa mpaka kufika eneo la Bunge asubuhi ni eneo lenye msongamano mkubwa sana. Nimeona orodha ya barabara zinatajwa hapa katika ukurasa wa 36 barabara ya Shabiby-Arusha-Dodoma *road-round about*, barabara ya Chimwaga-Chinyoya-Kikuyu, barabara ya Dar es Salaam-Nane nane na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, hizi barabara waziangalie kwa jicho la wepesi tena kwa kipaumbele kabisa *especially* haya malori makubwa yanayoingia mjini ile barabara ambayo ilikuwa imeandaliwa inayotokea Ihumwa basi ile barabara ijengwe kwa uharaka ili tupunguze magari makubwa ambayo yanaingia ndani ya Mji wa Dodoma na kusababisha msongamano mkubwa sana na ikitokea kwa mfano hapa Dodoma barabara moja tu ikapata hitilafu mji wote unasimama. Kwa hiyo, wanaweza kuona namna ambavyo haiko *networked* sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie hoja yangu kwa kusema naomba tuwe wakweli, naomba tunaposema tunaishauri Serikali tuseme ukweli, naomba tunapopewa ushauri na wataalam hasa katika maeneo haya ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Yako mambo mengi sana katika Wizara hii ambayo yamekuwa kama wimbo wa kawaida hivi upembuzi yakinifu, sijui uchambuzi wa kina yaani kuna ucheleweshwaji mwingi tunashindwa kusema ukweli kwamba bajeti yetu haikidhi haja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako, sikukusikia unaunga mkono hoja. Tunaendelea, narudi sasa kwenye dakika tano tano. Nitajitahidi kwa kadri nitakavyoweza naanza na Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pia naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi jioni hii ya leo ili na nitoe mawili, matatu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake na Watendaji wengine kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini bado naomba niendelee kumtia moyo sana Rais wetu nimefarijika sana kwa michango ambayo imeendelea kutoka kwa upande wa pili kwa sababu nimeona hakika msumari kwa kweli umeingia na ndiyo maana maneno ya kupinga kila kitu ambacho ni kizuri yameendelea kutoka ndani ya nyumba hii, hivyo naomba kuendelea kumtia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze mawili, matatu. Kwanza nipongeze sana kwenye mpango uliopo katika kitabu hiki hasa kwa upande wa Mkoa wangu wa Singida, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Nianze na upande wa Daraja la Sibiti pamoja na barabara aliyoitaja kutoka Mbulu kuja Haydom hadi Sibiti kwenda Maswa. Fedha

alizotenga kwa kweli ni ndogo sana sielewi hizo fedha ni za nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana barabara hiyo ya Sibiti pamoja na kwamba inaenda Mbulu, naomba itoke Sibiti ije Mkalama ije Nduguti ije hadi Iguguno iwe ya lami. Hatuwezi kujenga daraja zuri lenye kiwango kikubwa lakini barabara isiwe ya lami, naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Waziri ametaja daraja la Msingi, naomba sana daraja lile kuna madaraja mengine madogo madogo ambayo naamini *TARURA* itaenda kuyafanyia kazi, lakini naomba sana barabara ile ambayo imepita Kinampanda kushuka Msingi kwenda Gumanga imaliziwe iwe ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia barabara ya kutoka Singida Mjini kupita Sipuka hadi Ndago kwenda Kizaga. Ile barabara ni ya lami na ni ya ahadi ya Rais, naomba sana sijaona kama Mheshimiwa Waziri ameitaja, nashukuru kwa zile ambazo amezitaja, mimi nataja zile ambazo bado hajazitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa kipekee naomba Mheshimiwa Waziri apeleke salamu kwa Mheshimiwa Rais, barabara inayotoka Tanga inayopita Kondoa inakuja kwa Mtoro inakuja Simiyu hadi Singida barabara ile ni kwa ajili ya Bomba la Mafuta ambalo litakuja kuinua uchumi mkubwa sana kwa wananchi wa Singida. Napongeza sana na nashukuru lakini fedha walizotenga hazitutii moyo sana, naomba atakapokuja atutie moyo kwamba zitamalizika lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuwapongeza watu wa mawasiliano. Nawapongeza *TTCL* kuna mmoja alizungumza kwamba Watanzania sasa tujivunie shirika letu, ni kweli na naunga mkono. Naomba sana *TTCL* wapewe uwezo mkubwa wa kutandaza mtandao nchi nzima ili wananchi walioko vijijini waweze kupata mawasiliano ya kutosha, lakini naomba hasa kwenye maeneo ambayo ni

hatarishi kwa mfano Sekenke pale ukiwa unashuka ule mlima Sekenke hamna *network*, mtu akipata tatizo hawezi kuwasiliana. *TTCL* naamini wameshakuja vizuri wana-*perform* vizuri, wawezeshwe ili waweze kuweka mtandao nchi nzima wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBA* wamefanya kazi nzuri, naomba waongezewe bajeti ili waweze kukarabati na yale majengo ambayo yamechakaa sasa hivi. Kwa mfano ya hapa Dodoma wanayoishi Waheshimiwa Wabunge, yamechakaa waongezewe ili waweze kukarabati yale majengo. Wapeni nafasi waweze kujenga hapa Dodoma majengo ya Serikali kwa sababu majengo yao nikiyatazama ni yanadumu na ni imara, yanaishi kwa muda mrefu. Wawezeshwe ili waweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba sana kwenye upande wa barabara za vijijini kuna *TARURA, TANROAD* Mkoa na kuna Taifa. Mheshimiwa Waziri atakapokuja naomba aje atufafanulie vizuri barabara zipi hasa maana yake zile tunazozitaja, kwa mfano ukienda Singida kuna yale madaraja makubwa ambayo atasema hizo barabara ni za vijijini, lakini *TARURA* hataweza kwa sababu ya bajeti ndogo. Kwa hiyo, naomba sana watakapokuja hapa waje watufafanulie *TARURA*... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Richard Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwa sababu muda ni mchache sana nitakwenda haraka haraka. Kwanza naomba nimpongeze Waziri na Manaibu wake wote wawili na watendaji katika wizara kwa jinsi wanavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni tunashukuru Serikali kwa kujenga barabara ya Sumbawanga – Kizi- Kibaoni lakini kipande cha Kizi- Lyambalamfipa- Stalike ambacho ni kabla hujafika Hifadhi ya Taifa ya Wanyama ya Katavi kina kilometa 35.5, tunaomba Waziri atuambie ni lini ataiweka kwenye bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika barabara hiyo ambayo imeshajengwa na imekamilika ya Stalike – Mpanda bado kuna wananchi ambao bado wanadai fidia. Sasa tutaomba Waziri atuambie katika bajeti hii kiasi gani ataenda kuwalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru na kwenye kitabu nimeona barabara yetu ya kutoka Mpanda – Inyonga – Ipole – Sikonge – Tabora kilometa 346 na tayari wakandarasi wameanza *mobilization*. Sasa kwa sisi watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kuna fidia ya *utility facilities* yaani matenki ya kuhifadhi maji ambapo yapo mawili yanaenda kubomolewa, lakini kwa taarifa ambazo sio rasmi, kuna shilingi milioni 162 tu ambazo zipo katika mkataba ambazo haziendani na gharama halisi ya haya matenki ambayo tunatakiwa kufidiwa. Kwa hiyo, tutaomba Serikali iangalie uhalisia wa gharama za haya matenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la reli, treni yetu ya kutoka Tabora mpaka Mpanda, njia yake kwa kipindi hiki cha masika inasumbua sana, hapa siku tatu zilizopita wananchi wamelala siku mbili kati ya Kaliua na kilometa 60 kutokana na mvua na kokoto kuondoka. Kwa hiyo, tunaomba katika bajeti hii na ukarabati ufanyike kwa umakini na pia mabehewa yaweze kuongezwa kutokana na hasa kipindi cha kiangazi abiria wanakuwa ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wananchi pia wapo tayari kuachia maeneo ambayo yanamilikiwa na shirika letu la reli lakini upimaji wa ardhi mpya ulichelewa kwa hiyo tutaomba hisani ya Serikali watuvumilie kidogo wakati wananchi wanajenga maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *TAZARA,* kiuongozi tunaona Serikali ilete sheria iweze kuboreshwa ili angalau tuwe na kupeana miaka mitatu mitatu katika kuongoza shirika hili na lifanye kiufanisi zaidi na kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TTCL, TTCL* tumebadilisha sheria mwaka jana. Sasa niombe Wizara na Kampuni ya *TTCL* wakimbie na wasitembee. Walianzisha *code* yao 0732 lakini idadi ya wateja wao imekwishashuka na sidhani kama kuna watu wengi sana wanaotumia simu za mkononi za *TTCL.* Sasa kwa kuwa mkongo wa Taifa upo chini yao, wakimbie; amekuja juzi *Halotel* lakini ana wateja wengi, kwa nini *TTCL* bado anatambaa. Kwa hiyo, Serikali na uongozi mzima wa *TTCL* waje watueleze kwamba watafanya nini ili shirika liweze kufanya kazi kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TCRA,* Halmashauri zetu nchi nzima kuna minara ambayo kampuni za simu zina-*operate* na sasa hivi wameweka kampuni moja na haya makampuni ya simu yanapanga, sasa tunatakiwa tupate *service levy* kutokana na mapato ambayo wanaingiza katika kila eneo. Kwa hiyo, tuombe kama inashindikana basi *service levy* inayotoka *TCRA* iingie na iwe *ring fenced* labda kwenye Wizara ya Afya kwa ajili ya kusaidia vifo vya mama na mtoto kama inashindikana kila Halmashauri kuweza kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vivuko, tunaona kwamba katika barabara nyingi hakuna hizi *underground crossing.* Kwa mfano tu ukichukua eneo la *NARCO* ilitakiwa kuwe na kivuko cha chini ili wanyama waweze kupitishwa, sasa kwa nini *TANROAD* katika ku-*design* barabara maeneo mengine wasiweke vivuko vya kupita chini ili tuondoe ajali ambazo wananchi wetu na mifugo wanagongwa na hii itasaidia usalama kati ya wanyama na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni kuhusu *ATCL,* tunaipongeza Serikali kwa hatua kubwa, nimeona mchangiaji mmoja alisema kwamba kuwe na ndege za kampuni tofauti italeta changamoto kwenye suala la kuwa na hizi anga...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya, Mheshimiwa Dkt. Kawambwa na Mheshimiwa Profesa Maghembe wajiandae

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie katika Wizara hii ambayo nayo ni mhimili wa uchumi katika nchi yoyote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kujenga miundombinu ya reli lakini kutaka kuunganisha mikoa yote kwa njia ya barabara za lami. Dhamira hii ya Serikali ya kuunganisha mikoa kwa kiwango cha lami imekuwa ya siku nyingi lakini barabara ambazo hata Mheshimiwa Waziri ameionesha katika kitabu chake, barabara ya kutoka Makongolosi hadi Mkiwa, kuna kilometa 413, katika Jimbo ambalo mimi ndio mwakilishi wake ziko kilometa 219.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inajengwa kutoka Mbeya, Mbeya – Lwanjilo - Chunya, sasa wanajenga Chunya hadi Makongolosi katikati pale kilometa 43. Upande wa Singida barabara hii sijui kuna makosa gani ambayo watu wa Singida wamefanya hadi hii leo, mwaka jana katika kitabu cha Waziri alionesha dhamira kwamba barabara hii inajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati Naibu Waziri aliyekuwepo yeye mwenyewe Waziri amefika Itigi kuzungumza na wananchi kwamba barabara hii itajengwa na tukawaaminisha wananchi barabara hii sasa inajengwa. Ikatengwa pesa, ikatangazwa barabara na mkandarasi akapatikana. Hata hivyo, baada ya muda sijui kilizuka kitu

gani barabara hii nayo mwaka huu imewekwa katika mpango vilevile, mkandarasi alipatikana *Sinohydro* lakini sasa sijui wamemwondoa sijui wamemfanyaje, tunapata taarifa kwamba watatangaza lakini sio rasmi, hizi ni redio mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mwenyewe yupo hapa hebu atuambie na awaambie wapiga kura waaminifu kwa chama hiki ambacho Serikali yake na yeye ndio anatoka wamenichagua mimi kwa ajili ya kuhakikisha barabara hii sasa inajengwa. Atawaambiaje wananchi wa Itigi, mwaka huu tunaanza kujenga barabara au tutabaki na zile *story* za miaka nenda, miaka rudi toka enzi ya Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ina kilometa mia nne na kumi na, ni barabara pekee inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Singida, hakuna barabara mbadala na ukitoka Singida kwenda Mbeya lazima uje tena Dodoma – Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi Profesa Mbarawa yeye ni mwaminifu, ni mtu kweli; hebu sasa awaoneshe watu wa Itigi ukweli wake kwamba barabara hii mwaka huu wanaijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,nifurahie na niseme kwamba Serikali hii imeonesha usikivu kwa kuonesha kuunganisha Mkoa wa Singida na mikoa mingine kupitia barabara hii ambayo ameitaja katika kurasa zake wakati anazungumza katika ukurasa huo wa 147 amezungumzia barabara ya Handeni – Kiblashi – Kibaya, ni kilometa 460 ukitokea Singida mpaka pale Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali kweli imedhamiria kuijenga barabara ile kwa kiwango cha lami ina maana inaungana na mpango ule wa *East Africa* wa Serikali ya Uganda kupitisha bomba lile katika ukanda huu wa kwetu. Kwa hiyo, wananchi wanaotoka na mizigo yao katika Bandari ya Tanga na bandari ambayo tunaamini

Wizara hii inahusika itakuwa ni miongoni mwa bandari ambazo zitaihudumia sana nchi hii kuisaidia mzigo uliopo katika bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara hii ikijengwa itasadia mizigo ambayo inakwenda nchi jirani pamoja na nchi ya Kongo, watu hawatapita tena Dodoma na hapa makao makuu patapunguziwa mzigo, wajasiliamali hizi *by pass* tunazozijenga za mji zitapunguziwa mzigo, watu watatoka Bandari ya Tanga, watapita Handeni pale moja kwa moja wanatokea Singida, tayari tunaboresha uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la mawasiliano, baadhi ya maeneo ya Jimbo langu yana shida ya mawasiliano ya simu. Maeneo ya Mbugani, Kintanula, Gulungu nilishaandika barua, lakini na Wizara ilishatambua maeneo ya Lulanga na Itagata kuwa yana shida hii ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara hii sasa basi waweke mkazo katika suala hili ili wananchi ambao nao ni wa nchi hii wanufaike na rasilimali za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niisemee Serikali niipongeze kwenye suala la kuimarisha na kuhakikisha *TTCL* inasimama imara, lakini kuna tatizo ambalo *TTCL* wanalo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Profesa Jumanne Maghembe na Mheshimiwa Oliver Semuguruka wajiandae.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Nitangulie kwa kuunga mkono hoja na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na namshukuru Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wa wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 81 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri umetupa faraja sana sisi watu wa Bagamoyo, lakini tuseme kwa Taifa zima la Tanzania kwamba sasa majadiliano yanafikia ukomo. Mwezi Juni mwaka huu mkataba utasainiwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari kubwa ya Bagamoyo. Hii ni bandari ya ukombozi kwa dhana *(vision)* ya China *Merchant* na Serikali ya Oman kwamba hili ndilo lango kuu la uingiaji katika nchi za Afrika Mashariki, ni ukombozi kwa ajili ya uchumi wetu na 2025 bila shaka tutaweza kufika katika hali nzuri zaidi tukiwa na bandari hii kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani majadiliano yamechukua muda mrefu, sasa ni miaka sita na kwa maana hiyo naiomba Serikali yangu ijitahidi sasa katika utekelezaji wa mradi huu kwa sababu miaka sita ni kipindi kirefu. Kipindi hicho sisi tulikuwa tunafanya majadiliano lakini China *Merchant* wamejenga bandari Djibouti, Tin Can Island, Nigeria; Abidjan, Ivory Coast; Colombo Sri Lanka kwa hiyo, kipindi hiki tumepitwa na mambo mengi sana. Nadhani sasa niiombe Serikali yangu kufanya haraka sana katika kuhakikisha kwamba utekelezaji unaenda kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili utekelezaji huu sasa, mwekezaji aweze kuanza kazi, wananchi wangu wale 687 ambao hawajalipwa fidia walipwe fidia. Fidia ya jumla ambayo ilikuwa bilioni 57 na ikalipwa 45, ile tofauti nayo sasa ilipwe ili ardhi hii iwe *free* mwekezaji aweze mara moja kuanza kuweka miundombinu ya bandari katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kumaliza tatizo hilo litakuwa jambo zuri sana, lakini wananchi hawa kilio chao

kikubwa zaidi ni wapi wanaenda kuishi. Wananchi hawa ambao wanapisha bandari waliahidiwa na Serikali. Naomba niweke mezani barua hii ya *EPZ* ambayo iliwaahidi wananchi hawa kupewa sehemu ya kuweza kwenda kujenga makazi yao na eneo lilikuwa limeshatengwa na hivi sasa mpango huo upo kwenye mtihani haieleweki kama watapewa makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni kaya 460, Kijiji kizima cha Pande kinaondoka kwa ajili ya mradi huu; kaya 460, wananchi 1,670, tunapowaambia tu ondokeni nendeni mkaishi mahali popote wataenda kuishi wapi, kuna wazee, wajawazito, walemavu na watoto wadogo; wapi wanaenda shule yao na zahanati ipo pale, hawajui mahali pa kwenda. Wakitaka kwenda Zinga, Zinga ipo kwenye mpango wa *EPZ* ambao nao wanatakiwa waondoke kuna kaya 2,269, wakisema waende Kondo nayo inaondoka, kuna kaya 418, wakisema waende Mlingotini, nayo inaondoka kuna kaya 694 yaani hawana sehemu ya kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taratibu nzuri za nchi yetu ni kuhakikisha kwamba faida hii ya maendeleo ya Tanzania, basi wananchi hawa wanahama wanaenda mahali ambapo wataanza kuishi vizuri, vinginevyo tutatengeneza ombaomba, watu ambao hawana mahali pa kuishi. Kati yao wengi wamepata fidia ambayo haitawawezesha kununua ardhi wala kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila mpango wa *resettlement,* haitawezekana wananchi hawa wakaweza kuishi katika maisha ambayo yatakuwa ya heshima bila kutengeneza ombaomba katika mradi huu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisisitiza sana, hili wananchi wangu wanalia sana, lisipoweza kutokea maana yake tutakwenda kuwahamisha wananchi pale kwa mitutu ya bunduki na sidhani kama Mheshimiwa Rais wetu jambo hili anapenda kulifanya. Naomba sana Mheshimiwa Waziri alisimamie ili ahakikishe linafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 129 kuna habari njema ya ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Saadan – Pangani mpaka Tanga, hii ni habari njema ni ahadi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya miaka mingi. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuweka hili, lakini... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Oliver Semguruka na Mheshimiwa Flatei Massay wajiandae.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie katika hoja hii ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Muda wa dakika tano ni mdogo sana, lakini nataka niseme na kuipongeza sana Serikali kwamba katika sekta hii tumetoka mbali sana, tulikuwa tukisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza tunapitia Nairobi, safari ya siku moja tunakwenda siku mbili. *(Mkakofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeanza kujenga reli, tunaboresha Shirika la Ndege la Tanzania na tunaboresha *communication* nchi nzima, tusikate tamaa, pale tunapopata matatizo madogo madogo kwani hizi ndio changamoto za maendeleo na tuwe tayari kupambana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu mwezi Aprili, mwaka 2015 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akiwa Waziri wa Ujenzi alitutembelea kukagua barabara inayojengwa kwa lami kutoka Mwanga kwenda Usangi mpaka Uchamangofi. Barabara hiyo sasa inajengwa kwa nguvu kubwa kabisa na nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na kwa kazi ambayo anatufanyia pale kwenye Jimbo la Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha barabara hii ambacho kimebakia cha kutoka Kikweni kwenda Msangeni

– Kifula – Mwaniko mpaka Uchamangofi na chenyewe kimetengewa fedha katika bajeti hii na napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mkisikia kuna watu wanatoa hoja kuwapinga sana wapuuzeni, nendeni mbele kwa sababu hata Marekani leo inawekeza bado kwenye miundombinu, hata Uingereza ina kazi ya kuwekeza kwenye miundombinu. Matatizo tunayopata sasa hayawezi kwisha, kila siku yatakuwepo na kila siku tuwe tayari kupambana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niishukuru Serikali kwa kupandisha daraja barabara mbili, moja kutoka Lomwe - Ndolwe - Kilomeni - Lembeni kuwa barabara ya *TANROAD* na nyingine kutoka Kilya - Kitichamungu - Nyabinda - Kagongo - Lang'ata - Tingatinga - Kifaru na katika bajeti hii naona shilingi milioni 565 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Napenda nichukue fursa hii kuishukuru sana Wizara inayohusika, lakini pia kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana ambayo anafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa dakika tano ni mdogo sana, lakini napenda niseme kwamba katika barabara moja ambayo ndiyo kubwa sana ya *TANROADS* katika Wilaya yangu ya Mwanga kutoka Kifaru - Kigonigoni - Kichwa cha Ng'ombe kuna maeneo ambayo yameharibika sana na barabara wakati huu haipitiki kabisa kwa sababu ya mvua. Nawasihi sana, namsihi sana Mheshimiwa Waziri afanye kila juhudi ili eneo la kutoka Kisokoro - Kigonigoni - Mvuleni liweze kutengenezwa ili wananchi waweze kushughulika na shughuli zao za biashara kama ambavyo wamekuwa wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana pia nihimize kwamba maeneo ambayo hayafikiki kwa mtandao wa simu yawekewe juhudi maalum kule katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na maeneo ya Kisangara Juu na Jipendea yapate

minara mipya ya mawasiliano ili wananchi waweze kuendelea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Janeth Massaburi wajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge lako Tukufu. Pia nampongeza Rais wangu, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya za kujenga Taifa. Nawapongeza pia Mawaziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na Manaibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekee moja kwa moja katika mchango wangu. Kwa kuwa ukarabati unaoendelea wa Barabara ya Nyakanazi – Rusahunga - Rusumo haukidhi viwango kutokana na magari mazito yanayopita pale ya mizigo yanayoelekea nchi jirani za Rwanda, Burundi, Kongo na Uganda. Naomba sana Mheshimiwa Waziri husika na Wizara waweze kuangalia hii barabara itengenezwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waikarabati kwa kiwango kinachokidhi, kwa sababu kila siku kuna viraka vinavyowekwa pale. Mara leo kuna kiraka, mara kesho kuna kiraka, barabara inaendelea kuwa vilevile, bado kuna magari mazito yanayopita pale. Hii ni barabara ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa Taifa. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri naomba waliangalie hili kwa jicho la huruma na kwa kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kuna watu wana madaladala, wana teksi zinazotoka Ngara mpaka Kahama, kila baada ya mwezi wanabadilisha *shock up* na hali ilivyokuwa ngumu, kwa kweli inasikitisha sana. Naomba sana Serikali iweze kutuangalia kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuongelea huduma za ndege za Dar es Salaam *to* Bukoba, huduma za Dar es Salaam ni nzuri, abiria wameongezeka sana kutoka Dar es Salaam mpaka Bukoba, lakini *trip* ya Dar es Salaam *to* Bukoba ni moja tu. Naomba *trips* ziongezeke, sisi watu wa Kagera tumezoea sana kutumia ndege kuliko magari, kwa hiyo naomba mtuongezee *trips* angalau ziwe mbili au tatu, kwa kweli naomba watuangalie sana. Naomba sana sana iwepo *trip* ya mchana, tuna *trip* ya alfajiri tu, mtu unaamka saa kumi, saa tisa kuelekea *airport,* kwa kweli naomba Mheshimiwa Waziri hili waliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba kama inawezekana kuwepo na *trip* ya Dar es Salaam – Dodoma - Mwanza kwa sababu Kanda ya Ziwa kuna abiria wengi sana na Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Nchi, kwa nini wasituwekee ndege ya kutoka Dar es Salaam – Dodoma - Mwanza? Kama tuko hapa tunahitaji kwenda Mwanza na moja kwa moja inaenda Kagera bila shida, kwa kweli namwomba Mheshimiwa Waziri waweze kutuangalia sana watu wa Kanda ya Ziwa kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakandarasi walio-*supply* vifaa vya kujenga miundombinu katika Shule za Sekondari Ihungo na Nyakato wakati wa kipindi cha tetemeko bado wanadai pesa zao nyingi. Je, ni lini watalipwa pesa zao? Kwa sababu wame-*supply* majengo yamekuwa mazuri lakini hawajalipwa pesa zao. Kwa kweli naomba Wizara husika, Mheshimiwa kaka yangu Profesa Mbarawa, naamini ni mtu mzuri sana, hebu atuangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya usikivu wa simu yaliyopo Wilaya ya Ngara, Kata za Nyakisasa, Keza, Kabanga

na Rusumo yanaingiliana na Nchi za jirani za Rwanda na Burundi. Nimeshaongelea hili suala zaidi ya mara tatu ndani ya hili Bunge lako Tukufu, lakini sioni kinachoendelea. Wananchi wa Ngara tunapata shida, mtu unapiga simu uko Ngara inaingiliana na mtambo wa Rwanda, inaingiliana na mtambo wa Burundi. Kwa nini wasituangalie waongeze minara, waongeze mitambo ili tuweze kupata *communication* ambayo ni *within Tanzania,* kwa nini wasituangalie sana? Nimeshamwomba sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuongelea kuna uwanja ambao uko Ngara unaitwa *Ruganza Airstrip,* ule uwanja umesahaulika kabisa. Tumeutumia sana kipindi cha wakimbizi wakati nafanya kazi *UNHCR* ndiyo ulikuwa uwanja mkubwa sana na bado kuna madini ya Kabanga *nickel*, kule Kabanga *nickel* ndege zinatoka kule zinatumia ule uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, juzi kuna wakimbizi wamepata ajali wakati wanatoka Kigoma wanaelekea Burundi, wanapitia Kigoma – Kasulu – Kibondo – Ngara. Wamefika Ngara wakapata ajali, ule uwanja ndiyo ulitumika na watu wa *UN, UN* ni shirika kubwa la kimataifa lakini wametua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Ahsante. Mheshimiwa Flatei, Mheshimiwa Janet Masaburi na Mheshimiwa Dkt. Dalali.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kweli kwa kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kufanya kazi nzuri kwa maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri, naona kwa kweli anavyofanya kazi yake, yeye na timu yake, Manaibu wake wote wawili, kwa kweli niwapongeze sana, katika Awamu hii mnafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri anazofanya, nimesoma hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri hapa na nimeona kwa kweli barabara ambayo tumeiomba kwa muda mrefu, Barabara ya Mbulu ambayo imeelezwa hapa; Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti mpaka Lalago na huko Maswa na Bariadi. Barabara hii imeombwa kwa muda mrefu sana na ipo kwenye Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi, ukurasa wa 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafarijika kwamba kwa kweli leo nimeiona angalau imetambulika, ila ninavyoona hapa kadri barabara hii ilivyo na usumbufu kwa sasa ningeiomba Wizara na Mheshimiwa Waziri aone, najua hajawahi kutembelea barabara hii, najua hajafika kabisa, lakini aone kwamba barabara hii sasa ni hitaji kubwa mno la wananchi wa maeneo mengi; wananchi wa Karatu, wananchi wa Mbulu Mjini, wananchi wa Mbulu Vijijini, wananchi wa Mkalama, wananchi wa Singida, maeneo yote yale yanayopita moja kwa moja mpaka ufike Lalago, Maswa, mpaka kwako kule barabara hii inafika yenye kilometa 389. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni hiki; barabara hii itakapojengwa itafungua eneo kubwa ambalo limesahaulika kwa wingi na uchumi wa watu hawa utapanda. Nimeona kwamba mmeandika hapa kwenye ukurasa huu wa 38 kwamba itafadhiliwa na *KfW,* hawa Benki ya Ujerumani, sina tatizo, lakini ninachohofu; mwaka jana walisema ipo kwenye upembuzi wa awali, sasa hofu yangu mwakani watasema pia ipo kwenye upembuzi wa kati lakini baadaye mtatuambia tena iko kwenye upembuzi yakinifu, miaka mitano imekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ambaye yuko sasa wa Awamu ya Tano wa Hapa Kazi Tu ameahidi barabara hii na ipo kwenye Ilani na nini maana ya ilani; ni mkataba kati ya mtawala na mtawaliwa. Tumeahidi hii, ndugu yangu, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, aelewe, tumeahidi kwenye mikutano yetu, wananchi wa Mbulu na maeneo haya niliyoyataja wanaitegemea barabara hii na kule hatuna kitu kinaitwa lami kabisa, hatujawahi kuona tangu Mbulu imeanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe, Mbulu imeanzishwa 1905, haina barabara. Uchumi wa kule kwetu zaidi ya barabara hatuna lolote. Hatuna maziwa ambayo tungesema tungeweza kufanya usafirishaji wa maboti, meli na nini, hakuna huko na viwanja vya ndege kule hakuna. Kwa hiyo, tusipopata barabara hii ambayo naisemea sasa hatuna namna yoyote ya kufanya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa ndugu yangu Mheshimiwa Waziri aweke basi hela ambayo itaonesha namna nzuri ya kufanya upembuzi yakinifu mwakani. Najua ametenga milioni 50, milioni 50 sisi Wabunge saba tuliosema hapa tukichanga tunaweza kufika hizi hela, kwa nini nasema hivi? Sina nia ya kudharau alizoziweka hizi, lakini ni kidogo sana. Milioni 50 kwa barabara hii yenye kilometa 389, jamani sawasawa hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu barabara hii ni muhimu sana, muhimu mno, inaunganisha Mikoa ya Arusha na Manyara, Manyara na Singida na kutoka Singida inakwenda mpaka Meatu na Mheshimiwa Waziri anajua Simiyu iko kule. Kwa hiyo, niombe basi maana barabara hii ni muhimu na ni muhimu kwa sababu kuna Hospitali kubwa ya Haydom iko katikati ya mikoa hii ambayo watu wengi wanaitegemea kwenda katika hospitali hii. Basi nimwombe Mheshimiwa Profesa Mbarawa, anajua nampenda sana, lakini mapenzi haya yaende basi na kuweka hii barabara, awekea barabara ndugu yangu, aweke barabara narudia tena. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, najua wazi kwamba Rais wetu ni msikivu, ili asionekane Rais ambaye ameahidi halafu baadaye haikufanyiwa kazi, Mheshimiwa Waziri asimuangushe, amemweka hapa ili akamsaidie kazi hii. Aweke Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti – Maswa – Lalago, twende mpaka kwa Mheshimiwa Chenge kule. Kwa hiyo, naomba ndugu zangu wanielewe, Mawaziri wako watatu hapa wakumbushane katika ofisi yao basi, kwa kuwa barabara hii ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda nichangie mchango wangu wa dakika tano kwa kusemea barabara hii tu kwa sababu ndiyo kufa na kupona. Leo asipoiweka barabara hii akaiwekea fedha mwakani atakuwa hajatusaidia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, najua atatuwekea barabara.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Janeth Masaburi, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani na Mheshimiwa Ally Keisy Mohamed ajiandae.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea; nitaongea kwa uchache sana. Sichoki na sichoki tena katika kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watakumbuka ndugu zangu, huko nyuma sisi tunaokwenda Mara tulikuwa tunapita Nairobi, Sirari ndiyo tunaingia Mara; wanaokwenda Kagera walikuwa wanapita Nairobi, Kampala huko ndiyo wanaingia kule Bukoba. Lakini chini ya uongozi tukimkumbuka Mheshimiwa Rais wetu ambaye alikuwa Waziri wa Ujenzi,

hakulala, alikuwa analala kwenye mahema huko. Mheshimiwa Rais amejitoa muhanga katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia siachi kumshukuru na kumpongeza, amefufua Shirika la Ndege, huko nyuma tulikuwa tunapiga kelele nchi haina ndege, nchi inaliwa, yeye amekuja ameleta ndege kwa mkupuo. Tunasema watalii wamepungua nchi hii hatuna alama, ameleta ndege ili tutangaze nchi yetu katika utalii. Mheshimiwa huyu amefungua barabara ukihesabu toka miezi miwili iliyopita hawezi kukaa wiki moja bila kufanya kazi, haijawahi kutokea Rais wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tusichoke kumuunga mkono. Kwanza ametupa heshima katika Chama chetu cha Mapinduzi, nawashangaa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambao wanabeza mafanikio. Wengine wana hasira, kama hasira zako peleka nyumbani, lakini Chama cha Mapinduzi chini ya utekelezaji wa Ilani amefanya. Umpende usimpende, ndio Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wake, wote wamemwelewa. Maana yake nikianza kumchambua Waziri wa Ujenzi, nikichambua Mawaziri wengine ambao bajeti zao zimepita, wote kila mtu anafanya kazi kwa bidii na umakini. Naibu Mawaziri wanakimbizana utafikiri panya, huyu katokea huku, huyu kaenda huku, mwingine analia, mwingine anabeba ndoo, wote wana lengo moja katika kujenga nyumba moja ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani, juzi wameunga mkono bajeti ya afya kwa asilimia mia, hongereni sana. Kwa sababu wanaelewa ukweli na sisi kama kwa wenzetu wamefanya kitu kizuri kwa kupongeza Serikali ya CCM basi na sisi tuwapongeze. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kero ndogondogo ambazo najua zitafanyiwa kazi, lakini kuna baadhi ya ma-*engineer* hawako makini. Kuna barabara za ndani za Mkoa wa Dar es Salaam, ni mbovu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Waheshimiwa Wabunge, kusifia nitarudia bado naendelea! Maana yake hiyo inawachoma wengi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za ndani za Mkoa wa Dar es Salaam ni mbovu. Kwa mfano, ukiangalia Barabara ya Segerea Seminari kuelekea Majumba Sita kupitia Kituo cha Polisi pale Stakishari, barabara ni mbovu, lakini hiyo barabara Mheshimiwa Rais aliahidi akiwa kwenye mkutano pale Vingunguti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri aiangalie barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kinyerezi kwenda Malamba Mawili, tunaomba kasi iongezeke. Barabara tumeona imeharibika, Daraja la Kivule lile tunaomba pia kasi na umakini uongezeke; tunaomba ma-*engineer* wenye umakini waongezwe katika Mkoa wa Dar es Salaam maana kuna wengine hawako makini. Leo sipendi kuwataja watu, lakini kuna watu wanakera, tunaomba umakini katika kuangalia barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba Uwanja wa Ndege wa Musoma ujengwe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed ajiandae.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, hatimaye nimepata fursa hii kupitia wewe ya kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Niombe kuchukua fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, Rais wa hapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa kwa kazi kubwa anayoifanya ikiwa ni pamoja na kunifundisha mimi siasa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie baadhi ya michango ambayo ni kuongezea au kukazia ambayo wamechangia wenzangu. Moja, ni kuhusu barabara inayounganisha Mikoa ya Morogoro na Ruvuma kupitia Wilaya yangu ya Namtumbo. Barabara hii tulitoa matumaini mwaka jana mwezi Julai kwamba imetoboka na kwa matumaini yale kuna watu wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri nimemwandikia kilichotokea, naomba atusaidie kuikata zaidi ile barabara ili iweze kupitika, tuanze kupita kwa magari na pikipiki kabla hiyo lami haijaanza. Najua lami ni Ilani ya Uchaguzi ya Serikali ya Awamu ya Tano lakini vilevile ilikuwa Awamu ya Nne na tulianza usanifu Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, katika kipindi kifupi ameiwezesha barabara hii kukamilika kwa maana ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, umekamilika. Najua hii ni hatua kubwa sana katika ujenzi wa lami wa barabara hii. Nimwombe sana anisaidie kukikata kile kipande cha kuanzia Kilosa Kwampepo mpaka Londo ili tuweze kupita kutoka pande zote mbili; tukitoka Namtumbo kwa maana ya Kitanda, lakini vilevile tukitokea Kilosa, Kwampepo ambako sisi kule ndiyo nyumbani kwetu, kule ndiyo kuna mizimu yetu. Naomba sana atusaidie ili tuweze kufika katika maeneo ambayo ndiyo tunayaabudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa kwa jinsi alivyonisaidia kukubali kuanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati wa kampeni. Ni kiongozi pekee aliyepita Barabara ya Mtwara – Pachani – Ligera – Lusewa – Magazini – Likusanguse hadi Nalasi wakati wa kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa kutoa fursa hii ya kuanza kutekeleza ahadi hii kwa kumpata mkandarasi wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Namshukuru sana hii kazi inaendelea na naomba waendelee kutenga fedha ili Mhandisi Mshauri huyo aweze kuikamilisha hiyo kazi kwa wakati kwa maana ya mwakani, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF),* ameuwezesha kwa namna ya ajabu kabisa kukamilisha mawasiliano kwa sehemu kubwa sana ya Wilaya ya Namtumbo. Nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, akamilishe kipande hiki kidogo kilichobakia, tumebakiwa na kata kama tatu hivi ambazo hazina mawasiliano, mpaka leo bado wanalazimika kupanda kwenye miti au kusafiri umbali wa kilometa tatu, nne ili waweze kupata mawasiliano. Nimwombe Mheshimiwa Waziri anisaidie kupitia Mfuko huu wa Mawasiliano kwa Wote tukamilishe mawasiliano kwa Wilaya nzima ya Namtumbo kama ambavyo alianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri; kuna ahadi imetolewa na Taasisi yake ya *TEMESA* kutujengea kivuko. Sisi tunapakana na Msumbiji kwa maana ya Wilaya ya Namtumbo na tuna kivuko cha zamani sana, enzi na enzi, kinachotumika kufanya biashara kati ya Wilaya ya Mavago ya upande wa Msumbiji na Wilaya yetu ya Namtumbo. Nimwombe sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngonyani. Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia nikiwa mchangiaji wa mwisho. Kwanza kabisa, nampongeza Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kumteua Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa kushika nafasi ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Naibu Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu wake. Sina budi kabisa kumshukuru Mheshimiwa Profesa Mbarawa, kusema kweli wamenisaidia sana mimi katika Jimbo la Nkasi Kaskazini, kwa mara ya kwanza naisifu hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoomba; mchakato wa ile Barabara ya Kirando – Kazovu mpaka sasa umechukua mwaka mzima na juzi wamekufa vijana watatu kwenye ule mto kwa kuvuka kuja ng'ambo ya pili, mpaka leo maiti moja imeonekana, mbili hazijaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna siku tatu wanafunzi kutoka Katete na Chongo kwenda *Secondary School* ya Kirando wanashindwa kuvuka ule mto na pesa zina mwaka mzima, mkandarasi yupo, lakini urasimu wa watendaji leo, kesho, mpaka leo daraja halijajengwa wala hakuna mpango wa kujenga daraja hivi karibuni. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri akitoka hapa awahimize watu wake wajenge daraja haraka sana kuokoa maisha ya wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri Ziwa Tanganyika, leo ni mara ya nne, walituahidi kwanza meli mbili, sasa imekuwa meli moja na hiyo meli moja haijulikani. Cha ajabu Burundi wameshajenga meli kubwa sana, *DR Congo* wameshajenga meli kubwa sana, wametupiga bao. Sisi tunabaki kwa sababu tuna Bandari yetu ya Kigoma na Ziwa Tanganyika, ni ajabu watu wa Kongo ambao hawana

bandari upande wa pili na watu wa Burundi wasio na bandari watatumia ziwa letu kwa ajili ya kusafirisha mizigo. *DR Congo* wameunda mpaka meli ya kubeba mabehewa, sisi tumekaa tu tunaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu wa miaka nenda, miaka rudi, haiwezekani. Walitenga bilioni kumi kwa ajili ya ukarabati wa Lihemba lakini mpaka leo hakuna. Watumishi wa *Marine Service* miezi 23 hawajalipwa mshahara, kusema kweli hii inakuwa meli zetu zinakwenda kizobazoba tu, maana yake watumishi hawana mshahara, hawana chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza *TANROADS Manager* wa Mkoa wa Rukwa. Ukimpigia simu hata saa saba za usiku kwamba kuna shimo kwenye barabara au barabara imefanya hivi, mara ileile kesho yake tayari alishatuma watu kwenda kutengeneza. Kusema kweli *TANROADS Manager* wa Mkoa wa Rukwa anafanya kazi, halali usingizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza kabisa *Engineer* Eliud wa Mfuko wa Barabara, ndio alikuwa chachu kabisa kuisadia Barabara ya Kirando – Kazovu ambayo ndugu zangu wananchi wamenituma kule. Kuanzia sasa vijiji vyote vya mwambao wa Ziwa Tanganyika hawataki kusikia chama cha upinzani, pamoja na Madiwani wa CHADEMA wako kule kwetu, wameniambia kamwambie Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwamba kuanzia sasa sisi kura zote ni CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi kabisa, muulizeni hata Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Nditiye, alikwenda Kabwe akamkuta kule Diwani wa CHADEMA, amemhakikishia kabisa kura zote ni kwa CCM. Kwa hiyo, ndugu zangu CCM kusema kweli inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukimfufua mtu aliyekufa mwaka jana akaja leo akaangalia, atashangaa, itabidi arudi kaburini haraka kwa yale maendeleo aliyofanya Mheshimiwa

Dkt. Magufuli katika nchi hii. Tuache mchezo, Serikali ya Dkt. Magufuli inafanya maendeleo. Wilaya ya Nkasi naishukuru Serikali, Kabwe leo wametujengea bandari, ilikuwa miaka yote katika vitabu vyote inaandikwa, bajeti ya Bandari ya Kabwe, lakini leo kuna Mkandarasi yuko kazini na asilimia 20 ya kazi ilishaanza kufanywa, unasema huwezi kuishukuru Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, upinzani wapeleke huko huko. Mwaka 2020 ndugu zangu watapata aibu kubwa maana yake vitendo vinaonekana, Mawaziri wanapishana. Mimi kwangu Nkasi ni mbali sana kuliko sehemu yoyote lakini Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa amefika, Naibu Waziri amefika kuja kuangalia maendeleo yanayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mkurugenzi wa *TPA.* Mkurugenzi wa *TPA* ndio chachu ya maendeleo ya Bandari ya Ziwa Tanganyika, amefanya... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Inabidi tukakupime akili wewe!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Huyo ndio Mheshimiwa Keissy.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tumefika mwisho wa shughuli zetu kwa leo. Nawashukuru sana kwa msaada mlionipa kwa siku nzima na kwa michango yenu mizuri tu. Sahani na kikombe havikosi kukwaruzana, lakini kwa ujumla tumekwenda vizuri.

Nawashukuru sana.Hata hivyo, tuna Wabunge wawili upande wa Chama cha CHADEMA kwa dakika tanotano hawakupata nafasi, lazima tuwataje majina ili kambi yao kesho wajue, nisilaumiwe mimi au Mwenyekiti au kiongozi yeyote atakayekuwa hapa na vilevile wapo wanne kwa upande wa Chama cha Mapinduzi.

CHADEMA dakika tano tano walikuwa ni Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Joseph Mkundi. Kwa upande wa Chama cha Mapinduzi walikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu. Kwa hiyo, viongozi wa kambi husika naamini majina haya watayawekea utaratibu ili haki itendeke.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, Siku ya Jumanne, tarehe 24, Aprili, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 24 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*